# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 24 Aprili, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe.* Mussa Azzan Zungu*) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Kamati ya Viwanda Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. CECILIA D. PARESSO – (K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. CECILIA D. PARESSO - (K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA):**

Taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa mwaka 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 85

**Utaratibu wa kuwasimamisha kazi Watumishi wa Umma**

**MHE. MCH.PETER S. MSIGWA (K.n.y. MHE. RUTH H. MOLLEL)** Aliuliza:-

Nchi yetu inaendeshwa kwa kuzingatia Katiba, Sheria na Kanuni katika kuajiri na kuwasimamisha kazi watumishi wa umma. Kuna baadhi ya watumishi wa umma wamesimamishwa kazi na Mheshimiwa Rais, *RC* na hata *DC* bila kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

Je, Serikali inasemaje kuhusu hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za nidhamu katika utumishi wa umma hutekelezwa kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali. Kwa mujibu wa Ibara ya 36 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Rais ndiye mwenye mamlaka ya mwisho kuhusu usimamizi na uendeshaji wa utumishi wa umma, ikiwemo kuanzisha, kufuta Ofisi na kuchukua hatua za nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo ya 36(2) imempa Rais uwezo wa kukasimu madaraka yake kwa mamlaka mbalimbali ndani ya utumishi wa umma. Hata hivyo kukasimu madaraka hakuwezi kutafsiriwa kwamba Rais hana mamlaka hayo tena kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya

36(4) ya Katiba na Kifungu cha 21(4) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale maelekezo ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa umma yanapotolewa na Viongozi wa Serikali, Mamlaka za Nidhamu za watumishi husika ndizo zenye dhamana ya kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nakubaliana naye kwamba kwa mujibu wa Sheria na Katiba yetu, Rais ndiye mwenye mamlaka ya mwisho na ndiye Mwajiri Mkuu.

Swali la msingi limeulizwa kwamba kumekuwa na *practice* ya kuanzia Rais mwenyewe na ma-*DC* na *RCs* kutumbua au kuwasimamisha watu kwa njia ya mnada, kupigia kura atumbuliwe au asitumbuliwe, kwa hiyo, swali la msingi linaulizwa hapa, ni kwa nini Serikali isifuate utaratibu na kanuni na sheria ambazo sisi wenyewe tumeziweka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, hawa ma-*RC* na ma-*DC* ni kada ya kisiasa kama sisi Wabunge tulivyo, hawana weledi na ndiyo maana Baba wa Taifa alisema tuliweka sheria ngumu sana ili mtu asizuke tu na kufukuza watu ovyo ovyo. Kwa kumuenzi Baba wa Taifa ambaye alithamini sana kada ya watendaji wa umma; je, Serikali itatoa tamko sasa kwamba ma-*RC* na ma-*DC* wasikurupuke tu kuwafukuzisha watu bila kufuata taratibu na kanuni za nchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kuhusiana na kwa nini Serikali

isifuate utaratibu, napenda kuendelea kusisitiza kwamba Serikali inafuata uratatibu na kwamba kwa wateule ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais, hatua zao za kinidhamu huchukuliwa na Katibu Mkuu Kiongozi kwa mujibu wa kifungu cha 4(3)(d) cha Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema katika Ibara ya 36(4), Mheshimiwa Rais pamoja na kukasimu bado anayo mamlaka ya mwisho na hakatazwi kutumia mamlaka yake. Kwa watumishi wengine wa umma, kwa mujibu wa kifungu cha 6(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Mamlaka za Nidhamu zimepewa mamlaka yao ya mwisho kabisa ya kuweza kuchukua hatua kwa watumishi wengine ambao sio wateule wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuendelea kusisitiza kwamba jambo la msingi katika mamlaka za kinidhamu zinapochukua hatua, wanatakiwa wazingatie hatua tatu zifuatazo:-

Kwanza kabisa waweze kutoa hati ya nashtaka; pili, watoe fursa ya kujitetea kwa yule mtuhumiwa au mtumishi; na mwisho, tatu, uchunguzi wa kina uweze kufanyika ili kuthibitisha tuhuma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kusema, utaratibu mzima wa kina na mwongozo umefafanuliwa katika kanuni ya 46 na 47 za Kanuni za Utumishi wa Umma. Endapo kuna mtumishi wa umma anaona hajaridhika na hatua za kinidhamu zilizochukuliwa, anayo fursa kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria ya Utumishi wa Umma kuweza kukata rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la pili kwamba Serikali inatoa tamko gani katika hatua ambazo zimechukuliwa na ma-*RC* na ma-*DC?* Naendelea kusisitiza kwamba kifungu cha 6(1)(b) na kifungu cha 4(3)(d) kimeelekeza Mamlaka za Nidhamu ni zipi? Ndicho ambacho Serikali imekuwa ikifuata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde, ajiandae Mheshimiwa Chatanda.

**MHE. DAVID E. SILINDE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwenye majibu ya Mheshiwa Waziri amesema, endapo mtumishi hajaridhika na hatua za kinidhamu alizochukuliwa, akate rufaa. Sasa endapo mtumishi huyo ametumbuliwa na Mheshimiwa Rais na hajaridhika na hayo matokeo, wapi achukue hatua za kuja kukata rufaa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza Mheshimiwa Silinde ameuliza swali zuri sana; na kama atakuwa amefuatilia hata katika hotuba yangu ya bajeti ya Ofisi ya Rais (Utumishi), ziko kesi mbalimbali ambazo hata Ofisi ya Rais (Utumishi) pia tunashitakiwa. Wako ambao wanafungua kupinga maamuzi ya Mheshimiwa Rais, wako ambao wanafungua kesi kupinga maamuzi ya Katibu Mkuu Kiongozi, lakini pia katika Tume yetu ya Utumishi wa Umma ambayo ni mamlaka yenye Mamlaka ya Urekebu wamepokea kesi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, katika mwaka huu wa fedha tu peke yake, zaidi ya watumishi wa umma 76 wameweza kukata rufaa katika Tume ya Utumishi wa Umma na endapo hawataridhika, bado tunacho Kitengo cha Rufaa chini ya Mheshimiwa Rais pia *(Public Service Appeals)* wanaweza pia wakakata rufaa nyingine. Kwa hiyo, namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zipo na zinafuatwa na ziko wazi kabisa na wako ambao hata wanajikuta walikata rufaa dhidi ya Mheshimiwa Rais na wakaja kushinda endapo kama kuna taratibu inaonekana hazikufuatwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Utumishi kwa majibu mazuri sana. Nilitaka kuongezea, kuna moja ambalo limewataja Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuchukua hatua za kuwasimamisha au kuwafukuza kazi watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kifungu cha (5) cha Sheria ya Tawala za Mikoa, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ndio wawakilishi wa Serikali Kuu kwenye maeneo yao. Ukisoma pia kifungu cha 87 cha Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kinawataja hawa na kwa ajili ya usahihi wa nukuu, napenda nisome kwa sababu wakati mwingine tunauliza swali lile lile kila siku. Bahati mbaya imeandikwa kwa Kiingereza, inasema hivi; *"In relation to the exercise of the powers and performance of the functions of the Local Government Authorities confered by this Act, the role of the Regional Commissioner and the District Commissioner shall be to investigate the legality when questioned of the actions and decisions of the Local Government Authorities within their areas of jurisdiction and to inform the Minister to take such other appropriate action as may be required." (Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Yes!*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukisoma kifungu hiki unaona kabisa kwamba wao kuchukua hatua zozote zile, ziwe za kiutumishi ni sahihi, isipokuwa utaratibu aliouzungumza Mheshimiwa Waziri wa Utumishi ndiyo unaotakiwa.

Kwa mfano, Mkuu wa Mkoa anaposema wewe hufai, umefanya makosa haya, akasema *publicly,* siyo ndiyo kafanya tendo hilo la kumsimamisha au kumuadhibu yule mtumishi, anachofanya pale, baada ya tamko lile, sasa Mamlaka ya Nidhamu ya mtumishi husika ndiyo inachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika *level* ya Halmashauri, sasa Mkurugenzi atamwandikia barua kama ni ya kumsimamisha au kumtaka atoe maelezo fulani kulingana na maagizo ya Mkuu wa Wilaya, au Mkuu wa Mkoa atafanya hivyo. Kwa ngazi ya Mkoa, *RAS* ndio Mamlaka ya Utumishi, naye anaweza kuagizwa na kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo kutamka tu kwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, ndiyo tayari basi yule amemchukulia hatua za kinidhamu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Wizara ya Utumishi ina watumishi wanaofanya kazi vizuri, hawajatumbuliwa, Serikali kwa maana ya Chuo cha Ualimu, kutokana na swali langu namba 81 ambalo nilijibiwa kwamba suala la upandishaji madaraja na likizo za Watumishi wamelipwa kwa kiasi kile ambacho walikuwa wamekitaja.

Je, watakuwa tayari sasa kutoa orodha ile ya wale waliokwishalipwa kwa Chuo kile cha Korogwe cha Ualimu ili kusudi Walimu waweze kujitambua kwa sababu huwa kama wanawalipa, wanaingiza moja kwa moja kwenye mishahara, watakuwa tayari kuitoa hiyo orodha ili iende kwa Mkuu wa Chuo kila mtu aweze kutambua kile alichoweza kulipwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chatanda. Nimelifuatilia swali hili, nadhani wiki iliyopita lilijibiwa na Mheshimiwa Stella Manyanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kusema kwamba nitafuatilia na Wizara ya Elimu kwa karibu ili kuona waliolipwa ni akina nani na orodha iweze kutolewa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimwa Omari Mohamed Kigua.

Na. 86

**Kulinda na Kutunza Vyanzo vya Maji**

**MHE. OMARI M. KIGUA** Aliuliza:-

Serikali imekuwa ikisisitiza na kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kulinda na kutunza vyanzo vya maji kwa kutokata miti ovyo na kutojenga karibu na vyanzo hivyo, lakini wako baadhi ya wananchi wenye tabia ya kushirikiana na baadhi ya watumishi wachache wa Serikali kukata miti ovyo na kujenga karibu na vyanzo vya maji.

(a) Je, ni lini Serikali itasimamia kikamilifu sheria za kulinda mito na miti nchini?

(b) Je, Serikali haioni umefika wakati sasa kutunga sheria kali zaidi ili kujihami na *global warming?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua changamoto za uharibifu wa vyanzo vya maji na misitu nchini, Serikali imechukua hatua za kisera, sheria na kimkakati kukabiliana nazo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya mwaka 2004, kifungu cha 57(1) kinazuia shughuli yoyote ya kibinadamu yenye athari kwa mazingira kufanyika ndani ya mita 60 kutoka kwenye kingo

za bahari, mito, maziwa na mabwawa ili kulinda vyanzo vya maji.

Aidha, kifungu 55 cha sheria hiyo kimetoa mamlaka kwa Halmashauri kuweka miongozo ya kulinda vyanzo vya maji na kuchukua hatua kali kwa yeyote anayekiuka sheria. Vilevile Halmashauri zote nchini zimelekezwa kutunga na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo kwa ajili ya kulinda vyanzo vya maji na misitu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 imeweka utaratibu wa kusimamia na kuhifadhi ya misitu ikiwemo kutoa adhabu kwa uharibifu wa misitu na ukiukwaji wa miongozo ya uvunaji endelevu wa rasilimali za misitu. Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji na kuchukua hatua kali kwa wote wanaokiuka Sheria hizi kwa lengo la kulinda vyanzo vya maji na misitu nchini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, kifungu cha 75 (a) mpaka (e) inaelekeza hatua za kuchukua ili kulinda na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na kuongezeka kwa joto la duniani yaani *global warming,* katika sekta mbalimbali nchini. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2012 kupitia sekta, halmashauri, taasisi za umma na binafsi katika kutekeleza miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika maeneo yaliyoathirika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uharibifu wa mazingira umekuwa ni tatizo sugu sana hususan katika Jimbo langu la Kilindi katika Kata za Negero, Mkindi, Kilindi

Asilia pamoja na Msanja kutokana na shughuli za kibinadamu; je, Waziri yuko tayari kwa kushirikiana na Wataalamu wetu wa Chuo Kikuu cha *SUA,* kwa mfano, tuna Watalamu wazuri, akina Profesa Dhahabu na Mariondo kwa ajili ya kupeleka timu kule kuweza kufanya tathmini kubwa? *(Makofi)*

Swali la pili, suala hili la mazingira limekuwa ni sugu sana; je, Serikali iko tayari sasa kwa kushirikiana na Halmashauri kuhakikisha kwamba inapeleaka wataalamu wa kutosha wa mazingira kulinda maeneo yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshindwa kujizuia kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua. Nampongeza kwa swali lake zuri sana leo la mazingira hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yake ya nyongeza naomba niyajibu kama ifuatavyo:-

Moja, kwanza ofisi yangu inashirikiana vizuri sana na wataalam wa mambo ya mazingira hasa katika mambo ya hewa ya ukaa ambao wako pale *SUA.* Nimhakikishie kwamba ofisi yangu haina kipingamizi chochote cha kuja kufanya tathmini ya maeneo yaliyoathirika katika Kata alizozitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaunda hiyo timu, itakuja na hao wataalam na nimhakikishie kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais ina watalaam waliobobea katika mambo ya mazingira vizuri sana, kwa hiyo, hakuna kitu ambacho kitaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba wasiwasi wake kuhusu wataalam wa mazingira ambao anahisi

kwamba Halmashauri nyingi hazina wataalam na sekta nyingine, nimhakikishie tu kwamba hivi karibuni Waziri wangu anakamilisha orodha ya wataalam ambao tutawateua ambao ni Wakaguzi wa Mazingira *(Environmental Inspectors)* zaidi ya 400 hapa nchini na watasambazwa kwenye sekta mbalimbali. Hivyo basi, tatizo hili na kiu kubwa ya kuwahitaji wataalam hawa watakuwepo katika sekta kama Mheshimiwa Mbunge ambavyo ameomba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yussuf, ajiandae Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu yako mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kusema kwamba kuna sheria ya mita 60 kutofanya huduma yoyote kutoka kwenye chanzo cha maji, lakini bado vyanzo vya maji vinaendelea kuathirika katika maeneo ya wazi na mpaka ndani ya mbuga zetu ambayo ni maeneo yanayolindwa na kuhifadhiwa na Serikali.

Je, Serikali sasa ina mpango gani mahsusi wa kufanya utafiti wa miti ambayo inazalisha maji, iwe imepandwa kuzunguka vyanzo vya maji? Ni mkakati upi hasa mahsusi wa kudhibiti hivi vyanzo vya maji visiathirike? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mita 60 na vyanzo vya maji kuendelea kuharibiwa na utafiti ambao unafanyika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tulipokuwa tunaandaa Mkakati wa Kitaifa wa Upandaji Miti wa mwaka 2016 hadi mwaka 2021, tulizingatia hayo na mpaka sasa hivi tumeshabaini aina ya miti inayofaa kupandwa katika vyanzo vya maji na utaratibu huu tutausambaza kwa wataalam wote. Kwa kushirikiana na *TFS* na wataalam wa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, tumeshaandaa tayari aina ya miti ambayo inafaa kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vyetu vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jithada unaziona, juzi hapa Mheshimiwa Makamu wa Rais amezindua mpango mkubwa wa kuokoa hali ya uharibifu wa mazingira ambayo inaendelea katika Mto Mkuu Ruaha. Katika kufanya hivyo, hatuishii hapo, tutaendelea kufanya tathmini katika vyanzo vyetu vya maji vyote ili tuje na *solution* ya uhakika na tuweze kutenga fedha zinazokidhi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mazingira haya tunayalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la mazingira ni gumu sana, ulinzi wake ni mgumu. Inatakiwa kila mwananchi, sisi wenyewe Wabunge tuhakikishe kwamba tunasaidia kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanalindwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mheshimiwa Aweso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi athari zake zimeonekana wazi wazi katika Mji wa Pangani. Serikali pamoja na jitihada kubwa wanazozifanya kukarabati ukuta wa Pangani, lakini bahari imekula kwa kiasi kikubwa kwa eneo la *Pangadeco;* je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya haraka kuhakikisha kwamba inaanza ujenzi wa ukuta kwa eneo la *Pangadeco?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi, ni lini? Mwambie apitishe bajeti.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafanya tathmini katika eneo lililobaki la Pangani ambalo kwa jina maarufu *Pangadeco* katika mwaka ujao wa fedha wa 2017/2018. Serikali itafanya tathmini ya eneo hilo na kutafuta namna bora tutakayoitumia, aidha kujenga ukuta au njia nyingine.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Katiba, Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, kwa niaba yake Mheshimiwa Alberto.

Na. 87

**Kuvunjwa kwa Haki za Binadamu Nchini**

**MHE. SALEH ALLY SALEH (K.n.y. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED)** Aliuliza:-

Kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na matendo ya dhahiri yanayoonesha kuvunjwa kwa haki za binadamu hapa nchini bila ya Serikali kuchukua hatua yoyote.

Je, Serikali haioni kwamba wananchi watakosa imani na Serikali yao?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya jukumu la msingi kwa Serikali ni kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na wajibu wao hapa nchini. Jukumu hilo ni la kikatiba ambapo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ilivyorekebishwa mara kwa mara na Katiba ya Zanzibar ya 1984 kama ilivyorekebishwa mara kwa mara pamoja na kuainisha haki za binadamu, imeipa Serikali wajibu wa kukuza, kulinda na kuhifadhi haki hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, nchi yetu imeridhia mikataba mbalimbali ya Kimataifa na kikanda ambayo inaweka misingi ya haki hizo na wajibu wa Serikali katika kuhakikisha nchi inaendeshwa kwa kufuata misingi ya haki za binadamu. Aidha, Bunge lako Tukufu kwa nyakati tofauti limetunga sheria mbalimbali zinazolinda na kukuza haki za binadamu pamoja na kutoa

nafuu *(remedy)* kwa raia pale haki za binadamu zinapovunjwa aidha na Serikali au mtu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa, zinadumishwa na zinastawishwa hapa nchini, Katiba imeipa Mahakama mamlaka ya kusikiliza na kuamua mashauri yanayohusu haki za binadamu na wajibu wao kama ulivyoainishwa katika Katiba. Aidha, Serikali imeunda taasisi mbalimbali zinazoshughulikia hifadhi ya haki za binadamu. Taasisi hizo ni pamoja na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Mabaraza mbalimbali kama yale ya Ardhi na Kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama pamoja na taasisi hizi zimekuwa zikichukua hatua pindi vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu vinapotokea na kuripotiwa au kufikishwa kwa maamuzi. Serikali kupitia vyombo vyake, imejidhatiti kuhakikisha kuwa kitendo chochote kinachovunja haki za binadamu kinachukulia hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasihi Waheshimiwa Wabunge tushirikiane na vyombo vyetu vilivyopewa mamlaka na dhamana ya kulinda haki pale tunapopata taarifa za vitendo vya uvunjwaji wa haki za binadamu vimefanyika au vinaweza kufanyika ili hatua stahiki na za haraka za kisheria zichukuliwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alberto.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ahsante kwa mwalimu wangu. Napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mwalimu wangu utakuwa unajua kwamba katika siku za karibuni kumekuwa na vitendo vingi vya utesaji na vimekuwa vikitajwa hadharani, lakini Mahakama zitapewa nguvu zaidi kama Tanzania itaridhia mikataba ya Kimataifa. Kuna mkataba mmoja muhimu wa *Convention Against Torture* mpaka leo Serikali inasuasua kujiunga.

Je, ni lini Serikali itaridhia mkataba huo muhimu ili Mahakama zipate nguvu zaidi kushughulikia masuala haya? Pamoja na kwamba suala hilo limetajwa katika Katiba, lakini mkataba huo ni muhimu.

Swali la pili, hadi sasa mfumo uliopo hauruhusu Ripoti ya Haki za Binadamu kujadiliwa katika Bunge, inawasilishwa lakini haijadiliwi na kwa maana hiyo, Waheshimiwa Wabunge hawana uelewa wa pamoja au uelewa mkubwa wa kujua kiasi gani madhara ya haki za binadamu na namna zinavyokiukwa kwa kulinganisha hata ripoti ya karibuni ya *Amnesty International* inayoonesha kwamba ukiukwaji wa haki za binadamu Tanzania ni mkubwa sana.

Je, kwa weledi wako, ushawishi wako, karama ulizopewa na Mwenyezi Mungu, ni vipi utaweza kuishawishi Serikali ili ripoti hiyo iweze kujadiliwa ili Waheshimiwa Wabunge wajue yapi yanatokezea katika nchi yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kama alivyoeleza, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenyewe inakataza vitendo vyovyote vya kumtesa, kumtweza na kumdhalilisha mtu. Tafsiri ya Ibara hiyo ya Katiba imewekwa wazi na Mahakama na Rufaa katika kesi ya Mbushuu Mnyaroje dhidi ya Serikali ambapo Mahakama ya Rufaa ilieleza wazi kabisa kwamba vitendo vyovyote vinavyomtesa mtu, kumtweza na kumdhalilisha, havikubaliki na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Rufaa ilikwenda mbele zaidi, ilitumia mikataba ya Kimataifa ile ambayo Tanzania imeridhia na ile ambayo haikuridhia kama msaada kwao wa kutafsiri maana ya neno au maneno utesaji, udhalilishaji na utwezaji. Kwa hali hiyo basi, maoni hayo kwamba mkataba huu dhidi ya utesaji ambao tayari misingi yake imo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo tayari Mahakama ya Rufaa

ambayo ndiyo Mahakama ya mwisho ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeyakubali, yatafikiriwa ili kwa wakati muafaka jambo hilo lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ripoti ya *CHRAGG* kuletwa Bungeni, maoni hayo nimeyapokea na labda kwa upya wangu nitauliza ni jinsi gani yanafikishwa, maana hata kikao kimoja cha Baraza la Mawaziri sijakaa ili nijue utaratibu wa kuyafikisha, kujadiliwa ili nikiongozwa njia ya kuku mgeni kamba kuwa imefunguka, basi nitajua jinsi ya kwenda nalo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msabaha, ajiandae Mheshimiwa Selasini.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi naomba nimwulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kuna wananchi ambao wanakamatwa kwa uhalifu mbalimbali, aidha wa kubandikiziwa kesi na kupata kipigo kikali sana na kufanyiwa majeraha kwenye miili yao na kufikishwa kwenye vyombo vya mahabusu bila kupatiwa huduma za afya, hamuoni kama mnakiuka haki za binadamu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kama jambo hilo limetokea Zanzibar, pia kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, vitendo hivyo ni vitendo vya kukiuka Katiba kama vimetokea. Kwa yule viliyemtokea kama vimemtokea; moja, anayo nafasi ya kuiambia Mahakama ameteswa au amefanywa hivyo na hatua kuchukuliwa. Pia kuchukua hatua hizo kuziarifu mamlaka nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ushahidi upo kama ilivyovyoelezwa, Serikali na vyombo vyake inao utaratibu wa

kuchukua hatua dhidi ya vitendo hivyo ambavyo Katiba yenyewe imevizuia, sheria imevizuia, lakini hiyo haina maana hakuna binadamu wanaofanya hayo. Tumepewa amri kumi na Mwenyezi Mungu, mara nyingi tunazihalifu, lakini haina maana kwamba hazipo. Kwa hiyo, yakitokea hayo, tuarifiwe. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa katika swali hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa kwamba baadhi ya askari polisi wetu wanashindwa kutumia sheria ambayo inawaelekeza namna ya kukamata watuhumiwa na mara nyingi sana polisi wamekuwa wakiwahukumu watuhumiwa kwa kipigo kikali sana kabla hawajawafikisha Mahakamani na wakiwafikisha Mahakamani, Mahakama zinawaona watuhumiwa kwamba hawana hatia. Kama Mahakama ilivyoamua hivi majuzi kwenye kesi ya Bwana Mdude, Nyangari na wenzake huko Mbozi.

Je, Serikali iko tayari kwa Wizara hizi mbili; ya Sheria pamoja na Mambo ya Ndani kupiga marufuku na kuchukua hatua dhahiri na za wazi kwa polisi ambao wanaidhalilisha Serikali kwa kuwaumiza raia kwa kipigo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Selasini, naye ana heshima ya kuwa mdogo wangu kwa sababu Lamwai ni kaka yetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna umuhimu wa Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara na Mambo ya Ndani kukaa chini na kuyapitia mambo hayo. Moja ya msisitizo ambao umekuwepo katika Wizara hizi mbili ni kuendelea kuwapa polisi mafunzo ya juu

ya haki za binadamu, lakini pia jinsi ya kutumia mamlaka waliyonayo ya kukamata watu na kuzuia uhalifu kwa namna ambayo inaheshimu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaheshimu Sheria ya Kuanzisha Jeshi la Polisi na inaheshimu sheria zilizowekwa. Kwa hiyo, tutakaa na kulijadili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo.

Na. 88

**Umuhimu wa Kufanyia Maboresho Sheria Zilizopitwa na Wakati**

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO** Aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia baadhi ya sheria zetu hapa nchini kutoendana na mabadiliko na kasi ya maendeleo ya Taifa na kuonekana kuwa zimepitwa na wakati.

Je, ni lini Serikali italeta hoja ya kufanya marekebisho ya kuboresha baadhi ya sheria zilzopitwa na wakati?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia kupitia Wizara mbalimbali imekuwa ikiwasilisha Miswada ya Sheria mbalimbali Bungeni kwa lengo la kuhakikisha Taifa linakuwa na Sheria zinazochochea ukuaji wa uchumi, uboreshaji wa huduma na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali pia kupitia Bunge lako Tukufu imekuwa ikifanya marekebisho ya Sheria Mbalimbali ili ziendane na wakati kupitia Miswada ya Sheria

ya Marekebisho Mbalimbali *(Written Law Miscellaneous Amendments).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuboresha sheria ni endelevu katika kuhakikisha sheria zetu zinaendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii na kwa hiyo, Serikali itaendelea na utaratibu uliopo wa kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinaendana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria za nchi hubadilika kulingana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kisayansi na kiteknolojia. Mabadiliko yanapojitokeza, yanaweza kuathiri sheria zilizopo na hivyo kuonekana kuwa zimepitwa na wakati au kuwa na upungufu hivyo kutokidhi matakwa ya wakati. Hali hii hulazimu kufanyika kwa marekebisho ya sheria husika ili kuendana na wakati kulingana na mabadiliko yaliyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia ukweli huo, mwaka 1980 Serikali iliunda Tume ya Kurekebisha Sheria kama chombo maalum chenye dhamana ya kuzifanyia mapitio Sheria zilizopo ili kukidhi malengo na makusudio ya kutungwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani miaka 37 sasa tangu kuundwa kwa Tume ya Kurekebisha Sheria, imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali za sheria na kupendekeza maboresho pale inapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Maboresho hayo yanaweza kupelekea kufutwa, kutungwa upya au kufanyiwa marekebisho sheria iliyopo ili kuendana na wakati uliopo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ambayo kidogo hayajatosheleza, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hamu na haja ya Waheshimiwa Wabunge wengi, toka nimeingia Bungeni hapa

mwaka 2010, Wabunge wengi wanahitaji sana mabadiliko ya sheria ndogo ndogo ili mambo yaweze kuendana na wakati. Iko Sheria ya Ndoa ambayo inasema lazima mtoto awe na miaka 14 kuweza kuolewa; lakini mimi nimekuwa mwalimu muda mrefu, najua miaka 14 kwa sheria ya leo ilivyo ya elimu msingi, anakuwa bado ni mtoto yupo *form two* na tunasema elimu msingi mtoto atoke chekechea mpaka *form four* na ni elimu ya lazima. Kwa hiyo, unakuta ile sheria imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi nilisema hapa kuhusu Sheria ya *TMAA* ya Madini kwamba Halmashauri kule zinapata ile ruzuku *(service levy)* ambayo unakuta hawajui *source* yake imetoka wapi kwa sababu hawashiriki katika kuangalia pato lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ipo Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978, imepitwa na wakati. Sasa yote hayo nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka 1980 Serikali iliunda Tume kwa ajili ya kuangalia Sheria Mbalimbali na mabadiliko ili iweze kuletwa Bungeni, mpaka leo Tume hiyo ni kama vile imeshindwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, Bunge liwe na Tume yake, Serikali iwe na Tume yake ili na sisi tuonekane kweli tunatunga sheria. Maana toka nimekuja mwaka 2010 hapa sijawahi kuona Mbunge kaleta hoja binafsi hapa na ikapita. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wana hoja binafsi nyingi, lakini wakileta hapa hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iruhusu Bunge liwe na Tume ili sisi wenyewe tuanze kutunga sheria na Serikali iwe na Tume, tuzilete pamoja tuweze kujadili ili tuweze kufanya marekebisho ya sheria kadri mambo yanavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lini Serikali italeta hoja ya kuruhusu Bunge iwe na Tume yake binafsi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la nyongeza la Sheria kuliruhusu Bunge kuwa na Tume yake, liko nje ya mamlaka na uwezo wangu, kwa sababu ni suala la Bunge lenyewe, lakini nitalitolea indhari, haitakuwa muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kazi za Tume hii, Tume hii imefanya kazi nyingi na baadhi yake zimezaa matunda. Kwa mfano, sheria ambazo zimetokana na utafiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania ni pamoja na Sheria ya Upimaji wa Vinasaba wa Binadamu *(The Human DNA Regulation Act No. 8 of 2009);* Sheria ya Mtoto *(The Law of the Child Act No. 21 of* 2009); Sheria ya Makazi na Mahusiano Kazini *(The Employment and Labour Relations Act No. 6 of 2004);* Sheria ya Watu Wenye Ulemavu *(The Disability Act No. 9 of 2010);* hizi ni baadhi ya sheria tu ambazo zimetungwa kutokana na kazi ya Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa iko Sheria ya Ndoa ambayo mchakato wake unaendelea kuhusu moja, umri wa mtoto kuoa na kuolewa. Niseme leo, kuna jambo ambalo haliko sahihi; ukiangalia kuhusu umri wa miaka 14, naomba mwende muisome ile sheria, inaruhusu mtoto wa kike kuolewa na miaka 14 na mtoto wa kiume kuoa na miaka 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kile mwaka 1971 kiliwekwa ili kukidhi mahitaji ya jamii mbili, Wamasai na Mabohora. Sasa ikifika wakati hali imebadilika, umuhimu huo haupo, tutalijadili. Kwa hiyo, umri wa miaka 14, someni sheria, siyo kwa msichana tu, ni kwa hata mtoto wa kiume kuruhusiwa kuoa chini ya miaka 14 kama Mahakama imeruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakubali, mtoto wa kiume kuoa miaka 14 hajafikia umri wa kuoa; na mtoto wa kike kuolewa miaka 14 hajafikia umri wa kuolewa, lakini jambo hili linataka mwafaka wa kijamii kama ambavyo mwaka 1970 ilikuwa ni muhimu kuwaangalia Wamasai na Mabohora ambao ni sehemu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadam mchakato unaendelea, tunaendelea kuzungumza *Inshallah* siku itafika, jambo hilo litapita. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Waitara ajiandae.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Naomba nirudie hapo hapo aliposema Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Waziri, tarehe 08/07/2016 Majaji wawili; Jaji Lila na Jaji Munisi walitoa hukumu *in favour* ya Rebecca Gyumi kuhusiana na suala la vifungu vya 13 na 17 kwenye suala la Sheria ya Ndoa. Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza agizo la Mahakama Kuu ili kufuta vifungu vya 13 na 17? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maamuzi yale Serikali imekata rufaa. Kwa mujibu wa sheria ya *Basic Rights and Duties Enforcement Act*, kama ni kesi ya kikatiba, unapowasilisha *notice* ya kukata rufaa inasimamisha utekelezaji moja kwa moja wa maamuzi ya Mahakama. Kesi ile haikuwa na mambo haya ya ndoa tu, kuna mambo mengi yalijitokeza na hayo yote lazima tupate mwongozo wa Mahakama ya Rufaa.

Kwa hiyo, naomba kuwasihi Waheshimiwa Wabunge wawe na subira hadi hapo Mahakama itakapotoa maamuzi.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh, kaa chini kwanza. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ambaye ni mwalimu wangu

nampongeza sana kwa majibu mazuri. Kama hawatamharibu, ataenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba yeye mwenyewe kama mzazi na kama mwalimu umri wa mtoto wa kiume kuoa miaka 14 hakubaliani nao na umri wa mtoto wa kike kuolewa hakubaliani nao. Sasa Serikali kwa mujibu wa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, maana yake anataka kuniambia Serikali inataka watoto wadogo waendelee kuolewa. Kwa hiyo, watoto wa kike wasipate haki yao ya kucheza na kupata elimu na kuwa viongozi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hukumu ilikuwa ni miezi sita na imeshapita na rufaa haijakatwa. Sasa naomba niulize swali, kwa nini Mheshimiwa Waziri sasa asilete Muswada Bungeni ili amri hiyo ya Mahakama ya Rufaa itekelezwe ili kuwapa haki watoto wadogo wa kike na kiume wapate haki ya kusoma na kuwa viongozi wa Taifa hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wote ambao wamesoma *Legal Anthropology* wataelewa kwamba mambo ya mila, desturi, imani ya dini na itikadi hayataki haraka, yanataka muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yoyote na bahati mbaya, aah, kwenye Kiswahili hakuna bahati mbaya. Kuna umuhimu sasa wa vyuo vyetu kufundisha *Legal Anthropology*. Huwezi kubadili mila, desturi, imani ya dini na itikadi kwa kutumia sheria peke yake tu, utakuwa unajidanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka katika utamaduni ambao umekuwa na mila siyo nzuri ya ukeketaji. Sheria ipo, imezuia, lakini kwa sababu bado ni suala la imani na itikadi kwa watu, leo wamelihamishia kwa watoto

wachanga. Sasa nazungumza kama Profesa wa Sheria, ni hatari. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waitara Chacha, rafiki yangu mkubwa, anajua kabisa kuna mila na desturi za anakotoka leo, mimi siafikiani nazo, lakini zinahitaji elimu, zinahitaji uelewa. Ni vigumu sana mtu anayetoka nje ya eneo hilo kuelewa kwamba mapenzi ni pamoja na kipigo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kaa chini.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namsihi Mheshimiwa Waitara, tukae nje, tukutane. Namsihi na nimesema hivi kwa masihara haya kwa sababu ni mtu tumeshibana, hawezi kunichukulia tofauti. Tutalijadili, ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutalijadili, ahsante *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

Na. 89

**Nishati Mbadala kwa Ajili ya Kukausha Tumbaku**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** Aliuliza:-

Tumbaku ni moja ya zao la biashara ambalo ni muhimu sana kwa Mkoa wa Tabora, lakini ukaushaji wake umekuwa mgumu sana kwa wakulima kutokana na kulazimika kutafuta kuni kwa ajili ya kukaushia tumbaku

jambo ambalo linaathiri afya za wakulima hao pamoja na mazingira.

Je, ni lini Serikali itawasaidia wakulima wa tumbaku mkoani Tabora kupata nishati mbadala kwa ajili ya kukaushia tumbaku?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *order please!* Tunaomba utulivu ndani ya Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumbaku ni zao muhimu sana kwa Mkoa wa Tabora na Taifa kwa ujumla, kwani huwapatia wakulima kipato kikubwa na huchangia zaidi ya shilingi bilioni 14 kwa mwaka Mkoani Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya tafiti mbalimbali ili kupata nishati mbadala kwa ajili ya kukausha tumbaku badala ya kuni. Utafiti wa awali uliofanyika ni ule wa kutumia makaa ya mawe na umeme uliofanyika mkoani Iringa ambapo ilibainika kuwa na gharama kubwa kwa mkulima.

Aidha, kuanzia msimu wa kilimo wa 2015/2016, utafiti wa matumizi ya nyasi maalum umeanza kufanyika Mkoani Mbeya na Songwe katika wilaya zinazolima tumbaku. Utafiti huo umeanza kuonesha mafanikio na unatarajiwa kuwasaidia wakulima kwa kupunguza gharama na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasisitiza kuwa wakulima wa tumbaku nchini kutunza mazingira kwa kupanda miti ya kutosha na inayoendana na kilimo chao kwa mujibu wa sheria na kuacha kukata magogo na kutumia magogo kukaushia tumbaku badala yake watumie matawi ya miti. Pamoja na wito huo, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku imeagiza wakulima wote wa tumbaku kwa msimu 2017/2018 watumie majiko sanifu yanayotumia kuni kidogo na yenye ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majiko haya sanifu yanatumika katika nchi za Malawi na Zimbabwe na yanapunguza sana uharibifu wa mazingira na hayana athari kwa wakulima sababu moshi unapungua sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri ambayo hayaridhishi vizuri, napenda nimuulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kwenda kutoa elimu kwa wakulima hawa ili badala ya kutumia hayo magogo ambayo wanasema, basi waweze kutumia hayo matawi ili kuweza kukausha tumbaku zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuhakikisha wakulima hawa hawatumii tena kuni kwa sababu wanakata sana miti na badala yake walete hiyo nishati mbadala kwa haraka ili wakulima hawa waweze kuacha kukata miti? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, Serikali imeendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kutumia majiko sanifu na vilevile athari za mazingira zinazotokana na ukataji wa miti. Kwa hiyo, ni kitu ambacho kimekuwa kikiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namsihi tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine wanaotoka maeneo yanayolima tumbaku, waendelee kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira katika kilimo cha tumbaku kwa sababu tumbaku yetu inaweza ikawa na bei nzuri kwenye soko kama tutakuwa na tabia ambazo zinahifadhi mazingira. Inaitwa *compliance*, ni moja kati ya vigezo vinavyoangalia ubora wa tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kwa sasa Serikali inahimiza matumizi ya majiko sanifu na kuanzia msimu huu unaokuja, haitaruhusiwa tena kutumia majiko ya aina nyingine; itakuwa ni lazima kila mkulima atumie majiko sanifu wakati wa kukausha tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na nishati mbadala, kama nilivyosema, tayari tafiti zimeshafanyika kuangalia kama umeme na makaa ya mawe yanaweza yakawa nishati mbadala, lakini kwa sasa ilionekana kwamba nishati hizo zinakuwa na gharama kubwa kwa mkulima. Kwa hiyo, njia ambayo inaoneka ni ya gharama nafuu lakini vilevile ni rafiki kwa mazingira, ni kutumia majiko sanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine waisaidie Serikali kuendelea kuhimiza wakulima wetu watumie njia hiyo wakati wa kukausha tumbaku.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Ishengoma.

Na. 90

**Mfumo Mpya wa Kutoa Ruzuku ya Pembejeo**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** Aliuliza:-

Serikali ina mpango mzuri wa kuanzisha mfumo mpya wa kutoa ruzuku za pembejeo kwa wakulima ambao utawanufaisha zaidi.

Je, ni lini mfumo huo mpya utaanza kutumika ili wakulima waweze kupata pembejeo kwa wakati wote?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa ajili ya mahindi, mpunga na pamba kwa kutumia mfumo wa vocha kuanzia mwaka 2008/2009 hadi mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa vocha umetoa mafanikio mazuri ambayo ni pamoja na kueneza elimu ya matumizi bora ya pembejeo za kilimo kwa wakulima, kusogeza huduma ya upatikanaji wa pembejeo vijijijini na kuongezeka kwa uzalishaji wa mahindi, mpunga na hivyo kuongeza usalama wa chakula katika ngazi ya kaya na Taifa kwa ujumla. Aidha, kumekuwa na changamoto mbalimbali za kiutendaji zilizojitokeza katika kutekeleza mfumo huu hususan katika ngazi ya wilaya na vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika mfumo wa vocha, mwaka 2016/2017 Serikali imetoa ruzuku ya pembejeo kwa kutumia Kampuni yake ya *TFC* kusambaza mbolea hadi ngazi ya vijiji. Mpaka sasa *TFC* imesambaza tani 25,100 za mbolea ambazo ni sawa na asilimia 85 ya lengo la mbolea ya ruzuku. Pia makampuni ya mbegu yaliyoingia mkataba na Serikali wa kusambaza mbegu za ruzuku wamesambaza tani 429.4

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuandaa utaratibu wa kupunguza au kuondoa tozo mbalimbali za pembejeo zinazochangia ongezeko kubwa la bei ya mbolea. Serikali inatarajia kuanza kutumia mfumo wa manunuzi wa pamoja *(bulk procurement).* Utaratibu huu utawezesha kupunguza bei ya mbolea na hivyo kuweza kuwafikia

wakulima wote nchini kwa wakati na kwa bei iliyo nafuu ikilinganishwa na bei za sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu wa *bulk procurement* utaanza kutumika msimu ujao wa kilimo kwa kuanzia; na majaribio ya awali yataelekezwa kwenye mbolea za *DAP* na *UREA*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri na Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya ngongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 75 ya wakulima hapa Tanzania wakiwemo wakulima wa Mkoa wa Morogoro wanategemea kilimo kwenye uchumi wao. Serikali ina mkakati mzuri wa kupunguza bei kwenye mbolea kusudi iweze kuwa nafuu kwa wakulima. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha viwanda vya mbolea hapa nchini sambamba na Kiwanda cha Minjingu na Kiwanda cha Mtwara kinachotegea kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mbolea hasa ya *DAP* pamoja na *UREA* ni mbolea ambayo zinatumika sana kwenye kilimo chetu, *DAP* ikiwa ni mbolea ya kupandia na *UREA* ikiwa ni mbolea ya kukuzia. Hapa nchini tuna mbolea ya Minjingu ambayo inazalishwa Manyara.

Je, mbona haijawekwa kwenye mkakati huu kusudi wananchi waweze kupata hamasa ya kutumia mbolea ya Minjingu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ni mdogo na leo tuna Taarifa za Kamati nne kabla ya saa saba zinatoa taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la Serikali kuanzisha viwanda, ni kweli kabisa kwamba Serikali ya Awamu ya Tano moja kati ya mikakati yake ya kuendeleza uchumi ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na viwanda nchini.

Kwa hiyo, Serikali imekuwa ikihimiza na kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi na wadau wengine waweze kuanzisha viwanda nchini. Kwa sasa Serikali iko katika mikakati ya kushirikiana na sekta binafsi kuanzisha kiwanda cha mbolea Mkoani Lindi kwa kutumia gesi; na utaratibu huo ukikamilika, tunaamini kwamba mahitaji mengi ya mbolea yatakuwa yamepata suluhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna kiwanda cha mbolea kinajengwa Kibaha, kwa hiyo, tunaamini kwamba kadiri miaka inavyokwenda, tutakuwa tunazalisha mbolea zetu humu nchini, kuliko kuagiza ambayo inatusababishia kuwa na gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba katika utaratibu wa *bulk procument* (uagizaji wa mkupuo) tunaanza na mbolea za *DAP* na *UREA*, lakini baadaye tutaingia kwenye mbolea nyingine kama *NPK* na mbolea nyingine ambazo zinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwa nini hatujaweka mbolea ya Minjingu katika utaratibu huu? Ukweli wa mambo ni kwamba tunapozungumzia kuhusu uagizwaji wa mkupuo, tunazungumzia kuhusu mbolea kutoka nje.

Hata hivyo, bado kuna fursa ya kuendelea kuhimiza kiwanda cha Minjingu kiongeze uzalishaji, kwa sababu kwa sasa uwezo wao kwa mwaka ni tani 50,000 wakati mahitaji yetu ya mbolea ya aina hiyo kwa mwaka ni zaidi ya tani nusu milioni. Kwa hiyo, vilevile kuna suala la uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali iko tayari kushirikiana na Minjingu waongeze uzalishaji ili mbolea yao iweze kutumika kwa wingi zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Chuachua, Mbunge wa Masasi. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Nape.

Na. 91

**Malalamiko ya Wakulima wa Korosho Dhidi ya Mfumo wa Uuzaji Korosho**

**MHE. NAPE M. NNAUYE (K.n.y. MHE. RASHID M. CHUACHUA)** Aliuliza:-

Mfumo mzima wa ununuzi wa zao la korosho kuanzia kwenye ngazi ya Vyama vya Msingi umegubikwa na dhuluma na ukandamizaji mkubwa wa haki za mkulima kwa kila hatua. Hali hiyo imesababisha malalamiko yasiyokwisha ya wakulima wa korosho kila mwaka. Malalamiko ya wakulima ni uwepo wa makato yanayomuumiza mkulima, kutokuwepo kwa uwazi katika kumpata mshindi wa *tender,* kujitoa kiholela kwa makampuni yanayosababisha kushuka kwa bei ya korosho, kutolipwa kwa bei halali inayouzwa mnadani kwa Vyama vya Msingi, rushwa katika kila ngazi, pamoja na njama kati ya benki na kampuni zinazonunua korosho.

(a) Je, ni lini Serikali itaondoa na kushughulikia malalamiko ya wakulima wa korosho?

(b) Je, ni lini Serikali itadhibiti usambazaji wa pembejeo za ruzuku kwa watu ambao sio wakulima wa korosho?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUZI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Chuachua, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshashughulikia malalamiko ya wakulima wa korosho kwa kuondoa makato yasiyokuwa muhimu kama vile kufutwa kwa ushuru wa shilingi 20 kwa kilo kwa ajili ya Chama Kikuu cha Ushirika; shilingi 50 za usafirishaji wa korosho; shilingi 10 kwa kilo kwa ajili ya mtunza ghala na shilingi 10 kwa kilo kwa ajili ya kikosi kazi cha masoko. Aidha, tasnia ya korosho ina utaratibu maalum wa kupanga bei dira kwa kutumia vigezo vinavyokubaliwa kwa wadau wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu manunuzi ya pembejeo za korosho hufanywa kwa pamoja na vyombo rasmi ndani ya tasnia, awali ilikuwa ikisimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Korosho na sasa Bodi ya Korosho Tanzania. Kuhusu changamoto za namna ya kufikisha pembejeo hizo kwa wakulima wa korosho, hatua zimechukuliwa kwa kushirikisha Vyama vya Ushirika ili kudhibiti mianya ya pembejeo kwenda kwa wasio walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usambazaji wa pembejeo za korosho ambazo ni *sulphur* ya unga na dawa za wadudu, Serikali imeweka mfumo wa usambazaji wa pembejeo wenye lengo la kuhakikisha kwamba pembejeo hizo zinawafikia walengwa pekee. Utaratibu huo unazingatia kutambua wakulima wenye uhitaji wa pembejeo na hununuliwa kwa kutumia utaratibu wa ununuzi wa pamoja *(bulk purchase system)* na kusambazwa kwa wakulima kwa kutumia wakala walioteuliwa na kuthibitishwa na Halmashauri husika ambazo huwa zimeandaa orodha ya wanufaika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pamoja na kazi nzuri ambayo imeanza kufanywa ya kusaidia kuongezeka kwa bei ya zao la korosho kwa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani ambao ni wakulima wazuri wa korosho, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuweka kiwango cha elimu kwa viongozi wanaoongoza Vyama vya Msingi, kwa sababu ni moja ya changamoto kubwa sana ambayo imesababisha migogoro mikubwa kwenye Vyama vya Msingi na inasababisha hasara kubwa kwa wakulima wakorosho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, moja ya changamoto kubwa kwenye biashara ya korosho ni utaratibu wa wanunuzi wa korosho kutengeneza *cartel,* kutengeneza muungano wa pamoja ambao unakwenda kuathiri bei ya mnada kwenye ununuzi wa korosho. Sasa Serikali inachukua hatua gani kukomesha utaratibu huu? Kwa sababu kwa kweli, kwa namna moja ama nyingine umeathiri sana wakulima wa zao la korosho na bei inaendelea kushuka kila kunapokucha na hata sasa ambapo bei imekwenda vizuri, msimu ujao mpango huu wa *cartel* ukiachiwa ukaendelea, wakulima wetu wataendelea kupata umaskini na nchi yetu haitasonga mbele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na Mheshimiwa Nape kwamba zao la korosho ni zao la muhimu sana kwa mikoa inayolima hususan Mikoa ya Lindi na Mtwara. Katika msimu uliopita mikoa sita inayolima korosho, kwa uchache waliweza kuingiza shilingi bilioni 700 katika kipindi kifupi kwa ajili ya kuuza korosho. Yote imetokana na jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano ya kuendeleza zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kiwango cha elimu kwa Watumishi wa Vyama vya Ushirika, ni kitu kikubwa. Kimsingi tunategemea kurekebisha sheria ili kuweza kuongeza kiwango hicho, lakini tunasisitiza vilevile kwamba elimu pekee siyo kigezo, tunahitaji watu waadilifu, lakini zaidi watu ambao wanafahamu taratibu za tasnia ya korosho

inavyoendeshwa. Kwa hiyo, tutaleta marekebisho, lakini vilevile tutaangalia vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na namna ya kudhibiti *cartel,* kwa kutambua kwamba huko nyuma wanunuzi walikuwa wanatumia utaratibu huo wa *cartel* kuharibu bei ya korosho, kwa sasa tunaendesha minada kwa uwazi zaidi ili isitokee watu wakatengeneza utaratibu na watumishi wa Ushirika, vilevile na wa Vyama vya Ushirika wasio waaminifu ili kujitengenezea utaratibu ambao wanunuzi ni hao hao na hivyo kuweza kuharibu bei.

Kwa hiyo, kwa sasa kuna utaratibu wa kuuza korosho kwa uwazi zaidi, lakini vilevile pale mnunuzi atakaposhinda zabuni ya kununua korosho inatakiwa aweke dhamana ili baadaye asije akaacha kununua ili baei ije ishuke. Kwa hiyo, utaratibu huo unashughulikiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, muda wetu ni mdogo. Swali Namba 92, limeleta hisia za Wabunge wengi kutaka kuuliza maswali ya nyongeza, kwa hiyo, kwa upendeleo maalum na uzito wa swali, baada ya mwenye swali nitatoa nafasi mbili huku na mbili huku.

Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea.

Na. 92

**Ujenzi wa Barabara ya Nanganga – Nachingwea – Masasi**

**MHE. HASSAN E. MASALA** Aliuliza:-

Barabara ya Nanganga – Nachingwea – Masasi imeshafanyiwa upembuzi yakinifu toka mwaka wa 2015/2016.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MWASILIANO** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS),* ilikamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Masasi – Nachingwea hadi Nanganga. Aidha, katika mwaka wa 2017/2018 Wizara imeomba kutengewa shilingi bilioni 3.515 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini sambamba na hayo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya Masasi – Nachingwea – Nanganga inahudumia Wilaya tatu, hivyo umuhimu wake katika mkoa na Taifa unafahamika sana kiuchumi. Majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, naomba niyapokee kwa sababu kwanza wameonesha utashi wa kutenga shilingi bilioni tatu, lakini nilikuwa nataka nijue, kwa urefu wa barabara ile ambao tayari umeshafanyiwa upembuzi yakinifu kilometa 97, kwa kutenga shilingi bilioni tatu ambazo haziwezi kujenga hata kilometa zisizozidi 10, ni nini nia ya Wizara juu ya ujenzi wa barabara hii ambayo imekuwa kero kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi na Wilaya ya Nachingwea kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, naomba kujua pia kupitia Naibu Waziri, upembuzi yakinifu ambao ulifanyika

toka mwaka 2016 uwe umekamilika, umehusisha nyumba za wakazi ambao wamesimamisha shughuli zao. Nilikuwa nataka nijue, katika kiasi hiki cha fedha shilingi bilioni tatu, kinahusisha pia fidia kwa wale wananchi ambao wanapaswa kulipwa ili waweze kupisha ujenzi wa hii barabara? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina nia ya dhati ya kutaka kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami na ndiyo maana imeshatekeleza hatua ya kwanza muhimu sana ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa nini tumetenga fedha kidogo; kwanza hatujatenga; tunaomba tutengewe fedha kidogo siyo kwa sababu ya kutokuwa na dhamira ya dhati, bali ni kwa sababu ya fedha ambazo Wizara nzima inatarajia kuomba kutengewa imepungua sana ukilinganisha na mwaka uliopita. Kwa hiyo, tutagawana haka kasungura kadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaanza mwaka huo ujao na miaka inayofuata tutaendelea kukamilisha na hatimaye tutakamilisha hiyo barabara kuijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, naomba nimhakikishie kwamba tunapoanza kujenga na tunapotenga fedha kwa ajili ya ujenzi, inahusisha vilevile na fidia ya maeneo yale ambayo tutajenga katika mwaka huo wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa Keissy na Mheshimiwa Mwakajoka wajiandae. Tunaanza na Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wananchi wa Jimbo la Geita Vijijini miaka 56 ya uhuru hawajawahi kuona lami. Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni aliwaahidi lami kwenye barabara ya kutoka

Geita – Bugurula – Nzela mpaka Nkome. Sasa namUuliza Mheshimiwa Waziri, je, ni lini Serikali imejipanga kuanza kufanya upembuzi yakinifu na kuanza kutengeneza kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. Anataka kujua ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kawaida ya kutaja terehe kamili ya lini barabara itaanza kujengwa katika Wizara yetu kwa sababu taratibu zake za kufikia hadi ujenzi ni nyingi na zinahusisha taasisi mbalimbali ambazo huwezi ukazipangia muda wa kukamilisha hatua yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ni ahadi ya Serikali ya Awamu ya Tano kwamba suala hili tutalitekeleza kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi wakati wa kampeni katika kipindi hiki cha miaka mitano.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Barabara ya Nangurukulu – Liwale, Nachingwea – Liwale, ni barabara ambazo zimo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini mara nyingi nimekuwa nikiuliza barabara hizi, naambiwa itajengwa, itajengwa; sasa wana-Liwale wanataka kusikia ni lini barabara hizi zitaingia kwenye upembuzi yakinifu na hatimaye kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua tunayoifanya sasa ni kutafuta fedha. Nimhakikishie Mheshimiwa Kuchauka, mara tutakapopata fedha, suala la upembuzi yakinifu na usanifu

wa kina wa barabara hii ambayo imeahidiwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tutaitekeleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Cathy.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro, Mkoani Arusha, wamekuwa wakipata shida sana ya usafiri kutokana na ubovu wa barabara.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ambayo ilikuwa kwenye bajeti ya 2016/2017 ya kujenga barabara ya lami inayoanzia Loliondo hadi Mto wa Mbu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumhakikishia Mheshimiwa Magige na Mheshimiwa Olenasha kwamba mkandarasi tunatarajia kumpata muda siyo mrefu kwa sababu taratibu za kumpata mkandarasi zipo katika hatua za mwisho na mara tutakapompata mkandarasi barabara hii itaanza kujengwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya wananchi wa Mji wa Tunduma, napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wananchi wa Mji wa Tunduma wamekubali ushauri wa viongozi wao na kuondoa nyumba katika maeneo mbalimbali na kuhakisha kwamba barabara 42 zimepatikana kwenye Mji wa Tunduma, Serikali ina mpango gani wa kuwaunga mkono ili kuhakikisha kwamba barabara zile zinakuwa kwa kiwango cha lami kwenye Mji wa Tunduma, ukizingatia mji unaendelea kukua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu ndiyo hayo hayo, mpe. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukulie kwamba taarifa hii ni ombi na kule wakati tunapita kwenye kampeni tulitoa ahadi zinazofanana na hayo ambayo ameyasema. Nimhakikishie tu kwamba ombi hili tutalipeleka katika timu ya wataalam ambayo ndiyo huwa inaandaa vipaumbele kulingana na ahadi za viongozi wakuu, ahadi za Wabunge, na kadhalika, waweze kuliangalia ili tuweze kulitekeleza kama ambavyo tuliahidi wakati wa uchaguzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, barabara hizi zina michakato mingi sana, ni tofauti kabisa na mapenzi pamoja na kipigo. Tunaendelea na Wizara ya Afya na Maendeleo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Hawa Mchafu kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

Na. 93

**Ubia wa Sekta Binafsi Kwenye Ununuzi wa Vifaa Tiba**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE (K.n.y. MHE. HAWA M. CHAKOMA)** Aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali haitumii mfumo wa Ubia na Sekta Binafsi *(PPP)* kwenye mipango yake ya ununuzi wa vifaa tiba vya bei kubwa kama *MRI, CT-Scan* na *X-Ray?*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kukua kwa kasi ya sayansi na teknolojia ya uchunguzi wa magonjwa, Wizara inakubaliana kabisa na wazo la Mheshimiwa Mbunge juu ya kuangalia namna nzuri ya kushirikiana na Sekta Binafsi *(PPP)* katika utoaji wa huduma za uchunguzi wa magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeanza hatua za awali za uainishaji wa gharama, uandaaji wa mfumo mbadala *(Option Development)* na upembuzi wa kina wa aina ya ubia ambapo Wizara kwa kuanzia inafikiria ushirikiano kwa kupitia ukodishaji wa vifaa *(lease agreement)* ambapo Serikali itakodisha mashine hizo ambazo zitakuwa za mbia na Serikali haitahusika na ununuzi, ufungaji na matengenezo kinga ya mashine hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mfumo huu, Wizara itakuwa na jukumu la kusimamia utoaji wa huduma na itapata gawio lake kutokana na makusanyo yatokanayo na uchangiaji wa huduma kulingana na mkataba. Ni imani ya Wizara kuwa kutumia mfumo wa Ubia na Sekta Binafsi *(PPP)* huduma za uchunguzi wa magonjwa zitaimarika na kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Naipongeza Serikali kwa mtazamo huo mpya na ninaamini sasa huo ndiyo mtazamko chanya ambao tunapaswa kwenda nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa hivi katika ununuzi wa vifaa tiba tumekuwa tukivinunua bila kuwa na mpango wa matengenezo kwa maana ya *Plan Preventive Maintenance,* kuwekwa katika mpango wa manunuzi.

Je, sasa Serikali mtakuwa tayari kuhakikisha wakati mna-*negotiate* kununua zile mashine mnaweka mpango wa

*Preventive Maintenance* kwa sababu sasa hivi gharama zinazotumika kutengeneza vifaa tiba ni za juu sana?

Swali la pili, kwa kuwa, gharama za utengenezaji wa vifaa hivi ni kubwa sana, kwa maana ya *Preventive Maintenance* na pale vinapokuwa vinaharibika kwa hali ya kawaida:-

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kuingiza gharama za *PPM* ama *Plan Preventive Maintenance* katika gharama za vitendanishi, badala ya kutenga peke yake ambazo ni mabilioni ya hela ambapo mara nyingi Serikali inaishia kutozilipa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mhesimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakubaliana na wazo lake kwamba gharama za *Planned Preventive Maintenance* ni vema zikawa sehemu ya mkataba mkuu wa ununuzi wa vifaa tiba. Hivyo, ndiyo maana mikataba yote mipya ambayo itafungwa na Serikali na *Private Contractors* kwa sasa itahuisha uwepo wa *section* maalum ambayo ina *Planned Preventive Maintenance* katika *costs* zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili pia tunakubaliana naye kwamba ni lazima tuziingize gharama za *PPM* kwenye manunuzi ya vitendanishi. Pia tunakubaliana naye kwamba ni wazo zuri, naomba nilichukue na nitalifanyia kazi ndani ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba radhi sana, muda wetu umekwisha na tumeshatumia zaidi ya dakika 20 za mijadala inayokuja. Tunampa sasa Mheshimiwa Umbulla.

Na. 94

**Kukabiliana na Ukeketaji wa Wanawake Mkoa wa Manyara**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** Aliuliza:-

Kulingana na takwimu za mwaka 2010 Mkoa wa Manyara unaongoza kwa mila potofu ya ukeketaji wa wanawake kwa asilimia 71 hapa nchini hali inayotisha na kuhatarisha maisha ya wanawake.

(a) Je, Serikali katika kufanya utafiti imebaini ni Wilaya zipi na vijiji vipi vinaongoza?

(b) Je, hali hii na mila hii potofu imesababisha athari na vifo kiasi gani mkoani Manyara?

(c) Je, Serikali ina mikakati gani ya dharura ya kukabiliana na mila hii potofu ili kuondoa kabisa athari za ukeketaji?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WAZEE NA WATOTO** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, lenye vipengele (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti uliofanya na Serikali katika Mkoa wa Manyara, imebainika kuwa ukeketaji upo vijijini kwa asilimia 100. Wilaya karibu zote zinajihusisha na vitendo hivi hasa Wilaya ya Hanang. Makabila yanayofanya ukeketaji katika wilaya hiyo ni Wairak, Wabarbaig na Wanyaturu hasa katika maeneo ya Kata za Balanglalu na Basutu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, athari zinazotokana mila hizi potovu ni kubwa sana kwa wanawake husus an wakati

wa kujifungua. Kwani huweza kusababisha ulemavu wa kudumu; vifo kutokana na kutokwana damu nyingi; maumivu makali kupatwa na ugonjwa wa fistula na wakati mwingine kupata madhara ya kisaikolojia. Ni vigumu kutambua vifo vinavyotokana na ukeketaji kwani hufanyika kwa siri katika jamii hiyo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetunga sheria mbalimbali ili kukabiliana na tatizo hili. Hata hivyo, tunaamini kuwa sheria peke yake bila elimu kwa Umma haziwezi kumaliza tatizo hili. Ndiyo maana tunawawatumia Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii ili kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi kuondokana na mila za tamaduni hizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Umbulla.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa juhudi yake kubwa, amekuja mara nyingi katika Mkoa wetu wa Manyara kutatua kero mbalimbali za wananchi hasa katika sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kutoa masikitiko yangu kwamba sijaridhika na majibu ya Serikali katika swali langu hili la namba 94.

Kama tatizo liko kwa asilimia 100 katika mkoa, ina maana kwamba lazima kwa utafiti uliofanywa na Serikali kuna vigezo vilivyoonyesha kwamba lazima kuna takwimu ambazo zinaonyesha asilimia 100 imetokana na vitu gani, hasa vifo na adhari mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu (b) ya swali langu nilitaka kupata idadi ya vifo, siyo sababu zinazosababishwa na ukeketaji kwa sababu hizo tunazijua. Nilitaka kupata takwimu ni vifo kiasi gani na maeneo gani ili sisi viongozi wa Mkoa wa Manyara tuweze kupambana, tuongeze juhudi ya Serikali kapambana na janga hili ambalo liko kwa asilimia 100 katika mkoa wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, nini kauli ya Serikali kufuatana na hali hii mbaya katika mkoa wetu wa Manyara?

Swali la pili, kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema tunatumia Maafisa Maendeleo ya Jamii na Afisa Ustawi wa Jamii ili kutoa elimu kupambana na janga hili, lakini Maafisa Maendeleo ya Jamii na Afisa Ustawi wa Jamii wako siku zote na hali imefikia asilimia 100.

**MWENYEKETI:** Mheshimiwa Umbulla, jielekeze kwenye swali.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Sasa je, Serikali ina mikakati gani ya ziada ili kupambana na tatizo hili *specifically* kwa Mkoa wa Manyara ili na sisi Manyara tubaki salama?

**MWENYEKETI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, kwa maswali yake ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yetu ni kwamba kwanza, asilimia 100 siyo kwamba ni watu wote. Ni kwamba tatizo hili lipo zaidi Vijijini kuliko maeneo ya Mijini, lakini kiwango hasa cha kitakwimu kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na *National Bureau of Statistics* ni kwamba katika wanawake 100 wa Mkoa wa Manyara, basi wanawake 71 wamekeketwa. Idadi ya vifo hatukuweza kupata takwimu za idadi yake kwa uhakikika kwa sababu vitendo vya ukeketaji vinafanyika gizani, vinafanyika kwa siri na utamaduni umebadilika, badala ya kuwakeketa kipindi kile cha usichana mdogo, sasa hivi wanakeketa watoto wachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mbinu mpya ambayo wamegundua, wanawakeketa watoto wakati wakifanya tohara kwa watoto wa kiume. Kwa hiyo,

wanawachanganya, inakuwa kama ni sherehe ya tohara inayokubalika kisheria kwa watoto wa kiume wanawaunganisha na watoto kike. Kwa hiyo, kuna mbinu nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kujibu maswali yake, najibu tu yote kwa pamoja mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi akizungumza hapa, aligusia *Legal Anthropology.* Sisi kwenye tiba tunazungumzia *Medical Anthropology,* sasa tunapo-*approach* tatizo pamoja na kuwa na sheria, pamoja na kuwa na mambo mengine, hatuwezi kujikita kwenye sheria peke yake, ni lazima tuitazame jamii nzima *holistically,* lazima tuitazame jamii nzima kwa ujumla wake. Tuzitazame mila na desturi za jamii husika, tutazame namna ya kupenya kwenye hiyo jamii ili kuufikisha ujumbe wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa msingi huo, tumekuja na mkakati mpya sasa wa kutumia mbinu inaitwa kwamba *alternative right of passage.* Kwa sababu kwenye mila za kukeketa, imebainika kwamba ni lazima zifanywe na jamii zinazofanya mambo hayo kwa sababu wanataka kuwa-*graduate* watoto wa kike kutoka kwenye *status* ya usichana na kwenda kwenye *status* ya uanamke. Sasa kama wasipokeketwa, wanaume wanakataa kuwaoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili ku-*address* hili tatizo, huwezi kutumia sheria peke yake, ni lazima uelewe sababu hizo na sasa mbinu yetu mpya ya *ARP (Altenative Right of Passage)* tunaitumia kwa maana ya kuyafikia viongozi wa kimila na watu mashuhuri kwa jamii husika ili kufikisha ujumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo namshauri Mheshimiwa Martha Umbulla na viongozi wote wa kimila na Kiserikali katika Mkoa wa Manyara kuanza kuhamasisha jamii yao kuachana na mila hizi kwa hiari na kwa kuwaelewesha kuliko kutumia zaidi nguvu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu yamekwisha. Sasa ni muda wa wageni ndani ya Bunge.

Wapo wageni wawili wa Naibu Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, wanatokea jijini Dar es Salaam ambao ni Dkt. Sebastian Ndege na Ndugu James Mwakibinga. *(Makofi)*

Wapo viongozi wawili kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ambao ni Profesa Faustin Kamuzora, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira; Ndugu Mhandisi Ngozi Mwihava, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira; pia wameambatana na Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Maafisa mbalimbali waliopo chini ya Ofisi ya Makamu ya Rais, Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

Wengine ni wageni sita wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa January Makamba ambao ni Profesa Yunus Mgaya, Makamu Mwenyekiti Mfuko wa Taifa wa Mazingira; Mzee Job Lusinde, aliyekuwa Waziri wa Serikali ya Tanganyika na alishiriki kwenye mjadala na aliyependekeza aina ya Muungano wetu, karibu Mzee Lusinde. *(Makofi)*

Wengine ni Watanzania wanne walioshiriki kuchanganya udongo wakati wa tukio la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 24 Aprili, 1964 ambao ni Ndugu Sifaeli Shuma, Ndugu Elisaeli Mrema, Ndugu Hassan Mzee na Ndugu Khadija Rashid. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 19 wa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Luhaga Mpina ambao ni familia yake na wageni kutoka Jimboni kwake Kisesa, Mkoani Simiyu wakiongozwa na Ndugu Rudia Mpina, mke wake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge. Katibu. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumesema leo tuna taarifa ya Kamati nne.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana.

**MWENYEKITI:** Sasa mimi nasema na wewe unasema! Vipi? Umesahau mapenzi na kipigo? *(Kicheko/Makofi)*

Haya natoa miongozo miwili tu; mmoja huku na mmoja huku.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saed Kubenea na Mheshimiwa Kakunda. *(Makof/Kicheko)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa kanuni ya 68(7). Nilivyoingia hapa Bungeni tangu asubuhi nimepokea maswali na pole nyingi sana kutoka kwa Wabunge kutokana na tukio la kufukiwa kwenye mgodi wananchi wa Tanzania wanaochimba kule *Kitunda Gold Mine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi kamili ya wachimbaji katika Mgodi wa Kitunda haijulikani kwa sababu hakuna usajili wowote wa wanaoingia na kutoka au kutoka kwenye mgodi huo. Serikali inakadiria kwamba kuna wachimbaji kati ya 5,000 hadi 7,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usiku wa kuamkia tarehe 20 Aprili, 2017 machimbo haya yalipata ajali na walifukiwa wananchi ambao mpaka jana walifukuliwa maiti sita na

inasemekana mmoja kwa taarifa rasmi za Serikali anaitwa Joshua Charles hajulikani alipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa eneo hilo na wachimbaji wanaamini kwamba kuna wachimbaji zaidi bado wako chini ya machimbo hayo. Sasa kwa sababu ilitumika *excavator* ya ujenzi barabara badala ya vifaa maalum ambavyo huwa vinatumika kwenye migodi mikubwa kufukua ardhini kuokoa pamoja na kufukua maiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nitoe hoja Bunge hili lijadili hoja yangu kama kanuni zinavyotuongoza ili maazimio tutakayofikia yatoe mwongozo kwa Serikali kuweka utaratibu wa usimamizi, usajili, uratibu na msaada wa haraka matatizo kama haya yanavyojitokeza ili kuondoa kabisa manung'uniko ya wananchi na hata Wabunge yanapotokea majanga kama hili ya Kitunda kwenye migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) na ambayo naomba nisiisome kwa ruhusa yako ili kuokoa muda kama unavyosema muda hautoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Angellah Kairuki akijibu swali Na. 85 leo hii kwenye Bunge lako Tukufu alisema kwamba watumishi wa umma wanachishwa kazi kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa taratibu; lakini Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Simbachawene aliitetea akasema kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wana mamlaka ya kusimamisha

watu kutuhumu watu hadharani na kwamba baadaye vyombo vingine vya Utumishi ndiyo viweze kufanya kazi yake kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mwongozo wako kuhusu kauli ya Serikali kwenye jambo hili ni ipi? Ni ile ya Waziri wa Utumishi au ile ya Waziri wa TAMISEMI?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Subiri kwanza Mheshimiwa. Subiri! Umemaliza?

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea miongozo miwili, moja ya Mheshimiwa Kakunda. Kwanza Mheshimiwa Kakunda pole na wote ambao wamehusika na tukio hili licha kuwa hili janga halijatokea mapema leo Bungeni lakini bado ni suala la Kitaifa na ni zito. Naagiza Serikali ilifanyie kazi. Wizara zinazohusika, Waziri Nchi (Bunge) uko hapa, shikirikiana na maeneo yote pamoja na Mbunge mhusika ili mlifanyie kazi na kupata uhakika wa idadi kamili ya waathirika na kuhakikisha maeneo kama haya tena yasipate madhara makubwa.

Waheshimiwa Wabunge, vilevile sisi katika maeneo haya, tuisaidie Serikali, kwa sababu wakati mwingine Serikali inaweka sheria na masharti lakini sisi tunapenda kuvunja ili tu tupate *support* ya wapiga kura wetu.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu swali hili la pili, wenyewe wapo. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, hebu mjibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika kama Mheshimiwa Kubenea alinisikia vizuri. Nilichosema ni hivi, utaratibu ule wa kiutumishi wa kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi ni ule alioueleza Waziri wa Utumishi, hilo tu. *That is the bottom line.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema kwa sababu hawa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ni wawakilishi wa Serikali Kuu kwenye maeneo yao ya utawala, wanaweza wakakuta jambo ambalo haliko sawa linalomhusu mtumishi kutamka kwao kwamba huyu anafaa asimamishwe kazi, siyo ndiyo kusimamishwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema ni mpaka pale ambapo mamlaka yake ya ajira itakapomwandikia barua na hatua nyingine za kiutumishi kuchukuliwa, kwa mujibu wa maelezo aliyotoa Waziri wa Utumishi, yaani ile kusema tu wewe mbona unafanya uzembe huu? Kwa sababu wale ni wawakilishi wa Serilali Kuu kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema siku moja, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wana kofia mbili, kofia zile mbili zinakaa pamoja, kuna *Head of State* na kofia ile ya *Head of Government*. Zile kofia mbili zile wameshushiwa wao kwa pamoja pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wana masuala ya ulinzi na usalama pia. Ndiyo maana wanapokuwa wako kule, hata wakija mimi ndio Rais wa Wilaya au Rais wa Mikoa, ni maneno yanayoudhi kidogo kwa wengine ambao hawapendi, lakini maana yake haiondoki, inabakia kuwa ile ile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wanapokuwa wana jambo wanaliona haliko sawa, wakasema hatua fulani zichukuliwe, wameagiza mamlaka husika kufanya hivyo, haina maana kwamba wao ndio wamesimamisha. Ndicho nilichosema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ameshakuelewa. Katibu. *(Kicheko)*

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamba. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa hotuba yangu, napenda nieleze kwamba hotuba nitakayosoma hapa ni muhtasari wa kitabu cha hotuba yetu ambacho kinagawiwa. Kwa hiyo, tungependa maudhui ya kitabu hicho ndiyo yaingie kwenye kumbukumbu za Bunge kama ndiyo hotuba rasmi ya mawasilisho rasmi ya ofisi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu lilipokea taarifa zilizowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara na Mazingira na Mwenyekiti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka ujao wa fedha. Hivyo naliomba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha unaokuja.

Kabla ya kuwasilisha hoja yangu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi kilichopita. Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara, Mazingira chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo (Mbunge) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mbunge) kwa kupokea, kujadili na kupitisha taarifa yetu ya mwaka wa fedha 2016/2017 na malengo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru Wasemaji Rasmi wa Kambi ya Upinzani kwa upande wa masuala ya Muungano na upande wa masuala ya Mazingira kwa ushauri waliokuwa wanautoa kwa Ofisi yetu kuhusu utekelezaji majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima napenda kumshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uongozi wake mahiri wa Taifa letu. Namshukuru pia kwa kuendelea kuniamini kwa dhamana ya kusimamia masuala ya Muungano na Hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kipekee namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa miongozo na maelekezo aliyokuwa anatupa mara kwa mara sisi tunaofanyakazi chini yake. Namshukuru pia kwa uongozi wake makini ambao umewezesha kupatikana mafanikio katika masuala ya Muungano na Hifadhi ya Mazingira. Vile vile nampongeze Waziri wetu Mkuu kwa usimamizi mzuri wa shughuli za kila siku za Serikali uliowezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utendaji wa shughuli za kila siku za Serikali. Naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao Bungeni ambazo zimetoa tathmini ya jumla kuhusu utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha uliopita na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha unaokuja. Aidha, niwatakie Mawaziri wote watakaonifuatia kila jema naufanisi katika hoja zao na kazi zilizo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kusema kwamba kesho kutwa tarehe 26 mwezi wa nne Muungano wetu utatimiza miaka 53 tangu kuasisiwa kwake. Tunawakumbuka na kuwaenzi Waasisi wa Muungano wetu; Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee Amani Abeid Karume kwa hatua hiyo ya ujasiri iliyotujengea heshima duniani kote. Muungano wetu umedumu hadi sasa kutokana na uongozi mahiri wa awamu zote za uongozi kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia zaidi ya 93 ya Watanzania wamezaliwa baada ya Muungano na Muungano umeendelea kuwa utambulisho wa Utaifa na Taifa letu na fahari ya nchi yetu kote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyotambulisha awali nimepata heshima kubwa ya kuwatambulisha baadhi ya Watanzania wenzetu walioshirika katika kutengeneza hisotoria ya nchi yetu. Kama alivyotambulishwa yupo Mzee Job Lusinde ambaye ni mmoja wa walioshiriki katika majadiliano ya kuandika Hati ya Makubaliano ya Muungano, na pia alishuhudia wakati Mwalimu Nyerere na Mzee Karume wakisaini hati hiyo tarehe 22 Aprili,1964 kule Zanzibar. Pia Mzee Lusinde alikuwa katika Baraza la Mawaziri la Kwanza la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wamebakia wawili tu, Mawaziri wa kwanza katika Baraza la Kwanza la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, wapo vijana wa wakati ule, wawili kutoka upande wa Zanzibar na wawili kutoka upande wa Bara walioshiriki katika tukio la kihistoria la kuchanganya mchanga wa nchi zetu mbili kama ishara ya kuungana kwa nchi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hisani yako, naomba wasimame tena ili waweze kuonekana na kutambuliwa na Bunge. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoisha na malengo kwa mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yetu, Ofisi ya Makamu wa Rais imezingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dira ya Taifa ya maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Malengo ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa, Sera ya Taifa ya Mazingira na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa nchi yetu na maisha ya Watanzania, yanategemea kwa kiasi kikubwa rasilimali asili tulizonazo kama vile ardhi, maji, misitu na hewa safi. Uwepo rasilimali asili hizi kwa mahitaji yetu ya sasa na ya vizazi vijavyo hutegemea sana namna tunavyozitumia pamoja na uhifadhi wake. Changamoto tuliyonayo sasa ni pamoja na uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa hifadhi wa mazingira, lakini pia uwepo wa mabadiliko ya tabia ya nchi. Athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira ni pamoja na upungufu wa mvua, kupungua kwa misitu na uoto wa asili, kupungua kwa vyanzo vya maji na uchafuzi wa hali ya hewa na kuongezeka kwa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mazingira ya nchi yetu bado ni mbaya kiasi cha kutishia mustakabali wetu kama Taifa. Kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira sehemu kubwa ya nchi yetu inatishiwa kuwa jangwa. Pamoja na juhudi za Serikali kuhakikisha kwamba maisha ya Watanzania yanakuwa bora zaidi mazingira yasipotunzwa jitihada hizi zote za Serikali zinazofanywa kuwaletea wananchi maendeleo hazitaleta matunda tunayotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira unaathiri sekta na nyanja zote za maisha ya watanzania iwe ni kilimo, ufugaji, uvuvi, utalii, miundombinu, huduma ya afya, huduma ya maji, huduma ya umeme pamoja na maendeleo ya viwanda. Ili kuyanusuru mazingira ya nchi yetu ni lazima hatua za makusudi zichukuliwe kudhibiti uharibifu wa mazingira unaoendelea sasa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo sababu Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuyafanya masuala ya uhifadhi wa mazingira kama sehemu ya muhimili wa uchumi wa nchi yetu na maendeleo ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulinda hifadhi ya mazingira ya nchi yetu na kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira nchini, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeendelea kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mikakati na mipango mbalimbali ya hifadhi ya mazingira, lakini pia

mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya mazingira. Hatua hizi zinalenga kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali asili ili kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hiyo kwa mwaka wa fedha unaokwisha, yafuatayo yamefanyika:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni mapitio ya Sera Taifa ya Mazingira. Kama nilivyolitaarifu Bunge lako Tukufu, mwaka jana, ofisi yetu ilikuwa inafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997. Sera hiyo ni ya muda mrefu, miaka 20, masuala ya mazingira yamebadilika, kwa hiyo, tuliona haja ya kupitia ili kuunda sera mpya inayozingatia changamoto za sasa za hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninayofuraha kulialifu Bunge lako Tukufu kwamba ofisi yetu imekamilisha mapitio ya sera hiyo na sera hiyo itatolewa rasmi katika mwaka ujao wa fedha. Sera hii mpya imezingatia changamoto mpya za mazingira na mbinu na mikakati mipya ya kupambana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutimiza wajibu wetu wa kusimamia hifadhi ya mazingira nchini, ofisi yetu imeendelea kutengeneza na kusimamia na kuhamasisha utekelezaji wa mipango na mikakati ya kitaifa ya uhifadhi wa mazingira nchini katika ngazi mbalimbali za utawala wa nchi yetu. Katika mwaka wa fedha unaokwisha, ofisi iliwahimiza viongozi na watendaji katika ngazi na sekta zote Tanzania Bara kutenga fedha na kutekeleza na kutolea taarifa mikakati na mipango ya hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha ofisi yetu itajiimarisha katika wajibu wake wa kuratibu shughuli za hifadhi ya mazingira nchini na kuendelea kuwezesha sekta zote hapa nchini kupanga na kutekeleza mipango ya hifadhi ya mazingira pamoja na mipango ya maendeleo kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mipango na

mikakati iliyopangwa na kutekelezwa katika mwaka wa fedha unaokwisha ni pamoja na mkakati wa kupanda na kutunza miti wa 2016-2021, mkakati wa hifadhi wa Taifa wa hifadhi ya Baionuai, Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, Mkakati wa Kitaifa wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Pwani, Bahari, Maziwa, Mito na Mabwawa na Programu ya Taifa ya Kukabiliana na Kuenea kwa Jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwa kifupi Mkakati wa Kupambana na Uvuvi Haramu wa Kutumia Milipuko. Muheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoisha, ofisi ilichukua hatua madhubuti kabisa za kuhifadhi mazingira ya bahari kwa kupambana na uvuvi haramu wa kutumia milipuko. Ofisi ilianzisha na kuongoza jitihada zilizoshirikisha Wizara sita ambazo ni Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi lengo lilikuwa ni kuandaa mbinu na mipango na kufanya operesheni ya pamoja ya kukabiliana na uvuvi haramu ambao umekuwa ukiongezeka kwa kasi kubwa na kuathiri mazingira, mazalia ya samaki na viumbe hai wakiwemo samaki na matumbawe. Katika mwaka wa fedha unaokuja, ofisi itaendelea kuratibu na kusimamia jitihada hizi.

Muheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu litakumbuka kwamba ofisi imekuwa ikiendesha Tuzo ya Rais ya Upandaji Miti na Utunzaji wa Vyanzo vya Maji kuanzia mwaka 2010. Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokuja ofisi yetu itaihuisha tuzo hiyo na kupanua ili iwe kubwa zaidi ili endane na hadhi na nafasi ya Rais. Kwa maana hiyo kuanzia mwaka wa fedha unaokuja tuzo hiyo sasa itaitwa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira ambapo mchakato wa kuwapata washindi utakuwa mpana zaidi na wa wazi zaidi na zawadi kwa watu na taasisi zinazofanya kazi nzuri katika hifadhi ya mazingira na zawadi ya jumla ya hifadhi ya mazingira zitakuwa kubwa zaidi na zitatolewa kila baada ya miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi pia inawajibika kisheria kuandaa taarifa ya hali ya mazingira nchini kila baada ya miaka miwili. Katika mwaka wa fedha uliokwisha ofisi imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii na viongozi na watendaji katika Sekta ya Umma kuhifadhi mazingira na kuchukua hatua zilizobainishwa katika taarifa ya pili ya hali ya mazingira nchini ya mwaka 2014. Katika mwaka wa fedha unaokuja, ofisi imeandaa hadidu za rejea kwa ajili ya kuandaa taarifa ya tatu ya hali ya mazingira nchini ambayo inatarajiwa kuanza kaandaliwa katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka kwamba Mfuko wa Mazingira ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na mfuko huu ulitarajiwa kuwa chanzo muhimu cha fedha kwa ajili ya hifadhi ya mazingira nchini. Hata hivyo kwa miaka mingi sasa mfuko huu haukuwa umeanza kazi. Katika mwaka wa fedha unaokwisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amemteua kiongozi mahiri na mashuhuri katika sekta binafsi Ndugu Ali Mufuruki kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko na katika kipindi hicho, nimewateua wajumbe vilevile mahiri na makini akiwemo Makamu Mwenyekiti Profesa Yunusu Mgaya ambaye tuko naye hapa kuwa wajumbe wa Bodi hiyo na nimeizindua tarehe 2 Februari mwaka 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, teuzi hizi sasa zimefanya Mfuko huu kuanza kazi rasmi. Katika mwaka wa fedha unaokuja ofisi itakamilisha kanuni za kuendesha mfuko na itafanya juhudi ikiwemo kuomba ushirikiano wa Bunge hili Tukufu za kuuwezesha mfuko kuwa na uwezo na mamlaka makubwa zaidi ya kitaasisi na kutimiza majukumu yake kama ilivyotarajiwa, pia kupata fedha za kugharamia shughuli za hifadhi ya mazingira nchini, mafanikio ya mfuko huu yanategemea sana utashi wa Wabunge katika kuuwezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia shughuli za hifadhi ya mazingira katika mwaka wa fedha unaokwisha ofisi imefanya mawasiliano

na Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuhakikisha kwamba katika Bajeti za Wizara za Kisekta, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kunakuwa na kifungu cha bajeti au kasma au *subvote* cha hifadhi ya mazingira nchini. Ofisi inaamini kwamba kwa kuweka kifungu hiki, hata kama katika miaka ya mwanzo hakutapangwa fedha za kutosha kutaziamsha Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufikiria na kupanga kazi za hifadhi ya mazingira.

Muheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kukithiri kwa uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na mifuko ya *plastic* na vifungashio vya *plastic* katika mwaka wa fedha unaokwisha ofisi ilitoa tamko la dhamira ya Serikali kupiga marufuku mifuko ya *plastic* na vifungashio vya *plastic* katika hotuba yetu ya mwaka uliopita, na baadaye katika ujumbe wetu kwa umma uliotolewa mwezi Agosti 2016.

Katika kutekeleza dhamira hiyo na kwa mujibu wa kifungu cha 230(2)(f) cha Sheria ya Mazingira, ofisi iliandaa kanuni za kusitisha matumizi ya vifungashio vya pombe kali (viroba), ambayo ilichapishwa katika Tangazo la Serikali namba 76 la tarehe 24 Februari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza kanuni hiyo tarehe 01 Machi, 2017 Serikali ilianza kupiga marufuku uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya vifungashio ya *plastic* kufungia pombe kali. Ofisi yetu iliunda kikosi kazi cha kitaifa kwa ajili ya kufanya oparesheni maalum ya utekelezaji wa maelekezo ya kuzuia pombe za viroba. Operesheni hii imetekelezwa kwa mafanikio makubwa na kwa weledi mkubwa ambapo pombe za viroba kama mnavyoona zimetoweka kabisa mitaani na operesheni hii inaendelea kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya pamoja na Kamati za Mazingira katika Mikoa na Wilaya zote za Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja ofisi itakamilisha taratibu za ndani ya Serikali katika kufikia maamuzi ya kudhibiti uzalishaji, usambazaji, uuzaji na

matumizi ya *plastic* ya kubebea bidhaa mbalimbali lakini bila kuathiri uchumi na uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi inashirikiana na wadau katika kutatua changamoto mbalimbali za uchafuzi wa mazingira unaotokana na kutupwa na uteketezaji taka ovyo, utiririshaji wa maji taka na uchafuzi wa hewa unaosababishwa na mitambo ya uzalishaji wa viwandani na shughuli nyinginezo. Katika kukabiliana na changamoto hizi viongozi wameshiriki na kuhimiza utekelezaji wa sheria ya mazingira pale ambapo uvunjifu wa Sheria ulibainishwa adhabu mbalimbali zilitolewa na Baraza la Taifa la Hifadhi la Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja ofisi ilipokea maandiko kutoka kwa watu mbalimbali waliotaka kuwekeza katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia taka ngumu zinazozalishwa katika miji na majiji yetu. Kwa kuwa suala hili linahusu Wizara na sekta nyingi hakukuwa na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi hii ambayo ingeweze kusaidia kupunguza taka mijini, kuongeza ajira, kuzalisha umeme kwa bei nafuu, lakini pia kukuza pato la Taifa. Katika mwaka wa fedha unaokuja baada ya mashirikiano na wadau wote, ofisi yetu imeandaa mwongozo mahususi wa uwekezaji wa umeme unaotokana na taka ngumu na tunaamini kwamba mwongozo huu utarahisisha na kuharakisha uwekezaji katika eneo hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yetu pia inatekeleza mikataba mbalimbali ya kimataifa ya mazingira. Katika mwaka uliopita wa fedha ofisi yetu imeshughulikia kwa namna mbalimbali mikataba ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba mkubwa wa kwanza ni Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na Itifaki ya Tokyo. Ofisi inatekeleza miradi mikubwa miwili ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na mkataba huu. Kwanza ni Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii za Pwani Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi ambao unatekelezwa kwa

kushirikiana na Wilaya za Pangani, Rufiji, Bagamoyo, Mkoani (Pemba) pamoja na Mjini (Unguja) ili kunusuru maeneo hayo na kuongezeka kwa kina cha bahari. Mradi mwingine ni wa kuhimili kwa tabianchi unaotekelezwa katika Wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha, ofisi iliongeza kasi ya kuandaa miradi mbalimbali ya kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu chetu tumeorodhesha miradi hiyo, na imani yetu ni kwamba miradi hii itatekelezwa katika maeneo mbalimbali ya majimbo yetu, na pale maandalizi ya miradi hii yatakapokamilika ofisi yetu inaahidi kulijulisha Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge kuhusu miradi hii itakavyotekelezwa kataka maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wetu wa kukabiliana na ufinyu wa fedha ni kuandika miradi mingi zaidi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi ili tuweze kuongeza uwezo wa kirasilimali wa kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayofuraha vilevile kulialifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa mwaka wa fedha unaokwisha, ofisi yetu (Ofisi ya Makamu wa Rais) imeweza kufanikisha upatikanaji wa jumla ya shilingi bilioni 230 zitakazotumika katika mradi wa maji Simiyu kama sehemu ya mkakati wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Katika mwaka wa fedha unaokuja ofisi yetu itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya miradi mikubwa ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabia ya nchi katika sekta mbalimbali za uzalishaji mali na huduma za jamii.

Muheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mfano tu wa mambo tunayoweza kuyafanya, kwamba mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira unaathiri sekta za uzalishaji mali na unaathiri huduma za jamii. Mkakati wa ofisi yetu ni kujenga hoja kwamba moja ya changamoto tunazozipata na kuchelewa kwa ukuaji wa uchumi

kunatokana na athari hizo na hivyo kutafuta fedha za kuhimili *(adaptation)* madhara hayo. Kwa hiyo tumeanza kwa kupata hizi shilingi bilioni 230 na mkituunga mkono tutapata fedha nyingi zaidi za kutekeleza miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi iliyopo, kukamilisha miradi inayoandaliwa na kuandaa mapendekezo mapya ya miradi ili kuhakikisha kwamba Tanzania inanusuru mazingira yake na kufaidika na fursa zinazotokana na mkataba huu wa mabadiliko ya tabianchi ikiwemo Itifaki ya Tokyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu chetu kuanzia ukurasa wa 19 mpaka wa 24 tumeorodhesha mikataba mingine inayosimamiwa na ofisi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha ofisi imekamilisha mawasilisho ya miradi minne ambayo imekidhi vigezo vya kufadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(GEF).* Vilevile katika kipindi hicho ofisi imeendelea kushauri vikundi vya kijamii vipatavyo 53 kuhusu uandishi wa miradi midogo ili viweze kunufaika na ufadhili huo wa *GEF.* Katika mwaka wa fedha unaokuja ofisi imeendelea kuratibu maandalizi na kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya *GEF* hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliokwisha nilifanya ziara katika mikoa 14 nchini na mtakumbuka pia Mheshimiwa Naibu Waziri naye amekuwa anafanya ziara nyingi mikoani kuhimiza utunzaji wa mazingira, ikiwemo hifadhi ya vyanzo vya maji, maziwa, mito na mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara zetu tumebaini kwamba maeneo mengi yameharibika na mengine kina cha maji kimepungua na yapo hatarini kutoweka. Endapo hatua za makusudi hazitachukuliwa, maziwa, mito na mabwawa tunayotegemea kiuchumi na kwa ustawi wa kijamii yatakauka kama sio kutoweka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yetu sasa imechukua hatua madhubuti kabisa za kuokoa mfumo wa ikolojia wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Bonde la mto huu hutegemewa sana kwa uchumi wa nchi yetu. Bonde hili limeharibika, mtiririko wa maji umepungua na kuathiri maisha ya watu takribani milioni sita pamoja na uchumi wa nchi yetu ikiwemo uzalishaji wa umeme katika mabwawa ya Mtera na Kidatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba, tarehe 11 Aprili Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan alizindua Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Kuokoa Mfumo wa Ikolojia wa Bonde la Ruaha Mkuu na kutoa maelekezo yake ya kikazi. Kikosi kazi hiki kimeanza kazi, kimeanza vizuri. Dhamira yetu ni kuhakikisha kwamba Mto Ruaha Mkuu unarejea katika hali yake ya kutiririka maji mwaka mzima jambo ambao lilisimama kuanzia mwaka 1993.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegundua mambo ya ovyo sana katika kazi hii ikiwemo watu wakubwa na wazito wakiwa ndio wanaongoza kabisa katika kuchepusha maji yasiendelee na mto na sisi tumedhamiria kuchukua hatua bila kutazama ukubwa wa nafasi ya mtu wala uwezo wake wa kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunao uzoefu kama ofisi ya kurejesha hali ya mto katika mazingira yake. Mtakumbuka nilifanya ziara katika Mkoa wa Katavi na tukakuta Mto Katuma umeacha kutiririka na viboko wanakufa, watu wa chini hawapati maji kutokana na ujenzi wa makingio na michepusho ya mito karibu 42 na tulitoa maelekezo kwa uongozi wa mkoa na michepusho yote hiyo ilibomolewa na baadaye sasa mto umerejea katika hali yake.

Kwa hiyo, uwezo wa kusimamia sheria za mazingira na kuhakikisa kwamba mifumo yetu ya ikolojia inakuwa katika hali yake huo tunao. Kinachotakiwa ni utashi wa kisiasa pamoja na kuungwa mkono na Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha, kutokana na ziara tuliyofanya baada ya kuona uharibifu mkubwa wa mito, mabwawa na maziwa, ofisi yetu sasa itaandaa mradi mahsusi wa kuokoa mazingira ya maziwa madogo madogo nchini ikiwemo Ziwa Jipye, Chala, Manyara, Natron, Eyasi na mengineyo. Vilevile tutaanzisha miradi ya kufufua na kulinda mifumo ya ekolojia ya mito mikubwa hapa nchini ikiwemo mto Ruaha Mkuu, Wami, Ruvu, songwe, Ruvuma pamoja na mabwawa muhimu na ya kimkakati kitaifa ikiwemo Bwawa la Mtera, Kidatu, Kihansi na Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha ofisi yetu ilianza taratibu za kuyatangaza baadhi ya maeneo nyeti na muhimu kwa mazingira na ikolojia nchini mwetu kuwa maeneo lindwa kimazingira *(Environmentally Sensitive Area)* na maeneo ya mazingira tengefu (*Environmental Protected Areas).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mazingira inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya mazingira kutangaza eneo lolote hapa nchini ambalo halina ulinzi wa sheria nyingine kama eneo la mazingira lindwa ambapo linatolewa masharti ya matumizi ya eneo hilo. Katika mwaka wa fedha unaokuja tutatumia mamlaka hayo kwa nguvu kubwa ili kutangaza maeneo hayo kwenye gazeti la Serikali kama ni maeneo lindwa na kuyawekea masharti na nguvu ya kisheria ya ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa matumizi ya mkaa, kama nilivyogusia hapo awali ni dhahiri kwamba matumizi ya mkaa yamechangia kwa sehemu kubwa katika kuteketeza ya misitu yetu na kuaribu vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita ofisi yetu iliandaa kongamano kubwa la wadau mbalimbali wa sekta ya mkaa nchini ikiwemo Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Nishati na Madini, Wakala wa Misitu, Makampuni yanayouza gesi ya kupikia na wajasiriamali wanaotengeneza mkaa mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mashauriano na wadau wote ofisi yetu sasa imeamua kutoa Mwongozo wa Kitaifa wa Udhibiti wa Matumizi ya Mkaa. Mwongozo huo unatarajiwa kutoa njia ya *(road map) ya* kuondokana kabisa na matumizi ya mkaa katika nchi yetu. Vilevile ofisi itaendesha shindano la ubunifu wa nishati mbadala ya mkaa ambapo washindi watawezeshwa kwa mtaji na maarifa ya kukuza ubunifu na biashara zao ili ziweze kushindana na mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wa uthibiti wa mimea vamizi, katika rasimu ya Sera mpya ya Mazingira tumebaini mimea vamizi yaani *invasive alien species* kama janga kubwa la kimazingira linalonyemelea Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea *Ngorongoro Crater* na nadhani Mheshimiwa Joyce Mukya alizungumzia hilo, nikakuta takribani theluthi nzima ya shimo lile kwenye *crater* pamoja na kuwepo majani, majani yale hayaliwi na wanyama, wanyama wamejikusanya katika upande mmoja wa *crater,* majani yale yamevamia maeneo ya wafugaji. Majani haya vamizi ambayo hayaliwi na wanyama wala hayaliwi na mifugo ni janga kubwa sana nchini mwetu kwa sababu yanapunguza malisho pamoja na kupunguza mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi Ofisi ya Makamu wa Rais tumeamua kulivamia njunga jambo hili kwa kutumia magwiji na wataalamu wa utafiti hapa nchini ili watupatie jawabu. Kwa sababu bila kufanya hivyo tutajikuta kwamba tuna ukijani lakini ukijani hautumiki kwa manufaa ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie sasa kuhusu Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira. Katika mwaka uliopita baraza limefanya shughuli kadhaa ikiwemo uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ambapo miradi mbalimbali ilisimamiwa na ilifanyiwa ukaguzi. Miradi iliyofanyiwa ukaguzi katika mwaka uliopita ni miradi 724 ambapo miradi 237 iliyosababisha uchafuzi wa mazingira ilichukuliwa hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi katika sekta ya mazingira wiki iliyopita nilichukua hatua ya kihistoria ya kuteua wakaguzi wa mazingira 435 kutoka katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaingia mwaka wa jana tulikuta wakaguzi wa mazingira 69 tu nchi nzima, juzi tuliteua wakaguzi 435 ambao watasambazwa katika Halmashauri zote na wakaguzi hawa watatusaidia katika kusimamia na kufatialia vitendo vya uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali nilimuomba wanasheria waandamizi watatu kwa ajili ya *NEMC* na ametupatia na wao wanasaidia sana kuongeza uwezo wetu kama Serikali wa kushitaki wale wanaoharibu mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya athari kwa mazingira *(environmental impact assessment),* katika mwaka wa fedha unaokwisha ofisi ililielekeza Baraza la Taifa kutengeneza mkakati wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliyoyatoa kuhusu kuboresha zoezi zima la tathmini ya athari kwa mazingira na kujenga uwezo wa Baraza katika kukagua miradi ya ufuatililiaji wa uchimbaji wa gesi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira yetu ni kufanya mchakato ya kupata vyeti vya mazingira usiwe kikwazo cha uwekezaji na maendeleo katika nchi yetu na katika mwaka ujao wa fedha ofisi yetu imetoa maelekezo mahsusi kuhusu mbinu na mikakati za kurahisisha na kuarakisha utoaji wa vyeti hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha Baraza limeendelea kutoa elimu kwa umma kwa viongozi mbalimbali ikiwemo Wakuu wa Mikoa katika baadhi ya Mikoa na katika mwaka ujao wa fedha tutaongeza jitihada na kuhakikisha kwamba viongozi wote

kuanzia watendaji wakuu na viongozi wa kuchaguliwa kwenye ngazi za Halmashauri wanapata Semina na mafunzo kuhusu hifadhi ya mazingira. Mtakapotuwezesha kwa rasimali tutaweza kufanya kazi hiyo vizuri na kwa haraka zaidi na Waheshimiwa Wabunge tutawashirikisha katika semina hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Hifadhi ya Taifa ya Mazingira *(NEMC)* limetayarisha miongozo na nyaraka mbalimbali na kuwasilisha katika jopo linalofanyia Baraza Ithibati ili *NEMC* iwe Taasisi ya Kitaifa ya Kutekeleza Mpango wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi *(National Empremeting Entity for Adaptation Fund).* Hatua hii italiwezesha Baraza na nchi kwa ujumla kuweza kupata fedha nyingi zaidi za kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uratibu wa miradi ya kuhifadhi mazingira; katika mwaka wa fedha unaokweisha Baraza limesimamia utekelezaji wa miradi minne kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo. Mradi wa kwanza ni mradi wa kuhifadhi lindi maji la Bonde la Kihansi na dakio lake. Mradi huu umefikia hatua nzuri na tunataka mradi huu ufuzu sasa ili eneo hilo liwe sasa ni *environmental protected area.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni pamoja na mradi wa mafuta kwa maendeleo unafadhiliwa na Serikali ya Norway na kutekeleza kwa ushirikiano na Wizara ya Nishati na Madini na mradi wa kujenga uwezo na sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja baraza litaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi hii na kuandaa mafunzo ya tathimini ya adhari kwa mazingira katika maeneo ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la mafuta na gesi ni jipya ambapo *NEMC* pamoja na Serikali kwa ujumla inabidi ijenge uwezo wa kusimamia mazingira katika eneo hili, kwa sababu hatari ya uharibifu wa mazingira inayotokana na uchimbaji na utafutaji wa gesi ni kubwa sana, kwa hiyo, Serikali iwe na uwezo wa kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie masuala ya Muungano. Ofisi yetu imetekeleza majukumu yake ya kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano katika masuala yasio ya Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika mwaka wa fedha unaokwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizofanyika katika mwaka unaokwisha ni hizi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuondoa changamoto za Muungano; katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 ofisi imeendelea jitihada za kuondoa changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Vikao vya pamoja vya kamati ya pamoja kati ya Serikali Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibara vimekuwa nyenzo muhimu ya kusaidia kupunguza changamoto za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi imeratibu vikao hivyo kwa ngazi ya wataalam, Makatibu Wakuu na Mawaziri na kikao cha kamati ya pamoja kilichoongozwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais kilifanyika kwa mafanikio makubwa mwezi wa kwanza mwaka 2017 huko Zanzibar ambapo changamoto kadhaa zilipatiwa ufumbuzi katika kikao hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao hicho cha Zanzibar na kwa sehemu kubwa katika mwaka wa fedha unaokwisha changamoto za Muungano zilizoongelewa na kupatiwa ufumbuzi au kupangiwa mipango ya kupatiwa ufumbuzi ni pamoja na usajili wa vyombo vya moto, mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha kuhusu utaratibu wa kuchangia gharama na kugawana mapato ya muungano, Hisa za Zanzibar zilizokuwa kwenye Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki pamoja na gawio la Zanzibar katika faida ya Benki Kuu.

Vilevile tulizungumzia kuhusu ushiriki na ushirikishwaji wa Zanzibar kwenye masuala ya Kimataifa ikiwemo ziara za viongozi wa nje wanaotembelea Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuliongea kuhusu ushiriki na ushirikishwaji wa Zanzibar kwenye mmchakato wa bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile tulizungumzia kuhusu ushirikiano kati ya SMT na SMZ, ushirikiano kati ya wafanyabiashara wa Zanzibar na Tanzania Bara kwenye nyanja za uwekezaji, viwanda na biashara. Vilevile tulizungumzia kuhusu utaratibu wa usajili wa meli za kigeni kwa kutumia bendera ya Tanzania, pia tulizungumzia masuala mengi mengineyo yanayohusu mustakabali na ustawi wa pande zote mbili za Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao hicho kilipokea *report* ya utekelezaji wa masuala yaliyokwisha fanyiwa maamuzi huko nyuma na yanayoendelea kutekelezwa na kikao kiliridhishwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa katika kutekeleza masuala haya ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha ofisi ilisimamia na kutekeleza mwongozo wa utaratibu wa muda wa mgao wa ajira katika taasisi za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu ilikubalika kwamba kuwe na uwiano wa asilimia 79 kwa watu wanaotoka Bara na asilimia 21 waliotaka Zanzibar kwa ngazi ya wataalam kwa ajira katika Serikali ya Muungano na taasisi za Muungano. Katika kuwezesha utekelezaji wa haraka wa uwiano huu Sekretarieti ya Ajira katika ofisi ya Rais imefungua ofisi kule Shangani, Jimboni kwa Mheshimiwa Ally Saleh, Zanzibar, na sidhani kama atapiga kelele yoyote leo kwa sababu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja Serikali itaendelea kuratibu vikao vya wataalam, Makatibu Wakuu, Mawaziri pamoja na vikao vya pamoja vya SMT na SMZ pamoja na kufuatilia maagizo na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utafiti, utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta, katika mwaka wa fedha

unaokuja Baraza la Wakilishi wa Zanzibar kama mnavyofahamu lilipitisha Sheria ya Gesi na Mafuta, na Rais wa Zanzibar aliridhia sheria hiyo, ikiwa ni matokeo ya maridhiano ya pande zote mbili za Muungano. Maridhiano yaliyopelekea suala hili kuondolewa katika orodha ya changamoto za Muungano. Katika mwaka wa fedha unaokwisha ofisi yetu iliratibu mahusiano na mashirikiano kati ya taasisi za SMT na SMZ ili kuwezesha suala hili kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja ofisi yetu itaendelea kuratibu mashirikiano yatakayoiwezesha Zanzibar kujenga uwezo na kunufaika katika shughuliza uchimbaji na utafutaji wa gesi na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi pia imefuatilia utekelezaji wa miradi ya maendele ya pamoja iliyotekelezwa kwa pande zote mbili. Miradi iliyofuatiliwa na kutekelezwa ni miradi ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni mradi wa *TASAF* ambao kama inavyoeleweka lengo lake ni kunusuru kaya maskini na kuziwezesha kuongeza kipato na fursa nyinginezo na kujigharamia katika mahitaji muhimu. Hadi ilipofikia mwezi wa kwanza mwaka huu fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezajsi wa mpango huu ni shilingi 206,715,956,369; kati ya fedha hizo shilingi bilioni 199 zimepelekwa SMT na shilingi bilioni 7.4 zimepokelewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mradi mwingine uliotekelezwa ni program ya miundombinu ya masoko, uongezaji thamani na huduma za kifedha. Mradi huu una malengo ya kuanzisha na kuendelea miundombinu ya masoko na matumizi ya taaluma ya kuongeza thamani, kutanua wigo upatikanaji wa huduma za fedha na ushiriki makini wa taasisi za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umekuwa na mafanikio makubwa katika maeneo ambayo mradi huu umetekelezwa, ambapo barabara zimejengwa shughuli za

kiuchumi zimeongezeka na hivyo kuongeza kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mradi wa MKURABITA umetekelezwa kwa upande wa Zanzibar. Hadi kufikia mwenzi wa kwanza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepokea shilingi milioni 45.4 kwa mradi wa MKURABITA ambapo Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar imepokea shilingi milioni 41.7. Vilevile mradi mwingine ambao umetekelezwa kwa pamoja ni Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi wa Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi. Mradi huu unatekelezwa kwa miaka sita kuanzia mwaka 2015 mpaka 2021 na umefadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia. Mradi huu utashirikisha Wizara mbalimbali katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwezesha wavuvi wadogo wa ukanda wa Pwani kuwa na uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi machi mradi huu umepokea jumla ya shilingi bilioni mbili ambapo Zanzibar imepokea shilingi milioni 930 kati ya hizo, na Idara ya Uvuvi ya SMZ imepokea shilingi milioni 476; pamoja na Mamlaka Usimamizi wa Bahari Kuu imepokea shilingi milioni 608.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu ni muhimu sana ukizingatia kwamba Zanzibara kwa sehemu kubwa uchumi wake unategemea uvuvi na kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano imedhamiria kuhakikisha kwamba Zanzibar inanufaika na rasilimali hiyo kubwa katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna miradi ya Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* ambayo inatekelezwa kwa opande zote mbili. Kwanza ni mradi wa kujenga uwezo wa watafiti ambapo hadi kufikia mwezi wa kwanza mradi umepokea shilingi milioni 41.7.

Pia kuna mradi wa kujenga uwezo wa matumizi ya taarifa za kimtandao katika afya ya jamii ambayo umepokea shilingi milioni 43, mradi wa kuongeza uwezo wa uzalishaji wa mpunga na hili ni eneo muhimu sana; mradi wa kubuni

formula ya chakula kitakacho nenepesha mbuzi na nyama na mradi wa uwezeshaji waatamizi ambao umepokea shilingi bilioni mbili. Miradi hii katika kuhakikisha kwamba Muungano unatoa fursa zaidi ya ustawi wa watu wa Zanzibar na hili ndilo linalofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara za kazi; katika mwaka wa fedha unaokwisha ofisi imeendelea kuimarisha ushirikiano wa pande zote mbili za Muungano kwa kufanya na kuratibu ziara za kikazi za maafisa, wataalamu, watendaji na viongozi wa taasisi za Muungano. Taasisi zote za Muungano zilizopo Zanzibar mimi Naibu Waziri na Makamu wa Rais tumezitembelea na kujua changamoto zake na kujifunza kuhusu jitihada zinazofanyika za kuhakikisha kwamba uwiano wa ajira upo, lakini vilevile programu na bajeti ya mipango ya taasisi za Muungano inazingatia uwepo wa pande zote mbili za Muungano na maslahi ya pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za Baraza la Wawakilishi za Mawasiliano ya Ujenzi na Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa zilitembelea baadhi ya Wizara na taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha fedha kilichopita na kujenga ushirikiano wa karibu na taasisi hizo pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais inayoratibu masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hizo zimeonesha jitihada za makudi za Serikali zetu mbili katika kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mpango wa kazi kwa kila Wizara na taasisi ya Muungano unalenga katika kuboresha hali za maisha kwa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha zinazopelekwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika mwaka wa fedha unaokwisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kupokea fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo hadi kufikia mwezi marchi mwaka 2017 shilingi bilioni 1.4 za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na shilingi 15.75 za kodi ya mishahara *(PAYE)*

zilipokelewa na SMZ. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ofisi yetu itaendelea kuratibu na kufatilia uwepo wa utaratibu wa rahisi na haraka wa utolewaji wa fedha zinazostahili kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa kweli kwamba tumebaini hasa kwenye Mfuko wa Jimbo kumekuwa na changamoto ya fedha hizo kufika kwenye majimbo na kwa Wabunge kwa haraka. Kwa hiyo, ofisi yetu inaitambua hilo na italifanyia kazi kwa kuweka utaratibu ambapo fedha hizo zitatolewa na kufika haraka kule kunakostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano; ushirikiano kati ya SMT na SMZ kwa masula yasiyo ya Muungano umeendelea kuimarika. Serikali zetu mbili zimekubaliana kuwa na utaratibu wa vikao vya kisekta baina ya Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano kwa lengo la kuimarisha ushirikiano. Sekta hizo hushirikiana katika masuala ya mafunzo, sera na ushiriki katika nyanja za kimataifa ikiwemo kubadilishana ujuzi, utaalam na uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya wajibu wa ofisi yetu si tu kuratibu masuala ya Muungano bali pia masuala yasiyo ya Muungano na tumeona mafanikio makubwa sana katika eneo hili; ambapo ushirikiano umeongezeka katika sekta ya nishati; ambapo tumeelezea kuhusu vikao vya pamoja na shughuli zilizofanyika ikiwemo katika muktadha wa kuiwezesha Zanzibar kujitegemea na kunufaika katika hili suala la gesi na mafuta. Lakini pia tumeona ushirikiano katika sekta ya maji ambapo kumekuwa na shughuli za kubadilishana uzoefu na uwezo kuhusu utunzaji wa kumbukumbu za kielektroniki pamoja na taarifa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na ushirikiano kwenye utumishi na utawala bora; ambapo kumekuwa na vikao mbalimbali kwa ngazi ya Makatibu Wakuu na Mawaziri na kuainisha maeneo ya ushirikiano na pia kuandaa hati ya makubaliano ya kurasimisha ushirikiano huo. Taasisi za rushwa

za pande zote mbili pia zimeshirikiana na zimepanua wigo kwa aijili hiyo ambapo rasimu ya mkataba wa mashirikiano imeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kazi yetu katika Ofisi ya Makamu wa Rais ni kushauri sekta na taasisi zisizo za Muungano zinazoshirikiana kuwa na makubaliano rasmi ya mashirikiano hayo ili kuyapa hadhi na heshima, lakini pia uhalali. Sisi tunaona huo ndio mwenendo na tunafarijika sana tunapoona wenzetu ambao hawapo kwenye mambo ya Muungano wanashirikiana. Pia kumekuwa na ushirikiano katika sekta ya maliasili na utalii hasa katika masuala ya wanyamapori, misitu, ufugaji nyuki pamoja na mali kale. Mikataba ya kimataifa kuhusu usimamizi wa rasilimali za maendeleo, ushirikiano katika nyanja za utafiti na maendeleo pamoja na udhibiti wa usafirishaji haramu wa mazao ya maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya pia imeonesha mfano mkubwa sana wa ushirikiano, napenda kuwapongeza Mawaziri wa pande zote Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Mheshimiwa Mahamoud Thabit Kombo ambao kwa kweli wameonesha wao wenyewe kwa *initiative* yao ushirikiano wa hali ya juu. Kuna programu nyingi ambazo wanazitekeleza kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unakuja ofisi itaendelea kuharakisha na kuhakikisha kwamba sekta zisizo za Muungano ambazo zinashabihiana kimajukumu zinaratibiwa na kuhamasishwa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka. Vilevile kumekuwa na mashirikiano makubwa katika sekta ya mazingira na sisi kama ofisi hiyo hiyo ambayo inasimamia mazingira na Muungano; mazingira kama si jambo la Muungano tunapaswa kuonesha mfano wa mashirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano na mfano huo tumeuonesha na kama ambavyo mmeona miradi mingi sana ya maendeleo ya mazingira inatekelezwa kwa upande wa Zanzibar, vile vile tumeshirikiana sana katika suala la uvuvi haramu. Katika mwaka ujao wa fedha ofisi yetu itaendelea kuonesha mfano katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi. Katika mwaka wa fedha uliopita Ofisi yetu imeendelea kuimarisha maadili, utawala bora, demokrasia na dhana ya ushirikishwaji watumishi mahali pa kazi kwa kupitia vikao mbalimbali pamoja na vikao vya baraza la wafanyakazi. Vilevile sekta binafsi imeshirikishwa katika utoaji wa huduma katika Ofisi yetu na kueneza dhana ya ushirikishwaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuhamia Dodoma; mtakumbuka kwamba Serikali imetoa uamuzi wa kuhamia Dodoma; ofisi yetu imetekeleza kwa vitendo maamuzi haya kwa kuwahamisha viongozi wakuu pamoja na baadhi ya watumishi katika awamu ya kwanza. Vilevile Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira *(NEMC)* limenunua kiwanja tayari katika Manispaa ya Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha ofisi yetu inatarajia kuendelea na utekelezaji wa mpango wa kuhamia Dodoma ambapo inatarajia kuhamisha watumishi kwa awamu mbili na awamu ya tatu kwa kuzingatia ratiba inayotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hitimisho; kama tunavyoelewa nchi yetu ni nchi ya Muungano; Muungano wetu una umuhimu wa pekee kwa Taifa letu na umekuwa ndio utambulisho wa Taifa letu na kielelezo cha umoja wetu katika kudumisha amani na usalama wa nchi yetu. Natoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuuthamini, kuuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano wetu ili jitihada za kusukuma maendeleo yao kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa faida za pande zote mbili ziendelee kufanikiwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaitwa Muungano wa Tanzania, ndilo jina la nchi yetu, hakuna nchi inaitwa Tanzania. Inaitwa Muungano wa Tanzania; ni kwamba tulienda tukatengeneza tu *instrument* ya kutengeneza Jamhuri tukajiita Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, hakuna nchi bila Muungano, na sisi tunasema wale wote ambao wanaubeza, wanaupinga na kuhujumu

Muungano wetu wanalihujumu taifa letu na wanahujumu utaifa wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya uongozi wa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli na Makamu wake Mheshimiwa Samiah Suluhu Hassan, lakini pia chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein; Muungano wetu umeendelea kuimarika na kushamiri na hakuna changamoto yoyote ya Muungano inayoweza kutufarakanisha, kututenganisha wala kuturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yetu inayo faraja kubwa kwamba katika nchi yetu sasa kwa watu wa itikadi zote za kisiasa, kwa watu wa pande zote za Muungano mjadala sasa si uhalali wala umuhimu wa Muungano; mjadala sasa ni namna ya kuuimarisha na hayo ni mafanikio makubwa sana ya kazi ya ofisi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi na Serikali kwa ujumla itaendelea kuyafanyia kazi maoni na mawazo ya watu wote wenye nia ya kuona Muungano wetu unashamiri akiwemo Mheshimiwa Ally Saleh na wenzake kwa upande ule. Tunaamini wamo katika Bunge hili kwa sababu wanauamini na kuukubali Muungano. Bunge hili linaitwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haitegemewi mtu anaepinga Muungano awe katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yetu pia ni muhimu na yana mchango mkubwa katika maendeleo ya uchumi na viwanda. Ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kwamba mazingira na maliasili ya nchi yetu zinalindwa na kuhifadhiwa. Ofisi yetu ina dhamira ya kujenga utaratibu wa kumshirikisha kila Mtanzania katika wajibu huu ili ulinzi na hifadhi ya mazingira lisiwe suala la shuruti bali utamaduni. Napenda kutoa wito kwa Watanzania pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kuhakikisha kwamba dhamira ya Serikali ya kulinda na kuhifadhi mazingira inazingatiwa na kupewa kipaumbele kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokuja ofisi yetu itashika hatamu kwa uthabiti kabisa katika wajibu wake wa usimamizi wa uratibu wa shughuli za hifadhi ya mazingira nchini. Tutaandika kanuni na kutoa miongozo kadhaa ya hifadhi ya mazingira katika sekta na nyanja zote. Mtazamo wetu sasa kuanzia mwaka uja wa fedha ni kuongoza hifadhi ya mazingira kwa namna pana zaidi kwa kuangalia mifumo ya kiikolojia, mifumo ya uazalishaji mali na uchumi wa matumizi ya rasilimali asili. Mazingira tunataka kuyapa tafsiri pana zaidi kuliko uchafuzi wa mazingira. Mazingira kuyafungamanisha na maendeleo ya nchi yetu. Hatua tutakazochukua kuanzia mwaka ujao wa fedha ni za ku-*support* ukuaji wa uchumi kwa hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wote walionisaidia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi na shughuli zetu kwa ujumla. Shukrani za kipekee ziendee kwa Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake na dira na mwelekeo aliotupatia kuhusu majukumu yetu. Pia namshukuru kwa kipekee sana Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake makini uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge, Naibu waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano mkubwa alionipa katika utekelezaji wa kazi za ofisi na kwa kazi kubwa anayoifanya katika nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwashukuru Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa omba pesa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Profesa Faustin Kamuzora, Katibu Mkuu pamoja na viongozi wote wa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais ikiwemo Mfuko kwa ushirikiano waliotupa. Pia napenda kuwashukuru washirika wa maendeleo ambao tumefanya nao na tunaendelea kuwategemea katika shughuli zetu zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa Maombi ya Fedha. Ili Ofisi yetu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha unaokuja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya matumizi ya shilingi 4,914,608,000 fedha za matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2017/2018, hili ni Fungu 26. Kiasi hiki kinajumuisha fedha za mishahara ya watumishi shilingi 1,159,643,000 na fedha za matumizi mengineyo shilingi 3,754,965,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 31 Ofisi ya Makamu wa Rais ninaomba Bunge lako liidhinishe Makadirio ya matumizi ya shilingi 15,002,987,437 kwa fungu hili; kiasi hiki kinajumuisha shilingi 8,214,555,000 fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 6,788,452,437 fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi 3,120,324,000 kwa ajili ya mishahara ya watumishi, shilingi 2,215,044,000 ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na shilingi 2,879,167,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo ya idara na vitengo katika Ofisi yetu.

Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha fedha za ndani shilingi bilioni tatu na fedha za nje shilingi 3,788,452,437.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## DIRA

***Tanzania yenye muungano imara na mazingira safi, salama na endelevu.***

## DHIMA

***Kuimarisha muungano na kutoa miongozo itakayowezesha uratibu na usimamizi wa mazingira ili kuwa na maendeleo endelevu na ustawi wa Watanzania.***

## *MAJUKUMU YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS*

*Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ni:-*

*i. Kuandaa na kusimamia sera zinazohusu Mazingira;*

*ii. Kuratibu masuala ya Muungano na ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yasiyo ya Muungano;*

*iii. Kukuza uzalishaji unaozingatia mazingira na uchumi wa kijani;*

*iv. Hifadhi ya mazingira na uzingatiaji sheria ya Mazingira;*

*v. Kusimamia na kuendeleza watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais; na*

*vi. Kufuatilia na kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.*

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako tukufu limepokea taarifa zilizowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2016/17 na kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka wa fedha 2017/18. Hivyo,ninaliomba Bunge lako tukufu sasa, likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2017/18.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuwasilisha hoja yangu napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi kilichopita, nawaliowezesha kuandaa mipango ya mwaka wa fedha 2017/18 na kustawisha hoja ambayo ninaiwasilisha katika hotuba hii humu Bungeni. Aidha, ninawashukuru kwa dhati waheshimiwa wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo(Mb.), na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa(Mb.), kwa kupokea, kuchambua, kujadili, na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwamwaka wa fedha 2016/17 na Malengo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/18.

3. ***Mheshimiwa Spika,***ninatoa shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Ally Salehe Ally(Mb.), Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Masuala ya Muungano na Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul(Mb.),Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Hifadhi ya Mazingira kwa ushauri wao katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na taadhima, napenda kumshukuruMheshimiwaDkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano ya Tanzania, kwa uongozi wake mahiri wa taifa letu na kwa kuendelea kuniamini kwa dhamana ya kusimamia masuala ya Muungano na hifadhi ya mazingira. Aidha, kipekee kabisa, ninamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa miongozo na maelekezo aliyotupa mara kwa mara sisi tunaofanya naye kazi lakini pia kwa uongozi wake makini ambao umewezesha kupatikana kwa mafanikio katika masuala ya Muungano na hifadhi ya mazingira nchini.Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.); Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa usimamizi mzuri wa shughuli za kila siku za Serikaliuliowezesha kupatikana mafanikio makubwa katika utendaji wa Serikali katika kipindi kifupi cha utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano.

5. *Mheshimiwa Spika,* ninapenda kutumia fursa hii kukupongeza wewe, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Bunge letu kwa hekima na busara kubwa. Ninampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.),Naibu Spika, kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uaminifu.Aidha**,** ninatoa pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kujiunga na Bunge lako tukufu katika kipindi cha mwaka huu wa 2016/17,ambao ni Mheshimiwa Juma Ali Juma (Mb.), aliyechaguliwa na wananchi kwa kishindo kuwa mbunge wa Jimbo la Dimani, Zanzibar na Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela(Mb.); Mheshimiwa Alhaji Abdallah Majura Bulembo(Mb.); Mheshimiwa Prof. John Aidan Mwaluko Palamagamba Kabudi (Mb) na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete (Mb.). Pia, nampongeza Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare (Mb.) kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuingia katika Bunge lako tukufu katika nafasi ya Viti Maalum.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, marafiki na wananchi kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wao na kupoteza mali kutokana na majanga ya tetemeko la ardhi, mafuriko, moto na ajali za vyombo vya usafiri. Majanga yote yaliyotokea ni pigo kwa ustawi wa Taifa letu. Aidha, ninatoa salamu za pole kwako Mheshimiwa Spika pamoja na Bunge lako tukufu kwa kuondokewa na aliyekuwa Spika mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na aliyekuwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba Mheshimiwa Samuel John Sitta, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani, Zanzibar na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko MachaaliyekuwaMbunge wa Viti Maalum- CHADEMA. Tunaomba Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi,amina.

7. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshmiwa Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao katika Bunge lako tukufu, ambazo zimetoa taththmini ya ujumla kuhusu utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18. Aidha, niwatakie Mawaziri wote watakaofuata kila jema na ufanisi katika kazi iliyo mbele yetu.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kusema hayo, ninapenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 na malengo kwa mwaka wa fedha 2017/18.

## B: UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2017/18

9. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake, Ofisi ya Makamu wa Rais imezingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM

2015- 2020, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (*Sustainable Development Goals - SDGs*), Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 na Kanuni zake.

## I: HIFADHI YA MAZINGIRA

10. ***Mheshimiwa Spika,*** uchumi wa nchi yetu na maisha ya Watanzaniayanategemea kwa kiasi kikubwa maliasili tulizonazo kama vile ardhi, maji, misitu na hewa safi. Uwepo wa maliasili hizi kwa mahitaji yetu ya sasa na ya vizazi vijavyo hutegemea namna tunavyozingatia uhifadhi wake na matumizi endelevu. Changamoto tuliyonayo sasa ni uelewa mdogo wa jamii yetu kuhusu hifadhi ya mazingira na uwepo wa mabadiliko ya tabianchi. Athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira ni pamoja na upungufu wa mvua, kupungua kwa misitu na uoto wa asili, kupungua kwa vyanzo vya maji, uchafuzi wa hali ya hewa na kuongezeka kwa umaskini.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya mazingira ya nchi yetu bado ni mbaya kiasi cha kutishia mustakabali wetu. Kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira nchini, sehemu kubwa ya nchi yetu inatishiwa kuwa jangwa. Taarifa ya *National Forestry Resources Monitoring and Assessment* (NAFORMA) inabainisha kuwa kila mwaka tunapoteza takriban hekta 372,000 za misitu ya asili, hii inatokana na kufanya shughuli za kilimo na ufugaji kwa namna zisizo endelevu. Sababu nyigine ni moto kichaa na ukataji holela wa miti kwa ajili ya mkaa na kuni. Ni dhahiri kwamba, misitu yetu inaendelea kutoweka kwa kasi kubwa na hivyo kuwa na uwezekano wa kupata athari kubwa zaidi za mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na juhudi za Serikali kuhakikisha maisha ya Watanzania, hasa wanyonge, yanakuwabora zaidi, mazingira yasipotunzwa juhudi hizi za Serikali hazitaleta mabadiliko tunayotarajia.

12. ***Mheshimiwa Spika,***uharibifu wa mazingira unaathiri sekta na nyanja zote na maisha ya Watanzania. Uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji huathiri sana

upatikanaji wa huduma ya maji kwa Watanzania. Mafuriko yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi huathiri uchumi kwa kusababisha matumizi makubwa ya fedha ili kufanya marekebisho ya miundombinu. Uzalishaji wa umeme huathiriwa sana na ukame na hivyo kuathiri uzalishaji viwandani.Vilevile, sekta za kilimo, mifugo na utalii huathiriwa sana na ukame na mafuriko hivyo kusababisha umaskini kwa Watanzania. Uvuvi haramu wa kutumia milipuko husababisha uharibifu wa matumbawe,bioanuai na hivyo kuathiri maisha ya wavuvina ubora wa fukwe. Udhaifu katika udhibiti wa taka ngumu,uchafuzi wa hewa na utiririshaji wa majitaka au kemikali kutoka viwandani na migodini, huathiri afya za wananchi.

13. ***Mheshimiwa Spika,***ili kuyanusuru mazingira ya nchi yetu ni lazima hatua za makusudi zichukuliwe kudhibiti uharibifu wa mazingira unaoendelea. Hii ndio sababu Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuyafanya masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kama sehemu ya mhimili wa uchumi wa nchi na maendeleo ya watu.

14. ***Mheshimiwa Spika,***katika kulinda mazingira ya nchi yetu na kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira nchini, Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mikakati na Mipango mbalimbali ya hifadhi ya mazingira na piamikataba ya kimataifa ya mazingira, pamoja na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu mazingira. Hatua hizi zinalenga kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali ili kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Katika kutekeleza azma hiyo katika mwaka wa fedha 2016/17 yafuatayo yamefanyika:-

**Mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira**

15. ***Mheshimiwa Spika,***kama nilivyolitaarifu Bunge lako tukufu mwaka jana,Ofisi ilikuwa inafanyia mapitio Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997. Leo hii, ninayo furaha kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Ofisi imekamilisha Mapitio ya Sera ya Mazingira. Mchakato huu uliwashirikisha wadau wa sekta zote muhimu kote nchini. Rasimu ya Sera

hiyo na Mkakati wa Utekelezaji wake, ambazo zimeandaliwa kwa lugha za kiswahili na kiingereza, sasa zinapitia hatua za mwisho za mchakato wa kuridhiwa ndani ya Serikali.

**Mikakati na Mipango ya Kitaifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutimiza wajibu wetu wa kusimamia hifadhi yamazingira nchini,Ofisi imeendelea kutengeneza, kusimamia na kuhamasisha utekelezaji wa mipango na mikakati ya kitaifa ya hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini katika ngazi mbalimbali za utawala wa nchi. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi iliwahimiza viongozi na watendaji katika Sektretarietiza mikoa, mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta zote Tanzania Barakutenga fedha nakutekelezana kutolea taarifamikakati na mipango ya hifadhi na usimamizi wa mazingira.

**Mkakati wa Taifa wa Kupanda na Kutunza Miti 2016-2021**

17. ***Mheshimiwa Spika***, kama nilivyolieleza Bunge lako tukufu mwaka wa jana, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliandaa Mkakati wa Taifa wa Kupanda na Kutunza Miti utakaotekelezwa kwa muda wa miaka mitano (2016 hadi 2021). Mkakati huu unaelekeza kila kijiji, kitongoji, mtaa, kaya na taasisi kupanda na kutunza miti kwa malengo watakayowekewa. Lengo ni kuhakikisha nchi yetu inakuwa ya kijani. Mkakati huu umezingatia kurekebisha changamoto zilizojitokeza katika mikakati na kampeni zilizopita, ikiwemo motisha na ushiriki wa sekta binafsi katika biashara ya misitu. Aidha, baadhi ya mikoa imeanza utekelezaji wa mkakati huu kwa kupanda miti kwenye maeneo yao.

**Mkakati wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai (2015-2020)**

18. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kuusambaza na kuutolea elimu Mkakati wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai (2015-2020) katika wizara za kisekta

na mikoa yote ili wadau waweze kuutekeleza. Vilevile, Ofisi imendelea kuhimiza utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji (2006) na Mkakati wa Kitaifa wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Pwani, Bahari, Maziwa, Mito na Mabwawa (2008).

**Programu ya Taifa ya Kukabiliana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (2014-2018)**

19. ***Mheshimiwa Spika,***Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji waProgramu ya Taifa ya Kukabiliana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (2014-2018); na Mwongozo wa Kuhuisha Programu ya Taifa ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (2014-2018) katika sera, mipango na programu za kisekta kwa ajili ya kuhimiza usimamizi endelevu wa ardhi nchini.

**Mkakati wa Kupambana na Uvuvi Haramu wa Kutumia Milipuko**

20. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha 2016/17 hatua nyingine zilizochukuliwa na Ofisi ni kuhifadhi mazingira ya bahari kwa kupambana na uvuvi haramu wa kutumia milipuko. Ofisi ilianzisha na kuongoza jitihada zilizoshirikisha Wizara sitaambazo ni TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Mambo ya Ndani. Lengo lilikuwa ni kuandaa mbinu na mipango ya pamoja ya kukabiliana na uvuvi haramu ambao umekuwa ukiongezeka kwa kasi na kuathiri mazingira, mazalia ya samaki na viumbe wakiwemo samaki na matumbawe. Uvuvi kama huu huacha jangwa sehemu lilikofanyika na ili eneo lililoathirika liweze kurudi hali yake huchukua miaka 70 hadi 100.Ninapenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba, Mawaziri wa sekta husika walikubaliana kuhusu hatua za kutokomeza tatizo hilina kuanza kutekeleza.

21. ***Mheshimiwa Spika,***katika mwaka wa fedha wa 2017/18 Ofisi itaendelea kufuatilia na kushirikiana na

wadau wengine kuhakikisha hatua zilizopitishwa kuchukuliwa zinatekelezwa na kutoa taarifa za utekelezaji za mikakati na mipango hii.

**Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako tukufu litakumbuka kwamba Ofisi imekuwa ikiendesha Tuzo ya Rais ya Upandaji wa Miti na Utunzaji wa Vyanzo vya Maji kuanzia mwaka 2010. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/18, Ofisi itaihuisha Tuzo hiyo na kuipanua ili iwe kubwa zaidi kulingana na hadhi ya nafasi ya Rais. Kwa maana hiyo, kuanzia mwaka ujao wa fedha, Tuzo hiyo sasa itaitwa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira ambapo zawadi kwa watu na taasisi zilizofanya kazi nzuri katika nyanja mbalimbali za hifadhi ya mazingira, na zawadi ya jumla ya hifadhi ya mazingira, zitatolewa kila baada ya miaka miwili.

**Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya 2004**
**Taarifa ya Hali ya Mazingira Nchini**

23. ***Mheshimiwa Spika,***Ofisi inawajibika kisheria kuandaa Taarifa ya Hali ya Mazingira Nchini kila baada ya miaka miwili.Katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii na viongozi na watendaji katika sekta ya umma kuhifadhi mazingira na kuchukua hatua zilizobainishwa katika Taarifa ya Pili ya Hali ya Mazingira ya mwaka 2014.Aidha, Ofisi imeandaa hadidu za rejea kwa ajili ya kuandaa Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira nchini ambayo inatarajiwa kuanza kuandaliwa katika mwaka wa fedha 2017/18.

**Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko huu ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na ulitarajiwa kuwa chanzo muhimu cha fedha kwa ajili ya kuhifadhi mazingira nchini. Hata hivyo, kwa miaka mingi, Mfuko huo haukuwa umeanza kazi. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania amemteua kiongozi mashuhuri katika sekta binafsi, Ndugu Ali Mufuruki, kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko na katika kipindi hiki nimewateua wajumbe na kuzindua Bodi tarehe 2 Februari, 2017. Teuzi hizi sasa zimefanya Mfuko huu kuanza rasmi kazi. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi itakamilisha Kanuni za kuendesha Mfuko na itafanya juhudi, ikiwemo kuomba ushirikiano wa Bunge lako tukufu, za kuuwezesha Mfuko kuwa na uwezo na mamlaka makubwa zaidi ya kitaasisi kutimiza majukumu yake kama ilivyotarajiwa na pia kupata fedha na kugharamia shughuli za hifadhi ya mazingira nchini.

**Kasma/Subvote ya Hifadhi ya Mazingira Katika Bajeti za Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia shughuli za hifadhi za mazingira, katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Ofisi imefanya mawasiliano na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuhakikisha kwamba katika bajeti za Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kunakuwa na kifungu cha bajeti au kasma (*subvote*) cha hifadhi na usimamizi wa mazingira. Ofisi inaamini kwamba kwa kuweka kifungu hiki, hata kama kwa miaka ya mwanzo hakutapangwa fedha nyingi, kutaziamsha Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufikiria na kupanga kazi za hifadhi na usimamizi wa mazingira.

**Matumizi ya Mifuko na Vifungashio vya Plastiki**

26. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kukithiri kwa uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na mifuko ya plastiki na vifungashio vya plastiki, katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi ilitoa Tamko la Dhamira ya Serikali kupiga marufuku uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya mifuko ya plastiki ya kubebea bidhaa na vifungashio vya plastiki tarehe 18 Agosti, 2016. Katika kutekeleza dhamirahiyo, na kwa mujibu wa kifungu 230 (2)f cha Sheria ya Mazingira, Sura ya 191, Ofisi iliandaa kanuni za kusitisha matumizi ya vifungashio vya

plastiki vya pombe kali (viroba), ambayo iliyochapishwa katika Tangazo la Serikali Na. 76, la tarehe 24 Februari, 2017.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kanuni hiyo, tarehe 1 Machi, 2017, Serikali ilianza kwa kupiga marufuku uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya vifungashio vya plastiki kufungia pombe kali. Ofisi yetu iliunda kikosi kazi cha kitaifa kwa ajili ya kufanya operesheni maalum ya utekelezaji wa maelekezo ya kuzuia uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya vifungashio vya plastiki kufungashia pombe kali nchini. Operesheni hii imetekelezwa kwa mafanikio makubwa, ambapo pombe ya viroba imetoweka kabisa mitaani, na inaendelea nchini kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya pamoja na Kamati za Mazingira za Mikoa na Wilaya za Tanzania Bara.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Ofisi itaendelea kusimamia Kanuni za usitishaji uzalishaji, uingizaji, usambazaji na utumiaji wa vifungashio vya plastiki kufungia pombe kali nchini ili kulinda afya ya jamii, mazingira na kuokoa mapato ya nchi yetu yanayopotea kutokana na biashara holela ya pombe kali zinazofungashwa katika vifungashio vya plastiki. Aidha, Ofisi itakamilisha taratibu za ndani ya Serikali katika kufikia maamuzi ya kudhibiti uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya mifuko ya plastiki ya kubebea bidhaa mbalimbali bila kuathiri shughuli za uchumi na uzalishaji mali.

**Uchafuzi wa Mazingira Nchini**

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi inashirikiana na wadau kutatua changamoto za uchafuzi wa mazingira utokanao na uteketezwaji na utupwaji ovyo wa taka ngumu, utiririshaji wa majitaka na uchafuzi wa hewa unaosababishwa na mitambo ya uzalishaji viwandani na shughuli nyingine. Katika kukabiliana na changamoto hizi, viongozi wameshiriki na kuhimiza utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya 2004. Pale ambapo uvunjifu wa sheria ulibainishwa adhabu mbalimbali zilitolewa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

### Umeme Unaozalishwa Kutokana na Taka

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi ilipokea maandiko kutoka kwa watu mbalimbali waliotaka kuwekeza katika umeme unaozalishwa kwa kutumia taka ngumu. Kwa kuwa suala hili linahusu Wizara na sekta mbalimbali, ikiwemo TAMISEMI, Wizara ya Nishati na Madini, TANESCO, EWURA na wengineo, hakukuwa na mafanikio katika utekelezaji wa miradi hii ambayo ingesaidia kupunguza tatizo la taka katika miji yetu, ingeweza kuwapatia ajira vijana wengi lakini pia kuongeza uzalishaji wa umeme nchini. Katika mwaka ujao wa fedha, Ofisi, baada ya kikao cha mashauriano wa wadau wote husika, imepanga kutoa Mwongozo wa Uwekezaji wa Umeme Unaotokana na Taka Ngumu utakaorahisisha na kuharakisha uwekezaji kwenye eneo hili.

### Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na Itifaki ya Kyoto

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali imekamilisha hatua za mwisho za kuuleta Bungeni Mkataba wa Paris wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge lako tukufu. Wakati huo huo, Ofisi imeanza maandalizi ya Mpango wa Taifa wa muda mrefu wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*National Adaptation Plan -NAP*) kwa kukusanya maoni ya wadau katika kanda zote nchini. Mpango huu unalenga kuweka na kuanza kutekeleza vipaumbele vya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi inatekeleza miradi miwili mikubwa ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii za Pwani Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi ambao unatekelezwa kwa kushirikiana na wilaya za Pangani, Rufiji, Bagamoyo, Mkoani (Pemba) na Mjini (Unguja) ili kunusuru maeneo hayo na kuongezeka kwa kina cha bahari. Mradi mwingine ni wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi unaotekelezwa katika wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni katika mkoa wa Dar es salaam.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi inaandaa miradi ya kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo. Miradi hiyo ni: Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Vijijini (*Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience*); Mradi wa Kujiandaa Kutumia Fursa Zilizoko katika Mfuko wa Kuhimili na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund Readiness project-GCF)*; Mradi wa Kukabiliana na Kasi ya Uharibifu wa Ardhi na Kuongeza Upatikanaji wa Chakula katika Maeneo Kame Nchini (*Reversing Land Degradation Trends and Increasing Food Security in Degraded Ecosystems of Semi-arid Areas of Tanzania*); Mradi wa Kurejesha Ubora wa Mifumo ya Haidrolojia ili kupambana na uharibifu wa ardhi unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi (*Developing Hydrological Corridor Program to Address Land Degradation and Climate Change Issues;* na Mradi wa kujenga uwezo wa kitaasisi katika kuhuisha taarifa za mabadiliko ya tabianchi kwenye usimamizi wa mipango ya maendeleo (*Capacity enhancement for policy makers and support institutions for climate information generation, management and integration into development plans and programmes*). Miradi hii itatekelezwa katika maeneo mbalimbali ya majimbo yetu na itakapokamilika, Ofisi italijulisha Bunge lako tukufu na Waheshimiwa Wabunge kuhusu miradi itakayotekelezwa katika maeneo yao.

34. ***Mheshimiwa Spika***, ninayo furaha kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi iliweza kufanikisha upatikanaji wa jumla ya shilingi bilioni 230 zitakazotumika katika Mradi wa Maji Simiyu kama sehemu ya mkakati wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Katika mwaka ujao wa fedha, Ofisi itaendelea na jitihada za kutafuta fedha za miradi mikubwa ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta za uzalishaji mali na huduma za jamii.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi iliyopo, kukamilisha miradi inayoandaliwa na kuandaa mapendekezo mapya ya miradi ili kuhakikisha kwamba

Tanzania inanusuru mazingira yake na kufaidika na fursa zinazotokana na Mkataba wa Mabadiliko yaTabianchi ikiwa ni pamoja na Itifaki ya Kyoto.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi ilianza maandalizi ya kuishirikisha sekta binafsi hapa nchini katika kupata ithibati (accreditation) na utambulisho na kujenga uwezo wa kuandika, kutafuta fedha na kufadhili miradi ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kutoka katika mifuko mbalimbali duniani. Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Ofisi itakaa na taasisi za sekta hapa nchini ili kuzisaidia kuhusu mbinu za kuzifikia fursa za fedha za mazingira katika mifuko mbalimbali ya mazingira duniani inayotoa fedha mahsusi kwa sekta binafsi katika nchi mbalimbali.

**Mkataba wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katikamwaka 2016/17, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kukabiliana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame nchini. Miradi miwili inatekelezwa chini ya Mkataba huu. Miradi hiyo ni:- Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Maji katika Mto Zigi na Ruvu wenye lengo la usimamizi endelevu wa vyanzo vya maji naMradi wa Kuhuisha Usimamizi Endelevu wa Misitu ya Miombo ya Magharibi unaotekelezwa katika mikoa ya Tabora na Katavi kwa lengo la kuhifadhi mazingira na kuboresha maisha ya jamii. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba huu.

**Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai**

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Mkataba huu una malengo ya: Kuhifadhi bioanuai; Kuwa na matumizi endelevu ya bioanuai; na kuwa na mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na rasilimali za kijenetiki. Katika kutekeleza shughuli za Mkataba kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi imechapisha na kusambaza Taarifa ya Tano ya utekelezaji

wa Mkataba na Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai wa mwaka 2015 - 2020 kwa ajili ya utekelezaji katika Wizara na mikoa yote.

39. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi inatarajia kukamilisha taratibu za kuridhia Itifaki ya Nagoya inayohusu upatikanaji na mgawanyo sahihi wa faida zitokanazo na matumizi yya rasilimali za kijenetiki na Itifaki ya Ziada ya Nagoya Kuala-Lumpur inayohusu uwajibikaji kisheria na fidia dhidi ya athari zitokanazo na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa. Aidha, Ofisi itaandaa Mwongozo wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa ili kusimamia matumizi salama ya teknolojia hii nchini. Vilevile, itaendelea kukuza uelewa kwa wananchi, wataalam na watendaji kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa utafiti wa nje ya maabara.

**Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi na Uendelezaji Wa Mazingira na Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi**

40. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kulifahamisha Bunge lako kuwa Serikali imepitisha marekebisho ya Mkataba wa Nairobi na Itifaki yake ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi Kutokana na Vyanzo na Shughuli Zinazofanyika Nchi Kavu. Katika mwaka wa fedha wa 2017/18 Ofisi itaendelea kufuatilia ukamilishaji wa taratibu za kuridhia marekebisho ya Mkataba wa Nairobi na Itifaki yake.

**Mkataba wa Stockholm kuhusu udhibiti wa kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu**

41. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2016/17, Ofisi ilipitia Mpango wa Taifa wa utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm. Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kufanya utafiti kwa kushirikiana na *Tropical Pesticides Research Institute*- (TPRI) na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine - (SUA) kuhusu matumizi ya mimea katika kusafisha

maeneo yaliyochafuliwa na kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu(*phytoremediation technology*) katika Kituo cha Afya ya Mimea Tengeru, Arusha na Kituo kilichokuwa kinahifadhi na kusambaza pembejeo za kilimo kilichopo Manispaa ya Morogoro.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi itachapisha na kusambaza Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Mkataba ulioboreshwa kwa wadau na sekta muhimu nchini. Aidha, elimu itatolewa kuhusu madhara kwa afya na mazingira yanayosababishwa na kemikali zinazodhibitiwa na Mkataba huu.

**Mkataba wa Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Hewa ya Ozoni**

43. ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa shughuli za kupunguza na kusitisha matumizi ya kemikali zinazoharibu tabaka la hewa ya Ozoni na kukuza matumizi ya kemikali na teknolojia mbadala ambazo ni salama kwa mazingira kwa kuzingatia makubaliano ya Mkataba. Aidha, katikakuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni tarehe 16 Septemba, 2016 nilitoa tamko kupitia vyombo vya habari kuwakumbusha wananchi kuhusu tabaka la Ozoni, faida zake, madhara ya kuharibika kwa tabaka hili na matumizi ya bidhaa zenye kemikali rafiki kwa tabaka la Ozoni. Katika mwaka 2017/18, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba huu.

**Mkataba wa Basel na Mkataba wa Bamako Kuhusu Udhibiti wa Taka za Sumu**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba huu unaohusu udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka za sumu baina ya nchi na nchi na Mkataba wa Bamako unaozuia uingizaji wa taka za sumu barani Afrika. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi kwa kushirikiana na sekta ya Usafirishaji, Mawasiliano na Hali ya hewa (*Transport, Communication and Meterology - TCM)*ya Afrika ya Mashariki

iliandaa rasimu ya Mkakati wa usimamizi taka za kielektroniki katika kanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la Mkakati huu ni kusimamia na kudhibiti ongezeko la taka za kielektroniki zinazozalishwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya vifaa vya umeme na kieletroniki katika mawasiliano.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupunguza taka hatarishi za kieletroniki nchini, Ofisi ilitoa kibali kwa kampuni ya OK Plast ya Dar es Salaam kusafirisha tani 200 za taka hatarishi za vifaa chakavu vya kielektroniki vya kompyuta na simu za mkononi vilivyokusanywa nchini ili vipelekwe Ubelgiji kwa ajili ya urejelezaji na utupaji kwa njia salama.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi itaendelea kuratibu mikataba ya Basel na Bamako na kushirikiana katika nyanja za teknolojia rafiki katika usimamizi wa taka hatarishi. Aidha, Ofisi itakusanya maoni zaidi kutoka kwa wadau ili kukamilisha kanuni za usimamizi wa taka sumu za vifaa vya umeme na elektroniki na kuelimisha umma kuhusu matumizi ya kanuni hizi.

**Mkataba wa Minamata Kuhusu Udhibiti wa Matumizi ya Zebaki**

47. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi imeendelea kuratibu maandalizi ya kuridhia Mkataba wa Minamata Kuhusu Udhibiti wa Matumizi ya Zebaki ili kuondoa athari zitokanazo na kemikali hiyo. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi inaendelea kufanya tathmini ya awali ya matumizi ya zebaki itakayowezesha Serikali kuridhia Mkataba huu. Vilevile,Ofisi inaandaa Mpango-Kazi wa kitaifa wa kupunguza matumizi ya zebaki nchini. Katika mwaka 2017/18, Ofisi itaendelea kukamilisha taratibu za kuridhia Mkataba huu.

**Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*Global Enviroment Facility – GEF*)**

48. ***Mheshimiwa Spika,***katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi imekamilisha mawasilisho ya miradi

minneambayo imekidhi vigezo vya kufadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia. Hivyo, jumla ya miradi tisa iliyowasilishwa GEF imepata kibali cha kupatiwa ufadhili. Miradi hiyo inahusu hifadhi ya bioanuai, kuhimili mabadiliko ya tabianchi na usimamizi endelevu wa ardhi ambayo itatekelezwa na sekta na taasisi zilizoandaa maandiko. Vilevile, katika kipindi hicho, Ofisi imeendelea kushauri vikundi vya kijamii vipatavyo 53, kuhusu uandishi wa miradi midogo ili viweze kunufaika na ufadhili wa GEF. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi itaendelea kuratibu maandalizi na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya GEF hapa nchini.

**Mpango waKuokoa Mfumo Ikolojia ya Bonde la MtoRuaha Mkuu**

49. ***Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha 2016/17, nilifanya ziara katika mikoa kumi na nne kuhimiza utunzaji wa mazingira, ikiwemo hifadhi ya vyanzo vya maji,maziwa, mito na mabwawa. Maeneo mengi yameharibika na mengine kina cha maji kimepungua au yako hatarini kutoweka. Endapo hatua za makusudi hazitachukuliwa maziwa, mito na mabwawa tunayoyategemea kiuchumi na ustawi wa kijamii yatakauka kama sio kutoweka kabisa.

50. ***Mheshimiwa Spika*,** Ofisi imechukua hatua za kuokoa Mfumo Ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Bonde la mto huu hutegemewa katika shughuli za kilimo, uvuvi, uzalishaji wa nishati ya umeme, utalii na mifugo. Bonde hili limeonekana kuharibika na mtiririko wa maji yake kupungua na kuathiri shughuli za kiuchumi za wananchi katika wilaya zaidi ya 12 na pia uzalishaji wa umeme katika mabwawa ya Mtera na Kidatu na kuathiri bioanuai.

51. ***Mheshimiwa Spika*,**ninapenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba, tarehe 11 Aprili, 2017 Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Kikozi Kazi cha Kitaifa chaKuokoa Mfumo Ikolojia wa Bonde la Mto Ruaha Mkuuna kutoa maelekezo yake ya kazi hiyo. Kikosi Kazi hicho kinajumuisha wataalam na watendaji wa sekta zote husika

ili kuhakikisha kuwa sekta zote zenye maslahi au mamlaka katika bonde hilo kwa pamojazinakuchukua hatua za pamoja, endelevu na kwa haraka kunusuru maisha na ustawi wa Watanzania zadi ya milioni sita wanaotegemea Bonde hilo kwakuuwezesha mto kurudi katika hali yake ya utiririshaji wa maji kwa mwaka mzima.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi pia imechukua hatua ya kuokoa Bonde la Mto Katuma lililopo katika Mkoa wa Katavi ambalo lilikuwa linakabiliwa na changamoto za kukauka maji, hivyo kusababisha mgogoro wa kugombea maji kati ya wakulima, wafugaji na Hifadhi ya Taifa ya Katavi. Binafsi, katika ziara yangu kwenye Bonde hilo, nilishuhudia wanyama, hasa viboko, wakiwa wanakufa kwa kukosa maji. Baada ya ziara yangu hiyo, Ofisi yetu ilitoa maelekezo kwa uongozi wa Mkoa kuhakikisha kuwa michepusho na makingio zaidi ya 40 yaliyojengwa katika mto huo kinyume cha sheria yanabomolewa haraka na mtiririko wa maji wa mto unarejea katika hali yake ya kawaida. Maelekezo haya yalifanyiwa kazi na Mto huo sasa unatiririsha maji kama kawaida.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka ujao wa fedha, Ofisi itaandaa mradi mahsusi wa kuokoa mazingira ya maziwa madogo madogo nchini, ikiwemo Jipe, Chala, Manyara, Natron, Eyasi, Rukwa na mengineyo; mifumo-ikolojia ya mito mikubwa, ikiwemo Ruaha Mkuu, Wami, Songwe na Ruvuma na mabwawa muhimu ya kitaifa, ikiwemo Mtera, Kidatu, Kihansi na Nyumba ya Mungu.

**Kutangaza Maeneo ya Mazingira-Lindwa na Tengefu**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi ilianza taratibu za kuyatangaza baadhi ya maeneo nyeti na muhimu kwa mazingira na ikolojia nchini mwetu, ikiwemo maeneo ya haya maziwa, ambayo hayana ulinzi wa Sheria nyingine za nchi, kama Maeneo ya Mazingira Lindwa (*Enviromentally Sensitive Areas*) na maeneo ya Mazingira Tengefu (*Environmental Protected Areas*), kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004. Katika mwaka

wa fedha wa 2017/18, Ofisi inategemea kukamilisha taratibu hizi na kuyatangaza maeneo kadhaa, ikiwemo baadhi ya maeneo ya maziwa na mabwawa na vyanzo muhimu vya maji, katika Gazeti la Serikali (*Government Notice*) na kuyapa nguvu ya ulinzi wa kisheria wa mazingira.

### Udhibiti wa Matumizi ya Mkaa

55. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyogusia hapa awali, ni dhahiri kwamba matumizi ya mkaa yanachangia kwa sehemu kubwa katika kuteketeza misitu yetu na kuharibu vyanzo vya maji. Mbaya zaidi, sehemu kubwa ya mkaa unaotengenezwa nchini mwetu unasafirishwa kwenda nchi jirani na hatimaye kupekelekwa Uarabuni kwa ajili ya kuchomea nyama. Katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi ilichukua uongozi katika suala la matumizi ya nishati ya mkaa. Ofisi iliandaa kongamano kubwa la wadau mbalimbali wa sekta ya mkaa, ikiwemo Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Nishati na Madini, Wakala wa Taifa wa Misitu (TFS), makampuni yanayouza gesi ya kupikia na wajasiriamali wanaotengeneza mkaa mbadala nchini.

Ofisi pia imetoa maelekezo kwa Wizara ya Nishati na Madini kukamilisha Mkakati wa Nishati ya Tungamotaka (*National Biomass Energy Strategy*) na pia kuandaa Sera ya Taifa ya Nishati ya Tungamotaka (*National Biomass Energy Policy*). Katika mwaka ujao wa fedha, Ofisi, baada ya mashauriano na wadau wengine, itatoa Mwongozo wa Kitaifa wa Udhibiti wa Matumizi ya Nishati ya Mkaa. Mwongozo huu unatarajiwa kutoa mwelekeo (*roadmap*) wa kuondokana na matumizi ya mkaa nchini. Vilevile, Ofisi itaendesha shindano la ubunifu wa matumizi ya nishati mbadala wa mkaa ambapo washindi watawezeshwa kwa mitaji na maarifa ya kukuza ubunifu na biashara zao ili ziweze kushindana na mkaa.

### Udhibiti wa Mimea-Vamizi

56. ***Mheshimiwa Spika,*** rasimu ya Sera mpya ya Taifa ya Mazingira imebainisha Mimea-Vamizi (*Invasive Alien*

*Species*) kama janga kubwa la kimazingira linalolinyemelea taifa letu. Katika maeneo mengi ya nchi yetu, malisho ya mifugo na wanyamapori yanavamiwa na mimea hii na hivyo kupunguza maeneo ya kufugia na kulishia wanyamapori. Kutokana na kuenea kwa kasi kwa mimea hii, Hifadhi ya Ngorongoro ipo hatarini kutoweka kwani takribani theluthi moja ya eneo la shimo (*crater*), ambapo ndipo wanyama wanapata malisho yao, limevamiwa na eneo zaidi linaendelea kuvamiwa. Katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi ilishughulika na suala hili kwa kuelekeza kuundwa kwa kikosi cha wanasayansi magwiji kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, na waikolojia kutoka katika taasisi mbalimbali kukutana na kupendekeza hatua za haraka za kisayansi kukabiliana na janga hili.

**II: BARAZA LA TAIFA LA HIFADHINA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

57. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ni msimamizi mkuu wa uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira,Sura ya 191. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

**Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira**

58. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/17, Baraza limeendelea kusimamia na kutekeleza shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake kwa kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi/ taasisi728. Miradi/taasisi hizo ni viwanda, migodi, majengo, miundombinu ya kutibu majitaka, taka ngumu na taka dutu, machinjio, hospitali na vituo vya afya, masoko, mashamba, mitambo ya gesi na mafuta, vituo vya mafuta, hoteli, vyanzo vya maji na kambi ya wakimbizi.

59. ***Mheshimiwa Spika***, miradi 237iliyosababisha uchafuzi wa mazingira, ilichukuliwa hatua stahiki ikiwa ni

pamoja na: kupewa onyo, kutozwa faini, kupewa amri za kutimiza masharti ya mazingira, amri za katazo, amri za urejeshwaji wa mazingira, amri za kuzuia kutekeleza shughuli zenye madhara makubwa kwa mazingira na wahusika kushtakiwa mahakamani. Katika kuboresha ukaguzi wa mazingira na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Wakaguzi wa Mazingira 435wamependekezwa kutoka katika mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi za umma kwa ajili ya uteuzi utakaofanywa na Waziri mwenye dhamana ya mazingira. Uteuzi wa Wakaguzi hawa wapya wa Mazingira utaongeza uwezo wa Serikali kusimamia hifadhi ya mazingira nchini. Mafunzo kwa wakaguzi hao yatatolewa katika mwaka wa fedha 2017/18.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Ofisi iliomba na kupatiwa Wanasheria Waandamizi watatu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao waliongeza uwezo wa Baraza kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Baraza litaongeza uwezo na jitihada za kuadhibu vitendo vya uharibifu wa mazingira nchini, ikiwemo kuwapeleka mahakamani waharibifu wa mazingira.

61. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2016/17, Baraza limepokea malalamiko 572kutoka kwa wananchi kuhusu uchafuzi wa mazingira. Malalamiko hayo ni pamoja na utiririshaji wa majitaka nakuyaelekeza kwenye mazingira, vyanzo vya maji na mifumo ya maji ya mvua; utupaji holela wa taka dutu na ngumu kutoka kwenye makazi ya watu, migodi, hoteli na viwanda; umwagiliaji wa bustani kwa kutumia majitaka; utupaji taka holela kwenye makazi ya watu; uchimbaji wa mchanga katika mito, maeneo yasiyo rasmi na maeneo ya karibu na madaraja; kelele kutoka viwandani, maeneo ya starehe, migodini, matangazo ya biashara, vyombo vya usafiri, na nyumba za ibada; na vumbi na moshi toka viwandani na kwenye hifadhi za makaa ya mawe. Katika kukabiliana na malalamiko hayo, mamlaka mbalimbali zilishirikishwa kuchukuahatua stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake. Katika mwaka ujao wa fedha, Ofisi itaweka utaratibu rahisi wa

wananchi kutambua, kuripoti na kuchukua hatua juu ya vitendo vya uharibifu wa mazingira.

62. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamekusanya na kuteketeza tani 200.8 na mita za ujazo 973,752zataka dutu kutoka maeneo saba ambayo ni makampuni binafsi mawili, kituo cha mafuta, benki, vituo vya afya, mgodi pamoja na Mamlaka ya Chakula naDawa. Vilevile, maombi 48 ya ukusanyaji na usafirishaji wa vyuma chakavu, mafuta machafu, betri chakavu na vifaa vya umeme yalipokelewa, ambapo vibali 12 vilitolewa.Katika mwaka wa fedha 2017/18, Baraza litaendelea kusimamia uzingatiaji wa Sheria kwa kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi ya uwekezaji na kuchukua hatua stahiki kwa watakaokiuka Sheria yaMazingira na Kanuni zake.Baraza pia litaweka mkakati wa kuhuisha hifadhi ya mazingira katika mipango na mikakati inayohusu uendelezaji wa viwanda nchini.

**Tathmini ya Athari kwa Mazingira – TAM**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya miradi 1,058 ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa mchakato wa kupata hati za TAM. Katika kipindi hiki, miradi 475 imepata hati za TAM baada ya kukamilisha mchakato. Vilevile, Baraza lilisajili wataalamu binafsi 139na makampuni 26 kwa ajili ya kufanya TAM na ukaguzi wa mazingira, kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa. Hadi kufikia Januari, 2017, Baraza limesajili wataalamu elekezi wa mazingira 1,000 na makampuni 210. Baraza liliandaa mkutano wa wataalamu elekezi ili kuweka mikakati ya kuboresha taarifa za TAM na hivyo kusaidia kupunguza muda wa uhakiki wa taarifa hizo. Aidha, Baraza limepeleka Ofisa wake katika Kituo cha Uwekezaji (*Tanzania Investment Centre*) ili kutoa elimu kwa wawekezaji kuhusu mchakato wa TAM kwa lengo la kupunguza urasimu.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi ililielekeza Baraza kutengeneza mkakati wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu

wa Hesabu za Serikali (CAG)aliyoyatoa kuhusu kuboresha zoezi la mchakato TAM na kujenga uwezo wa Baraza kukagua miradi ya utafutaji wa uchimbaji wa gesi na mafuta nchini. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaelekeza nguvu na kuchukua hatua mahsusi za kuharakisha na kurahisisha mchakato wa kupata vyeti vya TAM ili kuondoa uwezekano wa mchakato huo kuwa kikwazo cha uwekezaji, ikiwemo kwenye sekta ya viwanda, nchini.

65. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limekamilisha mfumo wa kanzidata wa kuhifadhi taarifa za miradi iliyofanyiwa TAM na ukaguzi. Aidha, Baraza limehamishia shughuli za usajili wa miradi midogo ikiwemo vituo vya mafuta, majengo, minara ya mawasiliano, barabara za halmashauri na uchimbaji mdogo kwenye ofisi zake za kanda zilizopo katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Dar es Salaam, Mtwara na Mbeyaili kupunguza gharama na muda wa mchakato wa TAM.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Baraza litaendelea kufanya mapitio ya taarifa za TAM na taarifa za ukaguzi wa mazingira kwa miradi ya uwekezaji. Baraza litaendelea kusajili na kufuatilia utendaji wa wataalam (*environmental experts*) na kampuni za utaalam wa mazingira ili kuleta ufanisi katika mchakato wa TAM. Aidha, Baraza litaendelea kujenga uwezo wa Maafisa Mazingira wa Halmashauri katika kusimamia mchakato wa TAM.

### Elimu kwa Umma Kuhusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi kwa kushirikiana na Barazailiendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira. Katika kipindi hicho, matangazo maalum matatu kwenye televisheni na redio yalitolewa ili kuelimisha jamii kuhusu athari zitokanazo na vifungashio vya plastiki na azma ya Serikali ya kupiga marufuku uingizaji, uuzaji, utengenezaji na utumiaji wa mifuko hiyo kama vifungashio vya bidhaa. Kadhalika,

nakala 16,000za vibonzo na 7,000 za stika (*stickers*) zilichapishwa zenye ujumbe wa kuhamasisha jamii kuhusu athari za mifuko ya plastiki na kusambazwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro na Pwani. Ofisi pia iliandaa warsha kwa lengo la kukuza weledi kuhusu uzingatiaji, utekelezaji na ukusanyaji wa taarifa za mazingira kwa:- Wakuu wa mikoa ya Kanda ya Ziwa; Viongozi wa Manispaa za Dodoma, Arusha, Mbeya pamoja na Halmashauri za Lindi, Kilwa na Mtwara.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ilitoa pia elimu kwa wadau walioshiriki katika wiki maalum ya maonesho ya viwanda yaliyofanyika katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere (Saba Saba) Dar es salaam. Katika maonesho hayo Ofisi ilielimisha washiriki kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kwa miradi kama ya viwanda, majengo, barabara na shughuli nyinginezo za uwekezaji. Aidha, nakala 2,500 za vipeperushi zilizohusu hatua zinazopaswa kuzingatiwa na wawekezaji katika Tathmini ya Athari kwa Mazingira na 3,200 zilizohusu athari zinazosababishwa na matumizi ya mifuko ya plastiki party zaligawiwa kwa washiriki.

69. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi iliandaa ziara za mafunzo zilizojumuisha watendaji na viongozi wakuuwa Ofisi, ambapo walitembelea mikoa 18. Ziara hizi zilitumika kufanya mikutano ya kueneza elimu ya uhifadhi na kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali kama njia ya kupunguza uharibifu wa mazingira.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka wa fedha 2016/17 elimu kuhusu mazingira ilitolewa pia kupitia tamko la maadhimisho ya Siku ya Mazingira Afrika iliyofanyika tarehe 3 Machi 2017. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu kimataifa yatakuwa nchini Kanada na kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni “Mahusiano Endelevu Kati ya Binadamu na Mazingira” (*Connecting People to Nature*). Kitaifa siku hii itaadhimishwa mkoani Mara na Kaulimbiu yetu ni “Hifadhi ya Mazingira: Mhimili kwa Tanzania ya Viwanda”. Hivyo,

tuungane sote kuhamasishaujenzi wa viwanda na ukuaji wa uchumiunaozingatia hifadhi ya mazingira.

71. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwenye taasisi za elimu, watendaji katika ngazi za mikoa, wilaya na Wakaguzi wa Mazingira ili kuendeleza dhana na suala zima la ufuatiliaji, uzingatiaji na utekelezaji wa sheria, hivyo kuendeleza hifadhi ya mazingira nchini.

**Mipango na Utafiti wa Mazingira**

72. ***Mheshimiwa Spika***,katika mwaka wa fedha 2016/17,Baraza limeendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira *(National Environmental Research Agenda - NERA).* Katika kipindi hiki, Baraza lilikamilisha mapitio ya NERA ya zamani na kuandaa NERA mpya ya mwaka 2017 – 2022 ambayo itachapishwa mwezi Mei, 2017.Vilevile, Baraza limetayarisha ripoti, miongozo na nyaraka za usimamizi wa miradi na kuiwasilisha kwa jopo linalolifanyia Baraza ithibati(*accreditation panel*) ili kuwa taasisi ya kitaifa ya kutekeleza mpango wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi *(National Implementing Entity for Adaptation Fund - NIE*). Hatua hii italiwezesha Baraza na taifa kwa ujumla kuwa na uwezo wa kutafuta na kupata fedha kwa ajili ya miradi ya hifadhi ya mazingira nchini.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17, Baraza limeendelea kuratibu shughuli zinazofanywa na Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Kusimamia na Kuhifadhi Matumbawe *(National Coral Reef Task Force).* Kikosi kazi kwa kushirikiana na wadau katika sekta mbalimbali walifanya tafiti na kubaini uharibifu mkubwa wa matumbawe. Kikosi hiki kiliandaa ripoti ya kitaalamu kama mchango wa taifa katika Ripoti Kuu ya Dunia inayohusu hali ya matumbawe.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17, Baraza limeandaa maandiko ya miradi ya kuhifadhi mazingira mbalimbali ikiwa ni pamoja na andiko la mradi wa kuhifadhi Bonde la Mto Katuma, lililopo Mkoani Katavi;

na dhana dokezi (*concept notes)*tano kwa ajili ya kupata fedha za kuitekeleza. Baraza limeendelea kufanya tafiti zinazolenga kutatua matatizo ya mazingira yaliyojitokeza na kuripotiwa na wadau nchini. Aidha, Baraza lilifanya tathmini ya mazingira katika maeneo ya mabonde ya mito Mbori na Mzase na mradi wa umwagiliaji wa Msagali Wilayani Mpwapwa; Bonde la Mto Katuma, lililopo Wilaya ya Mpanda; na Ziwa Chala, Wilaya ya Rombo. Vilevile, Baraza lilifanya utafiti kuhusu tatizo la mmomonyoko wa fukwe katika eneo la Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, (TaSuBa) wilayani Bagamoyo na kutoa ushauri wa kitaalam wa kutatua tatizo hilo.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kuratibu shughuli za Hifadhi Hai nne za Dunia ambazo ni Serengeti–Ngorongoro, Ziwa Manyara, Usambara Mashariki na Jozani Chwaka Bay iliyopo Zanzibar. Aidha, Baraza liliandaa taarifa kuhusu hali halisi ya bioanuai, watu na mazingira katika Hifadhi Hai na kuwasilisha makao makuu ya *Biosphere Reserves* nchini Ufaransa. Vilevile, katika kipindi hiki Baraza lilipokea na kukabidhi cheti cha Hifadhi Hai ya Jozani Chwaka Bay kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Baraza limeendelea na mchakato wa kuiingiza Hifadhi ya Taifa ya Saadani katika Mtandao wa Hifadhi Hai wa Dunia *(World Network of Biosphere Reserves).*

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kufanya tathmini na ufuatiliaji wa mwenendo wa mazingira ya pwani na rasilimali zake za asili katika mikoa minne ambayo ni Mtwara, Lindi, Tanga, na Pwani ili kubaini changamoto mbalimbali za mazingira na kupanga mikakati ya kuzitatua.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/18 Baraza litaendeleakutekeleza yafuatayo:- Kuratibu na kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira (NERA 2017 – 2022);kukamilisha mchakato wa kuwa taasisi ya kitaifa ya kutekeleza mpango wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi;kuandaa maandiko ya miradi ya kuhifadhi mazingira na kuwasilisha kwa wafadhili;Kuratibu shughuli za

Hifadhi Hai;kufanya utafiti, tathmini na ufuatiliajiwa mwenendo wa mazingira; na kuanzisha Maeneo Tengefu ya Mazingira *(Environmental Protected Areas –EPAs).*

### Uratibu wa Miradi ya Kuhifadhi Mazingira

78. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa fedha 2016/17, Baraza limesimamia utekelezaji wa miradi minne kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo. Miradi hiyo ni:-

#### a) Mradi wa Kuhifadhi Lindimaji la Bonde la Kihansi na Dakio Lake

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa Kuhifadhi Lindimaji la Bonde la Kihansi na Dakio Lake *(Kihansi Catchment Conservation Management Project - KCCMP*) unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(Global Environment Facility - GEF).* Katika mwaka wa fedha 2016/17,mradi ulitekeleza shughuli zake za usimamizi wa rasilimali maji, hifadhi ya bioanuai, na shughuli za miradi ya kijamii kwenye vijiji 22 vilivyoko wilaya za Kilolo, Mufindi na Kilombero. Miradi hii ambayo inalenga kutekeleza mpango usimamizi husishi wa matumizi bora ya viuatilifu na visumbufu *(Integrated Pest Management – IPM*), utunzaji wa vyanzo vya maji na mafunzo ya matumizi sahihi ya viuatilifu, na kutoa elimu ya mazingira kwa ujumla.

80. ***Mheshimiwa Spika***, mradi umeendelea kutekeleza mpango wa ufuatiliaji wa Ikolojia ya Bonde la Kihansi ikiwemo kutunza vyura kwenye maabara na kuwarejesha kwenye makazi yao ya asili. Jumla ya vyura walioko kwenye maabara za Tanzania ni 3,049 na maabara za Marekani ni 5,564. Aidha, kuanzia mwezi Oktoba, 2012 hadi Desemba, 2016 jumla ya vyura 8,082 wamerejeshwa kwenye korongo la Kihansi. Sensa ya mwezi Februari, 2017 inaonesha takribani vyura 1,300 walionekana kwenye korongo la Kihansi. Hata hivyo vyura hao wanakabiliwa na changamoto kama vile magonjwa na maadui *(predators)*. Mradi unaendelea na tafiti za bioanuai nyingine ndwele ikiwemo kahawa pori (*wild coffee*) na vipepeo.

81. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeanza mchakato wa kuanzisha Maeneo Tengefu ya Mazingira *(Environmental Protected Areas –EPAs).* Hatua za awali za kulitangaza eneo la Kihansi kuwa eneo tengefu *(gazettement),* ikiwa ni pamoja na kufanya thathmini ya mazingira; kufanya mashauriano ya awali na wadau husika na pia kuandaa dhana-dokezi ya kuanzisha *'Kihansi Environmental Protected Areas –KEPA'* tayari zimekamilika na zoezi hili linatazamiwa kumalizika ifikapo mwezi Juni, 2017

82. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza kwa kushirikiana na Ofisi ya Bonde la Maji Rufiji linaratibu shughuli za usimamizi wa rasilimali maji katika bonde hilo ambapo vyanzo vya maji 906 vimeanishwa na kuwekewa mpango wa utunzaji. Mradi pia unaendelea na tathmini ya mahitaji ya maji kwa ajili ya mazingira.

### b) Mradi wa Mafuta kwa Maendeleo

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Mafuta kwa Maendeleo (*Oil for Development*) unafadhiliwa na Serikali ya Norway na kutekelezwa kwa ushirikiano na Wizara ya Nishati na Madini. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Baraza liliratibu ukusanyaji wa taarifa za zinazohusu mazingira katika ukanda wa bahari na kuwezesha kuwepo kwa atlasi ya awali ya mazingira ya pwani. Kupitia mradi huu watalaam kutoka sekta mbalimbali za Serikali wameendelea kujengewa uwezo katika kusimamia sekta ya mafuta na gesi. Aidha, mafunzo yametolewa kuhusu:- kukabiliana na uvujaji wa mafuta baharini endapo tatizo hili litatokea na ufuatiliaji na ukaguzi wa shughuli za utunzaji wa mazingira katika miradi ya mafuta na gesi.Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, chini ya mradi huu,mafunzo kuhusu mafuta na gesiyataendelea kutolewa kwa wadau.

### c) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Sekta ya Nishati

84. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unatekelezwa kwa fedha kutoka Benki ya Dunia na Serikali ya Kanada chini ya uratibu wa Wizara ya Nishati na Madini. Baraza kwa

kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, limekamilisha ujenzi wa maabara, ununuzi wa vifaa vya maabara na kutoa mafunzo kwa wataalamu nane wa maabara kuhusu utumiaji wa vifaa hivyo. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Baraza litaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi hii na kuandaa mafunzo ya tathmini ya athari kwa mazingira kuhusu mafuta na gesi.

## III: MASUALA YA MUUNGANO

85. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imetekeleza majukumu yake ya kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Katika mwaka wa fedha 2016/17 kazi zilizotekelezwa ni:-

### Kuondoa Changamoto za Muungano

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi imeendelea na jitihada za kuondoa changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano.Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ vimekuwa ni nyenzo muhimu ya kusaidia kupunguza changamoto za Muungano. Ofisi imeratibu vikao hivyo katika ngazi ya Makatibu Wakuu na Mawaziri wa (SMT) na (SMZ) na kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ. Vikao hivyo vilifanyika kwa mafanikio makubwa mwezi Januari , 2017 huko Zanzibar ambapo changamoto kadhaa zilipatiwa ufumbuzi.

87. ***Mheshimiwa Spika,***katika kikao hicho cha Zanzibar, na kwa sehemu kubwa katika mwaka wa fedha unaokwisha, changamoto za Muungano zilizoongelewa na kupatiwa ufumbuzi au kupangiwa mipango ya ufumbuzi ni pamoja na Usajili wa Vyombo vya Moto; Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha Kuhusu Utaratibu wa Kuchangia Gharama na Kugawana Mapato ya Muungano; Hisa za Zanzibar zilizokuwa kwenye Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na Gawio la Zanzibar kwenye Faida ya Benki Kuu; Ushiriki/

Ushirikishwaji wa Zanzibar kwenye Masuala ya Kimataifa ikiwemo Ziara za Viongozi wa Nje wanaotembelea Tanzania; Ushiriki/Ushirikishwaji wa Zanzibar kwenye mchakato wa bajeti ya SMT; Ushirikiano kati ya SMT na SMZ, wafanyabiashara wa Zanzibar na Bara, kwenye nyanja za uwekezaji, viwanda na biashara; utaratibu wa usajili wa meli za kigeni kwa kutumia bendera ya Tanzania; pamoja na masuala mengineyo. Kikao pia kilipokea ripoti ya utekelezaji wa masuala yaliyokwishafanyiwa maamuzi na yanayoendelea kutekelezwa.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** mwongozo wa utaratibu wa muda wa mgao wa ajira katika taasisi za Muungano umeendelea kutekelezwa. Tathmini ya utekelezaji wa mwongozo huo umefanywa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kubaini kuwa mwongozo unatekelezwa ipasavyokwa baadhi ya taasisi za Muungano kwa kuzingatia uwiano uliowekwa wa asilimia 79 kwa SMT na 21 kwa SMZ kwa ngazi ya wataalam. Aidha, katika kuwezesha utekelezaji wa haraka wa uwiano huo, Sekretarieti ya Ajira ya SMT imefungua Ofisi ShanganiZanzibar. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Ofisi itaendelea kuratibu vikao vya Wataalam, Makatibu Wakuu, Mawaziri wa SMT na SMZ na vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ pamoja na kufuatilia maagizo na utekelezaji wake.

### Utafiti, Utafutaji na Uchimbaji wa Gesi na Mafuta

89. ***Mheshimiwa Spika,***katika mwaka wa fedha uliopita, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar lilipitisha Sheria ya Gesi na Mafuta, na Rais wa Zanzibar aliiridhia, ikiwa ni matokeo ya maridhiano kati ya pande mbili za Muungano kuhusu masuala ya utafiti, utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta, maridhiano yaliyoliondoa suala hili kwenye orodha ya changamoto za Muungano. Katika mwaka unaoisha, Ofisi iliratibu mashirikiano na mahusiano kati ya taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuwezesha suala hili kukamilika. Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Ofisi itaendelea kuratibu

mashirikiano yatakayoiwezesha Zanzibar kujenga uwezo na kunufaika katika shughuli za uchimbaji wa gesi na mafuta.

**Uratibu wa masuala ya kiuchumi na kijamii**

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imefuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya pamoja inayotekelezwa pande mbili za Muungano. Baadhi ya miradi hiyo ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund* - TASAF III);Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA);Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini *(Market Infrastracture, Value Addition and Rural Finance* - MIVARF);na Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*South-West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth –SWIOFISH*). Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

91. **Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF III**

92. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la mfuko huu ni kunusuru kaya maskini kwa kuziwezesha kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu. Katika mwaka 2016/17 kazi zilizofanyika ni uhaulishaji wa fedha; miradi ya kutoa ajira za muda kwa kaya maskini; miradi ya kuendeleza miundombinu; teknolojia ya habari na mawasiliano; mpango wa kuweka akiba; mafunzo ya sera za kulinda mazingira na jamii; na kujenga uwezo wa watendaji. Hadi kufikia mwezi Januari, 2017 fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu ni shilingi206,715,956,369/=. Kati ya fedha hizo,shilingi 199,308,145,701/= zimepelekwa SMT na shilingi 7,407,810,668/ = zilipokelewa naSMZ.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** mfuko huu umekuwa na mafanikio kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Ruzuku zilizotolewa zimewasaidia walengwa kupata mahitaji ya msingi yakiwemo chakula, vifaa vya shule kwa watoto wao pamoja na kuanzisha miradi midogo midogo ya kujiongezea kipato.

**a) Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Kifedha Vijijini**

94. ***Mheshimiwa Spika,***programu hii (*Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural FinanceSupport Programme* - MIVARF) imelenga kuimarisha maendeleo ya kilimo kupitia:- uanzishwaji na uendelezaji wa miundombinu ya masoko; uendelezaji na matumizi ya taaluma za kuongeza thamani; na kutanua wigo wa upatikanaji wa huduma za kifedha kwa ushiriki makini wa taasisi za fedha.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17 maeneo yaliyotekelezwa ni pamoja na miundombinu ya masoko, uongezaji thamani mazao, kuwajengea uwezo wananchi na kuwaunganisha na masoko, huduma za fedha vijijini na uratibu wa programu. Programu hii imeboresha maisha ya wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Aidha, kwa maeneo yanayopitiwa na barabara zilizojengwa na programu hiishughuli za kiuchumi zimeongezeka hivyo kuongeza kipato cha jamii.

**b) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

96. ***Mheshimiwa Spika,***MKURABITA umejikita katika kuandaa, kuongoza na kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kitaifa wa umiliki rasilimali na uendeshaji biashara utakaoboresha sheria, kanuni na taratibu za kijamii.Faida ya mpango huu ni kuwa na mfumo mmoja wa kisheria na kitaasisi ambao walengwa wanautumia kurasimisha rasilimali na biashara wanazomiliki ili kuzitumia kupata mitaji na kuongeza kipato. Hadi kufikia Januari,2017SMTimepokea shilingi 45,468,800/= na SMZ imepokea shilingi 41,750,667/=

**c) Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi – SWIOFISH**

97. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unatekelezwa kwa miaka sita kuanzia 2015 - 2021 na umefadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia pamoja na Mfuko wa Kimataifa wa

Maendeleo ya Kilimo. Mradi huu unashirikisha Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya SMT, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo, na Uvuvi ya ya SMZ na Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu. Lengo la mradi ni kuwawezesha wavuvi wadogo wa ukanda wa pwani kuwa na uvuvi endelevu.Aidha, hadi kufikia Machi, 2017 mradi umepokea jumla ya shilingi 2,015,332,842/= ambapo Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ya SMTimepokea shilingi 930,437,776/=, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ya SMZimepokea shilingi 476,483,504/= naMamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu imepokea shilingi 608,411,562/=.

**d) Miradi ya Tume ya Sayansi na Teknolojia**

98. ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) inatekeleza kazi zake pande mbili za Muungano. Tume inatekeleza miradi mitano huko Zanzibar. Miradi hiyo ni:- Mradi wa Kujenga Uwezo wa watafiti ambao hadi kufikia Januari, 2017mradi umepokea shilingi 41,770,000/=; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Matumizi ya Taarifa za Kimtandao katika Afya za Jamii uliopokea shilingi 43,000,000/=; Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Mpunga uliopokea shilingi 43,000,000/=; Mradi wa Kubuni Fomula ya Chakula Kitakachonenepesha Mbuzi wa Nyama umepokea shilingi 43,000,000/=; na Mradi wa Uanzishaji wa Atamizi ambao umepokea shilingi 206,000,000/=.

**Ziara za Kikazi**

99. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi imeendelea kuimarisha ushirikiano wa pande mbili kwa kufanya na kuratibu ziara za kikazi za maafisa, wataalam, watendaji na viongozi.Taasisi za Muungano zilitembelewa kwa lengo la kuona namna zinavyotekeleza majukumu yao na changamoto zinazozikabili. Taasisi hizo ni:- Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima; Tume ya Pamoja ya Fedha; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Mamlaka ya Usafiri wa Anga Nchini; Mamlaka ya Hali ya Hewa; Shirika la Simu; Shirika la Posta; Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; Baraza la Mitihani la Taifa; Tume ya Nguvu za

Atomiki; Taasisi ya Sayansi za Bahari; Benki Kuu ya Tanzania, tawi la Zanzibar; Mamlaka ya Elimu Tanzania; na Tume ya Sayansi na Teknolojia.

100. ***Mheshimiwa Spika,***Kamatiza Baraza la Wawakilishi za Mawasiliano na Ujenzi na Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa zilitembelea baadhi ya Wizara na taasisi za SMTmwezi Desemba, 2016 na Januari, 2017 kwa lengo la kujenga ushirikiano wa karibu na taasisi hizo pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais inayoratibu masuala ya Muungano.

101. ***Mheshimiwa Spika***, ziara hizo zimeonesha jitihada za makusudi za serikali zetu katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mpango-kazi wa kila taasisi ya muungano unalenga katika kuboresha hali za maisha ya wananchi kiuchumi na kijamii.

**Fedha zinazopelekwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

102. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha2016/17 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kupokea fedha kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania,ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2017 shilingi bilioni 1.4 za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na shilingi bilioni 15.75 za kodi ya mishahara - PAYE zilizopokelewa na SMZ. Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Serikali itaendelea kuratibu na kufuatilia uwepo wa utaratibu rahisi na wa haraka wa utolewaji wa fedha zinazostahili kutolewa.

**Kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano**

103. ***Mheshimiwa Spika,*** ushirikiano baina ya SMT na SMZ kwa masuala yasiyo ya Muungano umeendelea kuimarika. Serikali zetu zimekubaliana kuwa na utaratibu wa vikao vya kisekta baina ya wizara, idara na taasisi zisizo za Muungano kwa lengo la kuimarisha ushirikiano. Sekta hizo

hushirikiana katika masuala ya mafunzo, sera na ushiriki katika nyanja za kimataifa, kubadilishana ujuzi, utaalamu na uzoefu.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17 sekta zifuatazo zisizo za Muungano zilikutana kujadiliana na kuainisha maeneo ya ushirikiano:-

**a) Sekta ya Nishati**

105. ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya nishati ya SMT na SMZ zilikutana mwezi Agosti, 2016 na Oktoba, 2016 na Januari, 2017. Katika vikao hivyo, wajumbe walibadilishana uzoefu katika masuala ya utafutaji mafuta na gesi asilia, mikataba ya utafitiwa mafuta na gesi asilia maeneo ya Unguja na Pemba, mfumo wa mawasiliano baina ya Shirika la Maendeleo la Mafuta Tanzania - TPDC na Shirika litakaloundwa Zanzibar pamoja na kuainisha maeneo ya ushirikiano.

**b) Sekta ya Maji**

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17 sekta ya maji ilikutana mwezi Septemba, 2016 na kubadilishana uzoefu kuhusu ukusanyaji, utunzaji na usambazaji wa taarifa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki pamoja na safari za mafunzo na uendeshaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji.

**c) Sekta ya Utumishi na Utawala Bora**

107. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba, 2016 Ofisi ya Utumishi (SMZ)na Ofisi ya Rais, Utawala Bora (SMT)zilikutana na kukubaliana utaratibu wa vikao vya ushirikiano katika ngazi ya Makatibu Wakuu na Mawaziri na kuainisha maeneo ya mashirikiano kwa ajili ya kuandaa Hati ya Makubaliano ili kurasimisha ushirikiano wao.Aidha,katika kuimarisha ushirikiano, mwishoni mwa mwaka 2016, TAKUKURU na ZAECA zimepanua wigo wa mashirikiano ambapo rasimu ya mkataba wa mashirikiano imeandaliwa.

### d) Sekta ya Maliasili na Utalii

108. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka wa fedha 2016/17 sekta hizi zilikutana na kujadiliana kuhusu usimamizi na uendeshaji wa maliasili wanyamapori, misitu, ufugaji nyuki na malikale; mikataba ya kimataifa kuhusu usimamizi wa rasilimali za maliasili na malikale; ushirikiano kwenye nyanja ya utafiti na maendeleo; na udhibiti wa usafirishaji haramu wa mazao ya maliasili.

### e) Sekta ya Afya

109. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/17,Sekta za Afya za SMT na SMZ wamekuwa na mashirikiano katika maeneo yafuatayo:-ugomboaji na uhifadhi wa chanjo zinazofadhiliwa na shirika linalojihusisha na masuala ya chanjo (*Vaccine Alliance*); uandaaji wa ripoti ya mwaka ya mpango wa chanjo; ufuatiliaji wa magonjwa yanayozuilika kwa chanjo; kutengeneza mpango-kazi mtambuka wa kitaifa wa afua lishe; kuzuia na kudhibiti madhara ya upungufu wa madinijoto nchini; na matumizi ya matone ya vitamini A na dawa za minyoo kwa watoto wa miezi sita hadi miezi 59.

110. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi itaendelea kuhakikisha kuwa sekta zisizo za Muungano za SMT na SMZ ambazo zinashabihiana kimajukumu zinaratibiwa na kuhamasishwa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka.

### (f) Sekta ya Mazingira

111. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha unaoisha Serikali za SMT na SMZ zimeshirikiana kwa karibu katika masuala ya hifadhi ya mazingira, ikiwemo suala la kukabiliana na uvuvi haramu wa kulipua mabomu. Vilevile, ipo miradi kadhaa ya mabadiliko ya tabianchi inayotekelezwa kwa upande wa Zanzibar kwa ushiriki na ushirikiano wa wataalam kutoka upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mwaka ujao wa

fedha, Ofisi yetu, ambayo ina dhamana ya mazingira kwa upande wa Bara, itaonyesha mfano wa ushirikiano wa kina na wa dhati wa pande zote mbili za Muungano katika êneo hili.

## IV: MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI

112. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi pamoja na Baraza zimeendelea kusimamia Sheria, Kanuni, Taratibu na Maadili ya Utumishi wa Umma na kuwawezesha watumishi wake kutekeleza majukumu yao. Katika kipindi hiki jumla ya watumishi 78wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo mbalimbali ili kuwajengea uwezo na kuongeza ujuzi. Katiya hao, watumishi 49 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na 19 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuhakiki kumbukumbu za watumishi na kuziboresha kupitia mfumo wa kumbukumbu na taarifa za watumishi na mishahara *(Human Capital Management Information System*) pamoja na kutekeleza zoezi la uhakiki wa vyeti vya kitaaluma.Aidha, utendaji wa watumishi umeendelea kupimwa kwa kutumia mfumo wa wazi wa Tathmini na Upimaji waUtendaji Kazi (*Open Performance Appraisal System*).

114. ***Mheshimiwa Spika***, mwaka wa fedha 2017/ 18,Ofisi pamoja na Baraza imepanga kuwawezesha watumishi 48kuhudhuria mafunzo kwa kuzingatia mpango wa mafunzo. Aidha, Watumishi 115wanatarajiwa kupandishwa vyeo na watumishi 12 wanatarajiwa kuthibitishwa kazini kwa kuzingatia utendaji wao wa kazi na miundo inayotawala kada zao. Kumbukumbu za watumishi zitaendelea kuboreshwa kwa kutumia mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara.

115. ***Mheshimiwooa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi imeendelea kuimarisha maadili, utawala bora, demokrasia na dhana ya ushirikishwaji watumishi

mahala pa kazi, kupitia vikao vya idara na vitengo, vikao vya kamati za maadili na uadilifu, vikao vya menejimenti na vikao vya Baraza la Wafanyakazi. Aidha, sekta binafsi imeshirikishwa katika utoaji wa huduma na bidhaa katika Ofisi ili kuendeleza dhana ya ushirikishwaji wa sekta binafsi.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kutendea kazi. Aidha, majengo ya Ofisi na mazingira ya kazi yaliboreshwa kwa kufanya ukarabati kulingana na fedha zilivyopatikana.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutoa elimu mahala pa kazi kuhusu UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) kupitia Kamati ya UKIMWI na MSY. Aidha, watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI wanaendelea kupewa huduma stahiki.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** katikamwaka wa fedha 2017/18, Ofisi itaendelea kusimamia Sheria, Kanuni, Taratibu na kuimarisha maadili na utawala bora katika utumishi wa umma. Aidha, Ofisi itaendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya UKIMWI na MSY, ushauri nasaha, na kupima afya za watumishi kwa hiari na kuwapatia huduma zinazostahili kwa watakaojitokeza na kuthibitika kuwa na Virusi vya UKIMWI.

**Serikali Kuhamia Dodoma**

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako tukufu litakumbuka kwambawakati akihutubia katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi tarehe 23 Julai, 2016, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli**,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa uamuzi wa kutekeleza azma ya kuhamishia shughuli za Serikali katika Mji Mkuu Dodoma. Ofisi yetu imetekeleza kwa vitendo maamuzi haya kwa kuwahamisha viongozi wakuu pamoja na baadhi ya watumishi katika awamu ya kwanza. Aidha, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)limenunua kiwanja eneo la Ndejengwa- Manispaa ya Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa ofisi zake.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/18 Ofisi inatarajia kuendelea na utekelezaji wa mpango wa kuhamia makao Makuu Dodoma ambapo inatarajia kuhamisha watumishi katika awamu ya pili na awamu ya tatu kwa kuzingatia ratiba iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

## C: SHUKRANI NA HITIMISHO

121. ***Mheshimiwa Spika,*** kama tunavyoelewa nchi yetu ni ya Muungano. Muungano wetu una umuhimu wa pekee kwa Taifa letu na umekuwa ni utambulisho wa taifa letu na kielelezo cha umoja wetu katika kudumisha amani na usalama wa nchi yetu. Natoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuuthamini, kuuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano wetu ili jitihada za kusukuma mbele maendeleo yetu kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa faida ya pande zote mbili ziendelee kufanikiwa zaidi.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya uongozi wa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Makamu wake, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Muungano wetu unaendelea kuimarika na kushamiri na hakuna changamoto yoyote inayoweza kutufaranisha, kututenganisha wala kuturudisha nyuma. Ofisi yetu inayo faraja kwamba, katika nchi yetu sasa, kwa watu wa itikadi zote na kutoka pande zote za Muungano, mjadala sio uhalali wa Muunganobali mbinu za kuuimarisha. Ofisi na Serikali kwa ujumla itaendelea kufanyia kazi maoni na mawazo ya watu wote wenye nia ya kuona Muungano wetu unashamiri.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** mazingira yetu pia ni muhimu na yana mchango mkubwa katika maendeleo ya uchumi wa viwanda. Ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa mazingira na maliasili za nchi yetu zinalindwa na kuhifadhiwa. Ofisi inadhamira ya kujenga utaratibu wa kumshirikisha kila Mtanzania katika wajibu huu ili ulinzi na hifadhi ya mazingira lisiwe suala la shuruti bali la utamaduni. Napenda kutoa wito kwa wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kuwa dhamira ya

Serikali ya kulinda na kuhifadhi mazingira inazingatiwa na kupewa kipaumbele kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Ofisi itashika hatamu kwa uthabiti kabisa katika wajibu wake wa usimamizi na uratibu wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Tutaandika Kanuni na kutoa Miongozo kadhaa ya hifadhi ya mazingira katika sekta na nyanja mbalimbali, ikiwemo nishati, kilimo, utalii, mifugo, afya, uvuvi, misitu, maji, viwanda, ujenzi, usafirishaji na maeneo mengine mengi. Mtazamo wetu ni kuongoza hifadhi ya mazingira kwa namna pana zaidi, kwa kuangalia mifumo ya kiikolojia, mifumo ya uzalishaji mali, na mifumo na uchumi wa matumizi ya rasilimali asili.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru walionisaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Shukrani zangu za dhati na za kipekee ni kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uongozi wake na dira na mwelekeo aliotupatia kuhusu majukumu yetu. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu.

Ninapenda kumshukuruMheshimiwaLuhaga Joelson Mpina, (Mb.), Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano alionipa katika utekelezaji wa kazi za Ofisi. Aidha, ninapenda kuwashukuru Profesa Faustin Rweshabura Kamuzora, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; MhandisiNgosi Charlestino Mwihava, Naibu Katibu MkuuOfisi ya Makamu wa Rais; Profesa Salome Barnabas Misana, Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira pamoja na wajumbe wa Bodi; Ndugu Ali Mufuruki, Mwenyekiti wa Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Mazingira na Wajumbe wa Bodi; MhandisiBonaventure Thobias Baya, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na watumishi wote wa Baraza

na Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa juhudi zao na utendaji katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imefanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo. Ninapenda kuwataja baadhi ya washirika wa maendeleo ambao Ofisi imefanya nao kazi kwa karibu kama ifuatavyo:

Serikali ya Norway; Serikali ya Kanada; Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea; Umoja wa Nchi za Ulaya (*European Union - EU*); Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*United Nations Development Programme – UNDP*); Shirika la Umoja wa Mataifa Elimu, Sayansi na Utamaduni (*United Nations Educational, Scientific and Cultural - UNESCO);* Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (*United Nations Environment Programme - UNEP*); Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(Global Environment Facility - GEF*); Shirika la Umoja wa Mataifa la Huduma za Miradi (*United Nations Office for Project Services-UNOPS*); Benki ya Dunia,Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB);Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO); Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la Denmark (*Danish International Development Assistance*DANIDA); *World Wide Fund for Nature - WWF;* Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (*International Fund for Agricultural Development - IFAD*); Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund - GCF*); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (*Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit - GiZ);* Kikundi cha Washirika wa Maendeleo kinachoshughulikia Mazingira (DPGE); Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE); na sekta binafsi. Kipekee nawashukuru Benki ya Dunia, wakiongozwa na Mkurugenzi wao hapa nchini, Mama Bella Bird, kwa kuamua kuingia katika mashirikiano mapya na Ofisi yetu ambayo yametoa matumiani mapya kuhusu ujenzi wa uwezo wa Ofisi na Baraza katika kusimamia hifadhi ya mazingira nchini.

Aidha, ninapenda nitumie fursa hii kuwaomba washirika wa maendeleo kuendelea kutoa ushirikiano katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika kulinda na

kuimarisha Muungano wetu na katika vita dhidi ya umaskini na juhudi za kuboresha maisha ya kila Mtanzania ili vizazi vya baadae vikute mazingira safi kwa ustawi wao kama sisi tulivyorithi pia.

## D: MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO

127. ***Mheshimiwa Spika***, ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2017/18 kama ifuatavyo:

### Fungu 26: Makamu wa Rais

128. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba Bunge lako tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya shilingi 4,914,608,000/=fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa fedha 2017/18.Kiasi hiki kinajumuisha fedha za mishahara ya watumishi shilingi 1,159,643,000/= na fedha za Matumizi Mengineyo shilingi 3,754,965,000/=.

### Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais

129. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba Bunge lako tukufu, liidhinishe makadirio ya matumizi ya shilingi **15,002,987,437/=**kwa Fungu hili. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi **8,214,535,000/=** fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **6,788,452,437/=** fedha za Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha shilingi **3,120,324,000/=** kwa ajili yamishahara ya watumishi, shilingi **2,215,044,000/=** ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na shilingi **2,879,167,000/=** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Idara na Vitengo katika Ofisi hii. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha Fedha za Ndanishilingi **3,000,000,000/=** na Fedha za Nje shilingi **3,788,452,437/=.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, tulivyotangaza wageni tulimwacha Profesa Salome Misana ambaye hakutambulishwa, naomba kumtambulisha kama yupo simama tafathali. Yeye ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya *NEMC,* kwa hiyo, ni mtu muhimu sana Wabunge mkamjua.

Sasa namwita Mwenyekiti Kamati ya Katiba na Sheria kuwasilisha taarifa yake. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la furaha na heshima kubwa kwa kamati yangu kuwasilisha taarifa yake kuhusu Ofisi ya Rais Muungano tukiwa tunaadhimisha miaka 53 ya Muungano wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Natoa pongezi kwa Serikali zote mbili kwa kuhakikisha kwamba Muungano huu unadumu na unaendelea kuwa na faida kwa pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016**,** naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa mwaka wa fedha 2016/2017; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 6(2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeendelea kutekeleza jukumu hili la kuisimamia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) toka kuundwa kwa kamati hii mwezi Januari 2016; na ndani ya miezi 15 iliyopita Kamati imetembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya ofisi hii pamoja na kupokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo chini ya Ofisi hii iliyotengewa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017 tarehe 22 Machi, 2017. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) tarehe 02 Aprili, 2017 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) pamoja na kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2016/2017, kwa ajili ya kufanya ulinganisho kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais ina mafungu mawili ya bajeti kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais; na
(ii) Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa manne yafuatayo:-

(i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

(ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017; na utekelezaji wa mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

(iii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2017/2018; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inahusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kamati ya Katiba na Sheria ilitembelea, kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi Na. 6309 – ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu – Unguja ulio chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais tarehe 22 Machi, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha mwaka 2016/2017 iingie kwenye *Hansard* za Bunge kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa taarifa Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2017/2017. Uchambuzi huu nao uingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 3.1 inahusu mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati. Kwa ujumla Kamati imeridhika kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni ya Kamati yaliyotolewa mwezi Mei, 2016 kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kwenye Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais zilizowasilishwa mbele ya kamati. Katika taarifa ya kamati iliyosomwa katika Bunge hili mwezi Mei, 2016 Kamati ilitoa maagizo, maoni na ushauri kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo kwa ujumla yamezingatiwa na kufanyiwa kazi na Ofisi ya Makamu wa Rais katika mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya maagizo ya Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ilikuwa ni kufanyia kazi mapungufu yaliyoonekana katika mradi Na. 6389 kuhusu ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais lililopo Dar es Salaam. Kamati imepokea taarifa ya utekelezaji kuhusu mradi wa jengo hili na inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kurekebisha kasoro zote zilizoonekana katika mradi huu bila

kutumia gharama nyingine za ziada kama zile za kuwalipa washauri elekezi *(consultants)* kama ilivyokusudiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Badala yake kamati inashauri Wakala wa Majengo *(TBA)* washughulikie mapungufu yaliyoonekana kwa gharama nafuu ili kuokoa fedha za walipa kodi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ni mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) imepanga kutekeleza malengo mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kuhusu uratibu wa masuala ya Muungano. Katika kuhakikisha kwamba malengo hayo yanafanikiwa, Ofisi ya Makamu wa Rais imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(1) Kuratibu vikao vya Kamati ya pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kushughulikia masuala ya Muungano pamoja na changamoto zinazojitokeza.

(2) Kuelimisha umma kuhusu Muungano;

(3) Kuratibu utekelezaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii kwa faida ya pande zote mbili za Muungano; na

(4) Kuratibu ushirikiano kwa kuhimiza Wizara na taasisi zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana kwa pande zote kukutana mara mbili kwa mwaka ili kuimarisha katika masuala yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano inahusu mapitio ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu namba 26 na Fungu namba 31. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaomba jumla ya shilingi 4,914,608,000 ambapo shilingi 3,754,965,000 ni kwa ajili ya matumizi mengine na shilingi 1,159,643,000 ni kwa ajili ya mishahara. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 26 ukilinganisha na kiasi kilichoombwa mwaka wa fedha uliopita wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu namba 31; katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Makamu wa Rais inaomba jumla ya shilingi 15,200,988,437 ili kutekeleza majukumu yake mbalimbali. Kati ya fedha hizo, shilingi 8,214,536,000 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 6,788,452,437 ni fedha za miradi ya maendeleo. Katika fedha ya matumizi ya kawaida inayoombwa shilingi 3,120,324,000 ni fedha za mishahara na shilingi 5,094,212,000 ni fedha za matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa bajeti unaonesha kwamba ukomo wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Fungu namba 31 umekuwa ukishuka toka mwaka wa fedha 2015/2016 kwa kiasi kikubwa. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 ukomo wa bajeti ulishuka kwa wastani wa shilingi bilioni 17 ukilinganishwa na bajeti ya mwaka 2015/2016. Ukomo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 umeshuka kwa wastani wa shilingi 5,000,000,000 ukilinganisha na kiasi kilichoombwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, hali hii kwa kiasi kikubwa inaathiri utekelezaji wa majukumu wa Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo katika kipindi cha mwaka 2017/2018, bajeti ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, Fungu namba 24 kwa ujumla imeongezeka kwa kiasi cha shilingi 1,265,424,000 ambalo ni ongezeko la wastani wa aslimia 25 na imepungua kwa shilingi 5,333,711,011 kwa Fungu namba 31 ambao ni upungufu wa wastani wa asilimia 26 kama inavyooneshwa kwenye jedwali ambalo litaingia kwenye Kumbukumbu za Kudumu za Bunge.

Sehemu ya sita inahusu maoni na ushauri wa Kamati ambapo naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala yaliyobainika wakati wa uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Fungu namba 31 na Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais Fungu namba 26 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Fungu namba 31. Kamati imeridhishwa na

utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais Mei, 2016 na hasa hatua za utekelezaji wa Mradi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam. Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kufanya rejea ya ushauri na maagizo ya Kamati na kuyatekeleza kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kwa kuwa Serikali tayari ina Wakala wa Majengo *(Tanzania Building Agency),* ili kuokoa fedha za walipa kodi wa Tanzania, Kamati inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kutumia ujuzi na utaalam wa Wakala wa Majengo badala ya kutumia fedha za ziada kuwalipa wataalam elekezi wengine kutoka taasisi nyingine za kitaalam kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa gharama za miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Kamati inapongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa kuendelea kuratibu vyema masuala ya Muungano na hasa kwa kuwezesha kufanyika vikao vya kujadili masuala ya Muungano katika ngazi ya Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambavyo vilifanyika mwezi Januari, 2016. Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kuratibu vikao hivi katika wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Serikali itenge bajeti ya kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati hasa kwenye miradi ya maendeleo ili kuongeza kasi na kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu na faida zinazotokana na Muungano wa pande zote mbili ili kuwawezesha wananchi kuuthamini, kuupenda, kuudumisha na kuulinda Muungano huu kwa maslahi ya nchi yetu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Serikali iendelee kuchukua jitihada za dhati katika kutatua kero za Muungano ili kuongeza tija katika shughuli mbalimbali za biashara na maendeleo kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, kwa kuwa uamuzi wa kuhamia Dodoma umeanza kutekelezwa na Serikali, Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuandaa mpango wa kutenga fedha zaidi ili kukamilisha awamu zilizobaki za kuhamia Dodoma kwa wakati. Sambamba na hili, Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais kuandaa mpango wa ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais katika Mji wa Serikali hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuandaa mpango wa ujenzi wa jengo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Unguja na Ikulu ndogo huko Pemba na kuhakikisha kwamba fedha kwa ajili ya ofisi hizi inatengwa katika miaka ijayo ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, kwa kuwa ujenzi wa jengo la ofisi na makazi ya Makamu wa Rais, mradi Na. 6309 lililopo Tunguu, Unguja umechukua zaidi ya miaka nane kukamilika, Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kukamilisha jengo hili katika mwaka ujao wa fedha ili lianze kutumika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, Kamati inapongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushughulikia mapungufu mbalimbali yaliyoonekana katika mradi Na. 6589 wa ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam na inaelekeza Ofisi ya Makamu wa Rais kushughulikia mapungufu yote ya kitaalam yaliyoonekana katika jengo hili ili lianze kutumika mapema iwezekanavyo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na moja, Kamati inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kuendelea kuzingatia uwiano wa ajira Serikalini katika pande zote mbili

za Muungano yaani Tanzania Bara na Zanzibar uliokubalika na pande zote mbili yaani uwiano wa asilimia 79 kwa asilimia 21. Kamati inapongeza uamuzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kufungua Ofisi za Sekretarieti ya Tume ya Ajira Visiwani ili kutekeleza makubaliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na mbili, ili kutekeleza vyema majukumu na dhamana yake iliyopewa Kikatiba, Kamati inashauri kwamba Tume ya Pamoja ya Fedha *(Joint Financial Commission)* ambayo imeanzishwa chini ya Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isimamiwe moja kwa moja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na si Wizara ya Fedha na Mipango kama utaratibu ulivyo sasa. Hii itaboresha utendaji kazi na ufanisi wa Tume katika kutekeleza majukumu yake Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, Fungu namba 26 iendelee kuwezeshwa ili kumuwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais kutimiza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inaishauri Ofisi ya Hazina kuendelea kutoa fedha kwa wakati katika ofisi hii ili kuiwezesha ofisi kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba na maagizo mbalimbali kutoka Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kwa kutambua umuhimu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Kamati inashauri fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais ziwekwe katika mfuko maalum ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii na hasa majukumu ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kukushukuru wewe binafasi kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu.

Aidha, hatuna budi kumpongeza Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa January Yusuf Makamba (Mbunge), Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Mheshimiwa Luhaga Mpina (Mbunge), Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais Profesa Faustin Kamuzora na watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa majadiliano ya pamoja kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Uzalendo na uchapakazi wao pamoja na ushirikiano mkubwa waliotupa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. Ninaomba majina ya Wajumbe wote wa Kamati hii yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kusaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Makatibu wa Kamati, Ndugu Angelina Sanga, Ndugu Stella Bwimbo, Ndugu Dunford Mpelumbe na msaidizi wa Kamati Ndugu Rachel Masima kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. Kipekee pia napenda kuishukuru Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa kuhakikisha kwamba taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, vilevile ahsante kwa kulinda muda Mheshimiwa Mwenyekiti.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimwa Spika,** napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, ni jambo la furaha na heshima kubwa kwa Kamati yangu kuwasilisha Taarifa yake kuhusu Ofisi ya Rais (Muungano) tukiwa tunaadhimisha miaka 53 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Natoa pongezi kwa Serikali zote mbili kwa kuhakikisha kwamba Muungano huu unadumu na unaendelea kuwa na faida kwa pande zote mbili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016**,** naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017; pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge,

Toleo la Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imeendelea kutekeleza jukumu hili la kuisimamia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) toka kuundwa kwa Kamati hii Mwezi Januari 2016 na ndani ya miezi 15 iliyopita Kamati imetembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya Ofisi hii pamoja na kupokea Taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi hii, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 tarehe 22 Machi 2017. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Raisi(Muungano) Tarehe 02 Aprili, 2017 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) pamoja na kuchambua Taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kufanya ulinganisho kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Rais ina mafungu mawili (2) ya bajeti kama ifuatavyo;

iii) Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais

iv) Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika, Taarifa** hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa manne (4) yafuatayo:-

v) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

vi) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; na Utekelezaji wa mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018;

vii) Maoni na Ushauri wa Kamati

**2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 98 (1) inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni hiyo, Kamati ya Katiba na Sheria ilitembelea, kukagua na kupokea Taarifa ya utekelezaji wa mradi Na.6309 –ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu- Unguja ulio chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais tarehe 22 Machi 2017.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa fedha 2016/ 2017, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Tisa Sabini na Tatu , Themanini na Tatu Elfu, Mia Nne Arobaini na Nane (10,973,083,448.00) kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Nane (8,000,000,000.00) ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Sabini na Tatu, Themanini na Tatu Elfu Mia Nne na Arobaini na Nane (2,973,083,448.00) ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2017 Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Thelathini na Saba, Laki Tano Sabini na Saba Elfu, Mia Tano Sitini na Nane (1,237,577,568.00) zilikuwa zimepokelewa. Fedha hii ni sawa na asilimia 11 ya fedha yote ya miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge mwezi Mei, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, mradi namba 6309 ambao ni ujenzi wa Makazi na Ofisi ya Makamu wa Rais Tunguu, Unguja katika Mwaka wa fedha 2016/2017 ulitengewa Shilingi Milioni Mia Saba (700,000,000.00).

**Mheshimiwa Spika**, kwa sababu Kamati ya Katiba na Sheria inasimamia masuala yote ya Muungano kwa

ujumla, ilionekana ni vema kukagua miradi mingine ya Maendeleo iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37) iliyopo Unguja na Pemba pamoja na Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) zilizopo Pemba. Taarifa za ukaguzi wa Miradi hii ya Maendeleo zipo katika Taarifa mahsusi za Kamati kuhusu Wizara/Ofisi hizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha kwamba Miradi mbalimbali ya maendeleo kama ile ya MIVARF (Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Financing) ulio chini ya Waziri Mkuu na ile ya TASAF iliyo chini ya Ofisi ya Rais inaendelea kuwafikia na kuwanufaisha wananchi wengi walioko Tanzania  Zanzibar. Wakati wa ziara kwenye miradi ya ujenzi wa masoko na barabara Unguja na Pemba, Kamati ilijionea jinsi miradi hii ilivyo na faida kubwa kwa wananchi wengi wa maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, miradi mingine chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais inayohusiana na masuala ya mazingira inasimamiwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Baadhi ya miradi hii inatekelezwa Unguja na Pemba.

**Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni yafuatayo ya jumla kuhusu miradi iliyokaguliwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kama ifuatavyo;

**MRADI NA.6309-UJENZI WA OFISI NA MAKAZI YA MAKAMU WA RAIS, UNGUJA ;**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu kwa mara ya kwanza, ulitengewa fedha katika bajeti ya maendeleo ya mwaka wa fedha 2008/2009. Lengo la mradi huu lilikuwa ni kukidhi mahitaji ya makazi na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kupata Ofisi inayoweza kutumiwa na watumishi wote wa ofisi hiyo waliopo Unguja na kupata makazi ya kudumu ya Mheshimiwa Makamu wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2016/

2017 mradi huu ulitengewa Shilingi Milioni Mia Saba (Shs.700, 000,000.00). Katika mwaka ujao wa Fedha 2017/2018 , mradi huu umetengewa Shilingi Milioni Mia Tatu (300,000,000.00).

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais umeshakamilika kwa kiasi kikubwa na mkandarasi amewasilisha hati ya kukamilisha ujenzi (Final Account) na muda wa matazamio umeshaisha. Kamati inatoa rai kwa Mkandarasi na Ofisi ya Makamu wa Rais kukamilisha mapungufu yaliyoonekana katika mradi na kuhakikisha kwamba changamoto zote zilizoonekana zinafanyiwa kazi na kukamilika katika mwaka ujao wa fedha.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016 Kamati ilikutana Dodoma Tarehe 02 Aprili, 2017 kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilizingatia mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Mwezi Mei, 2016 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi mwezi Machi, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 ili kujua vipaumbele vya kibajeti katika Mwaka wa Fedha Ujao.

## i) OFISI BINAFSI YA MAKAMU WA RAIS (FUNGU 26)

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, Fungu 26, ilidhiinishiwa Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Sita Arobaini na Tisa, Laki Moja Themanini na Nne Elfu (3,649,184,000.00). Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne Tisini na Tisa na Laki Nane (2,499,800,000.00) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Arobaini na Tisa, Laki Tatu Themanini na Nne Elfu (1,149,384,000.00) ni kwa ajili ya mishahara.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2017 Fungu 26 ilipokea kiasi cha Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tano Thelathini na Tatu , Laki Mbili na Arobaini na Sita Elfu, Mia Mbili Sitini na Tatu (3,533,246,263/= ) kutoka Hazina sawa na asilimia 97 ya Bajeti yote. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nane Arobaini na Nane, Laki Nane Sabini na Tisa Elfu, Mia Mbili Sitini na Tatu na Senti Tisini (2,848,879,263.90) ni za matumizi ya mengineyo sawa asilimia 113.9 ya bajeti ya matumizi mengineyo na Shilingi Milioni Mia Sita Themanini na Nne, Laki Tatu Sitini na Saba Elfu (684,367,000) ni za mishahara sawa na asilimia 59.5 ya bajeti ya mishahara.

**Jedwali Na.01: Mchanganuo wa Fedha Zilizoidhinishwa na Kupokelewa Chini ya Fungu 26 katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Hadi Kufikia Machi,2017**

| | Fedha Zilizoidhinishwa | Fedha Zilizopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Kawaida | Sh. 2,499,800,000 | Sh. 2,848,879,263.90 | 113.9 |
| Mishahara | Sh. 1,149,384,000 | Sh. 684,367,000 | 59.5 |
| Maendeleo | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **3,649,184,000** | **3,533,246,263.90** | **97** |

### ii) OFISI YA MAKAMU WA RAIS – (FUNGU 31)

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu 31, iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tatu Themanini na Sita, Laki Sita Tisini na Tisa Elfu, Mia Nne na Arobaini na Nane (20,386,699,448.00). Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Nne Kumi na Tatu, Laki Sita Kumi na Sita Elfu na (9,413,616,000.00) ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Tisa Sabini na Tatu, Themanini na Tatu Elfu ,Mia Nne na Arobaini na Nane (10,973,083,448.00) ni fedha za miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2017, Ofisi ilipokea Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Saba Tisini na Tatu, Laki Nne Tisini na Tatu Elfu, Mia Saba Thelathini na Saba (7,793,493,737.18) sawa na asilimia 38.2 ya fedha iliyoombwa. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tano Hamsini na Tano, Laki Tisa Kumi na Sita Elfu, Mia Moja na Sitini na Nane (6,555,916,168) zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo jumla ya Sh. Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Thelathini na Saba, Laki Tano na Sabini na Saba Elfu, Mia Tano Sitini na Nane na Senti Hamsini (1,237,577,568.50/=) ambayo ni sawa na asilimia 11 ya fedha yote ya miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge.

### 3.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, Kamati imeridhika kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni ya Kamati yaliyotolewa mwezi Mei 2016, kama ilivyoelezwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kwenye Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais zilizowasilishwa mbele ya Kamati. Katika Taarifa ya Kamati iliyosomwa katika Bunge hili Mwezi Mei, 2016 kamati ilitoa maagizo, maoni na ushauri kwa Ofisi ya Makamo wa Rais ambayo kwa ujumla yamezingatiwa na kufanyiwa kazi na Ofisi ya Makamu wa Rais katika mwaka huu wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** moja kati ya maagizo ya Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ilikuwa ni kufanyia kazi mapungufu yaliyoonekana katika mradi Na. 6389 kuhusu Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais lililopo Luthuli, Dar es Salaam. Kamati imepokea Taarifa ya utekelezaji kuhusu mradi wa jengo hili na inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kurekebisha kasoro zote zilizoonekana katika mradi huu bila kutumia gharama nyingine za ziada kama zile za kuwalipa washauri elekezi (Consultants) kama ilivyokusudiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Badala yake Kamati inashauri Wakala wa Majengo (TBA) washughulikie mapungufu yaliyoonekana kwa gharama nafuu ili kuokoa fedha za walipa kodi wa Tanzania.

## 4.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) imepanga kutekeleza malengo mbalimbali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kuhusu uratibu wa masuala ya Muungano. Katika kuhakikisha kwamba malengo haya yanafanikiwa Ofisi ya Makamu wa Rais imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i) Kuratibu vikao vya kamati ya pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar vya kushughulikia masuala ya Muungano pamoja na changamoto zilizojitokeza;

ii) Kuelimisha Umma kuhusu Muungano;

iii) Kuratibu utekelezaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii kwa faida ya pande zote mbili za Muungano;

iv) Kuratibu ushirikiano kwa kuhimiza Wizara na Taasisi zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana kwa pande zote, kukutana mara mbili (2) kwa mwaka ili kuimarisha katika masuala yasiyo ya Muungano.

## 5.0 MAPITIO YA BAJETI OFISI YA MAKAMU WA RAIS FUNGU 26 na 31 KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inaonyesha maombi ya jumla ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Fungu 26) na Ofisi ya Makamu wa Rais (Fungu 31) kulingana na vipaumbele vilivyowekwa.

### 5.1 OFISI YA MAKAMU WA RAIS (FUNGU 26)

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2017/18 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaomba jumla ya Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tisa Kumi na Nne, Laki Sita na Nane Elfu. (Sh.4,914,608,000.00) ambapo Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Saba Hamsini na Nne , Laki Tisa Sitini na Tano Elfu (3,754,965,000.00) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Hamsini na Tisa, Laki Sita Arobaini na Tatu Elfu (1,159,643,000.00) ni kwa ajili ya mishahara. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 26 ukilinganisha na kiasi kilichoombwa mwaka huu wa fedha (2016/2017).

**Mheshimiwa Spika**, fedha hizi zinategemewa kumwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na maagizo ya Mheshimiwa Rais pamoja na kufanikisha majukumu mengine muhimu ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.

### 5.2 OFISI YA MAKAMU WA RAIS (FUNGU 31)

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Ofisi ya Makamu wa Rais inaomba jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mbili, Laki Tisa Themanini na Nane Elfu, Mia Nne Thelathini na Saba (15,002,988,437.00) ili kutekeleza majukumu yake mbalimbali. Kati ya Fedha hizo, Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Mbili Kumi na Nne, Laki Tano Thelathini na Sita Elfu (8,214,536,000.00) ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Saba Themanini na Nane, Laki Nne Hamsini na Mbili, Mia Nne Thelathini na Saba

(6,788,452,437.00) ni fedha za miradi ya maendeleo. Katika fedha ya matumizi ya kawaida inayoombwa, Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Moja na Ishirini, Laki Tatu na Ishirini na Nne Elfu (3,120,324,000.00) ni fedha za mishahara na Shilingi Bilioni Tano, Milioni Tisini na Nne, Laki Mbili na Kumi na Mbili Elfu (5,094,212,000.00) ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa bajeti unaonyesha kwamba, ukomo wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Fungu 31) umekua ukishuka toka mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa kiasi kikubwa. Katika mwaka wa Fedha 2016/2017 ukomo wa bajeti ulishuka kwa wastani wa Shilingi Bilioni Kumi na Saba (17,000,000,000.00) ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2015/2016. Ukomo wa bajeti kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 umeshuka kwa wastani wa Shilingi Bilioni Tano (5,000,000,000.00) ukilinganisha na kiasi kilichoombwa katika bajeti ya mwaka wa Fedha 2016/2017. Hali hii kwa kiasi kikubwa inaathiri utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Hata hivyo katika kipindi cha mwaka 2017/2018 bajeti ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Fungu 26) kwa ujumla imeongezwa kwa kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Sitini na Tano, Laki Nne Ishirini na Nne Elfu (1,265,424,000.00) ambalo ni ongezeko la wastani wa asilimia 25 na imepungua kwa Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tatu Themanini na Tatu, Laki Saba Kumi na Moja Elfu na Kumi na Moja (5,383,711,011) kwa Fungu 31 ambayo ni pungufu ya wastani wa Asilimia 26 Kama inavyoonyesha kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali Na.02: Tofauti ya Kiasi cha Fedha Kilichoidhinishwa 2016/2017 na Kinachoombwa 2017/2018 Katika Mafungu 31 na 26.**

| Fungu | Fedha Iliyoidhinishwa 2016/2017 | Fedha Inayoombwa Mwaka 2017/2018 | Tofauti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 26 | Sh. 3,649,184,000 | Sh. 4,914,608,000 | Sh.1,265,424,000 | 25 % |
| 31 | Sh.20,386,699,448 | Sh.15,002,988,437 | Sh.5,383,711,011 | 26% |

## 6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala yaliyobainika wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Fungu 31 na Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais Fungu 26 kama ifuatavyo:

### 6.1 Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) - Fungu 31

i) Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais mwezi Mei, 2016 na hasa hatua za utekelezaji wa Mradi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, Luthuli Dar es Salaam. Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kufanya rejea ya ushauri na maagizo ya Kamati na kuyatekeleza kwa wakati.

ii) Kwa kuwa Serikali tayari ina Wakala wa Majengo (Tanzania Building Agency -TBA), ili kuokoa fedha za walipa kodi wa Tanzania; Kamati inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kutumia ujuzi na utaalamu wa Wakala wa Majengo badala ya kutumia fedha za ziada kuwalipa wataalamu elekezi wengine kutoka Taasisi nyingine za kitaalamu kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa gharama za miradi hii.

iii) Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa kuendelea kuratibu vema masuala ya Muungano na hasa kwa kuwezesha kufanyika vikao vya kujadili masuala ya Muungano katika ngazi ya Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambavyo vilifanyika mwezi Januari 2016. Kamati inatoa Wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kuratibu vikao hivi katika wakati muafaka.

iv) Serikali itenge Bajeti ya kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati hasa kwenye Miradi ya Maendeleo ili kuongeza kasi na kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo.

v) Serikali iendelee kutoa Elimu kwa Wananchi kuhusu umuhimu na faida zinazotokana na Muungano wa Pande zote mbili ili kuwawezesha Wananchi kuuthamini, kuupenda, kuudumisha na kuulinda Muungano huu kwa maslahi ya nchi yetu na kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

vi) Serikali iendelee kuchukua jitihada za dhati katika kutatua kero za Muungano ili kuongeza tija katika shughuli mbalimbali za biashara na maendeleo kati ya Tanzania Bara na Visiwani.

vii) Kwa kuwa uamuzi wa kuhamia Dodoma umeanza kutekelezwa na Serikali, Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuandaa mpango na kutenga fedha zaidi ili kukamilisha awamu zilizobaki za kuhamia Dodoma kwa wakati. Sambamba na hili, Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais kuandaa mpango wa Ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais katika mji wa Serikali hapa Dodoma.

viii) Kamati inatoa Wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuandaa mpango wa Ujenzi wa Jengo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Unguja na Ikulu Ndogo huko Pemba na kuhakikisha kwamba fedha kwa ajili ya Ofisi hizi inatengwa katika Miaka ijayo ya fedha.

ix) Kwa kuwa Ujenzi wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (Mradi Na.6309) lililopo Tunguu, Unguja umechukua zaidi ya miaka nane (8) kukamilika, kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kukamilisha jengo hili katika mwaka ujao wa fedha ili lianze kutumika kama ilivyopangwa.

x) Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushughulikia mapungufu mbalimbali yaliyoonekana katika mradi Na. 6389 wa ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais,

Dar es Salaam na inaielekeza Ofisi ya Makamu wa Rais kushughulikia mapungufu yote ya kitaalamu yaliyoonekana katika jengo hili ili lianze kutumika mapema iwezekanavyo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya Ofisi .

xi) Kamati inaishauri Ofisi ya Rais Muungano kuendelea kuzingatia uwiano wa ajira Serikalini katika pande zote mbili za Muungano yaani, Tanzania Bara na Zanzibar uliokubalika na pande zote mbili , yaani uwiano wa asilimia **79:21**. Kamati inapongeza uamuzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kufungua Ofisi za Sekretariati ya Tume ya Ajira Visiwani ili kutekeleza makubaliano haya.

xii) Ili kutekeleza vema majukumu na dhamana yake iliyopewa Kikatiba, Kamati inashauri kwamba, Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*) ambayo imeanzishwa chini ya Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, isimamiwe moja kwa moja na Ofisi ya Rais au Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na siyo Wizara ya Fedha na Mipango kama utaratibu ulivyo sasa. Hii itaboresha utendaji kazi na ufanisi wa Tume katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

## 6.2 OFISI BINAFSI YA MAKAMU WA RAIS (Fungu 26)

i) Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais iendelee kuwezeshwa ili kumwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais kutimiza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha Kamati inaishauri Ofisi ya Hazina kuendelea kutoa fedha kwa wakati katika Ofisi hii ili kuiwezesha ofisi kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na Maagizo mbalimbali kutoka Ofisi ya Rais.

ii) Kwa kutambua umuhimu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Kamati inashauri fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais ziwekwe katika Mfuko Maalumu ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii na hasa majukumu ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Aidha, hatuna budi kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa. Napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa January Yusuph Makamba (Mb), Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. Luhaga Mpina, Mb, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais Prof. Faustine Kamuzora na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais(Muungano) kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa majadiliano ya pamoja kuhusu Makadirio na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Uzalendo na uchapakazi wao pamoja na ushirikiano mkubwa walionipa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Ninaomba majina ya wajumbe wote wa kamati hii yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge (Hansard).

1) Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb, **Mwenyekiti**
2) Mhe. Najma Mutraza Giga, Mb, **M/Mwenyekiti**
3) Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb
4) Mhe. Ally Saleh Ally, Mb
5) Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
6) Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
7) Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb
8) Mhe. Seif Ungando Ally, Mb
9) Mhe. Ussi Pondezza, Mb
10) Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb
11) Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb

12) Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb
13) Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb
14) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb
15) Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb
16) Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb
17) Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb
18) Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb
19) Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
20) Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb
21) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb
22) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb
23) Mhe.Mathayo David Mathayo,Mb
24) Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb
25) Mhe. Juma Hamadi Kombo, Mb.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kusaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza Majukumu yake. Kipekee, nawashukuru makatibu wa Kamati Ndg. Angelina Sanga, Ndg. Stella Bwimbo, Ndg. Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndg.Raheli Masima kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. Kipekee pia napenda kuishukuru idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

**24 Aprili, 2017**

**MWENYEKITI:** Sasa ninamuita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, lakini yote ntakayosoma endapo muda hautaruhusu nitaomba yaingie kwenye *Hansard.*

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Fungu 31 kwa mwaka 2016/2017 na maoni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Fungu 31 kwa mwaka 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia nzuri ya Serikali katika kudhibiti kasi ya uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi bado jitihada za ziada zinahitajika. Shughuli za kibinadamu ndicho chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira ikiwemo shughuli za kilimo na ufugaji usiozingatia taratibu, uvunaji wa misitu usiozingatia taratibu na uvuvi haramu. Kwa mukhtadha huu Serikali inatakiwa kuchukua hatua za makusudi za kusimamia na kuhifadhi mazingira kwani kukwepa gharama za kutunza mazingira ni kukaribisha janga kwa nchi yetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha

2016/2017 kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kuchambua Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inalenga kuliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha maombi ya fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), lakini pia kutoa mapendekezo kwa Bunge kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi katika kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017; katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilijikita katika kuchambua mwenendo wa upatikaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo pamoja na fedha zilizotengwa ili kutekeleza majukumu mengine ya Ofisi. Katika kufanya uchambuzi Kamati ilitumia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, taarifa ya ziara kwenye miradi na mahojiano wakati wa vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Makamu wa Rais haikuwa na makusanyo ya maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) iliidhinishiwa jumla ya shilingi 20,386,699,448; na kati ya fedha hizo, shilingi 9,413,616,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 10,973,083,448 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shilingi 9,413,616,000 ambazo ni bajeti ya matumizi ya kawaida, shilingi 2,846,299,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, na shilingi 6,567,316,000 ni kwa ajili matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za matumizi mengineyo zilizoidhinishwa ni shilingi 2,314,680,000 ni ruzuku ya mishahara kwa Baraza la Taifa la hifadhi na usimamizi wa mazingira *(NEMC),* na kiasi kinachosalia shilingi 4,252,637,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* katika Idara na Vitengo vya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za miradi ya maendeleo, shilingi 10,973,083,448 zilizoidhinishwa shilingi bilioni nane ni fedha za ndani na shilingi 2,973,083,443 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizopokelewa hadi 15 Machi, 2017. Kati ya shilingi 20,386,699,448 zilizoidhinishwa kwa ajiliya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ni shilingi 7,793,493,737.18 tu ndizo zilikuwa zimetolewa hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2017. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 38.2 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya shilingi 9,413,616,448 zilizoidhinishwa kwa ajili matumizi ya kawaida ni shilingi 6,555,916,168.68 tu ndizo zilizokuwa zimetolewa. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 69.9 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida shilingi 1,905,596,990 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 2,964,514,853.84 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa shilingi 51,040,660 zililipa madeni ya watumishi, shilingi 177,099,664.84 zililipia madeni ya wazabuni na shilingi bilioni 1,857,670,000 ni ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kiasi kinachosalia kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi ni shilingi 1,278,710,526 ambazo hazikukidhi mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya shilingi 10,973,083,448 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 1,237,577,568.50 tu ndizo zilizopokelewa sawa na asilimia 11.3 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Aidha, kati ya shilingi 8,000,000,000 za bajeti ya

fedha za ndani ni shilingi 236,186,455 tu ndizo zilizopokelewa, sawa na asilimia 2.9 ya bajeti yote ya fedha za ndani, na shilingi 2,973,083,443 za bajeti ya fedha za nje ni shilingi 1,001,391,113.50 tu ndizo zilikuwa zimepokelewa, sawa na asilimia 33.6 ya bajeti yote ya fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida umeonekana kuwa wakuridhisha kwa kuwa unachangiwa na fedha za mishahara ambazo hutolewa kila mwezi. Katika bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), upatiakanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na miradi ya maendeleo si wa kuridhisha kabisa, hivyo kupelekea kukwamisha utekelezaji wa mipangoya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa; jedwali lifuatalo hapa chini linaonesha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na upatikanaji wa fedha hizo lakini kutokana na muda sitaweza kusoma jedwali hili hivyo naomba liingie kwenye *Hansard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niseme Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika bajeti ya 2016/2017 kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Fungu 31 iliidhinishiwa shilingi 5,894,633,000 kwa ajili ya Mradi namba 5301 wa *Climate Change Adaptation Programme,* ambao ni mradi wa ujenzi wa ukuta katika ukanda wa Pwani na Zanzibar kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko la usawa wa bahari linalosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya mradi huu ni *Ocean Road*, Kigamboni, Pangani, Kisiwa Panza kule Pemba na Kilimani - Unguja. Hata hivyo kwa sababu ya ufinyu wa muda Kamati ilifanikiwa kutembelea na kujionea hali ya utekelezaji wa mradi huu katika eneo la Pangani na *Ocean Road.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa Mabadaliko ya Tabianchi; mabadiliko ya tabianchi yamesabisha kuongezeka kwa usawa wa bahari *(sea level rise)* kwa sentemita 19 katika kipindi cha miaka 50 iliyopita. Ongezeko la usawa wa bahari linachangia uharibifu wa mwambao wa Pwani, na kutoweka kwa baadhi ya visiwa kama Panza kule Zanzibar, Maziwa – Pangani, Fungu la Nyani – Rufuji na baadhi ya visima vya maji baridi katika maeneo ya Bagamoyo kuharibiwa na maji chumvi. Maisha ya wananchi wanaoishi katika mwambao wa Bahari ya Hindi na kutegemea bahari yapo hatarini kutokana na kumomonyoka kwa fukwe na upotevu wa viumbe baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa ukuta wa Mto Pangani unajumuisha urefu wa mita 950 kwa upande wa Kaskazini (Pangani Mjini) na mita 660 upande wa Bweni. Ujenzi huu wa ukuta ulianza rasmi tangu tarehe 01 Machi, 2017, mkandarasi aliyepewa kazi hii ni *Dezo Civil Contractors.* Mradi huu unakisiwa kuwa utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 2.4 mpaka utakapokamilika. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za wafadhili kwa asilimia 90, kiasi cha shilingi bilioni 2.4, ambazo zimeshakutolewa kwa upande wa Pangani Mashariki, wakati asilimia 10 ya fedha za ndani ni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa upande Pangani Magharibi bado hazijatolewa. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Novemba, 2017 iwapo mipango yote itakwenda kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unakabiliwa na changamoto kuu tatu kama ifuatavyo:-

(i) Kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa ukuta wa Mto wa Pangani kumecheleweshа juhudi za kuanza mchakato wa kuanza upembuzi yakinifu kwa upande wa *PANGADECO;*

(ii) Kuendelea kuharibika kwa eneo la *PANGADECO* ambapo hali ni mbaya na eneo hili la ufukweni mwa mji wa Pangani ni hatarishi kwa maisha ya wanadamu, kwa hiyo zinahitajika juhudi mahususi ili kukabiliana na athari hizo; na

(iii) Upande wa Pangani Mashariki, mradi unatekelezwa kwa fedha za wafadhili hivyo utekelezaji wake unaendelea. Kwa upande wa Pangani Magharibi mradi unatekelezwa kutokana na fedha za ndani. Serikali bado haijapeleka fedha ilizotenga hivyo kuchelewesha utekelezaji na uharibufu kuongezeka kwa kadri siku zinavyokwenda.

Mheshimiwa Mweyekiti, ujenzi wa ukuta wa *Ocean Road;* katika utekelezaji wa mradi wa mabadiliko ya tabianchi kwa eneo la *Ocean Road* hali ya utekelezaji wa mradi inaendelea vizuri, mkandarasi amekwishaanza kazi baada ya kupata fedha za wafadhili kutoka *Adaptation Fund.* Kamati inapongeza hatua ya Wizara ya kuamua kutafuta wafadhili na kuutekeleza mradi huu kwa haraka kwani utekelezaji wa mradi huu utasaidia kukabiliana na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ongezeko la kina cha bahari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017; kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilishauri kuwa Serikali itoe kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya uhifadhi wa mazingira kwa kutenga fedha za kutosha, lakini pia fedha hizo zitolewe kwa wakati. Kwa mfano, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) mpaka kufikia tarehe 30 Januari, 2017 ilikuwa haijapokea kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, jambo ambalo hakika linakwamisha utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwa pamoja na nia yake nzuri ya kusimamia uhifadhi wa mazingira nchini iangalie namna ya kuongeza bajeti ya mazingira. Jambo hili litawezesha kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira na kupunguza uhitaji wa fedha nyingi zinazotumika katika kurekebisha miundombinu ya kimazingira na uoto wa asili. Usipoziba ufa, Waheshimiwa utajenga ukuta.

Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa jitihada wanazozifanya za kutafuta wahisani

ili kulinusuru taifa na janga la uharibifu wa mazingira. Kamati inawaomba waendelee na juhudi za kutafuta fedha kutoka kwa wahisani mbalimbali ili kuongezea kwenye fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya bajeti ya mazingira. Katika mradi wa Pangani Serikali ipeleke fedha za bajeti ya ndani asilimia 10 ya fedha zote za mradi ili utekelezaji huo usikwame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali na kutoa maagizo manane. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati. Hata hivyo kuna maeneo ambayo Serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali ianze kutekeleza ujenzi wa vituo vya kupumzikia wasafiri na wasafirishaji wanaotumia barabara kuu nchini haraka iwezekanavyo. Agizo hili lilikuwa miongoni mwa maagizo ya Kamati katika mwaka wa fedha 2014/2015 na kwa mwaka huo wa fedha Serikali ilifanikiwa kujenga kituo kimoja tu katika Wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa. Agizo hili liliendelea kusisitizwa na Kamati na kuwa miongoni mwa maagizo ambayo yatatekelezwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Serikali kuhusu utekelezaji wake ni kuwa Ofisi inaendelea kuhamasisha wadau wa mazingira na sekta binafsi kujenga vituo hivyo. Pia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imetambua maeneo ya ujenzi wa vituo hivyo katika mpango wa ujenzi wa barabara kuu. Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa agizo hili, pia inaitaka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kubainisha kuwa imebaini uhitaji wa vituo vingapi na ujenzi utaanza lini kuanzia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwamba bajeti ya kuendeleza upandaji wa miti iongezwe. Aidha, vyanzo vya fedha kwa ajili ya mfuko wa dhamana ya hifadhi ya mazingira

vitokane pia na Wizara nyingine. Vyanzo hivyo vitambuliwe na kuhamishiwa katika mfuko.

Serikali ilitoa maelezo kuwa zoezi la upandaji miti linafanya na kila Wilaya na kusimamiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ambapo kila Wilaya hutakiwa kupanda miti 1,500,000 kila mwaka. Kamati na inaamini kuwa miti 1,500,000 ni miti mingi sana kiasi kwamba kama ingekuwa imepandwa tayari athari *(impact)* yake ingekuwa imeonekana. Kamati inashauri agizo hili litekelezwe kwa haraka na baada ya kupandwa kuwa na ufuatiliaji kuhakikisha kwamba inakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mfuko wa mazingira, Kamati ilielezwa kwamba usimamizi wa mazingira kwa kipindi cha 2016/2017 Serikali imezindua rasmi Mfuko wa Mazingira na Bodi ya Wadhamini wa Mfuko imezinduliwa. Mapendekezo ya vyanzo vya mapato vya mfuko kutoka sekta nyingine yamewasilishwa Serikalini kwa ajili ya maamuzi. Kamati inapongeza Serikali kwa hatua iliyofikia lakini iongeze kasi ya utekelezaji. Kamati inaamini kwamba kupatikana kwa mfuko huu kutarahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na kupunguza utegemezi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; katika mwaka wa fedha 2017/2018, Fungu 31 hakuna mapato yatakayokusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla wake na kubaini kuwa mahitaji ya bajeti ya usimamizi na hifadhi ya mazingira ni makubwa kuliko kiasi kilichotengwa. Kamati haikuridhishwa na ukomo wa bajeti unaopitishwa kwa ajili ya Ofisi hii kwa kuwa haiendani na umuhimu wa ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) inaomba kuidhinishiwa shilingi 15,200,988,437 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha zinazoombwa shilingi

10,634,020,440 ni kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira, ambapo shilingi 6,788,452,437 ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 3,845,568,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za matumizi ya kawaida shilingi 2,215,044,000 ni ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, na kiasi kinachosalia cha shilingi bilioni 1,630,524,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi cha ruzuku kinachoombwa kwa ajili ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ni shilingi 2,215,044,000 kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia 4.3 ikilinganishwa na shilingi 2,314,680,000 bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Idara ya Mazingira imepangiwa jumla ya shilingi 3,845,568,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida; kiasi hiki ni zaidi kwa asilimia 5.5 ikilinganishwa na shilingi 3,647,654,000 bajeti inayotekelezwa sasa. Fedha zinazoombwa kwa ajili Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa kwa ajili ya miradi ya maendekeo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni shilingi 6,788,452,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kwamba Ofisi ya Makamu wa Raisi inaendelea kufanya mawasiliano na washirika wa maendeleo ambao wameonesha nia ya kusaidia katika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati...

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa muda wako umekwisha, umeshaumaliza, omba pesa, toa hoja umalize.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba yote niliyosoma yaingie kwenye *Hansard*, lakini kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa maoni, michango na mawazo yao mbalimbali katika kukamilisha taarifa hii, orodha yao ni ndefu naomba nisiisome.

Mheshimiwa Mwenyetiki, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa January Makamba, (Mbunge) na Naibu wake Mheshimiwa Luhaga Mpina, Makatibu Wakuu, watendaji wote wa Wizara kwa kutoa ufafanuzi mzuri wakati wa uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelezo mbalimbali ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za kamati.

Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, Mkurugenzi Idara ya Kamati na Wakurugenzi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio na Mapato na Matumizi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Fungu 31 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo ni kiasi cha shilingi 15,200,988,437.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante!

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA CHINI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) FUNGU 31 KWA MWAKA 2016/2017 NA MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya hifadhi na usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Fungu 31 kwa Mwaka 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,**pamoja na nia nzuri ya Serikali katika kudhibiti kasi ya uharibifu wa mazingira na athari za mabadiriko ya tabianchi bado jitihada za ziada zinahitajika. Shughuli za kibinadamu ndicho chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira ikiwemo shughuli za Kilimo na Ufugaji usiozingatia taratibu; uvunaji wa misitu usiozingatia taratibu; na uvuvi haramu. Kwa muktadha huu Serikali inatakiwa kuchukua hatua za makusudi za kusimamia na kuhifadhi mazingira kwani kukwepa gharama za kutunza mazingira ni kukaribisha janga kwa nchi yetu na vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za kudumu za Bunge katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017, kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za kudumu za Bunge Kamati ilipokea na kujadiri Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa mwaka

wa fedha 2016/2017 na kuchambua Mpango na Bajeti kwa mwaka fedha wa 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inalenga kuliomba Bunge lako tukufu kuidhinisha maombi ya Fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, lakini pia kutoa mapendekezo kwa Bunge kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi katika kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2016/2017 NA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 2.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilijikita katika kuchambua mwenendo wa upatikaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi ya maendeleo pamoja na fedha zilizotengwa ili kutekeleza majukumu mengine ya Ofisi. Katika kufanya Uchambuzi Kamati ilitumia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Taarifa ya ziara kwenye Miradi na mahojiano wakati wa vikao.

#### 2.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/ 2017 Ofisi ya Makamu wa Rais haikuwa na makusanyo ya Maduhuli.

#### 2.1.2 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha **2016/2017** Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **20,386,699,448.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi

**9,413,616,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **10,973,083,448.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika shilingi **9,413,616,000.00**ambazo nibajeti ya matumizi ya kawaida Shilingi **2,846,299,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishina na Shilingi **6,567,317,000.00** ni za matumizi mengineyo. Kati ya fedha za matumizi mengineyo zilizoidhinishwa Shilingi **2,314,680,000.00** ni ruzuku ya mishahara kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) na kiasi kinachosalia Shilingi **4,252,637,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo(OC) katika Idara na Vitengo vya Ofisi ya Makamu wa Rais.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha za miradi ya maendeleo Shilingi **10,973,083,448**.00 zilizoidhinishwa, Shilingi **8,000,000,000.00**ni fedha za ndani na Shilingi **2,973,083,443.00** ni fedha za nje.

**Fedha zilizopokelewa hadi 15 Machi, 2017**

**Mheshimiwa Spika,** kati ya Shilingi **20,386,699,448.00** zilizoidhinishwa kwa ajiliya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, ni Shilingi **7,793,493,737.18** tu ndizo zilikuwa zimetolewahadi kufikia 15 Machi, 2017. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **38.2**ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,**Kati ya Shilingi **9,413,616,448.00** zilizoidhinishwa kwa ajili matumizi ya kawaida ni Shilingi **6,555,916,168.68**tu ndizo zilizokuwazimetolewa. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **69.9** ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida Shilingi**1,905,596,990.00**ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi **2,964,514,853.84** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo(OC).

Kati ya fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa Shilingi **51,040,660.00**zililipa madeni ya watumishi, Shilingi **177,093,664.84** zililipia madeni ya wazabuni na Shilingi

**1,457,670,000.00** ni ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kiasi kinachosalia kwaajili ya uendeshaji wa Ofisi ni Shilingi **1,278,710,526.00** ambazo hazikukidhi mahitaji halisi.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya Shilingi **10,973,083,448.00** zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ni Shilingi **1,237,577,568.50** tu ndizo zilizopokelewa sawa na asilimia **11.3** ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Aidha kati ya Shilingi **8,000,000,000.00** za bajeti ya fedha za ndani ni Shilingi **236,186,455.00** tu ndizo zilizopokelewa sawa na asilimia **2.9** ya bajeti yote ya fedha za ndani na Shilingi **2,973,083,443.00** za bajeti ya fedha za nje ni **1,001,391,113.50** tundizo zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia **33.6** ya bajeti yote ya fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida umeonekana kuwa wakuridhisha kwa kuwa unachangiwa na fedha za mishahara ambazo hutolewa kila mwezi. Katika bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira, upatiakanajiwa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na miradi ya maendeleo sio wa kuridhisha hivyo kupelekea kukwamisha utekelezaji wa mipangoya Wizara.

## 2.2 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 2.2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** jedwali lifuatalo linaonyesha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017 na upatikanaji wa fedha.

| Mradi Na. | Jina la Mradi | Fedha zilizoidhinishwa 2016/17 | | Fedha zilizotolewa hadi tarehe 15 Machi, 2017 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Fedha za Ndani Sh. | Fedha za Nje Sh. | Fedha za Ndani Sh. | Fedha za Nje Sh. |
| 5301 | Climate Change Adaptation Programme | 3,200,000,000 | 2,694,633,448 | 0 | 911,151,113.5 |
| 5304 | Ozone Depleting Substances Project | 80,000,000 | 147,000,000 | 0 | 0 |
| 5305 | Stockholm Convention Implementation Project | 120,000,000 | 131,450,000 | 0 | 90,240,000.0 |
| 5307 | The National Environmental Trust Fund | 2,100,000,000 | 0 | | |
| 6309 | Construction of VP Office and Residence in Znz | 700,000,000 | 0 | 236,186,455 | 0 |
| 6389 | Construction and of VP Office Luthuli & Rehabilitation of State Lodges | 700,000,000 | 0 | | |
| 6569 | Lake Tanganyika Env. Mng. Programme | 600,000,000 | 0 | 0 | 0 |
| 6571 | EMA Implementation Support Programme | 500,000,000 | 0 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **8,000,000,000** | **2,973,083,448** | **236,186,455** | **1,001,391,113.5** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika bajeti ya 2016/2017 kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira Fungu **31**, iliidhinishiwa shilingi **5,894,633,000.00** kwa ajili ya Mradi namba 5301 wa *Climate Change Adaptation Programme* ambao ni mradi wa Ujenzi wa ukuta katika Ukanda wa Pwani na

Zanzibar kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko la usawa wa bahari linalosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Maeneo ya mradi huu ni Ocean Road, Kigamboni, Pangani, Kisiwa Panza (Pemba) na Kilimani Unguja.Hata hivyo kwasababu ya ufinyu wa muda Kamati ilifanikiwa kutembelea na kujionea hali ya utekelezaji wa Mradi huu katika eneo la Pangani na Ocean Road.

### 2.2.2 Mradi wa Mabadaliko ya Tabianchi

**Mheshimiwa Spika**, mabadiriko ya tabianchi yamesabisha kuongezeka kwa usawa wa bahari (sea level rise) kwa sentemita **19** katika kipindi cha miaka **50** iliyopita. Ongezeka la usawa wa bahari linachangia uharibifu wa mwambao wa Pwani, na kutoweka kwa baadhi ya visiwa kama; Panza Zanzibar, Maziwa Pangani, Fungu la Nyani Rufuji, na baadhi ya visima vya maji baridi katika maeneo ya Bagamoyo kuharibiwa na maji chumvi. Maisha ya wananchi wanaoishi katika mwambao wa Bahari ya Hindi na kutegemea Bahari yapo hatarini kutokana na kumomonyoka kwa fukwe na upotevu wa viumbe baharini.

### i) Ujenzi wa Ukuta wa Pangani

Ujenzi wa Ukuta wa mto Pangani unajumuisha urefu wa meta 950 kwa upande wa Kaskazini yaani Pangani Mjini na meta 660 upande wa Bweni. Ujenzi wa ukuta huu ulianza rasmi tangu tarehe 01Machi, 2017, Mkandarasi aliyepewa kazi hii ni DEZO Civil Contractors. Mradi huu unakisiwa kuwa utagharimu kiasi cha Shilingi **2.4** bilioni mpaka utakapokamilika. Mradi unatekelezwa kwa fedha za wafadhili kwa asilimia **90,** kiasi cha Shilingi **2.4** bilioni ambazo zimekwishatolewa kwa upande wa Pangani Mashariki, wakati asilimia **10** ya fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu kwa upande Pangani Magharibi bado hazijatolewa.Mradi huu unatarajiwa kukamilika Novemba, 2017 iwapo mipango yote itakwenda kama iliyopangwa.

**CHANGAMOTO**

**Mheshimiwa Spika,**Mradi huu unakabiliwa na Changamoto kuu tatu kama ifuatavyo:-

- Kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa ukuta wa mto wa Pangani kumecheleweshа juhudi za kuanza mchakato wa kuanza upembuzi yakinifu kwa upande wa PANGADECO;

- Kuendelea kuharibika kwa eneo la PANGADECO ambapo hali ni mbaya na eneo hili la ufukweni mwa mji wa Pangani ni hatarishi kwa maisha ya wanadamu kwahiyo zinahitajika juhudi mahususi ili kukabiliana na athari hizo.

- Upande wa Pangani Mashrariki mradi unatekelezwa kwa fedha za Wafadhili hivyo utekelezaji wake unaendelea. Katikaupande waPangani Magharibi mradi unatekelezwa kutokana na fedha za ndani. Serikali bado haijapeleka fedha ilizotenga hivyo kuchelewesha utekelezaji na uharibufu kuongezeka kwa kadri siku zinavyokwenda.

**ii) Ujenzi wa Ukuta wa Ocean Road**

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa eneo la *Ocean Road.* Hali ya utekelezaji wa Mradi inaendelea vizuri Mkandarasi amekwisha anza kazi baada ya kupata fedha za wafadhili kutoka *Adaptation Fund*. Kamati inapongeza hatua ya Wizara ya kuamua kutafuta wafadhirina kuutekeleza mradi huu kwa haraka. Kwani utekelezaji wa mradi huu utasaidia kukabiliana na kupungua athari za mabadiliko ya tabia ya nchi yanayosababisha ongezeko la kina cha Bahari yetu.

**2.2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2016/207**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilishauri kuwa Serikali itoe kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya uhifadhi wa Mazingira kwa kutenga fedha za kutosha lakini pia fedha

hizo zitolewe kwa wakati. Kwa Mfano Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira mpaka kufikia tarehe 30 Januari, 2017 ilikuwa hajiapokea kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo jambo linalokwamisha utekelezaji wa Miradi hiyo.

i) Kamati inaishauri Serikali kuwa pamoja na nia yake nzuri ya kusimamia uhifadhi wa Mazingra nchini, iangalie namna ya kuongeza bajeti ya Mazingira. Jambo hili litawezesha kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira na kupunguza uhitaji wa fedha nyingi zinazotumika katika kurekebisha miundombinu za kimazingira na uoto wa asili. **(usipoziba ufa utajenga ukuta);**

ii) Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, kwa jitihada wanazozifanya za kutafuta wahisani ili kulinusura Taifa na janga la uharibifu wa mazingira. Kamati inawaomba waendelee na juhudi za kutafuta fedha kutoka kwa wahisani mbalimbali ilikuongezea kwenye fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya bajeti ya mazingira; na

iii) Katika mradi wa Pangani Serikali ipeleke fedha za bajeti ya ndani asilimia **10** ya fehda zote za mradiili utekelezaji usikwame.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KUHUSU BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali na kutoa maagizo nane (8). Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maeneo ambayo serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii;

i) ***Serikali ianze kutekeleza ujenzi wa vituo vya kupumzikia wasafiri na wasafirishaji wanaotumia barabara kuu nchini haraka iwezekanavyo***.

Agizo hili lilikuwa miongoni mwa maagizo ya kamati katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 na kwa mwaka huo wa fedha Serikali ilifanikiwa kujenga kituo kimoja tu katika Wilaya ya Mufindi Mkoani Iringa. Agizo hili liliendelea kusisitizwa na Kamati na kuwa miongoni mwa maagizo ambayo yatatekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Maelezo ya Serikali kuhuusu utekelezaji wake ni kuwa, Ofisi inaendelea kuhamasisha wadau wa mazingira na sekta binafsi kujenga vituo hivyo. Pia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imetambua maeneo ya ujenzi wa vituo hivyo katika mpango wa ujenzi wa barabara kuu. Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa agizo hili, pia inaitaka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kubainisha kuwa imebaini uhitaji wa Vituo vingapi na ujenzi utaanza lini kuazia sasa.

ii) ***Bajeti ya kuendeleza upandaji wa miti iongezwe. Aidha vyanzo vya fedha kwa ajili ya Mfuko wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira vitokane pia na Wizara nyingine. Vyanzo hivyo vitambuliwe na kuhamishiwa katika Mfuko.***

Serikali ilitoa maelezo kuwa zoezi la upandaji miti linafanya na kila wilaya na kusimamiwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambapo kila wilaya hutakiwa kupanda miti **1,500,000** kila mwaka. Kamati na inaamini kuwa miti **1,500,000** ni miti mingi sana kiasi kwamba kama ingekuwa imepandwa tayari athari (impact) yake ingekuwa imeonekana. Kamati inashauri agizo hili litekelezwa kwa haraka na baada ya kupandwa kuwa na ufuatiliaji kuhakikisha inakua.

**Mheshimiwa Spika,**kwa upande wa Mfuko wa Mazingira Kamati ilielezwa kwamba usimamizi wa Mazingira kwa kipindi cha 2016/2017 Serikali imezindua rasmi Mfuko wa Mazingira na Bodi ya wadhamini wa Mfuko imezinduliwa. Mapendekezo ya vyanzo vya Mapato vya Mfuko kutoka sekta nyingine yamewasilishwa Serikalini kwa ajili ya maamuzi.

Kamati inapongeza Serikali kwa hatua iliyofikia lakini iongeze kasi ya utekelezaji. Kamati inaamini kwamba kupatikana kwa Mfuko huu kutarahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa RaisMazingira na kupunguza utegemezi kutoka Serikalini.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, **Fungu 31** hakuna mapato yatakayokusanywa.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Raisi kwa ujumla wake na kubaini kuwa Mahitaji ya bajeti ya usimamizi na hifadhi ya mazingira ni makubwa kuliko kiasi kilichotengwa. Kamati haikuridhishwa na ukomo wa Bajeti unaopitishwa kwa ajili ya Ofisi hii kwakuwa haiendani na umuhimu wa Ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha **2017/2018** Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inaomba kuidhinishiwa Shilingi **15,002,988,437.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha zinazoombwa Shilingi **10,634,020,440.00**ni kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira, ambapo Shilingi **6,788,452,437.00** ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na Shilingi **3,845,568,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Kati ya fedha za matumizi ya kawaida Shilingi **2,215,044.000.00**ni ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kiasi kinachosalia Shilingi **1,630,524,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi cha ruzuku kinacho ombwa kwa ajili ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ni Shilingi **2,215,044.000.00.**

Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **4.3** ikilinganishwa na Shilingi **2,314,680,000.00** bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha **2017/2018** Idara ya Mazingira imepangiwa jumla ya shilingi **3,845,568,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.Kiasi hiki ni zaidi kwa asilimia **5.5** ikilinganishwa na Shilingi **3,647,654,000.00** bajeti inayotekelezwa sasa.

**Mheshimiwa Spika**, fedha zinazoombwa kwa ajili Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kwa kwa ajili ya miradi ya maendekeo kwa mwaka wa fedha**2017/2018** ni Shilingi **6,788,452,437.00.**Kiasi hiki nipungufu kwa asilimia **38**ikilinganishwa na Shilingi **10,973,083,448.00** zilizoidhinishwa mwaka wa fedha **2016/2017**. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,000,000,000.00**ni fedha za ndani na Shilingi **3,788,452,437.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba Ofisi ya Makamu wa Raisi inaendelea kufanya mawasiliano na washirika wa maendeleo ambao wameonesha nia ya kusaidia katika maeneo ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi na matumizi endelevu ya kemikali. Ofisi pia imekamilisha mapendekezo ya vyanzo vya mapato na viwango vya uchangiaji kwa sekta nyingine katika Mfuko wa Mazingira. Mapendekezo haya yatawasilishwa katika ngazi husika kwa ajili ya maamuzi na utekelezaji.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1 HALI YA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika**, idadi ya Watanzania kwa sasa inakisiwa kuwa milioni **51**, ambapo inakisiwa kuwa kuna ongezeko la asilimia **2.7** kwa mwaka, na kuwa kutakuwa na watu milioni **100** ifikapo mwaka **2035.** Ongezekohili linaashiria ongezeko la mahitaji ya rasimali za asili hasa ardhi na misitu.

**Mheshimiwa Spika**, asilimia **90** ya nishati inayotumika nchini inatokana na misitu na hii inachangia upotevu wa

misitu yetu kwa asilimia **70**. Mfano Dar es Salaam peke yake hutumia magunia **200,000-300,000** (yenye wasitani wa kilo **50**) kila moja kwa mwezi ambayo kwa mwaka ni sawa na tani laki tano **(500,000).**

Aidha, Wastani wa matumizi ya magogo/kuni kwa mtu mmoja kwa mwaka ni wastani wa mita moja ya ujazo **(1m)** ambayo ni takribani mita za ujazo milioni **50**za magogo kwa mwaka kwanchi nzima. Madhara ya ufyekaji wa misitu ni pamoja na uharibifu wa mazingira inaharibu mifumo ya hewa na kusababisha mabadiriko ya tabianchi vilevile upungufu wa mvua.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia mwenendo wa uharibifu wa mazingira nchini zinahitajika jitihada za mahsusi za kuhifadhi mazingira. Hatua ambayo itaepusha gharama kubwa zinazotumika kurekebisha miundombinu mbalimbali ya kimazingira katika nchi yetu (mfano mikondo na maporomoko ya maji).

## 5.2 MAONI NA USHAURI

**Mheshimiwa Spika,** suala la uhifadhi wa Mazingira ni suala mtambuka hata hivyo linazihusu zaidi Wizara tatuMaliasili na Utalii, Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira na Wizara ya Kilimo na Mifugo ambapo imeonekena kuwa na muingiliano wa sheria.Kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kunamuingiliano katika sheria za misitu. Ambapo Wizara ya Maliasili na utalii misitu ni chanzo cha mapato, na Wizara ya Kilimo ya Mifugo inatumia misitu kama maeneo ya kilimo na malisho ya mifugo wakati Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inasimamia katika kuhifadhi misitu.Kamati inaishauri Serikalikuziangalia upya sheria zetu na kuhamasishaWizara hizi zifanye kazi kwa pamoja kwa manufaa ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, tozo zinazotokana na shughuli zinazochangia uharibifu wa mazingira ni nyingi lakini zinakusanywa na Taasisi au Idara nyingine za Serikali. Kamati inashauri tozo hizo walau kwa asilimia **5** ziingie katika mfuko

wa mazingira. Mfano tozo ya magari chakavu, tozo ya mkaa, tozo ya mafuta, tozo ya magogo n.k;

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mazingira nchini ipo lakini haijasimamiwa ipasavyo katika maeneo mengi nchini hivyo kundelea kushamiri kwa uharibifu wa Mazingira. Kamati inaishauiri Serikali kusimamia Sheria hiyo kikamilifu ili kulinusuru Taifa letu na kupunguza uwezekano wa kukumbwa na mabadiriko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza jitihada za upandaji miti aina ya mikoko katika mwambao wa bahari ya Hindi, pia udhibiti wa ukataji haramu wa mikoko unaofanywa na wananchi waishio katika mwambao wa bahari ya Hindi uimarishwe;

**Mheshimiwa Spika**, miradi mingi ya mazingira haikufanikiwa kutokana na ushirikishwaji mdogo wa jamii katika utekelezaji wake. Mfano mradi wa upandaji miti na mradi wa kukabiliana na mabadiliki ya tabianchi, wakati Serikali inasisitiza upandaji wa miti wananchi wamekuwa wakivuna miti bila utaratibu maalumu hivyo kusababisha majanga. Kamati inaishauri serikali iendelee kukuza uelewa kwa jamii kwa kuwashirikisha kikamilifu katika kutekeleza miradi yake ya mazingira;

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko la watu linalokadiriwa mpaka kufikia 2035 linaashiria ongezeko kubwa la uhitaji wa rasilimali hususani misitu kwa ajili ya nishati. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mkakati wa makusudi wa kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya utumiaji wa teknolojia za nishati mbadala (majiko bunifu na umeme wa jua) ili kupunguza uvunaji wa misitu kwa ajili ya nishati. Mkakati huu uweze kumsaidia mwananchi kuyatunza mazingira wakati huohuo anapata nishati mbadala kwa bei nafuu;

**Mheshimiwa Spika**, Mazingira ni suala mtambuka lakini katika Wizara na Idara za Serikali hakuna kifungu cha bajeti ambacho kinatengewa fedha kwa ajili ya masuala

yanayohusu mazingira. Hapo awali vifungu hivi vilikuwepo katika bajeti za Wizara zote ila viliondolewa na Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuwa katika bajeti za Wizara, Mikoa, Wilaya na Halmashauri zote nchini kuwe na kifungu cha bajeti ya Mazingira;

**Mhesimiwa Spika**, Kamati inaendelea kusisitiza suala la Serikali kukutana na wadau wa plastiki na kufanya mazungumzo ili kupata muafaka wa namna ya kusitisha utengenezaji wa bidhaa za plastiki bila kuathiri ajira na uwekezaji uliofanyika.

Seriakali itoe muda wa kutosha kwa wadau kuhamia katika teknolojia itakayowawezesha kuzalisha plastiki rafiki kwa mazingira ambazo pindi zitakapo kutana na jua na mvua zitaoza kwa haraka. Serikali iongeze nguvu katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya athari za uharibifu wa mazingira na umuhimu wa utunzaji wa mazingira; na kuhimiza uanzishwaji wa Viwanda vinavyotumia taka za plastiki kama malighafi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba suala mazingira linazungumzwa sana na viongozi wa Serikali, viongozi wa dini na Asasi mbalimbali za kiraia lakini halijapewa umuhimu unaostahili na Serikali yetu. Kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta ya mazingira katika Mikoa na Halmashauri zetu jambo linalosababisha ugumu katika kupambana na janga hili. Kamati inaishauri Serikali iangalie upya ajira za maafisa mazingira katika Mikoa na Halmashauri zote nchini. Hatua hii itasaidi katika utekelezaji wa masuala yanayohusu mazingira.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa maoni, michango na mawazo yao mbalimbali katika kukamilisha taarifa hii. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini.

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo Mb. | Mwenyekiti |
| (ii) | Mhe. Vicky Passcal Kamata, Mb | Mjumbe |
| (iii) | Mhe. Salim Hassan Turky, Mb | Mjumbe |
| (iv) | Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb | Mjumbe |
| (v) | Mhe Dkt. Dalaly Peter Kafumu | Mjumbe |
| (vi) | Mhe. Khatib Said Haji, Mb | Mjumbe |
| (vii) | Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb | Mjumbe |
| (viii) | Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb | Mjumbe |
| (ix) | Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | Mjumbe |
| (x) | Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb | Mjumbe |
| (xi) | Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa,Mb | Mjumbe |
| (xii) | Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb | Mjumbe |
| (xiii) | Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb | Mjumbe |
| (xiv) | Mhe. Balozi Dkt Diodorus Kamala, Mb | Mjumbe |
| (xv) | Mhe. Jesca David Kishoa, Mb | Mjumbe |
| (xvi) | Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb | Mjumbe |
| (xvii) | Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb | Mjumbe |
| (xviii) | Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb | Mjumbe |
| (xix) | Mhe. Faida Mohammed Bakar, Mb | Mjumbe |
| (xx) | Mhe. Suleiman Ahmed Sadick, Mb | Mjumbe |
| (xxi) | Mhe Ibrahim Hassanali Raza, Mb | Mjumbe |
| (xxii) | Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb | Mjumbe |
| (xxiii) | Mhe. Dkt. Raphael MMasunga Chegeni, Mb | Mjumbe |
| (xxiv) | Mhe. Sylvestry Francis koka, Mb | Mjumbe |
| (xxv) | Mhe. Gimbi Dotto Massaba, Mb | Mjumbe |
| (xxvi) | Mhe. Martha Mosses Mlata, Mb | Mjumbe |
| (xxvii) | Mhe. Joyce John Mukya, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu Rais Mungano na Mazingira, Mhe.January Y Makamba, Mbna Naibu wake Mhe. Luhaga Joelson Mpina, MbMakatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kutoa ufafanuzi mzuri wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati

Bw. Athumani Hussein, Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Bw. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira Fungu 31 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo ni kiasi cha Shilingi **15,002,988,437.00**.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**

24 Aprili, 2017

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo. Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Katibu wa Waheshimiwa Wabunge wa CCM anaomba Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi leo, baada ya kuahirishwa Bunge saa mbili usiku kutakuwa na *caucus,* kwa hiyo wote mnaombwa kuhudhuria na mahudhurio yatazingatiwa.

Sasa ninamwita Msemaji Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano. *(Makofi).*

**MHE. ALLY SALEH ALLY – MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kusoma hotuba hii, napenda kusema kwamba itakuwa muda mfupi kwa hiyo yale yote nitakayoyasema na ambayo yapo katika hotuba hii yaingizwe katika *record.* Lakini la pili napenda kumhakikishia sahibu yangu Mheshimiwa January Makamba,

kwamba mimi ni muumini wa Muungano lakini wa haki, usawa na mamlaka kamili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutupa uhai ili kufanya kazi hii ya kitaifa. Pia tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa shani yake alivyoamua kuwapenda zaidi Wabunge wenzetu wawili, sahibu yangu Marehemu Hafidh Ali Tahir na Marehemu Dkt. Elly Macha ikiwa ni ukumbusho kwetu kuwa dunia ni mapito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Mbowe pamoja na Mwenyekiti wa Kambi ya CUF Mheshimiwa Riziki Shahari kwa kutupa nguvu zilizotufanya UKAWA kuwa wamoja na kuwajibika kama wapinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kushuhudisha mengi yaliyotokea ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na nusu kwa sababu Wabunge wote wanayajua kama vile wananchi wanavyoyajua. Kwa ujumla tumefanya kazi yetu hapa Bungeni kama wapinzani iwe ya vuta ni kuvute na kuzongwa na changamoto zisizo na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni bajeti ya pili tokeo Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ambapo Mheshimiwa Rais Magufuli ameshika uongozi wa nchi. Imekuwa ni bajeti ngumu kutekelezwa kwa ushahidi wa fedha zilizotolewa ukilinganisha na zile zilizotengwa. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Wizara imekiona cha moto maana wamebanwa mpaka wamevunjwa mbavu. Eneo la miradi ya maendeleo limeumia zaidi...(Makofi/Kicheko)* **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alberto subiri kidogo.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu chini ya Kanuni ya 64(2) inasema; "Mbunge yeyote anayeamini kuwa Mbunge mwingine amevunja au amekiuka fasili ya (1) ya kanuni hii, atasimama mahala pake na kumwambia Spika wa Bunge "Kuhusu Utaratibu..."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a) inaelekeza Wabunge au taarifa ambazo si za kweli zisiletwe ndani ya Bunge. Maneno yanayosema kwamba kila Wizara imekiona cha moto maana wamebanwa mbavu wamevunjwa mbavu si ya kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujumbe wa Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani ungeweza kufika tu kwa yale maneno yanatosha. Ungeweza kusema kwamba fedha hazikutolewa za kutosha, lakini kwamba wamebanwa mpaka wamevunjwa mbavu na wakati watu hawajavunjwa mbavu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa aliondoe kwenye hiyo.

**MBUNGE FULANI**: Vionjo hivyo!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Hilo si vionjo, *this is not a term of art,* hii si fasihi. Lingine ni hili ambalo sio la kweli linalosema ukurasa wa...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima hebu subiri kidogo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata fursa ya kusoma hii.

**MWENYEKITI:** Wewe endelea.

**MWANASHERIA MKU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata fursa ya kuisoma hii taarifa yote, hatuwezi kuruhusu mambo ambayo ni kinyume cha Sheria na Katiba hapa. Tuyamalize kabisa kusudi tumelizane; na bahati nzuri Mheshimiwa Ally Saleh ni *classmate* wangu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hayo mambo yangewekwa na mtu ambaye ni *layman* tungeelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niseme kuwa pia maneno katika ukurasa wa tatu yanayosema...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa anawahisha Shughuli ya Bunge huyu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**:...kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa muhanga mkubwa wa kiti cha ngariba...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG,* twende kwa hatua.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaleta mgongano humu usiokuwa na sababu, kusimama simama.

**MWENYEKITI:** Usipate taabu nitakusaidia tu. Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumuombe asikiuke Kanuni kwa kuwahisha shughuli kwa kusoma kurasa ambazo hazijafikiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima endelea na hoja yako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** taarifa ninayompa, *facts* za taarifa za kamati, zinaonesha kwamba kwenye bajeti tuliyopitisha mwaka 2016/2017 bajeti ya fedha za kawaida fedha zilizotolewa hazizidi hata asilimia 70. Ukija kwenye bajeti

ya fedha za maendeleo, fedha zilizotolewa hazizidi asilimia 26 na Wizara tunayoijadili leo wamepata pungufu ya asilimia mbili, na taarifa za kamati zina sema hivo. Sasa kuna shida gani msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani akisema Wizara zimebanwa mbavu, tafsiri ya kubanwa mbavu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninampa taarifa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kaa chini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hoja anazozitoa ni za uongo na hazina ukweli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima kaa chini.

Waheshimiwa Wabunge, changamoto za bajeti hazipo Tanzania peke yake, na lugha za kutumia Bungeni zipo lugha sahihi ambazo zinatakiwa zitumike kistaarabu. Mnaweza kujenga hoja ya msingi kabisa, bajeti iliyotengwa changamoto zake hazikufikia malengo, *fine.* Sasa unapoanza kusema kila Wizara ina imekiona cha moto maana wamebanwa mpaka wamevunjwa mbavu. Kuna Waziri ambaye amevunjwa mbavu hapa? *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, naelekeza Mheshimiwa Alberto, kipande hiki kila Wizara... yatoke. Na ninaelekeza Katibu maeneo haya ukurasa wa pili, kila Wizara imekiona mpaka inapoishia mbavu yatoke kwenye *Hansard*. Endelea Mheshimiwa Saleh na ninaomba Waheshimiwa Wabunge hii bajeti itapita kwa utulivu na kwa kuelewana na kwa amani, mihemuko sitaki. *(Makofi)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY – MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea naomba unitunzie muda wangu. Lakini la pili pia msemaji aliyeinuka alisema nifute maneno kisu cha ngariba, je, na hayo pia tuyafute kwa sababu yapo mengi ya kuonesha kwamba bajeti haikutimizwa kama inavyotakiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alberto twende hatua na kwa hatua tutafika tu.

**MHE. ALLY SALEH ALLY- MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona Bunge ambalo likikutana pembeni na nilijua haya yatatokezea, walikuwa wakikutana lakini tutakwenda, haya sawa. Eneo la miradi ya maendeleo limeumia zaidi, huko asilimia zilizopelekwa mpaka zimeona aibu kutajwa hadharani.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watu wanasema kuna hatua iliyopigwa katika miradi basi itakuwa ni ile iliyopendelewa na kiongozi wa nchi lakini si ile ambayo Bunge ilipangia kutekeleza, ile ambayo inagusa maslahi ya kila mwananchi. Katika hali hiyo Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa mhanga mkubwa wa kisu cha ngariba. Fedha iliyoweza kushushiwa hazifanani na hadhi ya ofisi hii. (Makofi/ Kicheko)* **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG* ninakuruhusu ukurasa wa tatu tafuta maneno ambayo yanakiuka Kanuni ili ushauri!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua suala hapa kama ulivyokuwa umeelekeza ni lugha inayotumika na kanuni zetu zinakataa kutumia lugha ya kudhalilisha au ya kuudhi. Hizi fedha zinagawiwa kwa kisu? *That is the question here.* Hivi fedha hizi zinagawiwa kwa kisu? Na huyo anayegawa kwa kisu ni nani? Na ngariba ni nani? Yaani kugawa fedha ni kutahiriwa? *That is not so,* tutumie lugha nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba kushauri hii nayo tuiondoe. Mheshimiwa Ally Saleh angeweza ku-*communicate* tu kwamba fedha ambazo zimekuwa zikitolewa hazitoshi. Lakini hata hivyo mwaka wa fedha haujaisha. Inawezekana kuna changamoto sasa, lakini pia mwaka wa fedha haujaisha. Kwa hiyo, si kwamba hii lugha inadharilisha na kuudhi tu lakini pia si ya ukweli, kanuni zetu

zinatukataza kwa sababu fedha hazitolewi kwa njia ya visu. Kwa hiyo, ninaomba kumshauri Mheshimiwa Saleh, Mbunge, hii nayo aiondoe hii pia. *(Makofi)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY – MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** *Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa Waziri anayehusiana na mambo ya Kiswahili ananyamaza kimya, hainuki akasema kwamba hizi ni tamathali za semi ni maelezo ya Kiswahili. Ni tasbihi kuonyesha kwamba mgawaji wa fedha ameweza kuipa Wizara ya Mawasiliano asilimia 200 lakini wengine akawapa asilimia kumi, huyo ndiye ngariba. (Makofi)* **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh, katika hali ya Ofisi ya Makamu wa Rais, imekuwa mhanga wa kisu cha ngariba. Unapoelekeza hivi unamgusa mtu moja kwa moja kwa lugha ambayo haifai.

**MHE. ALLY SALEH ALLY – MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, yupi huyo?

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Waheshimiwa hebu tuwe na amani humu ndani, maana mkitaka kuleta mikwara mimi nina mikwara mingi hapa. Nina kadi nyekundu, kadi ya njano, leo ngariba naweza kuwa mimi nikawaumiza. *(Kicheko/ Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Ally Saleh zipo lugha nyingi za Kibunge, Kiswahili kipo, kinafahamika. Kwani ukimwambia mtu mkwara huko mjini ni neno la kawaida? Lakini huwezi kumwambia mtu mkwara ndani ya Bunge. Kwa hiyo suala la ngariba tunalitoa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY – MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea!

**MWENYEKITI:** Tunaendelea.

**MHE. ALLY SALEH ALLY- MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, mantiki kwa hali inavyokwenda hivi sasa inatupa tuamini kuwa Muungano si ajenda kubwa ya awamu hii kutokana na matendo ambayo tunayaona. Kama hali hii itaendelea kama ilivyo basi tunaona kuwa kidagaa kitamuozea mtu mkononi na maiti ataipakata yeye. (Kicheko/Makofi)* **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG,* Mheshimiwa Msigwa kaa kwanza.

**MBUNGE FULANI:** Kiswahili cha Kizanzibari hicho, mambo ya nahau.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza maneno ya kwamba Muungano si ajenda ya Serikali hii si ya kweli, ayaondoe tu. Lakini pamoja na hayo hata yale yanayofuatia pale, hivi kwa mfano unasema kwamba ishara ni pamoja na kukataa kabisa kuwa Serikali ya Muungano ni sehemu suluhu ya Muungano unaoendelea kwa kudhani kuwa Dkt. Ali Mohamed Shein kuendelea kukalia kiti kisicho chake.

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Haya na yenyewe, kwanza yale ya kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano haitilii mkazo Muungano si ya ukweli, ningeshauri ayaondoe. Pia mambo yote, ukurasa wa tatu mpaka wa nne, yanayohusina na Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar ambao unatawaliwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 yaondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili linasimamia Katiba ya Muungano, halisimamii Katiba ya Zanzibar, na Katiba ya Zanzibar si moja wapo ya masuala ya Muungano, kwa hiyo

mambo yote yanayohusiana na uchaguzi mkuu wa Zanzibar ukurasa wa tatu na nne nilikuwa pia naomba ayaondoe.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Sijui kwa nini tunarudia rudia, kwenye Kanuni zetu 64, naomba nisome mwanzoni na imeeleza mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Lakini inasema bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo ya majadiliano katika Bunge...

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo chini Kanuni zetu zimefafanua mambo ambayo yamekatazwa. Hili Bunge letu linaendeshwa kwa Kanuni, lakini vile vile linaendeshwa kwa utamaduni wa Mabunge ya *commonwealth.* Lakini mojawapo ya kanuni ambayo haiwezi kupindishwa kwenye *tradition* za *commonwealth* ni kwamba walio wachache wasikilizwe, walio wengi watoe maamuzi. Sasa Serikali hata sisi tulio wachache tunapojaribu kutoa *opinion* zetu, tunapotoa mawazo yetu nayo tunazuiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka nijue hivi *tradition* ya Bunge hii ni ipi? Maana kila tunachokiweka hapa *AG* badala ya kuisaidia Serikali kuinyoosha ifanye mambo vizuri amekuwa mtetezi na *AG* anapotosha hapa kwa sababu yeye ni mwanasheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndio mtazamo wetu na ndiyo maana ya upinzani, sasa tunatumia *tradition* gani ya Bunge? Ili lieleweke ni *Commonwealth Parliament* au ni Bunge la wapi? Kwa sababu kila tunachoandika kinapingwa, sasa tumekuja kufanya nini hapa? Hatupo kwa ajili ya kuwasiliza ninyi hapa, tuna mawazo yetu sisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante umeeleweka. Waheshimiwa Wabunge, na inawezeka kuwa ni kwa sababu chini ya awamu hii hakuna mkazo mkubwa katika Muungano...

**MHE. ALLY SALEH ALLY – MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Mantiki inatupa tuamini kuwa Muungano si ajenda kubwa ya awamu hii.

**MHE. ALLY SALEH ALLY – MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Ndivyo ninavyoamini.

**MWENYEKITI:** Ukija kwenye taarifa ya Waziri, ukurasa wa 44 utafiti na utafutaji wa uchimbaji wa gesi na mafuta, ofisi itaendelea kuratibu mashirikiano yatakayowezesha Zanzibar kujenga uwezo wa kunufaika katika shughuli za uchimbaji wa gesi na mafuta. Hilo dogo?

**MHE. ALLY SALEH ALLY – MSEMAJI KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, dogo.

**MWENYEKITI:** Ukija ukurasa wa 47...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Sasa ninayesema si mimi? Waheshimiwa tuelezane, hebu subirini, tulizeni, subiri, subiri.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ukija ukurasa 47, Miradi ya Tume ya Sayansi, ukija ukurasa wa 48, ziara za kikazi. Masuala ya Muungano yote yameainishwa humu, isipokuwa kama...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** ...ngojeni basi. Waheshimiwa ninaesema ni mimi kila mtu nitampa fursa, sasa ninyi mkisema hatupo mpirani hapa kila mtu nitampa fursa.

Kwa hiyo, lugha kama hii ni lugha ambayo inaleta uashiria kuwa Muungano huu hauna umoja wa kusaidiana au wa kufanyiana kazi na kwa namna hiyo mnapeleka *wrong signals* kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni lazima niyazuie kwa sababu siyo maneno sahihi, mnaleta maneno ambayo hayapo katika uasilia, kwa hiyo ukurasa wa tatu kwenye namba tatu, kwenye mantiki inatoka, kwa Dkt. Shein kukalia kiti ambacho si chake nayo inatoka kwa sababu amechaguliwa kihalali. Waheshimiwa, niwasaidie... *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Usipotoshe ukweli.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa niwasadie, ukija ukurasa wa nne, Mheshimiwa Ally Salleh nisikilize vizuri.

Ukija ukurasa wa nne taarifa yako inazungumzia mambo ambayo yapo Mahakamani. Ukurasa wa nne wote unazungumzia mambo ambayo yapo Mahakamani, na kwa mujibu wa Kanuni zetu hatuwezi kuzungumza vitu au kujadili ambayo yapo Mahakamani na Mahakamani mmekwenda wenyewe.

Ukija ukurasa wa tano, suala la Msajili wa Vyama vya Siasa nalo lipo Mahakamani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi ninasimamia Kanuni hapa. Kwa hiyo, ushauri wangu kwako, ukurasa wa nne wote yatoe, ukurasa wa tano yatoe...

**MBUNGE FULANI:** Yatoe yote.

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa tano wote utoe, nakuomba tafadhali sana usicheze na *patience* yangu umesikia?

**MBUNGE FULANI:** Mwambie asisome yote.

**MWENYEKITI:** Nimeshakwambia, kwanza hurusiwi kunijibu mimi, kaa kimya.

Nisikilize vizuri Mheshimiwa Ally Saleh na Makatibu nisikilizeni vizuri. Ukurasa wa tano ambao una suala la Msajili. Ukurasa wa nne ambalo nalo liko Mahakamani kwa mujibu wa Katiba haya yasiingie kwenye *Hansard.* Ukurasa wa saba ambayo nayo yako Mahakamani.

Waheshimiwa Wabunge, nayakataza sababu yako Mahakamani, siyakatazi kwa sababu yoyote nyingine, Kanuni yetu iko *very clear*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ally Saleh unaweza ukaanza ukurasa wa Nane ukiukwaji wa haki za binadamu.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa heshima yako yote kumbe *freedom in this House is not to that extent.* Nilipoingia hapa nilikuwa naona jinsi Mawaziri walipokuwa waki- *convene* nilijua haya yatatokea, waulize wenzangu nilivyowaambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba kuwasilisha ili ngariba aichanje kama anavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

# MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO), MHESHIMIWA ALLY SALEH (MB) KUHUSU MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) KWA MWAKA 2017/2018 KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

(Kanuni ya 99(9) ya *Kanuni za Kudumu za Bunge,Toleo la Januari, 2016*)

## I. UTANGULIZI

### 1. Mheshimiwa Spika

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyenzi Mungu kutupa uhai ili kufanya kazi ya kitaifa. Tuzidi kumuomba kutupa nafasi kwa kadri ya utashi wake. Pia tumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa shani yake alivyoamua kuwapenda zaidi wabunge wenzetu wawili sahib yangu Marehemu Hafidh Ali Tahir na Marehemu Dr Elly Macha ikiwa pia ni ukumbusho kwetu kuwa dunia ni mapito tu. Pia kwa kutukumbusha baadhi yetu kwa kututunuku maradhi na hatuna budi kumuomba atupe afua.

Nichukue fursa hii kumpongeza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mhe Freeman Mbowe pamoja na Mwenyekiti wa Kambi ya CUF Mheshimiwa Riziki Shahari kwa kutupa nguvu zinazotufanya UKAWA kuendelea kuwa wamoja na kuwajibika kama Wapinzani na kufanya kazi kama timu kabambe tukiisimamia Serikali.

Tunamshukuru Mola kwa kutupitisha katika kipindi kigumu sana kama Kambi humu Bungeni kutokana na vitimbi mbali mbali na hila dhidi yetu ili kutukwaza. Sasa upinzani umekuwa mgumu zaidi kwa sababu Serikali haithamini upinzani na kukubali kuwa ni taasisi muhimu sana katika kujenga demokrasia. Mungu anawaona.

Sina haja ya kushuhudisha mengi yaliotokea ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na nusu kwa sababu Wabunge wote

wanayajua kama vile wananchi wanavyojua. Kwa ujumla kumefanya kazi yetu hapa Bungeni kama Wapinzani iwe ya vuta nkuvute na kuzongwa na changamoto zisizo na sababu. Lakini hilo halikutuvuruga bali imekuwa ndio gundi la kutugandisha zaidi.

**2. Mheshimiwa Spika**

Hii ni Bajeti ya pili tokea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ambapo Rais John Pombe Magufuli ameshika uongozi wa nchi. Imekuwa ni Bajeti ngumu kutekelezeka kwa ushahidi wa fedha zilizotolewa kulinganisha na zile zilizotengwa. Kila Wizara imekiona cha moto, maana wamebanwa mpaka wamevunjwa mbavu.

Eneo la miradi ya maendeleo limeumia zaidi, maana huko asilimia zilizopelekwa mpaka zinatia aibu kutajwa hadharani, au tunaweza kusema haijawahi kutokea. Na kama kuna watu wanasema kuna hatua iliopigwa katika miradi basi itakuwa ni ile iliyopendelewa na kiongozi wa nchi, lakini sio ile ambayo Bunge ilipangia kutekelezwa na ile ambayo inagusa maisha ya kila siku ya mwananchi.

Katika hali hiyo Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa mhanga mkubwa wa kisu cha ngariba. Fedha ilizoweza kushushiwa hazifanani na hadhi ya Ofisi hii , au hata kukatiwa fedha au kupunguziwa mpaka ikawa inachusha. Haipendezi. Na inaweza kuwa ni kwa sababu chini ya awamu hii hakuna mkazo mkubwa katika Muungano.

***(Aya ya 3 mpaka ya 4 zilifutwa na Bunge)***

## III. UKIUKWAJI WA HAKI ZA BINADAMU

**5. Mheshimiwa Spika**

Eneo ambalo tutapenda tujielekeze nalo kwa sasa ni lile la Haki za Binadamu ambalo lina uzito wake katika jamii yoyote ya kisasa ambayo imeazimia kujenga nchi ya demokrasia na misingi ya utawala bora. Tungependa nchi yetu isigande katika nia bali isonge mbele katika kuhakikisha haki za

binadamu zinakuwa msingi wa maamuzi yetu yote, kama ilivyo kwa utawala bora.

Tunalitaja suala la haki za binadamu kwa sababu Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini ni **kero mama ya kero** zote za Muungano, lakini ambayo bado haijamurikwa kurunzi kama ambavyo inastahili. Na sisi tumeamua kuivalia njuga kero hiii.

Mwaka huu unaomalizika taasisi yenye dhamana ya kusimamia haki za binadamu na utawala bora ilipunjwa sana kutiliwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake na Wabunge wengi walilisemea hilo kwa uchungu mkubwa. Lakini aliyekuwa Waziri katika Wizara hiyo alionekana kutokuwa tayari kuombewa fungu kupitia Kamati ya Bajeti, hapana shaka hili litakuwa limeathiri utendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAG).

Na ndio maana kutokana na upungufu wa nyenzo ya fedha, pamoja na kuwa na ofisi zake Unguja na Pemba, CHRAG kwa muda sasa haikuweza kujitokeza waziwazi katika suala la haki za binaadamu huko Zanzibar ambalo lilikuwa katika kiwango kibaya kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2015 na hata Uchaguzi wa marudio na hali hiyo kuonekana hadi 2017 kwa kiasi fulani.

Hali hiyo tunaamini imeipa nguvu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa lakini pia Wizara ya Mambo ya Ndani kudai mara kadhaa kuwa haijui kabisa juu ya madai ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaofanywa na vyombo vya dola lakini pia kundi la mgambo lililopewa jina la ***Mazombie*** na ambalo wazi wazi limekuwa likibeba silaha na kutumia magari ya Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamekuwa wakisema wamefungwa mikono kuchukua hatua yoyote kwa sababu watu wanaodai haki zao kunyongwa huwa hawaripoti Vituo vya Polisi na kwa hivyo haiwezekani kuanza hatua bila taarifa kuwepo rasmi katika mkondo wa kiserikali.

**6. Mheshimiwa Spika**

Kwa kweli Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani wamekuwa hawasemi kweli juu ya jambo hili kwa sababu kuna taarifa za kutosha juu ya watu walioripoti vituo vya Polisi zikiwa ni pamoja na majina yao na nambari za RB au na wengine hata kesi zao baada ya kufikishwa Mahakamani. Orodha tulionayo inaonyesha karibu watu wote tuliokusanya majina yao walikamatwa kwa sababu tu ya kuwa wapenzi au wanachama wa CUF na wengi walipigwa au kuteswa na kufikishwa Polisi au Mahakamani ili kuwazuia wao wasitoe madai ya uonevu wanaofanyiwa. (Kiambatisho 1)

Tunapenda kuwasilisha kama kiambatanisho orodha hio na huku tukikumbusha kuwa bado ipo haja ya Bunge kuchukua hatua juu ya vitendo vinavyofanyiwa wananchi Zanzibar na Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ***Mazombie*** kwa kujua kuwa suala la haki za binadamu linasimamiwa na Serikali ya Muungano ambapo ndio mas-uul katika jumuia ya kimataifa.

Ieleweke kwamba katika orodha nzima ya watu tulioiwasilisha hapa Bungeni leo, asilimia zaidi ya 95 hawakupelekwa mahakamani na hivyo kutakiwa kuripoti mara kadhaa katika vituo vya polisi, wachache wale waliopelekwa Mahakamani hakuna hata kesi moja iliyosimama na mtu kutiwa hatiani.

**Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi Bungeni inarudia tena kauli yake kuwa kuna haja na hasa ulazima wa Bunge lako tukufu kupitia Kamati yake ya kudumu ya Ulinzi, usalama na Mambo ya Nje kufanyia uchunguzi vitendo vyote vinavyofanywa na vikundi hivyo na mara kadhaa kama si zote kuhusisha Jeshi la Polisi na Vikosi vyote vya SMZ yaani KMKM, Valantia, Zima Moto, JKU na Mafunzo.**

**7. Mheshimiwa Spika**

Serikali ya Muungano katika kile kinachoweza kutafsiriwa kuingilia mambo ya ndani ya Zanzibar, yaani yale ambayo

kikatiba ni mamlaka ya Zanzibar na kwa hivyo hayawezi kuchukuliwa na Serikali ya Muungano ni katika suala la masheikh wa Zanzibar ambao wanashtakiwa au labda tuseme watashtakiwa kwa kesi ya ugaidi kwa sababu hadi leo kesi zao hazijaanza.

Kwa mujibu wa Katiba na Sheria ni wazi kuwa mamlaka ya Mahakama Kuu ya Tanzania ni sawa na yale ya Mahakama Kuu ya Zanzibar. Kitendo cha masheikh hao kukamatwa au hasa tafsiri sahihi kutekwa  Zanzibar ambako pia ndiko kunakodaiwa kufanyiwa kosa la vitendo vya kigaidi, ikiwa pia ni eneo la mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar, na watuhumiwa hao kupelekwa Dar es salaam hakuna tofauti na kupelekwa nchi ya nje, hakikubaliki.

Na kwa miaka 4 sasa Serikali ya Muungano  imejibereuza kujifanya haijui uharamu huo, kwa sababu tu Wazanzibari ni Watanzania. Hio si haki na si halali. Ni haramu na mutlak.
Mheshimiwa Spika, ni lazima Ofisi ya Makamu wa Rais iondokane na misimamo ya kizamani na iwe inahoji mambo yanayotokea na ambayo yanaweza kuwa kisababishi cha Muungano kuchukukiwa na kukataliwa. Kukaa tu na kusema hilo haliko chini yao hakusaidii kama ambavyo hivi sasa lisivyosaidia.

**Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupaza sauti ya Wazanzibari wengi na wapenda haki kuwa ni lazima sasa maamuzi yafanywe juu ya suala la masheikh ambao wanaozea rumande.  Kwa binaadamu kutendeana hivi si haki kabisa na bila ya shaka kwa Mungu ni kujipa mamlaka yasiomithilika, iwapo wapo wacha Mungu katika wanaofanya maamuzi juu ya maisha ya wenzao.**

***8. Mheshimiwa Spika***

Usalama wa raia na mali zao  ndio kazi kuu ya dola, lakini ni vyema tukaleta mbele yako suala muhimu sana kwa sababu ya kutokea matendo ambayo tumeyataja hapo juu na kuongezeka mengine ambayo yamekuwa yakitokea upande wa Tanzania Bara hivi karibuni.

**Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Utesaji na Vitendo vya Kudhalilisha** ulioanza Juni, 1987 ni muhimu sana na unaleta maana sana wakati kama huu ambapo vitendo tulivyovitaja juu. Katiba yetu imetaja hilo katika sehemu ya Haki za Binadamu.

Lakini inasikitisha kuwa mpaka hivi leo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Tanzania haija ridhia (***Ratified)*** mkataba huo na hivyo kukwepa wajibu wake wa kimataifa. Katika kikao cha Bunge lilopita tulishuhudia Waziri wa Serikali akitetea vitendo vya utesaji kwa au dhidi ya watu ambao wamezuiliwa wakihojiwa kwa madai ya makosa mbali mbali.

**Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itimize wajibu wake kwa kuchukua hatua ya kutia saini Mkataba huo ili sio tu kuweka imani ya Watanzania lakini pia kuweka heshima ya nchi kuwa miongoni mwa zinazoheshimu raia wake na kujenga taswira ya kimataifa.**

**IV. TNAHITAJI MFUMO SAHIHI WA MUUNGANO**

**9. Mheshimiwa Spika,**
Mfumo wa Muungano ulivyo hivi sasa umepigiwa kelele sana kwamba hauipi fursa Zanzibar nafasi kubwa na pana ya kujitafutia maendeleo yake wenyewe. Mara nyingi kama si zote Serikali ya Zanzibar hufanya utaratibu hata ikiwa ni wa kutumia mabavu au kukiuka sheria na katiba ili kujitafutia maendeleo yake na sababu kubwa ni kuwa Zanzibar huhitaji kupumua.
Na hii ilianza zamani. Katika Mambo 11 ya Muungano ya awali suala la bandari lilikuwa mojawapo lakini kwa akili ya kawaida tu ilitarajiwa nini hasa kwa Zanzibar? Wakati Zanzibar ni nchi ya kisiwa na ulazima wa kumiliki na kupata mapato kutokana na bandari ni jambo la lazima. Zanzibar imelikataa hilo kimya kimya kwa hivyo kuna **Tanzania Ports Authority** na kuna **Zanzibar Ports Corporation**, kuna Bodi ya Mikopo ya Tanzania na kuna Bodi ya Mikopo ya Zanzibar ilhali suala la elimu ya juu ni la Muungano. Pia kuna sheria ya **Maritime Authority Act.**

**10. Mheshimiwa Spika**

Wakati pande hizi hazifanani kwa rasilmali na upande mmoja ukiishika Serikali ya Muungano na kuifanya kama yake peke yake, ingetarajiwa kungeoneshwa kujali na kumekuwa na hasira ya kudumu huko Zanzibar kuwa upande wa Muungano kwa miaka 53 umeshindwa kufunguka inavyostaki na kwa hivyo kutarajia Zanzibar yenye rasilmali chache ijietegemee na ipige hatua, wakati vyanzo vya uchumi vimebanwa.

Serikali ya Muungano haijawahi kuota kuwekeza Zanzibar ambapo jambo kama hilo lingefanywa kungeonesha tofauti kubwa lakini badala yake kiwango cha maendeleo na mabadiliko pande mbili hizi hakifanani utadhani ni nchi mbili tofauti au pande zisizo na mafungamano kabisa.

Uwekezaji uliofanywa na Serikali ya Muungano haukidhi na hauakisi kabisa dhana ya kuitakia maendeleo na mabadiliko Zanzibar na sababu au kisingizio ni kuwa Zanzibar ina Serikali yake na ina utaratibu wake wa masuala ya kiuchumi na kimaendeleo. Lakini ukweli ni kama umemfunga mtu miguu na ukamtake asimame na atembee.

Serikali ya Muungano haijawahi au tuseme haijathubutu kuwekeza au kama inavyowekeza katika miradi ya Tanganyika ambayo si ya Muungano kwa kutumia rasilmali za Muungano. Kwa maneno mengine haijaona usawa tu wa kimantiki kuwa pesa ya Muungano pia Zanzibar ina haki nayo sawa na mshirika wake Tanganyika. Ni kama baba mwenye watoto wa wawili lakini ikawa anamtunza mmoja tu na mwengine akimuacha katika idhlali na unyonge

Na kwa hivyo fedha za Muungano zinazotumika Zanzibar ni kwa ajili ya miradi ya kimkakati tu kama vile jengo la Benki Kuu, Jengo la Mamlaka ya Kodi (TRA), Jengo la Uhamiaji na Mamlaka ya Bahari Kuu.

Hakuna Muungano usio na maslahi ya kiuchumi tusidanganyane. Na kusema kweli sisi Zanzibar hatujaona

kabisa maslahi ya kiuchumi katika Muuungano huu wa miaka ayami Muungano huu umekuwa wa kisiasa na tena wa kulaliana.

Kambi Rasmi inatoa wito kwa Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar kulirejelea suala la Mfuko wa Pamoja wa Fedha ambao umeundwa zama hizo lakini kwa sababu ya woga wa Serikali ya Muungano kubaiika kuwa kumbe inafaidika zaidi na makusanyo ya Muungano kuliko mshirika mwenziwe Zanzibar, kama ambavyo utafiti uliofanywa. Zanzibar jamani imepunjwa muda wote wa Muungano.
Kwa wasiojua imethibitika mapato ya Muungano yanaweza kuendesha Serikali ya Shirikisho na washirika wawili wakiachiwa kudhibiti vyanzo vyao vya fedha watajiendesha wenyewe bila ya tatizo lolote.

**Kambi Rasmi ya Upinzani inaitolea wito Serikali ya Muungano na ya Zanzibar, pamoja na kuwa hakuna nia ya kisiasa ya kwenda katika Katiba Mpya, ifanye halan kurudisha mjadala wa Mfuko wa Pamoja wa Fedha ambao unahitajika hata hivi sasa mfumo wetu wa aina ya kiini macho – wa Serikali Mbili katika Mamlaka Tatu.**

## V. UWEKEZAJI MIRADI YA MUUNGANO ZANZIBAR

**11. Mheshimiwa Spika,**
Ukitoa miradi hiyo ya kimkakati Serikali ya Muungano haijawahi kuweka au kuwekeza katika mradi wowote ule wa kiuchumi huko Zanzibar. Haina kikataa wala shamba, haina karakana wala kiwanda, haijawahi kuwa na kihori wala meli na kwa ufupi tuseme haina hainani na ikiitwa haiungami.

Ndio kusema pamoja na mifano mingi duniani SMT imeshindwa kwa miaka yote ya Muungano kutengeneza mazingira ya kisheria ambayo yangeshawishi makampuni, mabenki au watu binafsi kuwekeza Zanzibar kwa utaratibu kama ufuatao
1. Mabenki, taasisi au hata mifuko ya hifadhi kuwa na utaratibu maalum wa kushashamua uchumi wa Zanzibar, utaratibu ambao utakuwa ni wa kisheria

2. Serikali ya Muungano kuweka utaratibu maalum kwa wawekezaji wa ndani kutoka Bara kuwekeza Zanzibar kwa mfano kama kupata msamaha wa kodi

3. Serikali yenyewe ya Muungano kuwa na miradi ya kiuwekezaji inayoonekana

4. Serikali ya Muungano kuipa Zanzibar maeneo ya uwekezaji kama inavyowapa wageni wanaotaka kuwekeza

5. Kwa kuwa uchumi wa Zanzibar ni wa visiwa, SMT isiwe kipingamizi kwa Zanzibar kujijenga katika uchumi wa aina hiyo kama ilivyo kwa Singapore, Seychelles, Madagascar na Mauritius.

6. Serikali ya Muungano ilipaswa katika miradi yake kielelezo basi mmoja ungewekwa Zanzibar ili kuonyesha nia njema ya kuijenga Zanzibar kiuchumi.

7. Serikali ya Zanzibar iwe na uhuru kamili kiuchumi na kifedha (economic and fiscal) kuweza kijisimamia wenyewe.

Lakini kinyume chake hatujaona kabisa hatua zozote za makusudi zikichukuliwa na Serikali ya Muungano kuhusiana kuupembejea uchumi wa Zanzibar zaidi ya kubanwa kwa kodi, ilhali ikieleweka kuwa soko la Zanzibar halifanani kabisa na la Tanzania Bara na halikadhalika vyanzo vya mapato au rasilmali.

Ndio maana tunasema Muungano utakuwa imara zaidi kwa kila upande kupata haki na stahili zake chini pale pande hizi mbili zitakapokuwa zinaongozwa na Serikali ya Ukawa kwa maana CUF kwa upande wa Zanzibar na Chadema kwa upande wa Tanganyika pamoja na washirika wa Ukawa.

**Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini tutaposhika madaraka tutaibadilisha hali hii kwa sababu tunaamini kuwa Zanzibar imara kiuchumi na yenye haki haki zake ndio kuimarika kwa Muungano na tunashauri mapendekezo tuliyoyatoa hapo juu yafanyiwe kazi ili kuitononesha Zanzibar.**

## VI. UWEPO WA MIRADI YA MFANO

**12. Mheshmiwa Spika,**
Mara chache kumekuwa na miradi ambayo inatafutwa na Serikali ya Muungano na ambao inafika hadi Zanzibar kama ilivyokuwa kwa mradi uliojulikana kwa jina la MANCEP-(***Marine Conservation and Environmental Management Project)*** Lakini kinachotokea ni mara chache kuwepo na miradi kama hii na hutokea kwa nadra kama vile kupigwa radi, maana kwa watendaji wa Serikali ya Muungano wanaotafuta miradi Zanzibar sio kipaumbele hata chembe.

Mradi mmoja hata hivyo, ambao ni karibuni, umekuwa wa kupigiwa mfano ambao ungeweza kuwa kielezo cha mafungamano ya Muugano ni ule uitwao Mradi wa Miundombinu, Masoko na Uongezaji Thamani Bidhaa *MIVRAF* ambao umeweza walau kuleta chachu huko Unguja na Pemba, ingawa umekuwa kwa muda mfupi na unaweza kuwa unafikia mwisho iwapo hazikupatikana fedha za wafadhili kuuongeza na hivi sasa mazungumzo yakiwa yanaendelea na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Waliobuni mradi huu angalau kwa uchache waliweza kufikiria Zanzibar ambao mradi huu husaidia kutengeneza mifumo ambayo inapelekea kuongeza thamani ya mazao na kwa hivyo hujenga barabara, hujenga masoko na kutoa fursa za mafunzo kuongeza uzalishaji na kukuza huduma za masoko.

Mradi huu pia umesaidia kuvipa nguvu vikundi vya SACCOS na kunyanyua biashara kwa kuzitafutia masoko, japo hadi sasa masoko hayo ni ya ndani tu. Ila imebainika fedha zilizotumika hazifanani na faida inayoweza kuonekana.
Ila Waswahili walisema chema hakidumu. Serikali ya Muungano imelezwa kuburura miguu, hasa Wizara ya Fedha kukamilisha nyaraka ili mradi huo unaokwisha muda wake uweze kupata upya ufadhili, lakini pia Wizara hiyo hiyo ilichelewa kukamilisha taratibu ili mradi upate msaada (Grant) toka European Union wa Euro 400,000 kutoka Jumuia ya Ulaya.

Kambi Rasmi ya Upinzani ina laani umangimeza mkubwa uliopo Wizara ya Fedha na kwa hili ukigusa maslahi ya Zanzibar katika mara chache ambapo inapata mwanya wa kusaidiwa kupitia mgogngo wa Serikali ya Muungano.

**Pamoja na uzuri wa mradi huo na faida iliyopatikana, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo;**

**1. Juhudi zifanywe kuona mradi huu unaendelea**

**2. Serikali itafute mradi mwengine wenye malengo yanayofanana na haya**

**3. Zanzibar ifaidike zaidi ili kuifukuzia Tanzania Bara kimaendeleo**

**4. Serikali ya Muungano iiunge mkono Serikali ya Zanzibar kupandisha kiwango cha barabara kutoka udongo hadi lami**

**5. Serikali ifanye ukaguzi mkubwa wa thamani ya mradi katika maeneo ya ujenzi wa barabara na Soko la Kinyasini ili kubaini kama miradi hiyo ina thamani iliyowekezwa**

**6. Wakati uwe umefika sasa kwa Serikali ya Muungano kuwa na maelekezo rasmi juu ya kuitizama Zanzibar kwa kila mradi ambao inaomba kwa wafadhili yaani Zanzibar Main Streaming (ZMS)**

## VII. MUANACHAMA WA ZANZIBAR KWENYE VYAMA VYA KIMATAIFA VYA MICHEZO

**13. Mheshimiwa Spika,**

Hivi karibuni au kwa uhakika zaidi Machi 16,2017 Zanzibar ilikaribishwa kuwa mwanachama wa 55 wa Shirikisho la Soka la Afrika (CAF) kwa kupigiwa kura nyingi na wajumbe waliotoka pande zote za Afrika yaani Kusini, Kaskazini, Magharibi, Mashariki na Kati ya Afrika.

Kati ya wengi waliosimamia suala hilo ni pamoja na Shirikisho la Soka la Tanzania Jamal Malinzi kama walivyofanya

wenziwe Muhiddin Ndolanga na Leodgar Tenga. Pia kama walivyofanya mawaziri wenziwe waliopita akina Professa Juma Kapuya na basi pia mchango mkubwa ulitolewa na aliyekuwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo Mhe. Nape Nnaye.
Juhudi kama hizo zilichukuliwa Zanzibar tokea enzi za uenyekiti wa Ali Ferej Tamiam na pia Rais Ravia Idarous na mawaziri waliolipigia chapuo ni pamoja na Haroun Ali Suleiman na Ali Juma Shamhuna.

Zanzibar mara mbili imekataliwa kuwa mwanachama wa Shirikisho la Soka Duniani FIFA, japo ilikubaliwa kuwa Mwanachama Shirikishi miaka 6 iliyopita na sababu au hoja kubwa ya FIFA kwa maamuzi yake ni kuwa uanachama wa FIFA unatambulika kwa nchi na Zanzibar haikuwa inakidhi vigezo hivyo.

**14. Mheshimiwa Spika**
Mara hii wanaharakati hatukukubali kungojea kufanyiwa maamuzi bila ya kuwaelewesha wafanya maamuzi yaani Marais wa Vyama vya Soka Afrika ambao ni wapiga kura, walijue suala hilo kwa undani ili wafanye maamuzi yenye uelewa.

Tuliwaeleza kuwa Tanzania ni Jamhuri, ni muungano, ni mamlaka tatu, ni shirikisho na ni serikali mbili. Tuliwaambia kila upande una mamlaka kamili na ushahidi katika hili la michezo ni kuwa kila upande una Wizara yake, Waziri wake, Baraza lake la michezo, vyama vyake vya michezo ikiwa ni pamoja na Chama cha Soka cha Zanzibar.

Zaidi tukawaeleza kuwa pamoja na Tanzania Football Federation kuchukua jina la Tanzania, lakini kubwa ni kuwa haina mamlaka yoyote Zanzibar, haiandai program yoyote na wala haisimamii mashindano yoyote yale na kwa miaka yote ya Muungano hakuna Mzanzibari aliyeshika uongozi TFF wala Mtanganyika kwa ZFA, yaani kama ilivyo kwa michezo mengine kama riadha, hoki, baskeli na kadhalika na kuwa kwa miaka yote katika mashindano yote ya kikanda Zanzibar na Tanzania Bara tumekuwa tukipeleka timu tofauti.

**15. Mheshimiwa Spika,**

Napenda kukuarifu faraja kubwa tuloipata kwamba Afrika imetuelewa na ndio maana nchi zote zilipiga kura kuikaribisha Zanzibar katika CAF kwa kuelewa kuwa Tanzania ni Jamhuri, ni muungano, ni mamlaka tatu, ni shirikisho na ni serikali mbili. Lakini cha muhimu zaidi ni kuwa kila Serikali inayo haki ya kuwakilisha watu wake inayosimamia.

Afrika kwa hali hiyo imetupa suluhu ya masuala mengi ambayo tulikuwa tukijiuliza na hata kushindwa katika majaribio ya kutafuta suluhu. Afrika imetuambia kuwa njia iliokuwa imechukuliwa na Tume ya Katiba ya Jaji Joseph Warioba ilikuwa na mwelekeo na kwa hivyo kutuzindua kuirudia.

Kwamba Zanzibar inaweza na ina hakika ya kusimama wenyewe. Iachiwe isimame

## VIII. UMUHIMU WA KUWA NA KATIBA MPYA

**16. Mheshimiwa Spika**

Tukio la Zanzibar kukubaliwa kuwa mwanachama wa CAF linachagiza na kukumbusha suala la Katiba Mpya na hasa kurudi katika Rasimu ya pili ya Katiba ya Jaji Warioba na sio kuchukua vipande vipande vyake na kuvipachika pachika kuvia sheria mbalimbali na hata maelekezo mengineyo.

Hivi karibuni Serikali ilifikisha Muswada Bungeni kurekebisha Sheria ya Madeni na Mikopo na kupenyeza kipengele cha Zanzibar kuweza kukopa kama ambavyo ilijitokeza kuwa moja ya dai kubwa la wananchi wa Zanzibar ili kuonyesha kuwa Zanzibar ina mamlaka ya maamuzi juu ya maendeleo yake.

Rasimu ya pili ya Katiba ya Jaji Warioba iliweka kipengele cha madhumuni hayo na Katiba Pendekezwa ikafanya ilivyoona inafaa, lakini wakati tukingojea Serikali ama ilipeleke suala la Katiba Mpya kwa umma kupitia utaratibu wa Kura ya Maoni au ilirudishe tena kwenye mchakato kwa

kuwa hakuna maridhiano, Serikali ya Dk John Pombe Magufuli imeamua kufanya ukarabati suala la kikatiba kupitia kwenye sheria.

Kitu chengine ambacho tulitaraji kingesimama vilivyo kupitia kwenye Katiba Mpya ni suala la haki ya Wazanzibari katika kupata ajira kwenye Wizara na Taasisi za Muungano, jambo ambalo pia lilitolewa pendekezo na Katiba ya Warioba na lilitakiwa liwekewe misingi ya kikatiba ili liweze kusimama

Kambi Rasmi ya Upinzani imepata taarifa kuwa Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar zimefikia makubaliano katika kile kinachoitwa Utatuzi wa Kero za Muungano, kwamba mfumo wa ajira hizo uwe kwa 79:21 yaani kila Watanganyika 79 watakaoajiriwa katika Wizara na Taasisi za Muungano basi 21 watoke Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Ofisi ya Wizara ya Nchi Utumishi ya Jamhuri ya Muungano.

Hii ni hatua njema lakini hadi sasa haina msingi wa kikatiba na bado kabisa haina nguvu ya kisheria na kwa kweli tutakuwa hatuna hakika utekelezaji wake japo kuna nia njema, lakini watendaji wanaweza kuharibu kama ilivyo tokea kwa mambo mengine kadhaa.

**Kambi Rasmi ya Upinzani inataka mabadiliko ya sheria yaletwe Bungeni ili kurasimisha uamuzi huo ili ikachukuliwa kuwa ni jambo la hisani tu.**

**Hali kadhalika kila panapofikiwa hatua na kusemwa kuwa kero imemalizwa basi tabaan Serikali ilete sheria Bungeni ili sio tu kurasimisha, lakini pia kuweza kusimamiwa kiuekelezaji.**

**17. Mheshimiwa Spika**

Tukibaki hapo hapo kwenye suala la Kero za Muungano hahaioni sababu kuendelea kutatua hizo zinazoitwa kero bila ushiriki mpana wa wadau wa Muungano. Ndio maana makubaliano yanayofikiwa na SMT na SMZ kwanza huchelewa na wakati mwengine hayawekwi kabisa kwenye misingi ya

kikatiba au kisheria lakini pili yanakuwa magumu kukubalia na kumilikiwa na umma (Public ownership)
SMT na SMZ wamekuwa na dhana kongwe kuwa taasisi hizo mbili ndio walinzi na wasimamizi wa Muungano ilhali Muungano ni dhana ambayo inasimama kikamilifu kwa marefu na mapana yake na umiliki wa umma au Watanzania wote.

Kudhani kwamba ziitwazo Kero za Muungano zinaweza au zinastahiki kutafutiwa suluhu na taasisi hizo mbili ni wazo la kale mno na ndio sababu moja ya kuvia kwa Muungano. CCM imekuwa haina mpya wala haina tena ubunifu kuhusu Muungano.

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona wakati umefika sasa kupanua wigo wa washiriki katika kuzitizama Kero za Muungano ikiwa ni pamoja na ushiriki wa Bunge kwa sababu chombo hicho kina ridhaa ya umma na taasisi muhimu sana katika nchi yetu na tusilisubirishe Bunge kuja kupitisha tu yanayotajwa kuwa utatuzi wa kero, lakini kila siku zimebaki kuwa kero na kuzidi kuwa akhasi.**

**18. Mheshimiwa Spika**
Sisi tunaamini kuwa Kero za Muungano ziko zaidi ya zinazosemwa. Ni zaidi ya za kikatiba na kisheria. Tunavyoona ni pamoja na kutochukua hatua au pia kuchukua hatua zisizofaa dhidi ya maslahi ya Zanzibar kunakofanywa na taasisi, kwa wazi tunayoyaona lakini pia kwa siri ambayo hatuyaoni lakini matokeo yake yanatudhihirishia.

Kazi kuu ya dola ya Jamhuri ya Muungano ni kuhakikisha usalama wa raia. Ni raia ambao kwa mmoja mmoja ana haki ya kujikusanya, kujiunga na kushiriki siasa. Na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na sheria za nchi ni kwamba taifa hili linaendeshwa kwa misingi ya siasa za ushindani na vyama vingi na kila raia ana haki kushiriki katika siasa.

Hata hivyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano bado haiamini na haikubali kuwa Zanzibar pia kuna siasa za ushindani na

vyama vingi na kwa maana hiyo Wazanzibari wana vyama vyao na wana haki ya kuvipigia vyama hivyo na kwa kwamba pia kuna haki ya chama kinachoshinda kipewe haki ya kutawala kwa mujibu wa Katiba na sharia.

Tunachokiona ni kuwa Serikali ya Muungano haitaki kuheshimu matakwa ya Wazanzibari na inaonekana iko tayari kwa lolote lile iwapo kitakachoumia ni CUF bila ya kujali kuumia kwa Zanzibar na watu wake.

Miaka kadhaa iliyopita Zanzibar iliamua kujiunga na Jumuia ya Kiislamu Duniani Organization for Islamic Conference ( OIC ) kwa nia ya kujitafutia njia zaidi za kufunguka kiuchumi na kulizuka mjadala mkubwa sana na hata kutishia uhai wa Muungano pale aliyekuwa Rais wa Zanzibar Dk Salmin amour kusisitiza kuwa uamuzi wa Zanzibar ni kwa maslahi ya Zanzibar.

Tanzania iliahidi kujiunga na OIC ili kuizuia Zanzibar isijiunge peke yake lakini hadi leo hakuna kilichotokea huku nchi hii ikiwa na Ubalozi wa Vatican lakini hivi karibuni pia kufungua ubalozi huko nchini Israel na huku pia ikijiburura kufungua Ubalozi nchini Iran. Nchi hiyo ina Ubalozi Dar es salaam na inaweza kuwa mlango wa fursa nyingi kwa Tanzania. Tunashindwa kuisoma Serikali yetu.

Miaka 25 tokea SMT kuikatalia SMZ kujiunga na OIC bado Serikali ya Tanzania haijafanya uamuzi wa kujiunga na jumuia hiyo na bila kuiachia Zanzibar ijiunge yenyewe.

**Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na maamuzi kama haya ambayo yanakuwa magumu kufanywa kwa maslahi ya Zanzibar na tunaamini ni wakati sasa Zanzibar kuweza kujiunga katika jumuia za kikanda na zile ambazo Tanzania hazina maslahi nazo lakini kwa upande wa Zanzibar kuna faida zitakazopatikana kama vile Jumuiya ya Visiwa vya Bahari ya Hindi na kadhalika.**

## IX. HADHI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS

**19. Mheshimiwa Spika**

Ofisi ya Makamu wa Rais inasimamiwa na Kamati ya Katiba na Sheria ambayo mara hii ilisikitishwa sana na kujua kuwa Ofisi hiyo imepunguziwa Bajeti yake ya mwaka huu hasa Ofisi Binafsi ya Makamu. Hili haliwezi kukubalika.

Kamati iliarifiwa kuwa shughuli za Makamu wa Rais sio tu ziliathirika lakini pia zilisuasua. Ofisi hiyo imebidi kukopa na kubabibabia ili kumhudumia Makamu wa Rais na hivi sasa imekusanya madeni mengi hasa yale ya safari za ndege. Hii ni aibu ijapo madeni hayo yatatafutiwa taratibu za ndani kulipwa.

Tunaamini kuwa Makamu wa Rais ni alama (brand) muhimu kwa nchi yetu na si vyema kupunguza Bajeti yake katika hali ambayo itaathiri utendaji wake akiwa ndio msaidizi wa karibu kabisa wa Rais wa Jamhuri

**Kambi Rasmi ya Upinzani inaungana na mawazo ya Kamati ya Katiba na Sheria kuwa jambo hilo lirekebishwe na kuipa haki yake Ofisi ya Makamu wa Rais. Pia Kambi Rasmi ya Upinzani inaungana na mawazo ya Kamati ya Katiba na Sheria kuiwekea Ofisi hiyo bajeti yake katika Mfuko Mkuu wa Hazina kama zilivyo taasisi nyengine kubwa na muhimu katika taifa.**

**20. Mheshimiwa Spika**

Mwaka wa fedha unaomalizika Kamati ilitembelea Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es salaam na kugundua mambo kadhaa juu ya jengo hilo na kutoa maagizo ili yafanyiwe kazi kuhusu marekebisho lakini pia ikaagizwa kuwa Mkandarasi asipewe fedha iliyobakia na pia kutaka Mamlaka ya Nyumba Tanzania TBA ambao ndio waliokuwa wasimamizi wawajibike kwa hili.

Lakini Kamati imearifiwa hilo halikufanywa na badala yake Ofisi ya Makamu iko njiani kuingia gharama nyengine kutafuta utaalamu wa kuikagua Ofisi yaani Mtaalamu Mwelekezi ili

kubaini makosa ya kiufundi na ya kiusalama na gharama inayokisiwa kutolewa ni kwa mamilioni. Hii haikubaliki.

**Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana na msimamo wa Kamati ya Katiba kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais afuate maagizo yaliotolewa na Kamati kufanya marekebisho bila ya gharama kwa sababu ya kuwajibika kufanya hivyo yupo – ni mkandarasi na gharama zisizokuwa za mkandarasi bila ya kuingia hasara ya kutafuta Mtaalamu Mwelekezi**

**21. Mheshimiwa Spika**

Baadhi yetu bado tunatafakari ni vipi Ofisi ya Makamu wa Rais ilivyoathirika na kile kinachoitwa Ukomo wa Bajeti ambapo inaleta mkandamizo mkubwa katika kufikia lengo linalopangwa, ilhali ikieleweka kuwa taswira ya Ofisi ya Makamu wa Rais ni ile ya kitaifa.

Ofisi ya Makamu wa Rais imepata kiasi cha asilimia 11 tu ya fedha zilizopangwa kutekeleza miradi na hatuoni kuwa hili ni sahihi. Si sahihi kabisa kwa sababu kufanya hivyo ni kama kuishushia hadhi Ofisi hiyo ambayo umma unatarajia kuiona ina akisi hali ya taifa. Kama Ukomo wa Bajeti umekwenda hata kuinyima Ofisi hii fedha za maendeleo tunaona dhahiri kuwa Serikali ya CCM haina kingine inachoshindwa kufanya.

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Ofisi ya Makamu wa Rais ipewe hadhi inayostahiki. Watimiziwe Bajeti waliyoomba kwa hali yoyote na isiwe kupunjwa kupitia kiasi na kuleta dhana kwa umma kuwa Ofisi hii ina hadhi ya chini zaidi isiyofanana, wakati Ofisi hii inayongozwa na mtu ambae kikatiba ana hadhi kubwa.**

**22. Mheshimiwa Spika**

Ofisi ya Makamo wa Rais imekuwa na miradi miwili mikubwa ya ujenzi Zanzibar. Mmoja ni wa Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano ambao umeshakamilika na mwengine ni makaazi ya Makamo wa Rais, ambayo bado kukamilika.

Ofisi ya Bunge hata bila ya kutumiwa na ikiwa imekaa bure (White Elephant) iko katika hali mbaya na jengo la makaazi

ya Makamu wa Rais linataka kutupiwa jicho la undani kurekebisha mambo kadhaa ambayo yamebainiwa na Kamati ya Katiba na Sheria.

**Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai ya kufanya utaratibu wa kutumia jengo la ofisi iliopo Tunguu na sio kukaa bure kama lilivyo hivi sasa, ikiwa ni pamoja na kukodishwa ofisi za Serikali ama za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Muungano.**

## X. HITIMISHO

**23. Mheshimiwa Spika,**

Bado Kambi Rasmi inaendelea kulilia na kusimamia yafuatayo:

a) Haki ya vyama vya Upinzani kufanya siasa kwa uhuru
b) Haki ya Wananchi kuliona Bunge lao wakati wa mijadala
c) Haki ya kuishi kwa salama, amani na uhakika wa maisha ya kila siku
d) Haki ya kuheshimu matakwa ya wananchi katika maamuzi ya kisiasa yaliofanywa Oktoba 25, 2015 Zanzibar
e) Haki ya kutoteswa na kudhalilishwa kwa kila raia
f) Haki ya mazingira bora, salama kwa kila raia
g) Haki ya raia kujua matumizi ya Serikali yao na Serikali kuwajibika kwa maamuzi ya Bunge

**24. Mheshimiwa Spika,**
Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

……………………………………..
**Ally Saleh Ally (Mb)**
**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.**
**24/04/2017**

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Msemaji Kambi Rasmi....

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Aongee nini sasa?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, fursa ya kusoma taarifa ya Kamati ni wajibu wa Kikanuni, fursa mmepewa mmeamua kukaa chini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, subirini basi, wala haitaki ugomvi. Umeomba taarifa yako ulivyooanza umeanza kwa taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard* yale ambayo yanatakiwa yaingie kwenye *Hansard* yataingia na yale ambayo yamekuwa *omitted* hayataingia.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Msemaji Kambi Rasmi ya Upinzani Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu mazingira.

**MHE. PAULINE P. GEKUL-MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niseme yanayohusu upande wa Mazingira japo upande wa Muungano umeamua kuyakata kwa kisu cha ngariba, lakini naamini yatakuwa yameingia kwenye *Hansard.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naongeza nusu saa, tuendelee.

**MHE. PAULINE P. GEKUL-MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote

napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwa kunipa uhai, afya na kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya leo. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa sala na maombi yao nilipokuwa hospitali baada ya kupata ajali nikiwa kwenye kazi zangu za kuwahudumia wananchi wa Jimbo langu la Babati Mjini. Nawashukuru sana na nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri katika ofisi hii pia ambaye alijumuika nami wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa pekee naomba niishukuru familia yangu kwa uvumilivu wao mkubwa kwangu, wananchi wa Jimbo la Babati Mjini, kwa ushirikiano wanaonipa katika kutimiza wajibu wangu, nawaahidi kuwa sitowaangusha. Pia niwapongeze Viongozi wote wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Freeman Mbowe (KUB), kwa kumaliza ziara walioifanya katika Kanda zote 10 katika nchi yetu, katika kuimarisha uongozi na wanachama wetu, kutimiza wajibu wao katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabadiliko ya tabianchi; mabadiliko ya tabianchi ambayo pia huchangiwa na uharibifu mkubwa wa mazingira umeleta athari kubwa katika sekta mbalimbali za maendeleo ya jamii na sekta zingine ziko katika hatari ya kuathirika pia. Sekta hizi ni nishati, kilimo, usalama wa chakula, maji, mifugo, uvuvi, misitu, wanyamapori, afya na miundombinu, utalii na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba mabadiliko ya tabianchi ni jambo la uhalisia usiokuwa na hata chembe ya mashaka kama ripoti mbalimbali za kisayansi zinavyothibitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ikiwa ni moja ya nchi zinazoendelea inahitaji wananchi wake wote kujengewa uwezo wa kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi na hiyo kuwa ni kipaumbele cha kwanza, upunguzaji wa uzalishaji wa ongezeko la gesi la joto iwe ni kipaumbele cha pili, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa,

kwa kuzingatia mambo haya mawili ni dhahiri madhara yanayojitokeza au yanayonyemelea sekta muhimu kwa uchumi wa nchi zitakuwa zimesalimika au madhara yatapungua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli kwamba mabadiliko ya tabianchi ambayo yamebadili majira ya mwaka kwa kuchelewesha au kuwahisha na madhara yanayotokea kutokana na mabadiliko hayo, mara nyingi yanakuwa ni kuharibika kwa miundombinu na pia watu kupoteza maisha. Kambi Rasmi ya upinzani inasema kwamba, uwekezaji unaofanyika kwenye miundombinu kwa kiwango hicho hicho kiwekezwe katika sekta za kuzuia na kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kusisitiza kuwa athari ya mabadiliko ya tabianchi ni kubwa sana kiuchumi, kijamii na kiusalama na hata hivyo inahitajika kuandaa sera mahsusi ili kuyapa uzito unaostahili. Aidha, tunataka kujua tumejipanga vipi kutekeleza kwa vitendo mikataba yote ya Kimataifa ambayo tumeridhia inayohusiana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yenye harufu ya ufisadi; katika hotuba yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya mwaka 2016/2017, tuliongelea ufisadi kwenye miradi miwili. Mradi wa kwanza ni mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam. Mradi wa pili ni mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Pwani yaani Bagamoyo, Pangani, Rufiji na Zanzibar."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliomba Ofisi ya Makamu wa Rais imtake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Kaguzi wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum (*special audit)* wa miradi tajwa hapo awali ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na miradi mingine yote iliyosimamiwa na Kitengo cha Mabadiliko ya Tabianchi kilichopo chini ya Idara ya Mazingira na katika Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na Muungano.

Tunaomba tufahamishwe mrejesho wa hiyo *special audit* kama kweli tunatumbua au utumbuaji wa majipu ni kweli au unaangalia sura za wahusika tu?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira; kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikisisitiza kuwa kila sekta ina muktadha wake wa uharibifu wa mazingira na kila sekta inahitaji mbinu tofauti ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira kwenye sekta husika. Hivyo basi, hoja ya msingi ni kwamba bila nia ya dhati ya utoaji wa fedha zinazohitajika kwa ukamilifu wake kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mazingira, basi sheria na miongozo inakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo huo wa Serikali kutoa fedha, progamu nyingi za mazingira ya kuhifadhi misitu zimekwama kutekelezeka na hivyo athari nyingi za kimazingira zimeanza kuonekana na nchi inaingia kwenye majanga ambayo yangeweza kuzuilika kama Serikali ingechukulia kwa umakini unaotakiwa kwa mipango na programu za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia randama za Wizara kwenye Idara hii ya Mazingira, zaidi ya asilimia 80 ya fedha za utekelezaji kwa miradi ya programu zinategemewa kutoka nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema huu nao ni udhaifu kwani pale washirika wakishindwa kutimiza miadi tu au wakichelewa kutoa fedha basi program na miradi inasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka kipaumbele kama ambavyo inawekwa kwenye sekta zingine katika kuhakikisha inatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha mipango inayopangwa kuhusiana na mazingira inatekelezwa kwa kadri ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Dhamana wa Hifadhi ya Mazingira; Mfuko huu ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kama chanzo cha fedha, kwa ajili ya kuhifadhi mazingira

nchini, lakini cha kushangaza hadi leo 2017 ndiyo Serikali inazindua Mfuko huu pamoja na Sekretarieti ya Bodi ili kufanya kazi za Mfuko. Hata hivyo, katika bajeti ya mwaka huu ni shilingi milioni 334 ndizo zilizotengwa kwa ajili ya Mfuko huu muhimu sana ambao ungesaidia kutatua changamoto za kimazingira, fedha ambazo ni chache sana kukabiliana na masuala ya mazingira nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kubainisha vyanzo vya mapato vya Mfuko huu ili uwe endelevu na uwe na nguvu ya kifedha kuliko ilivyo sasa. Mfano wa vyanzo hivyo inaweza kuwa ni asilimia 10 ya kila makusanyo ya leseni za viwandani, madini, usafirishaji, utalii, tozo mbalimbali zinazotozwa na *TFS* na pia tozo ya asilimia 20 ya jumla ya fedha zinazotozwa kwa bidhaa zinazoingizwa nchini na kutozwa ushuru wa uchakavu kwa ajili utunzaji wa mazingira. Kwa fedha hizi ni dhahiri Halmashauri zetu zitaweza kutekeleza miradi yote inayohusu utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Rufaa la Mazingira; Baraza hili lipo kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, kwa lengo la kusikiliza rufaa za wananchi ambao hawataridhika na maamuzi ya Waziri na masuala mbalimbali katika utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Taarifa ya utekelezaji ya mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, inasema kuwa, sasa hivi ndiyo ofisi imeandaa hadidu za rejea za kutayarisha mpango mkakati wa Baraza la Rufaa la Mpango wa Mazingira ambao ukikamilika ndipo Baraza litaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Waziri mwenye dhamana ya mazingira amekuwa akionekana mara nyingi akitembelea viwanda na kutoa adhabu ya fedha au kusitisha uzalishaji wa viwanda husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata maelezo je, kama waathirika wa maamuzi ya Waziri hawataridhika watapataje haki zao wakati Baraza la kupeleka malalamiko yao halijaanza kazi bado? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani baada ya kupitia randama ya Wizara imeshindwa kuona Kifungu kinachoanzisha Baraza la Rufaa la Mazingira, hivyo ni rai yetu kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atuoneshe kifungu kinachotoa fedha za uanzishaji na utendaji wa kazi za Baraza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampeni ya kitaifa ya upandaji miti; Kampeni ya kitaifa ya upandaji miti inayoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Halmashauri zetu zimepewa lengo la kupanda na kutunza miti isiyopungua miti milioni 1.5 kila mwaka. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa Halmashauri zetu hazina fedha za kuzalisha miche ya miti kwa idadi tajwa na pia haina uwezo wa kutunza miti hiyo kutokana na ukweli kwamba maeneo mengi hali ya maji siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aeleze Bunge lako Tukufu, ofisi yake inatoa kiasi gani au mchango gani wa kuzisaidia Halmashauri zetu ili ziweze kutekeleza zoezi la upandaji na utunzaji miti kwa ukamilifu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunauliza hivyo kutokana na ukweli kwamba Halmashauri zetu hazina vyanzo vya mapato vya kuweza kutekeleza agizo la ofisi ya Makamu wa Rais. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Wakala wa Huduma za Misitu *(TFS)* ipewe jukumu la kuzalisha miche nchi nzima ambayo inalingana na aina ya udongo na hali ya hewa ya eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji na matumizi ya mifuko ya plastiki; ni kweli kwamba Bunge la Afrika Mashariki lilipitisha Muswada wa *The East African Community Polythene Materials Control Bill,* 2011 ambao ulikuwa na lengo la kupiga marufuku uzalishaji, uuzaji na uingizaji wa matumizi ya *polythene materials* na Serikali kupitia kwa Baraza la Usimamizi wa Mazingira lilipiga marufuku hapa Tanzania ili kukazia sheria iliyotungwa na Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vifungashio vya plastiki vinachafua mazingira na hilo halina mjadala, lakini mazingira kuwa machafu ni tatizo la uchafu wenyewe au ni tabia ya watu? Kwa kuwa, vifungashio hivyo vina- *recycle* na kuweza kutoa bidhaa zingine na kwa kuwa, bidhaa nyingi zinazotoka nje ya nchi zinakuja zimefungashwa kwa vifungashio vya plastiki, hii ni ishara kwamba nchi ambazo ni tajiri kutuzidi na hatuwezi kujilinganisha nao katika maendeleo ya kiuchumi, bado wanazalisha na kutumia vifungashio vya plastiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa ni busara mamlaka husika kuliangalia suala hili kwa upande wa kuwa fursa zaidi kuliko inavyoliangalia sasa kuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati mbadala; kuna tatizo kubwa sana la nishati mbadala hapa nchini na hivyo kupelekea matumizi ya kuni na mkaa kuwa chanzo kikuu cha nishati inayotumiwa na Watanzania zaidi ya asilimia 90. Jambo hili ni chanzo kikubwa cha ukame unaoyakumba maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati ya gesi kwa matumizi ya majumbani imekuwa ni tatizo kubwa sana kutokana na bei yake kuwa juu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, kama kweli Serikali ingekuwa imedhamiria suala hili la nishati ya gesi kuwa mbadala kwa nishati ya kuni, kama ingeunganisha nguvu za waingizaji wa nishati hiyo toka nje ili wajenge kiwanda cha kuchakata gesi iliyoanzishwa hapa kwetu na kuiweka kwenye mitungi na kuisambaza nchi nzima, tunaamini kwamba bei ya gesi itakuwa ni nafuu zaidi kuliko gesi inayoingizwa kutoka nje ya nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mwenyekiti taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa msomaji hapo wa Kambi ya Upinzani, alipokuwa anazungumzia kuhusu Muswada wa *The East African Community Polythene Materials Control Bill,* anasema imepitishwa bado haijapitishwa na unaendelea kujadiliwa utaletwa mwezi wa Tano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL-MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atulie tu atachangia baadaye. Naomba niendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takataka kuzalishwa nishati mbadala na mbolea, taka ni changamoto karibu kila mahali kwa sababu tunaendelea kuzalisha taka nyingi sana. Kama tunavyoona kwenye maeneo yanayotunzunguka taka kutokana na plastiki, glasi na chuma haziozi. Katika kuliona hilo Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni kwa kushirikiana na Jiji la *Hamburg* - Ujerumani walianzisha mradi wa kuchakata taka ili kuzalisha umeme na mbolea, lakini mradi huo hadi sasa bado haujaanza kutokana na mambo ambayo hadi sasa hayajakaa vizuri kwa upande wa ushuru wa kuingiza mitambo hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo ni jema kuwa mfano wa kuigwa na Majiji na Miji mingine hapa nchini kwani ni chanzo cha ajira pamoja na uzalishaji wa mbolea. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira inafahamu kuwa mradi huo wa kuchakata taka kwa Halmashauri ya Kinondoni umekwama wapi na inasaidia vipi katika kuhamasisha miradi mikubwa ya kuweka mazingira na miji yetu kuwa safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017 na mpango wa maendeleo wa mwaka 2017/2018. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Ofisi ya Rais, Mazingira; taarifa za utekelezaji hadi mwezi Machi 2017 zinaonyesha kuwa, kati ya kiasi cha shilingi bilioni 10.97 zilizopitishwa na Bunge ni asilimia 11.28 tu, sawa na shilingi bilioni 1.24 zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 236.19 ni fedha za ndani na shilingi bilioni moja ni fedha za nje. Hapa ndiyo kuna kisu cha ngariba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia muhtasari wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017, inaonyesha kuwa fedha za ndani zilizopitishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni nane, hadi mwezi Machi, 2017, Serikali imetoa shilingi milioni 236.17 ambazo ni sawa na asilimia 2.9 tu. Hii maana yake ni kuonesha kuwa, kukabiliana na athari za mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi kwa ujumla wake siyo kipaumbele cha Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza tena kuwa ni muhimu taarifa ya utekelezaji ikaoneshwa kwa kila mradi na kiasi gani kimetolewa hadi mwezi Machi, 2017, wakati Wizara inapotayarisha taarifa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na mchanganuo wa makadirio ya miradi ya maendeleo inaonesha kuwa, kati ya fedha za ndani bilioni tatu, shilingi bilioni moja ni fedha ambazo matumizi yake hayaendani na usimamizi wa mazingira kama ambavyo ilikuwa katika mpango wa mwaka uliopita. Aidha, kwa miradi inayosimamiwa na *NEMC* shilingi bilioni 2.056 ni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; Mahtma Gandhi Baba wa Taifa la India aliwahi kusema kwamba *“Earth provides enough to satisfy every man’s need, but not every*

*man's greed".* Kwa taarifa isiyo rasmi ni kwamba dunia ina kila kitu cha kutimiza mahitaji ya mwanadamu, lakini siyo kutimiza matamanio na ulafi wa binadamu. Kwa muktadha huo ni kwamba, uchafuzi na uharibifu mkubwa wa mazingira katika dunia hii, Tanzania ikiwa ni mojawapo ni tabia ya binadamu ya ulafi wa kutaka kumiliki kila kitu na katika mchakato wa kumiliki kila kitu, ndipo uharibifu unapotokea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, subiri kidogo Gekul, naomba *Hansard* ielewe, kwa tafsiri isiyo rasmi siyo kwa taarifa isiyo rasmi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL-MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo mwingine ni kwamba kitendo cha kutompatia au kummilikisha binadamu kile kinachoweza kuendesha maisha yake na familia yake ndiyo ni tatizo kwani kinachofanyika ni kutokutumia kiuendelevu rasilimali zilizomzunguka. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa ushauri kwamba ni muda muafaka wa Serikali kuondokana na ile dhana kwamba maliasili ni mali ya umma, kwani kuwa mali ya umma hakuna mwenye uchungu nayo katika suala zima la matumizi endelevu ya rasilimali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda muafaka sasa Serikali kulipa kipaumbele suala la uendelevu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika utoaji wa fedha kama ambavyo sekta zingine za kiuchumi zinavyopewa kipaumbele katika upangaji na utoaji wa fedha za utekelezaji miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha, kwa sababu nimesoma *summary* naomba hotobu yote ingie kwenye *Hansard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante.

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA, MHESHIMIWA PAULINE PHILIPO GEKUL (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS –MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*Chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,Toleo la Januari, 2016*

## A. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwa kunipa uhai na afya ya kusimama hapa mbele ya Bunge lako tukufu siku ya leo, pia niwashukuru waheshimiwa wabunge na wananchi wote kwa sala na maombi yao nilipokuwa hospitalini baada ya kupata ajali nikiwa kwenye kazi zangu za kuwahudumia wananchi wa Jimbo langu la Babati Mjini. Nawashukuru sana tena sana!!!!

**Mheshimiwa Spika,** natoa shukurani zangu kwako wewe kunipa fursa ya kusimama hapa kuweza kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuhusu utendaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa pekee naomba niishukuru familia yangu kwa uvumilivu mkubwa, na pia niwapongeze viongozi wote wa chama cha Demokrasia na Maendeleo wakiongozwa na Mwenyekiti wake ambaye pia ni KRUB kwa kumaliza salama ziara waliyoifanya kanda zote za kichama za nchi yetu na kuweka uongozi.

## B. MABADILIKO YA TABIANCHI

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko ya mfumo wa hali ya hewa yanayosababishwa na kazi za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja za binadamu, ambazo zinaongeza gesi joto (Greenhouse Gases) na

kubadilisha mchanganyiko wa viwango vya gesi katika angahewa la dunia, ambayo pia ni nyongeza ya mabadiliko ya asili ya mfumo wa hali ya hewa yaliyotathminiwa na kulinganishwa kwa muda mrefu (usiopungua miaka thelatini na zaidi).

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Mabadiliko ya tabianchi kwa kiasi kikubwa (zaidi ya 95%) yanasababishwa na shughuli za kibinadamu ikiwemo uzalishaji wa viwanda unaotoa gesi ukaa (carbondioxide) kwa kiwango kikubwa sana.. Matokeo au athari za mabadiliko ya tabianchi ni; kuongezeka kwa joto, mvua kali/kubwa na za muda mfupi, mafuriko, mvua ya mawe ikiambatana na upepo mkali, mvua fupi zisizo za msimu, na ukame wa muda mrefu na unaojirudia mara kwa mara. Haya mambo yote tayari yanajionesha hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi, ambayo pia huchangiwa na uharibifu mkubwa wa mazingira umeleta athari kubwa katika sekta mbalimbali za maendeleo ya jamii na sekta zingine ziko katika hatari ya kuathirika pia, sekta hizi ni nishati, kilimo na usalama wa chakula, maji, mifugo (kwa kuzuka kwa magonjwa ya milipuko, ukosaji wa malisho na maji), uvuvi, misitu, wanyamapori, afya, miundombinu, utalii, n.k

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba mabadiliko ya Tabianchi sio nadharia za kwenye vitabu tu kama ambavyo watu wengi pamoja na Serikali inavyoamini, bali ni jambo la uhalisia usiokuwa na hata chembe ya mashaka kama ripoti mbalimbali za kisayansi zinavyothibitisha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara ya kwanza katika uwepo wa Wilaya ya Karagwe ambayo ni moja ya wazalishaji wakuu wa zao la Kahawa na wazalishaji wakubwa wa ndizi, walikumbwa na ukame ambao ulikausha mibuni na migomba na ikalazimu kuomba msaada wa chakula, na pia ni wafugaji wakubwa wa ng'ombe aina ya Nyankole, lakini na mifugo yao ilikufa na wafugaji wengine iliwalazimu kuhamia maeneo mengine ya nchi ambayo yalikuwa

hayajaathirika na ukame ili kunusuru mifugo yao iliyobakia jambo ambalo linaweza kusababisha migogoro (ikiwemo kati wakulima na wafugaji). Kambi Rasmi ya Upinzani inatahadharisha kuwa hizo dalili zinaingia moja kwa moja kwenye kuporomoka kwa uchumi wetu, kama tutashindwa kuwekeza vyema katika kupambana na kuthibiti mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ikiwa moja ya nchi zinazoendelea inahitaji wananchi wetu kujengewa uwezo wa kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi na hiyo kuwa ni kipaumbele cha kwanza. Upunguzaji wa uzalishaji na ongezeko la gesi joto iwe ni kipaumbele cha pili. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kwa kuzingatia mambo haya mawili ni dhahiri madhara yanayojitokeza au yanayonyemelea sekta muhimu kwa uchumi wa nchi zitakuwa zimesalimika au madhara yatapungua kwa kiwango kikubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi hii ya Makamu wa Rais inatambua uzito wa tatizo la mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa joto kali hadi kufikia nyuzi joto 36, sambamba na hayo kumekuwa na mvua kubwa na za muda mfupi zilizosababisha mafuriko katika maeneo mbalimbali nchini, kuyeyuka kwa theluji ya mlima Kilimanjaro, kupungua kwa vina vya maji katika mabwawa, mito, maziwa, kuingia kwa maji chumvi katika nchi kavu/mashamba na vyanzo vya maji (kunakotokana na kuongezeka kwa kina cha bahari), kubadiliko kwa majira ya mwaka n.k

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukweli kwamba mabadiliko ya tabinchi ambayo yamebadili majira ya mwaka kwa kuyacheleweshа au kuyawaisha, na madhara yanayotokea kutokana na mabadiliko hayo mara nyingi yanakuwa ni kuharibika kwa miundombinu na pia watu kupoteza maisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba; uwekezaji unaofanyika kwenye miundombinu kwa kiwango hichohicho kiwekezwe katika sekta za kuzuia na kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Mfano, ujenzi wa

viwanja vya ndege, mvua ya siku moja au masaa kadhaa tu inaweza kuharibu uwekezaji uliofanyika kwa miaka kadhaa, au miundombinu ya barabara na madaraja vinaweza kuharibiwa kwa muda mfupi sana.

**Mheshimiwa Spika,** kiangazi kilichopilitiliza muda wake kikiwa na joto kali sana, kilivyoteketeza mifugo na wanyamapori na hivyo kusababisha umasikini mkubwa kwa familia za wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa watu ambao wanaishi karibu na mito miaka hiyo haikuwa na shida, lakini kwa sasa inaonesha kuwa wanaishi mabondeni. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mito mingi imejaa michanga au udongo na kusababisha mito kupanuka/ kusambaa na pindi mvua kidogo ikinyesha basi yanatokea mafuriko makubwa na kuathiri watu waliokuwa wanaishi hapo miaka yote. Mfano mzuri ni mto Msimbazi kwa miaka ijayo ule mto utapotea kabisa na maji yatakuwa yanapita kila pahala na hivyo kupelekea madhara makubwa. Mfano mwingine ni ziwa Babati ambalo mvua kidogo zikinyesha husababisha madhara makubwa.

**Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni,** tunatambua mchakato unaondelea wa kupitia Sera ya Taifa ya Mazingira (1997) ikiwa na lengo kati ya mengine kujumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

Tunapenda kusisitiza kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi ni kubwa sana kiuchumi, kijamii na kiusalama na hivyo inahitajika kuandaa sera mahususi ili kuyapa uzito unaostahili Aidha tunataka kujua tumejipanga vipi kutekeleza kwa vitendo mikataba yote ya kimataifa ambayo tumeiridhia inayohusiana na mabadiliko ya Tabianchi.

## C. MIRADI YENYE HARUFU YA UFISADI:

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka 2016/17 tuliongelea ufisadi kwenye miradi miwili;

a. mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya jiji la Dar es salaam.

b. mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi maeneo ya pwani (Bagamoyo, Pangani, Rufiji na Zanzibar.

**Hivyo basi, Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni,** iliomba Ofisi ya Makamu wa Rais imtake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanyie ukaguzi maalum (**Special Audit**) wa miradi tajwa hapo awali ya kupambana na mabadiliko ya Tabianchi, pamoja na miradi mingine yote iliyosimamiwa na kitengo cha Mabadiliko ya tabianchi kilichopo chini ya Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano. Tunaomba kufahamishwa mrejesho wa hiyo special audit, kama kweli utumbuaji wa majipu ni ukweli au unaangalia sura za wahusika tu.

## D. MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika,** kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikisisitiza kuwa kila sekta ina muktadha wake wa uharibifu wa mazingira. Na kwa kila sekta inahitaji mbinu tofauti ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira kwenye sekta husika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kilimo, dhana ya mazingira inajikita zaidi kwenye uharibifu wa udongo ***(Soil degradation)***, au kupungua kwa rutuba ya udongo na hivyo kupelekea mimea kushindwa kustawi vyema. Uharibifu wa udongo kwa kiasi kikubwa unasababishwa na shughuli za kiuchumi za kila siku zinazofanyika, ziwe za kilimo, uchimbaji wa madini na mafuta, utumiaji uliopitiliza wa mbolea na viatilifu vyenye kemikali, ufugaji uliopitiliza katika eneo moja. Hizi shughuli zinazosababisha uharibifu wa udongo zimetungiwa sera, sheria na miongozo lakini bado hali ni mbaya.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kurudia mambo ambayo yapo na yanaeleweka ni kama kupoteza muda wa Watanzania. Hoja ya msingi ni kwamba bila ya nia ya dhati ya utoaji wa fedha zinazohitajika kwa ukamilifu wake kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mazingira, basi sera, sheria na miongozo inakuwa ni kazi bure.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo huo wa serikali kutokutoa fedha, programu nyingi za mazingira ya kuhifadhi misitu zimekwama kutekelezeka na hivyo athari nyingi za kimazingira yameanza kuonekana na nchi inaingia kwenye majanga ambayo yangeweza kuzuilika kama serikali ingechukulia kwa umakini unaotakiwa wa mipango na progamu za mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** ukiangalia randama ya Wizara kwenye Idara hii ya Mazingira, ni kwamba program na mipango karibia yote ya kuhifadhi mazingira inayosimamiwa na Baraza la Taifa la Uhifadhi na usimamizi wa mazingira pamoja na uratibu wa utekelezaji wa mikataba ya kimataifa inayohusu mazingira. Zaid ya asilimia 80 ya fedha za utekelezaji kwa miradi na program husika zinategemewa kutoka nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema huu nao ni udhaifu kwani pale washirika wakishindwa kutimiza miadi tu au wakichelewa kutoa fedha, basi program na miradi inasimama.

**Mheshimiwa Spika**, tukumbuke kwamba watu wanaopata madhara kutokana na athari za kimazingira kwenye maeneo husika ni Watanzania, hivyo basi, ni jukumu la msingi kwa Tanzania kulinda na kuhakikisha usalama wa wananchi wake na usalama wa mazingira yanayowazunguka.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka kipaumbele kama inavyoweka kwenye sekta zingine katika kuhakikisha inatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha mipango inayopangwa kuhusiana na mazingira inatekelezwa kwa kadri ilivyopangwa. Sambamba na hilo ni kwamba katika miradi inayofadhiliiwa na taasisi na mashirika ya kimataifa kuna uwezekano mkubwa wa

kuchepusha fedha au kutumika mbali ya kile kilichokusudiwa, hivyo ni muhimu sana miradi hiyo kuifanyia ukaguzi wa karibu na mara kwa mara. Mfano miradi ya kujengea watu uwezo ni rahisi sana fedha kutumika vibaya.

**Mheshimiwa Spika,** katika muktadha mzima wa uhifadhi wa mazingira, suala la maji ndiyo nguzo kuu. Hoja ya kwanza ni maji kiasi gani yanahitajika katika uhifadhi, maji hayo yanapatikana kutoka wapi, maji hayo yanakuwa katika aina ipi na je maji hayo yakishatumika kuna uwezekano wa maji hayo kutumika tena kwa kazi zile zile au kwa kazi tofauti? Na hoja nyingine ni je maji yakishatumika yanahifadhiwaje? Je kama ni maji ya mvua (run off) yanaingiaje kwenye mto na ni madhara gani yanatokea kwenye mto husika? Pia, utafiti katika kiwango na upatikanaji wa maji ardhini (underground water) bado hauridhishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba hayo mambo tajwa ndiyo yanatoa uendelevu wa matumizi ya maji katika uhifadhi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, mazingira kwa muktadha wa uzalishaji na uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani "**e**missions, Effluent and Waste". Kuanzia hapo utunzaji wa mazingira ni kufahamu katika mchakato mzima wa uzalishaji viwandani ni wakati au eneo gani katika mchakato mzima wa uzalishaji unaozalisha kwa wingi gesi ukaa, ambayo inaleta madhara makubwa kwa watu na mazingira? Je kuna mbadala unaoweza kutumiwa katika hatua hiyo ya uzalishaji ili kukabiliana au kupunguza au kusitisha kabisa uzalishaji wa gesi ya ukaa katika mchakato huo wa uzalishaji bidhaa?

**Mheshimiwa Spika,** ni muhimu vile vile kufahamu ni wakati au hatua gani katika uzalishaji bidhaa unatoa taka "wastes" nyingi? Na taka hizo zinatunzwa au teketezwa vipi ili kuhifadhi mazingira? Na je kuna teknolojia mbadala ya kuzifanya taka hizo kutumika tena kwenye uzalishaji wa bidhaa hapo kiwandani au pahali pengine?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani, inafahamu kuwa kazi hizi ambazo zikifanywa na Wizara hii ya Mazingira, kwa kiasi kikubwa ili kuwa ni kutembelea viwandani na kukagua mifumo yao ya maji taka. Hoja ni kwamba viwanda vingi hapa nchini teknolojia yake ya uzalishaji imepitwa na wakati ambayo inapelekea uchafuzi wa mazingira. Hivyo viwanda kupigwa faini kutokana na kuzalisha kwa teknolojia iliyopitwa na wakati nakupelekea viwanda hivyo kufungwa na mwisho kulazimika kupunguza wafanyakazi na kutengeneza tatizo lingine la ukosefu wa ajira.

## E. MFUKO WA TAIFA WA DHAMANA YA HIFADHI YA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika**, mfuko huu ulianzishwa kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa mazingira wa mwaka 2004 kama chanzo cha fedha kwa ajili ya kuhifadhi mazingira nchini. Lakini cha kushangaza hadi leo 2017 ndio Seriali inazindua mfuko huu pamoja na Sekretariat ya bodi ili kufanya kazi za mfuko. Hata hivyo katika bajeti ya mwaka hi shilingi milioni 334 zilizotengwa kwa ajili ya mfuko huu muhimu sana ambao ungesaidia kutatua changamoto za kimazingira fedha ambazo ni chache sana kukabiliana na masuala ya mazingira nchini.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kubainisha vyanzo vya mapato vya mfuko huu ili uwe endelevu na uwe na nguvu ya kifedha kuliko ilivyo sasa. Mfano wa vyanzo hivyo inaweza kuwa 10% ya kila makusanyo ya leseni za viwandani, madini, usafirishaji, utalii, tozo mbalimbali zinazotozwa na TFS. Na pia tozo ya 20% yajumla ya fedha zinazotozwa kwa bidhaa zinazoingizwa nchini na kutozwa ushuru wa uchakavu kwa ajili ya utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa fedha hizi ni dhahiri halmashauri zetu zitaweza kutekeleza miradi yote inayohusu utunzaji wa mazingira.

## F. BARAZA LA RUFAA LA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika,** Baraza hili lipo kwa mujibu wa sheria ya mazingira ya mwaka 2004, kwa lengo la kusikiliza rufaa za wananchi ambao hawaridhiki na maamuzi ya Waziri na masuala mbalimbali katika utekelezaji wa sheria ya mazingira.

**Mheshimiwa Spika**,taarifa ya utekelezaji ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/17 inasema kuwa sasa hivi ndio Ofisi imeandaa hadidu za rejea za kutayarisha Mpango Mkakati wa Baraza la Rufaa la Mazingira ambao ukikamilika ndipo baraza litaanza kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba Waziri mwenye dhamana na Mazingira amekuwa akionekana mara nyingi akitembelea viwanda na kutoa adhabu ya fedha au na kusitisha uzalishaji wa viwanda husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata maeleze, Je, kama waathiriwa wa maamuzi ya waziri kama hawaridhiki, wanapataje haki zao wakati baraza la kupeleka malalamiko yao halipo?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani baada ya kupitia randama ya wizara imeshindwa kuona kifungu kinachoanzisha Baraza la Rufaa la Mazingira, hivyo tuna muomba Mheshimiwa Waziri Mwenye dhamana atuoneshe kifungu kinachotoa fedha za uanzishwaji na utendaji kazi wa Baraza.

## G. KAMPENI YA KITAIFA YA UPANDAJI MITI

**Mheshimiwa Spika,** kampeni ya kitaifa ya upandaji wa miti inaratibiwa na ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, lakini halmashauri zetu zimepewa lengo la kupanda na kutunza miti isiyopungua milioni 1.5 kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa halmashauri zetu hazina fedha za kuzalishaji miche ya miti kwa idadi tajwa na pia haina uwezo wa kutunza miti hiyo kutokana na ukweli kwamba maeneo mengi hali ya maji sio nzuri.

**Mheshimiwa Spika**, kila eneo katika nchi yetu ina aina yake ya miti inayostawi kulingana na aina ya udongo kwenye maeneo husika, aidha, wilaya moja inaweza kuwa na aina tofauti za udongo kuweza kuhimili ustawi wa aina moja ya miti.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana alieleze Bunge, Ofisi yake inatoa kiasi gani au mchango gani wa kuzisaidia Halmashauri zetu ili ziweze kutekeleza zoezi la upandaji na utunzaji miti kwa ukamilifu wake? Tunauliza hivyo kutokana na ukweli kwamba Halmashauri zetu hazina vyanzo vya mapato vya kuweza kutekeleza agizo hilo la Ofisi ya Makamu wa Rais.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri wakala wa huduma za misitu (TFS) ipewe jukumu la kuzalisha miche nchi nzima ambayo inalingana na aina ya udongo na hali ya hewa ya eneo husika. Aidha, kwa udhibiti wa fedha kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais itakuwa ni rahisi kuzifanyia udhibiti kuliko kupeleka fedha kwenye Halmashauri zetu. Hivyo basi, Shilingi bilioni 105 zinazohitajika katika utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya Upandaji wa Miti zitakuwa salama zaidi, bila ya kubadilishiwa matumizi yake.

## H. UZALISHAJI NA MATUMIZI YA MIFUKO YA PLASTIKI

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba Bunge la Afrika ya Mashariki lilipitisha Muswada "***The EAC Polythene Materials Control Bill, 2011***" ambao ulikuwa na lengo la kupiga marufuku uzalishaji, uuzaji, na uagizaji na matumizi vya "**polythene materials". ** Na Serikali kupitia kwa Baraza la Usimamizi wa Mazingira likapiga marufuku hapa Tanzania ili kukazia sheria iliyotungwa na Bunge la Afrika ya Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, ni kweli vifungashio vya plastiki vinachafua mazingira na hilo halina mjadala, lakini mazingira kuwa machafu ni tatizo la uchafu wenyewe au ni tabia ya watu. Jambo hili linaweza kuwa jepesi kutamkwa lakini ni gumu kutekelezwa kutokana na ukweli kwamba uchafu huo

vifungashio vya plastiki unaweza kuwa ni fursa kwa nchi yetu. Kwa kuwa vifungashio hivyo vina **"recycle"** na kuweza kutoa bidhaa zingine, na kwa kuwa bidhaa nyingi zinazotoka nje ya nchi vinakuja vimefungwa kwa vifungashio vya plastiki, hii ni ishara kwamba nchi ambazo ni tajiri kutuzidi na hatuwezi kujilinganisha zao katika maendeleo ya kiuchumi bado wanazalisha na kutumia vifungashio vya plastiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa ni busara mamlaka husika kuliangalia suala hili kwa upande wa kuwa fursa zaidi kuliko linavyoangaliwa. Mfano mzuri sana ni kwa upande wa bidhaa hasa maziwa, lita moja iliyofungwa kwenye mifuko ya plastiki ni shilingi 500/- na kwa ujazo huo huo kwenye chupa yanauzwa kwa takriban shilingi 1500/-. Tuangalie uhalisia wa wananchi wetu vijijini na aina gani ya vifungashio wanavovitumia zaidi. Baada ya kufanyia kazi jambo hilo ndio uamuzi stahiki unaweza tolewa.

## I. NISHATI MBADALA

**Mheshimiwa Spika**, kuna tatizo kubwa sana la nishati mbadala hapa nchini na hivyo kupelekea matumizi ya kuni na mkaa kuwa chanzo kikuu cha nishati inayotumiwa na zaidi ya watanzania asilimia 90. Jambo hili ni chanzo kikubwa cha ukame unaoyakumba maeneo mengi hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Nishati ya gesi kwa matumizi ya majumbani imekuwa ni tatizo kubwa sana kutokana na bei yake, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kama kweli Serikali ingekuwa imedhamiria suala hili la nishati ya gesi kuwa mbadala wa nishati ya kuni kama inge unganisha nguvu za waagizaji wa nishati hiyo toka nje ili wajenge kiwanda cha kuchakata gesi inayozalishwa hapa kwetu na kuiweka kwenye mitungi na kuisambaza nchi nzima. Tunaamini kabisa kwamba bei yake itakuwa ni nafuu zaidi kuliko gesi inayoagizwa toka nje ya nchi.

## J. TAKATAKA KUZALISHA NISHATI MBADALA NA MBOLEA

**Mheshimiwa Spika,** Taka ngumu kawaida huitwa majina mengi-takataka, uchafu, masalia, mabaki na majina

mengine, taka ngumu hazipaswi kusababisha matatizo ya kiafya. Zinaweza hata kuwa chanzo cha pato na rasilimali za kutengenezea bidhaa mpya. Lakini pale ambapo taka ngumu hazikusanywi ipasavyo, kutenganishwa, kutumika tena, kurejeshewa thamani au kuangamizwa kwa usalama, huweza kusababisha kichefuchefu, kutoa harufu mbaya, na kusababisha matatizo makubwa ya kiafya.

**Mheshimiwa Spika**, Taka ni changamoto karibu kila mahali kwa sababu tunaendelea kuzalisha taka nyingi sana. Na kama tunavyoona kwenye maeneo yanayotuzunguka, taka kutokana na plastiki, glasi na chuma haziozi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuliona hilo Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni kwa ushirikiano na Jiji la Humburg Ujerumani walianzisha mradi wa kuchakata taka ili kuzalisha umeme na mbolea, lakini mradi huo hadi sasa bado haujaanza kutokana na mambo ambayo bado hayajakaa vizuri kwa upande wa ushuru wa kuingiza mitambo hiyo hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** jambo hilo ni jema kuwa mfano wa kuigwa kwa majiji na miji mingine hapa nchini, kwani ni chanzo cha ajira pamoja na uzalishaji wa mbolea. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira inafahamu kuwa mradi huo wa kuchakata taka kwa Halmashauri ya Kinondoni umekwama wapi? Na inasaidia vipi katika kuhamasisha miradi mikubwa ya kuweka mazingira ya miji yetu kuwa safi?

## K. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2016/17 NA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2017/18

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira taarifa za utekelezaji hadi mwezi March, 2017 inaonesha kuwa kati ya kiasi cha shilingi bilioni 10.973 zilizopitishwa na Bunge ni asilimia 11.28 tu sawa na shilingi bilioni 1.24. zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kati ya fedha hizo shilingi milioni 236.19 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1.001 ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, ukiangalia muhtasari wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/17 inaonesha kuwa fedha za ndani zilizopitishwa na bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 8 na hadi mwezi March, 2017 serikali imetoa shilingi milioni 236.17 ambazo ni sawa na asilimia 2.95 (2.95%). Hii maana yake ni kuonesha kuwa kukabiliana na athari za mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi kwa ujumla wake sio kipaumbele cha Serikali yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kuna tatizo lingine katika taarifa za utekelezaji ambalo tunashindwa kufahamu kwamba kati ya fedha za ndani za miradi zilizopangwa, ni kiasi gani cha fedha kwa kila mradi zimetolewa hadi mwezi March, 2017. Kwani takwimu zinawekwa kwa ujumla tu, na hili linafanya tushindwe kuhoji kwa mradi fulani fedha zimetolewa au bado na kwa mwaka unaofuata kwa nini bajeti ipande au kushuka? Mfano Mradi ***Na. 5301- Climate change Adaptation Programme,*** fedha za ndani zilitengwa shilingi 3,200,000,000/- na fedha za nje, shilingi 2,594,633,448/-. Mradi huo huo kwa mwaka 2017/18 fedha za ndani umetengewa shilingi 850,000,000. Na fedha za nje shilingi 1,400,000,000/. Mradi Na. 5307 National Environmental Trust Fund mwaka unaomalizika ulitengewa fedha za ndani shilingi 2,100,000,000/. Haieleweki ni kiasi gani kimetolewa na mwaka huu wa fedha mradi huo huo umetengewa jumla ya shilingi 334,454,000/.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza tena kuwa ni muhimu taarifa ya utekelezaji ikaonesha kwa kila mradi ni kiasi gani kimetolewa hadi mwezi March, 2017 wakati Wizara inapotayarisha taarifa hizo.

**Mheshimiwa Spika,**mpango wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/18 mchanganuo wa makadirio ya miradi ya maendeleo inaonesha kuwa kati ya fedha za ndani shilingi bilioni 3, shilingi bilioni 1 ni fedha ambazo matumizi yake hayaendani na usimamizi wa mazingira kama ambavyo ilikuwa katika mpango wa mwaka uliopita. Aidha kwa miradi inayosimamiwa na NEMC shilingi bilioni 2.056 ni kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** inaonesha kuwa mradi wa Kihansi Catchment Conservation Management Project wa gharama ya shilingi bilioni 2.057 unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Mheshimiwa Spika, haya maneno ya "ufadhili wa benki ya Dunia" kwa urahisi utadhani ni bure, lakini hakuna benki ambayo inatoa fedha za bure, ni lazima kuna masharti ya urejeshwaji wake. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ingekuwa vyema kwa umuhimu wa sekta ya mazingira Serikali na taasisi zake ipange matumizi ya utekelezaji wa miradi yake kwa kutumia fedha za ndani, kwani kutegemea ufadhili ni rahisi kutokea mkwamo ambao ungeweza kutatuliwa kama fedha zetu za ndani zingepangwa kwa shughuli hizo.

## L. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** "Mahatma Gandhi" baba wa Taifa la India aliwahi kusema kwamba ***"Earth provides enough to satisfy every man's need, but not every man's greed"***, kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, *"dunia ina kila kitu cha kutimiza mahitaji ya mwanadamu, lakini sio kutimiza matamanio na ulafi wa binadamu".* Kwa muktadha huo ni kwamba, uchafuzi na uharibifu mkubwa wa mazingira katika Dunia hii, Tanzania ikiwa ni mojawapo ni tabia ya binadamu ya ulafi wa kutaka kumiliki kila kitu na katika mchakato wa kumiliki kila kitu ndipo uharibifu unapotokea.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mtazamo mwingine ni kwamba, kitendo cha kutompatia au kummilikisha binadamu kile kinachoweza kuendesha maisha yake na familia yake nalo ni tatizo, kwani kinachofanyika ni kutokutumia kiuendelevu raslimali zilizomzunguka. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa ushauri kwamba, ni muda mwafaka kwa Serikali kuwa na ile dhana kwamba maliasili ni mali ya umma, kwani kuwa mali ya umma hakuna mwenye uchungu nayo katika suala zima la matumizi endelevu ya raslimali zetu.

**Mheshimiwa Spika,** ni muda mwafaka sasa kwa serikali kulipa kipaumbele suala la uendelevu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika utoaji wa fedha kama

ambavyo sekta zingine za kiuchumi zinavyopewa kipaumbele katika upangaji na utoaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**Pauline Philipo Gekul (Mb)**
**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.**
**24/04/2017**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jioni mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Ahmed Ngwali atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka saa 11. 00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Mheshimiwa Ahmed Ngwali na Mheshimiwa Shamshi Vuai Nahodha ajiandae.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza nianze kwa kumpongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake ambayo pamoja na mambo mengine neno Ngariba lilizua taharuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja yangu kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nyuma huku kwenye Katiba katika orodha ya

Mambo ya Muungano orodha ya kwanza, Kifungu Na. 15 kinachohusu mafuta na gesi, ambacho hivi karibuni mwaka 2015, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha sheria tatu, Sheria ya *Petroleum*, Sheria ya Mafuta na Gesi ya *Revenue* na Sheria ya Ustawi wa Mafuta na Gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo linanisikitisha sana dhamira na lengo ya sheria hizi tatu ilikuwa ni kwamba, zinapitishwa sheria, baada ya kupitishwa sheria tunapitisha Katiba mpya, baada ya kupitishwa Katiba mpya, mafuta yanaondolewa katika Mambo ya Muungano. Jambo la kusikitisha ni kwamba, sheria zinaendelea kufanya kazi, kila mmoja kwa upande wake, lakini bado Katiba inatambua kwamba mafuta na gesi ni mambo ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la ajabu sana, Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mara ya kwanza kabisa na kwa ajabu kabisa, katika Sheria ya *Oil and* Gas *Revenue Management Act* ya mwaka 2015, Kifungu Na. 2 (2) kimetoa mamlaka kwa Baraza la Wawakilishi kutunga sheria, zinazohusiana na mambo ya *revenue* za mafuta na gesi. Jambo ambalo tunajiuliza Bunge la Jamhuri ya Muungano linapata wapi mamlaka ya kuitungia sheria, maana yake kuliagiza Baraza la Wawakilishi litunge sheria. Maana yake ni kwamba unafanya Baraza la Wawakilishi wanatunga sheria kwenye Mambo ya Muungano, jambo ambalo ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 64 (3). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chukua Katiba uangalie, kwa hivyo sasa jambo hili limetutia mashaka sana na Baraza la Wawakilishi tayari wameshatunga Sheria ya *Oil and Gas* ya mwaka 2016, sheria Na 6, Sheria ambayo inafanana kabisa copy *and paste* na sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, *Legislature* mbili zina sheria mbili za *oil and gas.* Jambo ambalo ukisoma Katiba Ibara ya 63 ile sheria ya Zanzibar inakuwa batili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu mimi na wanaojua sheria na watu wengine, Baraza la Wawakilishi la

Zanzibar, linatunga sheria kutokana na Katiba ya Zanzibar, kwa hivyo, kuiamuru maana yake hata ungeiamuru kwa mfano, sheria ile madhali imepewa amri na sheria nyingine ile sheria itakuwa ndogo haiwezi kuwa sheria sawa na hii. Kwa hivyo, jambo hili linaleta utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hata ukizitazama hizo sheria zenyewe lengo lilikuwa ni kuyaondoa mafuta katika Muungano, lakini sheria zile ukiziangalia zote zinasema sheria hizi zitatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, sasa unajiuliza ikiwa lengo kuyaondoa mafuta katika Muungano mbona hizi sheria bado ni za kimuungano,. Hilo ndilo jambo ambalo ni la kujiuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la kushangaza Katiba mpya ambayo ilikusudia kuja kuondoa hayo mambo ya mafuta na gesi katika Mambo ya Muungano haipo. Ukitizama Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020, nimeipitia ukurasa kwa ukurasa, hakuna mahali popote panapozungumzia kutakuwa na Katiba mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama ahadi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna mahali popote ambapo kaahidi kuleta Katiba, ukifuatilia maneno yake, maneno yake yalisema kabisa kwamba Katiba siyo ajenda yake, lakini jambo la mwisho hata ukitazama fedha zilizotengwa kwenye bajeti hakuna fedha kwa ajili ya Katiba mpya. Kwa maana hiyo, Katiba mpya haipo. Kwa hivyo, zile sheria kuendelea kufanya kazi pande tofauti ni makosa, ni kuvunja Katiba na ninyi watu mnaohusika na Muungano mpo, Mawaziri mpo, Mwanasheria Mkuu upo! Pia unatunga sheria za Muungano mambo ya mipaka baharini huweki, sasa mafuta ambayo yatagundulika baharini itakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupendekeza kwamba, kwa sababu pesa hamna za kuanzisha Katiba mpya, leteni Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tutumie kipengele Namba 98(1)(b) tuondoe mambo ya mafuta katika mambo ya Muungano. Itakuwa kazi rahisi

sana, tutapiga kura tu *third majority* kwa kila upande kwa Muungano, tutaliondoa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka nilisemee ni suala zima linalohusu fedha za misaada, nakusudia kusema *GBS* pia na nizungumzie suala zima linalohusu *Pay As You Earn* na mambo mengine. Fedha hizi za *Pay As You Earn* zimekuwa ni tatizo kubwa sana, haziendi kwa wakati unaotakiwa Zanzibar, kwa hivyo Zanzibar inapata shida sana kwenye fedha hizi. Tunawaomba fedha hizi zifike kwa wakati unaotakiwa ili Zanzibar ipate kufanya shughuli zake.

Pili; fedha ambazo zinatoka katika *Institution* za Muungano ambazo zina-*genarate fund,* hizi fedha haziendi kabisa, tunaomba Serikali ya Muungano kwamba fedha hizi mzipeleke kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Wizara ya Fedha, miradi ambayo imeiva Zanzibar ni miradi ya *International* kama *UN* na mambo mengine na misaada mbalimbali inayotoka nje za nchi. Mnapopelekewa miradi ile iliyoiva Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anachelewesha sijui kwa makusudi tuseme ama vipi, lakini ile miradi inakaa mpaka inafika wakati sasa hata gharama hiyo ya miradi yenyewe inakuwa imekwenda sana. Kwa hivyo tuiombe Serikali jambo hili pia nalo mlifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la fedha za Mfuko wa Jimbo; fedha za Mfuko wa Jimbo zinazokwenda Zanzibar hazijawahi kukaguliwa, nasema tena hapa kwamba hazijawahi kukaguliwa kwa miaka saba, hii ni kutoka na sheria. Ndiyo maana Jaji Warioba alipokuja na Tume yake akasema, tuna sababu ya kuwa na Serikali tatu, kwa sababu sheria haimruhusu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano kukagua fedha zile katika Hazina ya Zanzibar, kwa hivyo, fedha zile hazijakaguliwa na aje mtu anisute. Kwa hivyo, fedha za Serikali zinatoka kutoka Serikali Kuu ya Jamhuri ya Muungano, kwanza zinachelewa,

zinakopwa na Serikali ya Mapinduzi, lakini hazikaguliwi, kwa hivyo sasa ifanywe kama ambavyo imefanywa kwa *MIVARF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *MIVARF* baada ya kukamilisha utaratibu wa mchakato wa tenda wa kufanya kazi pesa za *MIVARF* ambazo zinatolewa na Benki ya Afrika pamoja na *IFAD* zinakwenda moja kwa moja katika akaunti ya........

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, ajiandae, Mheshimiwa Asha Abdallah Juma.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimefarijika sana kutokana na mambo mawili. Kwanza, mwaka 2008 nilipokuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, lilipitisha Azimio la mapendekezo ya kuondolewa suala la mafuta na gesi katika orodha ya Muungano. Azimio hili, liliungwa mkono na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi. Wawakilishi, kutoka Chama cha Mapinduzi waliunga mkono na wawakilishi kutoka Chama cha *CUF* waliunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Uchaguzi Mkuu uliopita wa Oktoba, 2015, suala la mafuta na gesi lilikuwa ni ajenda muhimu sana katika uchaguzi huo. Chama cha *CUF* kililitumia suala hilo katika kuombea kura na Chama cha Mapinduzi kikafanya hivyo kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi Wazanzibari tumekuwa tukiiomba Serikali ya Muungano

itafute njia ya uchumi itakayoisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kushughulikia masuala ya kupunguza umaskini na kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. Kutokana na umuhimu wa sekta hii, kwa uchumi na maendeleo ya Zanzibar, Serikali ya Muungano sasa imeridhia suala la mafuta na gesi kuondolewa katika orodha ya mambo ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Muungano imefanya busara ya hali ya juu sana, naipongeza sana. Jambo hili lina maslahi makubwa sana kwa Zanzibar na kwa Muungano, lakini inanisikitisha sana wapo miongoni mwetu ambao tumekuwa tukipigania jambo hili litolewe kwenye orodha ya Muungano ili Zanzibar iweze kutafuta mafuta na gesi kwa maslahi ya Zanzibar, sasa hivi tunaanza kuwa na kiguu cha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza nasikia baadhi yetu wanasema oooh, suala hili limefanywa kinyume na misingi ya Katiba na hao tunaosema haya ni kule upande wa Zanzibar ambao tungepaswa jambo hili tuliunge mkono. Naiomba sana Serikali ya Muungano wa Tanzania tusivunjwe moyo na jambo hili, tuendelee mbele jambo hili lina maslahi makubwa sana kwa uchumi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nilipokuwa nikichangia bajeti ya Wizara hii hii mwaka jana, nilisema kuna haja ya uchumi mkubwa kusaidia uchumi mdogo. Mwaka huu, napenda niseme nimefarijika sana kwa kumsikia Waziri Mheshimiwa Makamba akitupa taarifa hapa kwamba kuna mradi maalum unaosimamia uvuvi wa ukanda wa Pwani ya Magharibi ya bahari ya Hindi. Mradi huu bila shaka una umuhimu mkubwa sana kwa uchumi wa Zanzibar. Kama tunavyojua Zanzibar inategemea sana uvuvi na kwa maana hiyo ikiwa asilimia 50 ya wananchi wa Zanzibar wanategemea uvuvi, bila shaka mradi huu utatoa mchango mkubwa sana. Tumeambiwa hapa kiasi cha milioni mia nne sabini na sita, zimepelekwa Zanzibar ili kusaidia wavuvi wadogowadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa kupitia mradi huu, mradi wa usimamizi wa Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bara Hindi, ni vizuri ukaanzisha mradi maalum au mfuko maalum wa kusaidia wavuvi wadogowadogo. Nalisema hili kwa sababu fedha ambazo hivi sasa zinatolewa si haba, lakini si nyingi sana, kwa maana hiyo naomba Wizara hii, ama mradi huu unaweza kuwekwa chini ya mradi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, ama unaweza kuwekwa chini ya usimamizi wa mradi huu nilioueleza. Mheshimiwa Waziri uamuzi ni wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ninayoieleza hapa ni kwamba, kuna haja ya kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi wadogowadogo pia kwa ajili ya kuimarisha mazingira ya baharini. Kama unavyojua, kipindi kilichopita kiasi cha miaka miwili, mitatu hivi iliyopita, tulikuwa na mradi wa kuwasaidia wavuvi wadogowadogo pamoja na ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SHAMSHI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutamka rasmi kwamba naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, ajiandae Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya, nikasimama mbele ya Bunge hili Tukufu ili kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati pamoja na pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi anavyosimamia, kuiendesha Serikali hii na kwa lengo la kuwapatia wananchi wote ustawi na

maendeleo. Mheshimiwa Magufuli amefanya kazi nzuri na katika kazi yote hiyo iliyonifurahisha, moja inathibitisha kudumisha Muungano na inanifurahisha zaidi ni hii ya *standard gauge* nchini, Bombadia hewani, wabadhirifu, wafujaji na mafisadi kwapani. *(Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kutoa utaratibu wa muda ukiangalia toka tumeanza sasa hivi ni saa 11.17 *already* wameshaongea watu wawili, kwa hiyo nataka saa iangaliwe vizuri inawezekana inaminya muda wa watu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba kama uta-*notice* Mheshimiwa Nahodha alipunguza mazungumzo yake, endelea Mheshimiwa Asha.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pongezi hizo za Dkt. Magufuli zinaenda pia kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa jinsi anavyoendeleza kazi zake, Mheshimwa Samia kwa kushirikiana na timu yake na vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu na Timu yote nzima ya Mawaziri na Watendaji, wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nasimama kifua mbele hapa kutoa tena pongezi nyingine kwamba watu kule Uyui katika Uchaguzi Mdogo tumewabandika matokeo Chama cha Mapinduzi, katika Vijiji 14 tumepata na CHADEMA moja, Vitongoji 51 na kwa CHADEMA saba, CCM mbele kwa mbele. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ongelea Muungano.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hawa unaposema wewe wanakuwa wanaumia, wanakiherehere, lakini kila ukipigwa ngumi ndiyo unazidi kuwa imara. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua umuhimu wa Muungano na ndiyo maana leo mimi niko hapa bila ya Muungano nisingekuwa na sauti hii ya kusimama hapa kusema. Umuhimu wa Muungano unajulikana, una tija, unaleta mshikamano, unaleta udugu. Sisi wengine tuna watoto mwisho wa reli huko, kwa sababu ya Muungano, hivyo hatuwezi kukubali Muungano huu ukatawanyika na Muungano huu una faida nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru mpaka sasa hivi kwenye ripoti hii tumeambiwa kero nyingi sana zimemalizika, zimebaki kama kero tatu hilo ni jambo la kupigiwa mfano, hongereni sana Wizara ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea sana lazima niseme hapa maana yake mimi bila ya kuletwa na Zanzibar haiwi. Natoa pongezi za dhati kwa Dkt. Shein kuendelea kuishikilia na kuiongoza Serikali ya Chama cha Mapinduzi bila wasiwasi, maendeleo yanaonekana, kazi nzuri inafanyika na wale wanaongoja zamu yao wangojee mpaka hapo 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mazingira ambalo limeonekana kuwa ni tatizo kubwa sana. Mazingira yanaharibiwa vibaya sana, vyanzo vya maji, ukataji miti hovyo, ukataji mikoko ya baharini. Kwa mfano, kama sehemu za visiwa ile mikoko iko pale kwa kazi maalum ya *biodiversity* kulinda maji yasiingie zaidi, sasa inapokatwa maji yanasogea ardhi ambayo ingeweza kuwa ya kilimo inakuwa ya chumvi, kwa hivyo tija inapungua. Nafikiri iko haja ya kuendelea kuimarisha zaidi udhibiti wa maeneo haya au vilevile kutangaza maeneo ya hifadhi zaidi ya hayo yaliyopo ili kuzuia mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba kuna tabia ya watu kuchukua maji kutoka kwenye mito kupeleka kwenye sehemu zao wanazozitaka matokeo yake ni kuleta shida, kwa nini na sisi hatufanyi kama vile walivyotangaza wenzetu kule India ule Mto Ganges na mito yetu na sisi tukawa tunaiangalia kwamba mtu atakayechafua chafua

au atakayeharibu anakuwa sawa na ku-*temper* na uhai, kwa hivyo lazima kuwa na udhibiti muhimu, tuziimarishe hizo sheria zetu za kudhibiti kwa sababu tunajua mazingira yakiharibika ndiyo uhai unapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka niligusie kwa haraka haraka ni suala la ajira. Tunajua kwamba yalikuwepo makubaliano ya tutapata asilimia ishirini na moja ya *share* ya ajira kwa Zanzibar kwa nafasi za kutoka kwenye Taasisi za Muungano, sasa nimeambiwa nafasi hizo zipo lakini nataka Waziri akija hapa atuambie katika nafasi hizo wamepata Wazanzibari wangapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba kwa nafasi ya Majeshi na Polisi huko hatuna tabu vijana wetu wengi wanapata ajira. Kwa hivyo, tunaomba tufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu hizo nafasi kwa sababu katika kuzipata hizo nafasi kwa vijana wetu yako malalamiko ya kusuasua katika kupatikana nafasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni hili la kuhusu makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais kule Zanzibar bado hayajawa katika hali nzuri sana yamechoka, nafikiri iko haja ya kufikiria kufanya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nataka nizungumzie ukiunganisha na hiyo kwamba bajeti inayotolewa kwa Ofisi hii naona haitoshelezi, iko haja ya kuongezwa. Kwa mfano, Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais kupata 3.7 kwa mwaka mzima bado ni ndogo sana. Kwa mwaka jana Wizara hii ilipangiwa billioni nane lakini imeweza kupata millioni mia mbili, sasa inawakwaza watendaji wa Wizara hii, pamoja na Mawaziri ambao wanafanya kazi nzuri sana, lakini tusipowapatia pesa za kutosha inakuwa ni kikwazo. Tunawapa kazi lakini hatuwapi nyenzo za kufanyia kazi za kutosha, hivyo iko haja ya kufikiria ili kuongeza kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kusema, ni muhimu kuhakikisha Muungano huu unadumu na

unaendelea kudumu kwa sababu ziko tija tunazozipata na usalama tunao na tunaona faida zake. Kwa hivyo siyo Muungano wa kufanyia masihara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuwa na maneno mengi, maneno yangu ni kwamba Muungano udumu na tunaona kazi inayofanywa na viongozi wetu kwa hivyo tuwape *support.* Wanawake kwa upande wetu tunashukuru viongozi wetu wametupa nafasi za kutosha, lakini tunataka zaidi lakini kila tukisema tunataka zaidi Mheshimiwa Rais anasikia na anatuongezea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na Mheshimiwa Dkt. Sware jiandae.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kwa siku ya leo. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya bora kabisa. Awali ya yote kwanza kabisa Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nitoe pongezi nyingi sana kwa wananchi wa Uyui kwa ushindi mkubwa walioupata. Kama tulivyosikia katika Uchaguzi Mdogo wa Vijiji CCM imepata viti 14 sawa na asilimia 93.3 hongera sana. Katika Vitongoji viti 58 CCM imechukua 51 sawa na asilimia 88 hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kutoka katika Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa hotuba nzuri kabisa ambayo imejaa ukweli na uwazi. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyozungumzia zaidi masuala ya mazingira ameeleza kwa uwazi kabisa kwamba hali ya mazingira nchini kwetu siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ni suala mtambuka, tunatambua wazi kwamba nchi yetu sasa inakwenda kuwa ni nchi ya viwanda kwa hiyo tunapokuwa na mazingira ambayo siyo ya kuvutia inatupa hali ngumu

sana kuona kama kweli nchi yetu inakwenda kwenye viwanda. Tunahitaji juhudi za ziada kuhakikisha kwamba tunatunza mazingira yetu ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitizama juhudi za Serikali kwa namna moja au nyingine tumejitahidi, lakini tunahitaji juhudi zingine nyingi za ziada kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanakuwa siyo tishio tena kwa viumbe wanaoishi juu ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mabadiliko ya tabianchi yameleta mabadiliko makubwa sana, ukitizama hata kimo cha bahari kinaongezeka. Kimeongezeka kwa sentimeta 12, maana yake ni kwamba zile kingo ambazo ziko kwenye upande wa baharini na zenyewe ziko katika mazingira hatari ya kuweza kufunikwa na maji na baadhi ya maeneo mengine kuna visiwa vimeanza kufunikwa. Hii ni hali mbaya kwa sababu bila kuchukua tahadhari ya kutosha tutajikuta tuko katika mazingira magumu sana miaka ijayo. Kwa hiyo, ndugu zangu tunahitaji tuungane na mikakati ya Kimataifa pamoja na ile mikataba ambayo Tanzania imesaini ya Kimataifa kuhakikisha kwamba tunashiriki katika kudhibiti uharibifu wa mazingira unaotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kuongelea suala la Mfuko wa Mazingira. Tunatoa pongezi kubwa sana kwenye Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Februari, 2017 umeanzishwa huu Mfuko wa Mazingira ambao Mheshimiwa Ndugu Ali Mufuruki amechaguliwa kuwa Mwenyekiti. Huu Mfuko wa Mazingira ni muhimu sana tuufanyie kazi. Mfuko huu wa Mazingira tuuwezeshe, tuhakikishe kwamba tunaupa nguvu ya kuweza kufanya kazi ya kutekeleza au kusimamia ile Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Tunaomba Serikali izingatie kuusaidia na kuhakikisha kwamba huu Mfuko unafanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitizama suala la mazingira kama tunavyosema ni suala mtambuka, lakini ukitizama

Wizara hii haipewi fedha za kutosha, haipewi *facilities* za kutosha kuhakikisha inafanya kazi inavyostahili. Ukitazama katika tozo kuna tozo mbalimbali zinazohusiana na mazingira, ukiangalia tozo kwenye magari chakavu, ukiangalia tozo kwenye mkaa, ukiangalia tozo kwenye mafuta, tozo kwenye majengo, kwenye migodi, kuna magogo yanatozwa kodi ya mazingira, lakini Mfuko huu haupewi chochote maana yake nini?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hata katika Kamati ya Mazingira imeeleza angalau asilimia tano ya hizi tozo iende kwenye Mfuko wa Mazingira ili kusudi Mfuko huu uweze kupatiwa nguvu ya kuweza kufanya kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama hapa katika Mfuko huu wa Mazingira na juhudi kamili ambazo zinaendelea katika Wizara hii, utaona kuna mwingiliano wa hali ya juu katika Wizara zingine. Wizara ya Mazingira ina-*insist* watu waweze kutunza mazingira, waweze kupanda miti na kuacha ile misitu ya asili iendelee kukua, lakini kuna Wizara zingine kwa mfano, Wizara ya Maliasili kupanda miti siyo *priority* kwao, wao kuvuna miti ndiyo kipato kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iangaliwe namna ya kuweza ku-*harmonize* hizi sheria ili kusudi hawa wote wawe na majukumu sawa ya kuweza kutunza mazingira. Ukitazama Wizara ya Maliasili wao misitu wanaitumia kwa ajili ya kutunzia wanyama lakini masuala ya kupanda na kuhakikisha kwamba misitu inalindwa hiyo inakuwa ni kazi ya Wizara ya Mazingira chini ya Mheshimiwa Makamu wa Rais. Sasa hapa hizi Wizara zote mbili au tatu zihakikishe kwamba wana-*harmonize* hizi sheria kuhakikisha kwamba Wizara ya Mazingira inakuwa na nguvu kuhakikisha kwamba inasimamia Sheria ya Mazingira na Sheria hizi zinahakikisha kwamba zinatunza mazingira kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kuongelea kuhusu bajeti ya mazingira, bajeti ya mazingira leo imeombwa hapa, lakini inasikitisha sana ukiangalia bajeti

ya mwaka 2016/2017, walikuwa wametengewa shilingi billioni 20 lakini ile bajeti *ceiling* kwa mwaka huu imepungua. Tunaomba Serikali iangalie uwezekano wae kuitengea bajeti ya kutosha Wizara hii. Hii Wizara ni nyeti lakini inaonekana kama vile haipewi *priority* kama Wizara zingine, wanapewa pesa kidogo na kweli uharibifu wa mazingira ni mkubwa kiasi kwamba hapo baadae watashindwa kufanya kazi na mazingira yetu yatazidi kuwa mabovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kutoka billioni 20 ya mwaka 2016/2017, angalau wangerudia kupewa kiasi kile kile, sasa bajeti imepigwa panga imekatwa kutoka billioni 20 inakwenda kwenye billioni 15. Matokeo yake ni nini? Hawa wanafanya kazi kwa kutegemea Mfuko wa *NEMC* na *NEMC* ndiyo inayowalisha Wizara ya Mazingira na *NEMC* inalalamikiwa kwa kutoza watu tozo na *penalty* nyingi ambazo kwa kweli zinafanya watu wasijisikie vizuri na *NEMC* inavyofanya kazi. Kwa hiyo, naomba mambo haya yote yazingatiwe vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake kwa kutuwezesha Mkoa wa Simiyu kupata pesa za mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kiasi cha dola za Kimarekani millioni 100 sawa na billioni 230. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Simiyu, kwa niaba ya wana-Maswa na Wilaya zingine zote za Mkoa wa Simiyu, tuna uhakika sasa tutapata maji kutoka Ziwa Victoria na tutahakikisha kwamba tutapata maji ambayo yatatusaidia kutunza mazingira ya Mkoa wetu wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyotambua Mkoa wetu wa Simiyu ni Mkoa kati ya mikoa nane ambayo iko katika tishio ya kuwa jangwa hatuna vyanzo vya maji , hatuna vyanzo ambavyo ni vya uhakika kuweza kupata maji, kuweza kumwagilia na kufanya shughuli za kiuchumi kwa maana ya kilimo na shughuli zingine za kufuga na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupata mradi huu tunashukuru sana kwamba sasa Mkoa wa Simiyu utaamka na utakuwa ni mkoa ambao utalima mazao mengi kwa kupitia mradi huu kwa maana ya kumwagilia, tutalima mpunga mwingi wa kutosha na tutatunza mazingira ya kutosha na mkoa wetu utakuwa ni *green,* tunasema ni mkoa ambao ni wa kijani. Tunawashukuru sana na tunaomba wana Simiyu wajiandae kwa miradi hii mikubwa inayokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni matumizi ya plastiki, tumeona jinsi juhudi za Serikali ilivyofanya tunawapongeza Serikali kwa kuweza ku-*burn* viroba, viroba ilikuwa ni moja ya vitu vinavyochafua mazingira. Ninachotaka kusema ni kwamba katika vile viroba vya pombe, uchafuzi wa mazingira wa viroba vya pombe ulikuwa ni kama niasilimia *0.001 something* kule. Sasa kuna mifuko ya plastiki na yenyewe tulishatoa tamko katika Kamati yetu kwamba watengenezaji wa vifungashio vya plastiki watoke katika teknolojia ya sasa hivi ya mifuko ambayo haiozi waende kwenye teknolojia ambayo ni *bio-degradable* ambayo mifuko ukiisha i-*produce* baada ya miezi mitatu ukiitupa kwenye udongo mifuko ile inaoza. Tunaomba waende kwenye hiyo teknolojia, dunia yetu itakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *at the same time* Serikali itoe elimu ya kutosha jinsi ya utupaji wa plastiki, watu wafahamu namna ya kutunza mazingira na mwisho Kamati iliishauri Serikali kwamba Serikali i-*insist* sasa kuwawezesha Wajasiliamali waweze kuanzisha viwanda vya bidhaa......*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware na Mheshimiwa Ali King ajiandae.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nitatoa mchango wangu katika sekta ya mazingira katika Wizara hii, ningependa tu tukumbushane

na kusisitiza kwamba mazingira ni suala mtambuka, mazingira ni uhai, mazingira ni kila kitu. Mazingira haya ni ardhi, ni hewa, ni maji, ni kila kitu ambacho kinatufanya sisi kama Watanzania tuishi au kama binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba mazingira ukiangalia kwenye mfumo mzima wa Wizara zote hizi tulizonazo hata ukiangalia katika bajeti kipaumbele chake kipo kidogo sana. Hii iko dhahiri kabisa hata kwenye masuala ya maendeleo bajeti ya maendeleo ilivyo finyu au mfuko wetu wa maendeleo ulivyofinywa, hii inachanganya kidogo. Sasa hatuwezi kukuza sekta za kiuchumi au za kijamii tukiweka mazingira kando. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia suala la ardhi, ardhi tunaitumiaje katika masuala ya madini, ukulima, ufugaji, kila kitu kinatoka ardhini lakini ardhi yetu ukiangalia kwa Tanzania karibu asilimia 61 ya ardhi yote ina mmomonyoko wa udongo, hali ya ardhi ni duni. Sasa kama una ardhi duni ina maana hata misitu haifanyi vizuri, mazao hayafanyi vizuri, na hii hali inaendelea namna hii na hatuna mipango mikakati au madhubuti ambayo iko-*reflected* kwenye bajeti ya kutunza ardhi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye masuala ya bahari na mambo ya mwambao, bahari yetu ina matumbai karibu ukubwa wa hekari 3,580 za mraba, tuna misitu katika mwambao wetu yenye karibu hekari 70,000 inakatwa hovyo, matumbai yanapigwa mabomu kwenye uvuvi wa haramu tunaharibu mazingira. *Effect* yake tunakuja kuiona pale tunapoharibu mazingira baharini na misitu ya mwambao, hii yote inakuja kuleta madhara kwenye hali ya hewa. Tunaongelea mafuriko, tunaongelea mabadiliko ya tabianchi, hii inatokana na sisi kuharibu mazingira yetu ya baharini na hata kwenye ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la misitu nchini kwetu. Kuna uvunaji holela na ukataji wa holela na uuzaji holela wa misitu. Misitu ndiyo hii inayofanya tupate maji kiasi gani au hali ya hewa iendeleeje, kwa hiyo kunahitajika

kuonesha *reflection* kwamba kuna haja ya kutunza mazingira ukiangalia hasa katika sekta ya misitu. Mfano Tanzania tunapoteza karibu hekari laki tatu na sabini kwa ukataji holela wa misitu, je, tunai-*replace* vipi? Mikakati madhubuti hatuioni ikiwa *reflected* kwenye sekta hii ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili nataka niligusie kwa urefu kidogo na hili ni kuhusu usimamizi wa taka, taka ngumu, taka kwenye maji na taka za kielektroniki. Kwa mfano, Mji wetu wa Dar es Salaam una-*potential* ya kuwa mji *popular* duniani ni mzuri na wenye kuvutia, lakini takwimu na *information* za mwaka 2010 inaonyesha Mji wa Dar es Salaam umeshika namba nane dunia nzima kwa uchafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuangalii tu mandhari ya uchafu lakini zile *impact* na *effects* zinazoletwa na uchafu. Kwanza ni magonjwa, karibu asilimia 80 hapa nchini kwetu hatuna mfumo mzuri wa ukusanyaji wa taka na kuzitenga zile taka. Taka ngumu, taka ambazo haziwi *degraded biologically,* zote zinachanganywa na ukiangalia kwa Mji mkubwa kama Dar es Salaam ambao unaongoza kwa idadi ya watu tuna sehemu moja tu ya *dumping site*- Pugu ambayo ina eneo karibu la hekta 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile takataka zinazotupwa kule Pugu jinsi ambavyo zinakuwa *treated* haziendani sawasawa na utunzaji wa mazingira. Zinatupwa, hamna *mechanism* maalum ya kuzuia uchafu ule wenye sumu usisambae katika mifumo ya maji, hakuna njia ya kuzuia kwamba unapochoma moto ule moshi una madhara gani kwenye hali ya hewa na hata kwenye afya za binadamu. Kwa hiyo, kunahitajika kuwe na mfumo madhubuti wa kuchanganua taka na jinsi ya kuzi-*treat* hizo taka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna vifaa vya simu, tuna *computer, fridge, television,* lakini hakuna mfumo madhubuti wa kuhakikisha kwamba taka za aina hii ya elektroniki zinatunzwaje au zinatolewaje katika mazingira ili zisilete madhara yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitagusia pia kwenye Mfuko wa Mazingira. Tumejiwekea mkakati, tumeweka mfumo mzuri lakini kwa bahati mbaya hatujawa *serious* au makini na mfuko huu. Ni kwa sababu pia hatuja-*reflect* umuhimu wa kutunza mazingira na kusimamia mazingira. Sasa hivi Serikali yetu tunataka kuwa na mfumo wa viwanda lakini huoni ile *link* ya hii *system* mpya kwamba tuwe na mfumo wa viwanda au uchumi wa viwanda ina-*link* vipi na mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hatujajua au hatujachanganua kwamba hivi viwanda vinatumia rasilimali gani na rasilimali hizi tunazozivuna na zinazoenda kuwa *treated* huko kwenye viwanda zitakuwa zina *effect* gani kwenye mazingira. Mfuko huu hauna fedha, kwa mfano kwenye kitabu hiki cha maendeleo ya bajeti, zimetengwa milioni mia tatu tu na chenji, utafanya nini na milioni mia tatu kwenye suala la mazingira ambalo ni mtambuka? Je, mta- *address* nini? *Issues* za hewa, za maji, za ardhi au *issues* zinazotokana na uharibifu wa mazingira kutokana na viwanda. Je, mikakati ni ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu unaweza ukawa na *sources* nyingi za kujipatia fedha, mfano *TRA* wanavyoweka *extra charges* kwenye magari chakavu au yaliyozeeka na kadhalika hela hizi zinatumikaje? Kwa hiyo, kuna umuhimu wa Serikali kuweka kipaumbele kwenye mfuko huu kwa ajili ya utunzaji wa mazingira na usimamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *National Environment Action Plan* yetu ya 2013-2018. Hii imekaa kimaandishi tu lakini *action plan* yetu hii haina *budget line* na haina *indicators* au *indicators* zilizopo ni chache. Hii inaonesha dhahiri kwamba hatujawa waangalifu au hatuoni uthamani wa mazingira, mazingira ambayo yanayotufanya tuwe tumesimama hapa tukiwa tuna afya. Kwa hiyo, naomba hili liangaliwe upya. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, kuna msemo ambao unasema kwamba kama huna *information* au *data then*

huna *right* ya kuongea. Sasa ukiangalia *research* ambayo inasimamiwa na taasisi yetu ya *NEMC* haina hela ya kufanya tafiti. Sasa tunapokaa tunasema kwamba kuna mafuriko, kuna mabadiliko ya tabianchi, hali ya hewa haieleweki, mvua za masika hazieleweki, hatuwezi kusema kwa *confidence,* tunakuwa tu tunahisi au tunafikiria itakuwa hivyo lakini hatuna *data* ambazo zina *back up* kwamba hali ya hewa inakuwaje, ardhi yetu tuitumiaje, sasa tutafanyaje hizi kazi kama *NEMC* haipewi hela ya *research?* Yote yanakuwa batili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo kwa kusisitiza kwamba, mazingira ndiyo yanayoshika rasilimali zetu tunazotumia, *natural resources,* tusiidharau, tutazidi kulalamika kwamba hakuna maendeleo endelevu kwa sababu kutwa tunaharibu mazingira yetu na mazingira yetu hatuyatunzi wala hatuyapi kipaumbele katika kuyafanyia *research,* katika ku-*disseminate* hiyo *information, awareness raising* haipo wala usimamizi wake ambayo iko *reflected* kwenye bajeti haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKTI:** Ahsante kwa mchango mzuri sana. Naielekeza Meza ya Makatibu, *issue* hii ya mazingira bajeti yake iende kwenye Kamati ya Bajeti na Waziri na Mwenyekiti mje mtetee hoja hizi ili mtazame kama mnaweza kuongezewa pesa kwa sababu bila mazingira *we don't have a country.* Kuna *issue* ya *fridges, computers,* na hizi *fridges* zinazoletwa hapa ndiyo zinaharibu *ozone layer* yetu. Kwa hiyo Makatibu mchukue *note* hiyo.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Ali King, ajiandae Mheshimiwa Khadija Aboud.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai na tumefika leo hapa kujadili masuala haya ya mustakabali wa nchi yetu katika Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufunguzi wa neno langu kubwa ambalo napenda nilitumie ambao ni msemo wa wahenga unasema anayekufukuza akishaona hakupati basi nyuma huku hukurushia matusi. Kwa hiyo, namwomba Waziri wangu wa mambo ya Muungano, mambo ambayo yameandikwa yakawa *presented* hapa, haya mengine wewe yachukulie tu. Hawa wako mbali sana, kwa hiyo lazima watarusha maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza utekelezaji wa mambo ya Muungano ambayo Mheshimiwa Waziri ameyataja kwenye kitabu chake kuanzia ukurasa wa 42 mpaka ukurasa wa 52 ambayo pamoja na mengine siyo ya kimuungano lakini ni ya ushirikiano ambayo ni sekta siyo za Muungano lakini tulishirikiana pamoja na Zanzibar. Kwa hili nakupa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kikubwa ambacho nakisema hapa labda pengine kwa watu wengine ambao wanasema kwamba labda Serikali hii haina kipaumbele au haijaweka mtazamo mkubwa katika kuangalia masuala ya Muungano ili waelewe, tunaelewa sisi kuna fedha za maji ambazo zimepita katika Jamhuri ya Muungano mkopo kutoka India, ni zaidi au karibu robo ya bajeti ya Zanzibar ambazo zimeenda kule, wasiojua walijue hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hili kwa sababu wakati mwingine mtu ukiambiwa kipofu siyo lazima kwamba haoni, inawezekana mtu akapofua fikra. Kwa hiyo, humu kuna watu wamepofua fikra zao, zile fikra zao ndiyo vipofu hawawezi kuona, hata kama wana macho hawataweza kuona, hata kama wana masikio hawataweza kusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi labda nimnukuu Spika kwamba kumbe walemavu kweli wamo wengi humu, kwa sababu fikra pia nazo zinampeleka mtu kulemaa, akafikiria hata jambo la kuliona wazi asiweze kuliona. Kwa hiyo, hilo ni moja katika kuangalia mambo mazuri ambayo yamepangwa na yamefanyika katika Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipengele ambacho Mheshimiwa amekizungumzia katika ukurasa wa 51, ushirikiano katika mambo ambayo siyo ya Muungano hasa katika masuala ya afya na nakwenda katika Bima ya Afya. Mfuko wa Bima ya Afya unafanya kazi Zanzibar, pia Mfuko huu wa Bima ya Afya unafanya kazi Tanzania Bara ambapo uko chini ya Wizara ya Afya. Jambo ninaloliomba hapa, muundo wa Halmashauri ambao uko huku ambao Wazee wanapata Bima ya Afya ni tofauti na muundo wa utawala kule Zanzibar ambapo mara nyingi Majimbo huwa yanajitegemea, tunajua Wazee kuna fedha zinatengwa kwa ajili ya kupatia Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu au ushauri wangu, kwa nini tusiendeleze ushirikiano tukachukua katika ngazi ya Majimbo, likazungumzwa, likatazamwa kwamba linafanywaje ili tuweke huu ushirikiano katika kuwapatia wazee Bima ya Afya kama vile ambavyo wazee wanapata Bima ya Afya kupitia katika Halmashauri za Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili binafsi katika Jimbo langu niliwahi kulitekeleza lakini zikatokea changamoto. Kwa hiyo kutokana na hizo changamoto zilizojitokeza, mwaka huu tumesimama. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu sikivu, hapa tuweze kuliratibu hili kama linaweza kufanyika hata katika ngazi ya Majimbo, kwa sababu katika Serikali ya Zanzibar hakuna utawala ambao uko maalum katika Halmashauri ambao unapelekewa fedha ili kuhudumia sekta za jamii. Majimbo yenyewe pengine kupitia Mbunge na Mwakilishi wanaweza wakafanya hili jambo, kwa hiyo tunaiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano iliangalie hili kupitia mzungumzo ya Wizara hii ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine alizungumza hapa Mheshimiwa Shamsi Vuai kwamba tuangalie jinsi gani uchumi mkubwa unaweza ukasaidia uchumi mdogo. Hapa moja kwa moja nije katika *corporate tax.* Tunajua kwamba *pay as you earn* inapatikana kama ilivyopangwa na makubaliano yalivyo. Nafikiri Mheshimiwa Waziri hili

analifahamu. Pia *custom duty* na *excise duty* kwa Zanzibar wanakusanya wenyewe, lakini *corporate tax* inakusanywa kwa mujibu wa kampuni iliposajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa usajili mara nyingi, mtu atafanya usajili sehemu ambayo kuna urahisi wa kusajili na urahisi wa kusajili unakujaje, alipo *regulator* kwa mfano, benki nyingi sana haziwezi kuja *ku-register* Zanzibar, zita- *register* Tanzania Bara. Kwa hiyo, kwa kuwa zitakuja ku-*register* Tanzania Bara ina maana kwamba hata kodi yake itakuwa inalipwa Tanzania Bara. Kwa hiyo mapato haya yanayotokana na kodi ya kampuni tujaribu kuangalia kigezo kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kigezo kingine kwa sababu makampuni haya yanafanya kazi katika mazingira ya Zanzibar, wanawatumia wateja wale wa Zanzibar, wanafanya shughuli zao pale na mazingira ambayo yamewekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini bado c*orporate tax* zao wanalipa kwa Tanzania moja kwa moja. Tunaomba kungekuwepo kigezo cha *operation* au kama itakavyoonekana katika mazungumzo kwamba pia hizi c*orporation tax* pia ziwe zinakusanywa Zanzibar kwa *portion* ya zile benki au taasisi za simu zinavyofanya kazi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika hili, tumebadilisha Sheria kadhaa ambazo zinahusiana na mambo ya mapato ikiwemo ku-*charge transactions whether* za kwenye simu, miamala ya kifedha, lakini bado miamala ya kifedha kwa kuwa kwamba hivi vyombo vimesajiliwa Tanzania Bara haziwezi kwenda Zanzibar. Kwa hiyo, tutafute mazingira kwa sababu na Zanzibar wanatumia hizi benki, Zanzibar wanatumia hizi *transaction,* miamala hii waweze pia kuipitia na Zanzibar waweza pia kunufaika. Hili ni jambo ambalo nashukuru sana kama litafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nianze na msemo mdogo unaosema kwamba muungwana ni yule ambaye akinena halafu anatekeleza. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Muungano aliniahidi kwamba atakuja

kunitembelea Jimboni na nashukuru akafanya uungwana ule akaja kunitembelea Jimboni, akaona mazingira niliyomuhadithia hapa, namshukuru sana. Namkumbusha tena Mheshimiwa Waziri aliwaahidi wananchi wangu baada ya kuja Jimboni kwamba atakuja kufanya jambo fulani la kimazingira ambayo aliyaona. Kwa hiyo namkumbushia na hili nalo pia aliangalie. Hili ni muhimu kama litafanyika kwa ajili ya kuboresha Muungano wetu na kufanya mambo ambayo yataweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie kuna msemo hapa ulisemwa, *"kilitajwa kisu sijui cha ngariba, lakini ngariba mzuri haogopi mikojo na aliyewahi kutahiriwa na ngariba kwa bati lenye kutu hawezi kumsahau". **(Maneno hayo siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)***

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa King, jielekeze kwenye hoja, haya maneno tulishayasuluhisha asubuhi. Nakuomba jielekeze kwenye hoja, hayo maneno yafuteni kwenye *Hansard.*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hayo maneno yasiingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni uvuvi wa bahari kuu. Katika uvuvi wa bahari kuu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipanga kujenga bandari ambazo zitakuwepo Zanzibar pamoja na chombo cha kufanyia *survey* kwa uvuvi wa bahari kuu. Mpaka sasa hivi tunaona masuala haya yamekwama. Labda kupitia mazungumzo haya katika Wizara hii ya Muungano iweze kuangalia, kwa sababu Bandari ambazo ziko hata meli ziki-*register* kuja kuvua Zanzibar au kuja kuvua katika uvuvi wa bahari kuu, haziwezi tena kurudi kwa sababu mazingira ya bandari zetu kwa Tanzania Bara pamoja na Zanzibar siyo mazuri. Kwa hiyo, tufanye hayo mazingira yawe mazuri na tuweze kuendelea kunufaisha watu wetu katika uvuvi huu wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, sina mengi ya kusema, naunga mkono hoja, Waziri wetu piga kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Khadija Aboud, jiandae Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kwa dhati kabisa kuwapongeza Viongozi wetu Wakuu wa nchi, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Viongozi wote wa Serikali pamoja na Wizara hii ambayo leo tunajadili bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ni suala pana na linahitaji mbio za haraka ili kunusuru nchi yetu. Kama lilivyoelezwa na Wizara yenyewe na hatua mbalimbali ambazo wanachukua napongeza kwa jitihada hizo ziendelee na wazo la kuongeza fedha katika bajeti ya Wizara hii ni muhimu kwa sababu ndiyo urithi wa nchi yetu na vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya Muungano ni pana, hivi sasa vizazi vingi tuliopo tumezaliwa baada ya Muungano. Kwa mantiki hiyo, vijana sisi ambao wengi wetu ni raia wa Tanzania tunaoishi sasa tunaupenda na tuko tayari kuupigania kwa nguvu zote Muungano wetu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie changamoto za Muungano. Nashauri changamoto za Muungano pale zinapotatuliwa zitangazwe bayana kila mwananchi azielewe, kwa sababu ni changamoto nyingi zimefanyiwa marekebisho na zimeshafanyika kazi lakini bado wananchi hawaelewi. Nasisitiza pia ushirikiano wa sekta ambazo siyo za Muungano, kwa sababu raia wa nchi mbili hizi au wa Jamhuri ya Muungano wanatumia fursa mbalimbali kwa nchi zote mbili Zanzibar na Jamhuri ya Muungano kama hospitali, elimu na mengineyo, pamoja na utamaduni na mila zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa jina la sasa Tanzania una umri wa miaka 53, ni chombo muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya

Watanzania na hasa Wazanzibari wapenda amani, utulivu na maendeleo. Yeyote anayebeza au kudharau Muungano huu na kuwa hautakii mema tunamjua ni mmoja katika maadui wa nchi yetu. Dunia, Afrika na majirani zetu wanafahamu kwamba Tanzania ni nchi ya amani na hususan ikiwemo Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muungano huu na Mapinduzi ya Zanzibar, majaribio mengi ya *vitimbakwiri* yalifanyika kutaka kudhoofisha au kuondosha kabisa, lakini kwa uimara wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano wa Tanzania majaribio hayo yameshindwa. Moja kati ya jaribio hilo ambalo limeshindwa lilisababisha kifo cha muasisi wa Mapinduzi na Muungano Mheshimiwa Abeid Amani Karume, lakini kwa uimara wa Serikali zetu majaribio hayo yameshindwa na yataendelea kushindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie miradi ambayo inatokana na fedha na mambo yanayohusu Muungano. Naomba nichukue nafasi hii kwa kifupi sana kwa wale wasiofahamu umuhimu na maendeleo ya Muungano. Kwanza ni ulinzi na usalama, hilo sina shaka nalo ni faida moja ya Muungano, nikigusia kwenye elimu kuna miradi mikubwa ya uanzishwaji wa shule za sekondari 19 pamoja na ujenzi wa Chuo cha Benjamin Mkapa kule Pemba, hizo ni faida za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa shule sita za sekondari zikiwemo shule tatu zilizomo katika Jimbo la Mheshimiwa Ally Saleh shule ambazo ni Forodhani, Hamamni na Tumekuja, zimo ndani ya Jimbo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mifuko hii ya Muungano tumepata mafunzo ya Walimu ambapo jumla ya Dola za Kimarekani milioni 42 zilitumika kwa mkopo wa Benki ya Dunia zilizokopwa na SMT. Pia kuna dola milioni 10 kwa ujenzi wa *school* mpya sita Unguja na nne Pemba. Hayo ni matunda na mafanikio ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu, kuna miundombinu ya barabara ikiwemo Mkapa *road* Mkoa wa Mjini Magharibi, kuna barabara Pemba zilizojengwa kwa Mfuko huu wa Muungano.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi tu tarehe 4 Julai, Mkopo wa India wa *USD* 92.1 milioni kwa ajili ya mradi mkubwa wa maji Mkoa wa Mjini Magharibi. Pia kuna uimarishaji wa miundombinu ya maji mijini na vijijini kwa mkopo wa *ADB* wa dola milioni 21. Pia tumesikia leo miradi ya mazingira kupitia *TASAF* na mifuko mingineyo kuhifadhi mikoko, ujenzi wa kuta, kuzuia bahari, bahari inakula visiwa vyetu lakini Mifuko ya Muungano inakwenda kusaidia kulinda bahari isile visiwa vyetu kule Zanzibar. Pia kuna miradi mikubwa ya mikopo ya SMT ndiyo inayodhamini Zanzibar pale ambapo itashindwa SMT inalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoona Mifuko ya *TASAF* imesaidia wajasiriamali wetu wadogowadogo, pia imesaidia masoko, ujenzi wa vituo vya afya na zahanati, imesaidia kaya maskini, yote hayo ni matunda na faida za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Muungano wetu imara tutaulinda, tutaudumisha, kwa maslahi wa wananchi wote wa Tanzania, vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Dunia inaona, Afrika inaona na sisi tuko imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Aeshi dakika tano.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante angalau kwa dakika tano. Nashukuru kwa kunipa nafasi, naomba kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mwisho, nimpongeze Waziri kufanya ziara kwa kuja kutembelea Mkoa wetu wa Rukwa na hatimaye kuliona Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziwa letu linakauka, ziwa ambalo ndiyo jina la Mkoa wetu wa Rukwa, lakini kwa sasa linaelekea kukauka. Nakuomba Waziri, Mheshimiwa January Makamba uendelee na nguvu hiyo na utenge fedha kwa ajili ya kusaidia Ziwa letu la Rukwa lisiweze kukauka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umenipa dakika tano lakini naona zinataka kunichanganya ni chache sana. Niombe tu kwamba katika huu Mfuko wa Mazingira basi ianzishwe sheria kama ambavyo ilivyo sheria kwenye mifuko mingine. Hakuna maendeleo bila uwekezaji katika mazingira, hakuna maendeleo bila utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa ambalo nataka kuongelea leo ni suala la Serikali yetu kupiga marufuku viroba. Hili nataka kuliongelea kwa uchungu kidogo kwa sababu, sisi ndiyo Wawakilishi wa wananchi. Wananchi wanatakiwa sisi tuwatetee ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ambaye anapinga uharibifu wa mazingira, lakini suala la kupiga marufuku viroba tungelipa nafasi kidogo. Kuna watu wamenunua viroba hivi, kuna watu wametumia fedha nyingi sana, kuna watu wamekopa fedha nyingi na hatimaye tumezuia biashara hii ambayo naamini kabisa biashara hii ilikuwa halali haikuwa haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimuulize Mheshimiwa Waziri kama biashara hii ilikuwa halali na leo hii tumepiga marufuku, wananchi hususan wafanyabiashara wa Mkoa wa Rukwa na Jimbo la Sumbawanga Mjini walinunua kwa wingi wakitegemea wakienda kuuza watapata faida, lakini tumevizuia. Niombe tu kauli ya Serikali kwa hawa ambao wamezuiliwa je, hatuna haki ya kuwalipa fidia?*(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Wengine wamekufa.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tuliangalie hili kwa uchungu, kwa hisia kali. Leo hii mtu amekopa fedha benki, kachukua fedha zile kaenda kufanya biashara, amekopa viroba vyake akauze, leo hii tumevizuia, hebu niambie ni hisia gani anapata na uchungu gani mkubwa anaoupata. Kuna mtu amejiua Dodoma hapa, leo hii ukienda kwenye vituo vya Polisi kuna viroba vimejazana, matokeo yake wanachukua kimoja kimoja wananyonya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu nikuombe sana, kwa sababu nahisi, najua uchungu wa mtu anavyofilisika. Kwa hiyo, hili liangalieni upya, litoleeni maelezo, ni bora tukazuia *production,* bora tukazuia kule ambako vinatengenezwa, tuwape muda wafanyabiashara hao waliovinunua wauze mpaka viishe, naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu kule kuna wafanyabiashara watano, mpaka leo wamekamatiwa mali zao, wamefilisika na nyumba zao zinauzwa. Nimwombe sasa Mheshimiwa Waziri anapokuja kutujibu hoja yetu hapa, naomba hili alitolee ufafanuzi, ni lini hawa wafanyabiashara wataruhusiwa kuuza viroba vyao au Serikali itoe tamko iwalipe fidia ichukue viroba wakaviteketeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa ilikuwa ni hiyo, kwa sababu sioni mantiki yoyote ya kile kitu ambacho ilikuwa ni halali, mtu akachukua fedha zake akaenda akanunua tena amenunua kiwandani, siyo haramu hiyo hapana, amenunua ili akauze apate faida, sisi tunazuia tunawanyang'anya tunakwenda kuvitunza kwenye maeneo mengine watu wanaumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge ndiyo wawakilishi wa wananchi, tunatakiwa tuwatetee wananchi, tusipowatetea humu ndani hakuna kwa kuwatetea kwingine. Naomba sana tuungane katika hili, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu aje atusaidie hili. Wananchi hawa ni wa kwetu sisi wote, ndiyo kazi yetu kuwawakilisha ndani ya Bunge, siyo

kila kitu tunakiunga mkono hapana! Katika hili Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuomba sana, binafsi kwa niaba ya wananchi nikuombe sana usaidie jambo hili waweze kuliruhusu.

## TAARIFA

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa msemaji anayezungumza, kwamba hata katika kutunga sheria yoyote katika nchi yoyote, ni marufuku kutunga sheria kuhusiana na mambo ambayo yamefanyika nyuma. Kwa hiyo, watu ambao huko nyuma walikuwa tayari na uhalali wa kufanya biashara ya viroba, haiwezekani kwa baadaye mkaweka sheria au matamko kwa ajili ya kudhibiti vitu ambavyo vimefanyika nyuma, huo ni uonevu. Kwa hiyo, nampa taarifa kwamba ni mambo mazuri anayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea taarifa hiyo na kuna watu wamelipa kodi katika jambo hilo.

**MWENYEKITI:** Taarifa umeipokea na muda wako umekwisha kaa.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Kicheko)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARTHA J.UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu kwa hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuthamini shughuli ndogo ndogo za wananchi katika kuzalisha mali, lakini naomba kutoa masikitiko yangu kuhusu wajasiriamali

wadogo wanaonyweshea mbogamboga kutumia maji machafu yanayotiririka kwenye mifereji, Jijini Dar es Salaam. Mboga hizi huuzwa kwenye mahoteli mbalimbali jijini humo na kusababisha madhara kiafya pia inasababisha kinyaa kwa walaji. Kero hii inajulikana na watu wengi wakiwepo viongozi wanaoweza kufanya uamuzi kupiga marufuku kutumia maji hayo. Vinginevyo Serikali ishughulikie kusafisha mifereji yote michafu ili maji yanayotiririka humo yawe salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Sekta ya Kilimo, kuna athari kubwa sana ya uharibifu wa mazingira kwa mfano robo tatu ya ardhi ya Wilaya ya Kiteto imelimwa, (kuacha mapori yasiyofaa kwa kilimo na ufugaji) kwa sababu hiyo miti yote katika maeneo hayo yamekatwa na ardhi kubakia tupu (bila miti). Nini mikakati ya Serikali katika kunusuru Wilaya hiyo (ardhi yake) kugeuka kuwa jangwa? Tuliambiwa ardhi hiyo imepimwa miaka mitatu iliyopita, lakini hadi leo wakulima wakubwa wanaendelea kulima na ardhi inaendelea kuwa finyu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Sekta hii; sehemu kubwa asilimia 80 inategemea fedha za nje, hali inayohatarisha kutekelezeka kwa miradi ya mazingira kwa sababu fedha za nje mara kwa mara haziletwi kwa wakati. Naomba kujua Serikali inasemaje kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa Mungu kwa kuniwezesha kunipatia muda huu wa kuchangia ndani ya Bunge lako Tukufu angalau kwa maandishi. Nipende kumpatia hongera sana Mheshimiwa January Makamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa kazi nzuri anayoifanya, pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira na hasa matumizi ya mkaa. Nchi nzima wananchi karibu asilimia

80 wanatumia mkaa na kuni kama chanzo cha nishati. Pamoja na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na ujenzi Serikali ni vyema isimamie kikamilifu kuhusu uharibifu wa mazingira haya la sivyo nchi itakuwa jangwa. Mheshimiwa Waziri ni vizuri atoe tamko na kukumbusha tena wananchi na viongozi husika, kuhusu kusimamia Sheria ya Mazingira. Ni ukweli miti inapandwa, ambayo, miche 1.5 milioni kila halmashauri inapandwa, tatizo ufuatiliaji wa kuona ni mingapi inaendelea kukua kila mwaka baada ya kupanda ni tatizo, ingekuwa vizuri ufuatiliaji wa miche inapoendelea kukua ukajulikana badala ya kujali kufahamu takwimu za upandaji tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mkaa ni vizuri likaangaliwa kwa undani, ni nini kifanyike kunusuru uharibifu unaojitokeza, ukataji miti kwa kibali uendelee kusimamiwa kwa muda wote na viongozi husika. Elimu kwa wananchi izidi kutolewa kuhusu utunzaji wa mazingira. Bado uharibifu wa vyanzo vya maji unaendelea licha ya mikakati yote ya Serikali ya kukabiliana na tatizo hili, ni vyema Sheria ya Mazingira ifuatwe na kusimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa vyanzo vya maji unasababisha uhaba wa maji, mabadiliko ya tabia nchi, upungufu wa rutuba ya ardhi na matatizo mengi zaidi ya uharibifu wa ardhi. Uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira kuhusu milima ya Uluguru Mkoani Morogoro, wataalam wa *SUA* wamejitahidi katika mapando ya kuhifadhi milima hiyo lakini tatizo bado lipo pale pale. Kilimo kisichokuwa na tija na ujenzi wa nyumba kama makazi ya wananchi vinaendelea katika milima hiyo, vyanzo vya maji vimekauka kiasi wananchi wa Morogoro Manispaa hawapati maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Serikali yangu sikivu, iweke mkakati maalum wa kunusuru milima hii ya Uluguru ili hali yake ya uoto, kijani na utiririshaji wa maji (mito) irudie kama ilivyokuwa miaka ya 80. Serikali kuu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa naamini inawezekana kurudisha hali ya milima ya Uluguru ilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uharibifu wa mazingira unaotokana na uchimbaji wa madini na mchanga. Nashauri sheria ndogo katika Halmashauri husika na Sheria ya Mazingira zisimamiwe na kufuatwa, wananchi waendelee kupewa elimu tosha kuhusu utunzaji wa mazingira, wananchi wa pande zote za nchi Bara na Visiwani (Tanzania) wapewe elimu ya faida za mazingira ili kudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya mazingira kampeni ya utunzaji wa mazingira; iwepo kampeni ya utunzaji wa mazingira kwa wananchi wote kuanzia mashuleni, Vyuoni, Vitongoji, Kata, Vijiji, Wilaya, Mikoa na Taifa. Mkakati uwekwe wazi ili kila mwananchi ajue faida za utunzaji wa mazingira na hasara za kinyume chake mfano mito kukauka, ukosefu wa mvua na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampeni ya upandaji miti; iwekwe au iandaliwe kampeni ya upandaji miti kwa kila kaya na kuhakikisha inakua kampeni/zoezi endelevu, mfano kila kaya ipande miti 10 kila mwaka na kuhakikisha inakua. Halmashauri zihakikishe zinaandaa vitalu vya miche kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampeni ya kuzuia ukataji wa miti na uchomaji moto; kampeni hii iwe ni ya kuhakikisha miti inalindwa na wananchi wenyewe, kampeni kama "Panda Miti Kata Mti", wavunaji halali wa miti. Halmashauri zote ziwe na Sheria ndogo za kudhibiti uchomaji moto wa misitu/mapori, hii italinda misitu yetu na miti hivyo kuokoa vyanzo vya maji. Wenzetu Burundi ni kosa kubwa kuchoma moto au kukata miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Serikali ishughulikie nishati mbadala ya mkaa ili kupunguza matumizi ya mkaa na hiyo kuokoa miti na misitu kuteketea mfano, Watanzania wanufaike na gesi ya Mtwara kutumika majumbani kwa

gharama nafuu *Affordable cost,* haiingii akilini mtungi wa gesi kuuzwa kwa Shilingi 55,000- 60,000 kule Kakonko (Kigoma), wakati gesi ipo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya wakimbizi kwenye mazingira, Mkoa wa Kigoma una wakimbizi wapatao laki tano kwa sasa toka Burundi na DRC wakimbizi hawa wanatumia kuni kupikia hivyo wanakata miti kila siku. Hivyo miti 500,000 inatumika kama kuni kwa siku kwa mwaka ni miti 182,500,000 kiasi ambacho hakina *replacement* yake kwani haipandwi miti mingine. Mapendekezo; *UNHCR* wahakikishe wakimbizi wanapikia gesi ili kuokoa uharibifu wa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viroba vilivyokamatwa vilitozwa kodi na ilikuwa biashara halali, hivyo wamiliki waruhusiwe kuuza ili kulinda mitaji yao. Serikali ingezuia uzalishaji ikatoa muda wa kuvimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za Muungano zielezwe wazi kwa wananchi wote na wananchi waelezwe kama kweli wanaridhika na jinsi Muungano unavyokwenda. Ni muda muafaka sasa wananchi waulizwe kama wanataka Muungano au la ili isionekane Serikali inawaburuza wananchi au kuwa lazimisha kuwa kwenye Muungano. Magari yaliyosajiliwa ZNZ kwa nini yakiwa bara yanatozwa ushuru tena kwa vile yanatoka nchi nyingine wakati ni nchi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM Zanzibar ikae na *CUF* ili kuleta muafaka juu ya maridhiano. Haileti afya ya kitaifa kuendelea kuishi kibabe hasa CCM wanapojinadi kuwa hawako tayari kukaa na *CUF* kutafuta muafaka au suluhu, duniani kote wagombanao ndio wapatanao.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uongozi kwenye Wizara za Muungano; pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kujaribu kutatua kero za Muungano lakini bado kumeibuka kero nyingine ya kuwabagua Wazanzibari kwenye nafasi za uongozi ndani ya Wizara za Muungano. Sasa hivi zipo Wizara za Muungano kama vile

ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Fedha zote zinaongozwa na upande mmoja wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji mashirika ya Muungano; kero nyingine ya Muungano inatokana na Mashirika yanayowekeza Tanzania yanafanya uwekezaji wake Tanzania Bara pekee. Natolea mfano wa Shirika la *AICC* ambalo limefanya uwekezaji mkubwa Tanzania Bara na bado katika mipango yake ya baadaye haijaonyesha nia ya kufanya uwekezaji upande wa Zanzibar. Ikumbukwe kwamba mbali na pato la Serikali linalotokana na uwekezaji wa mashirika pia umekua ukitoa ajira na kunyanyua uchumi wa wananchi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za wafanyabiashara wa Zanzibar; ni muda mrefu sasa wafanyabiashara kutoka Zanzibar wamekuwa wakilalamika *TRA* kuendelea na tabia yao ya kuwatoza wafanyabiashara wa Zanzibar kodi mara mbili pale wanapotoa bidhaa zao kutoka Zanzibar kuingia Tanzania bara. Tabia hii ni sawa na kupunguza harakati za wafanyabaiashara wa Zanzibar kuingiza bidhaa zao Tanzania bara na kudhoofisha uchumi wa Wazanzibari. Naomba Wizara husika ifanye ufumbuzi wa haraka wa suala hili kwa faida ya pande zote za Muungano. Naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Utunzaji wa mazingira ni muhimu sana katika kuleta maendeleo, kuleta hewa safi, kuongeza mvua na kadhalika. Sisi wote ni mashahidi katika nchi yetu, kumekuwepo na ukame wa kupitiliza kiasi hata mazao hayawezi kulimwa, vyanzo vya maji vinakauka na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, Serikali kwa kupitia kila Kitongoji na Kijiji zile Kamati za Mazingira ziimarishwe, ziwezeshwe kama ilivyokuwa miaka 30 iliyopita. Ilikuwa ni lazima kupanda miti kila shule kuwa na vitalu vya miche, mfano Kilimanjaro ilikuwa hairuhusiwi kulima au kujenga kandokando mwa mto na mifereji iliyokuwa inatiririka maji na mito lakini sasa hivi yote imekauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuyeyuka kwa theluji ya mlima Kilimanjaro, miaka ya hivi karibuni Profesa L. Thomson kutoka *University* ya *Ohio* kule Marekani walikuja kufanya utafiti ni kwa nini theluji inapungua kwenye mlima Kilimanjaro, walibeba barafu nyingi sana *(in tons)* kuzipeleka Marekani. Je, Serikali mmefuatilia walibaini ni kwa nini theluji inapungua katika mlima Kilimanjaro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukisubiri sababu ni vizuri kuhimiza miti kupandwa kwa wingi ili wananchi waweze kupata maji na mvua, kwa sasa hivi Mji wa Moshi ndio wenye joto kubwa kuliko popote hapa nchini na Moshi ipo chini ya Mlima Kilimanjaro hii ni hali ya hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa, ni vizuri Wizara hii na Wizara ya Nishati na Madini waangalie ni jinsi gani wanaweza kushusha bei ya gesi ya kupikia ili kila mwananchi aweze kununua gesi ya kupikia. Hii itasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira, miti haitakatwa kwa sababu ya mkaa.

**MHE. WAITARA M. MWIKWABE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maoni yangu katika suala la mazingira. Ni muhimu Wizara ya Mazingira na Muungano ibainishe na kutambua maeneo ambayo watu wamejenga katika kingo za mito na mabonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maeneo hayo yatambuliwe na kuagiza wahusika wote wahame kwa mujibu wa Sheria na hili lisimamiwe wakati wote sio wakati wa mvua tu na kila mtu ajue kwamba maeneo hayo hayajengwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sheria itekelezwe wakati wowote na Viongozi wa Serikali ambao watahusika kuuza au kushawishi watu kujenga au kuwaandikia vibali ili waishi kwenye kingo na mabondeni washughulikiwe kisheria ili kuondoa malalamiko na usumbufu wakati wa mvua.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iweke utaratibu wa kushirikiana na halmashauri kwa ajili ya miradi ya utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kuweka miradi ya kilimo au vinginevyo kwa ajili ya vijana kwenye umbali unaokaribia mita 60 za hifadhi za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya kadhaa ikiwemo Biharamulo zina maeneo makubwa ambayo ni hifadhi za Taifa. Mfano 54% ya eneo la Wilaya ya Biharamulo ni hifadhi za Taifa, kwa sababu hiyo wananchi wanalazimika kutunza hifadhi na mazingira kwa kuwa *population density* ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya Wizara hii kubaini wilaya zote za aina hii na kukaa nazo na kubuni suluhisho la pamoja kwa maana ya kupata rasilimali fedha pamoja na utashi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongelea vijana kupewa miradi kwenye maeneo karibu na mita 60 za hifadhi ya vyanzo vya maji, lengo ni kuwatumia vijana, wawe walinzi wa vyanzo vya maji wakati wakitekeleza miradi yao katika maeneo jirani na vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ushahidi kuwa asilimia kubwa ya mkaa unaotengenezwa hapa nchini unatumika katika Jiji la Dar es Salaam na Majiji mengine. Je, Serikali haioni haja ya kuweka tozo kwenye kila gunia la mkaa unaoingia Jiji la Dar es Salaam kutumia tozo hiyo kutoa ruzuku kwa matumizi ya gesi ili wananchi wanunue mitungi ya gesi kwa bei ya chini.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Bila mazingira nchi hii tunakwenda kuangamiza vizazi vyote katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iongeze fedha za mazingira katika bajeti. Bajeti ya mazingira kila mwaka haieleweki ingawa suala la mazingira ni mtambuka.

Hivyo ni wakati sasa umefika wa kutilia mkazo suala la mazingira ili kuwepo na watumishi na Idara ya Mazingira. Ni ukweli usiopingika kwamba mazingira yanaharibiwa ngazi ya mitaa na vijiji, mijini na vijijini. Hivyo mkiimarisha Idara hiyo kwa kutengewa fedha za kutosha mtanusuru na kulinda mazingira.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi ambayo yamebadili majira ya mwaka kwa kuyachelewesha au kuyawahisha na madhara yanayotokea kutokana na mabadiliko hayo mara nyingi yanakuwa ni kuharibika kwa miundombinu na pia watu kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali iwekeze katika sekta za kuzuia na kupambana na mabadiliko ya tabia nchi. Mfano kusimamia sheria za utunzaji wa mazingira kama vile upandaji miti, kuzuia watu wanaokata miti ovyo na wanaochoma ovyo misitu na kusababisha ongezeko la ukaa. Wachukuliwe hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji na matumizi ya mifuko ya plastiki. Kwa kuwa vifungashio vya plastiki vinachafua mazingira, basi naishauri Serikali ione utaratibu wa kufanya *recycling* ili isiathiri mazingira na isiathiri wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati mbadala; ili kupunguza au kuondoa kabisa uharibifu wa mazingira kupitia ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa, basi Serikali waje na mkakati wa kutafuta wawekezaji wajenge kiwanda cha kuchakata gesi hapa Tanzania na kuiweka kwenye mitungi na kuisambaza nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takataka; Miji yetu inazalisha taka nyingi zikiwemo taka ngumu na taka za maji. Hakuna mfumo rasmi unaotumika ili kuhakikisha taka mbalimbali zinakusanywa ipasavyo. Naishauri Serikali kuweka mfumo rasmi wa kutupa taka hizo. Naomba kuwasilisha.

**MHE. SABREEN H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kumekuwa na kero kubwa kuhusu ushuru wa vifaa vinavyopita bandarini hapa Dar es Salaam na bandari ya Zanzibar hali inayopelekea uwepo wa bandari bubu hasa Ukanda wa Pwani. Je, ni lini Serikali itaondoa hizi kodi za kero kwa wasafiri wa kawaida kabisa ambao si wafanyabiashara wanaotumia bandari hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kero ya mifereji mikubwa hasa maeneo ya mijini kujaa taka hususan wakati wa mvua hali ambayo inahatarisha maisha ya Watanzania. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia taka hizi ili zisilete magonjwa ya milipuko hasa maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na kero kubwa ya ukosefu wa maji hasa maeneo ya mwambao wa Ziwa Tanganyika kwa mfano uwepo wa Kambi kama Bulombola na maeneo mengine Mkoani Kigoma. Ukosefu wa maji kwenye kambi hizo unapelekea uchafuzi wa maji kwa kuwa vijana wengi kwenye kambi hizo wanategemea Ziwa Tanganyika kwa shughuli za kuoga, kufua na kujisafisha. Je, ni lini Serikali itazuia uchafuzi huu wa mazingira.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujikita katika mchango wangu moja kwa moja katika suala la mazingira. Mazingira yaliyoimarika ni suala muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu na dunia kwa ujumla na ndiyo maana leo kila pembe ya dunia kama siyo nchi huunda vikundi ama asasi mbalimbali kwa ajili ya kutoa elimu ya mazingira. Sasa basi nikija katika nchi yetu uharibifu wa mazingira unazidi kuwa mkubwa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote ni kwa sababu, kwanza, elimu ya mazingira kwa wananchi ni duni mno haiwafikii wananchi kwa ukamilifu unaotakiwa. Nitolee mfano Wilaya ya Kondoa na Chemba ambapo kule napo uharibifu ni mkubwa kutokana na ukosefu wa elimu watu

wanakata miti ovyo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kuni, mkaa na hata maandalizi ya mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo linasababisha uhaba wa mvua na ukosefu wa maji tena kwa kiasi kikubwa mno, lakini mpaka leo hii watu walio wengi wa Kondoa na Chemba hawaelewi ni kwa nini wanakosa maji. Wenyewe wanasema ni "wenye ardhi ndiyo hawataki na maji yao." Sasa ukiwauliza hao wenye ardhi ni akina nani na wako wapi wanakujibu, hata wao wanasikia tu kuna wenye ardhi. Unaweza kuona ni kwa kiasi gani elimu inahitajika katika maeneo mengi ili kunusuru mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linalochangia uharibifu wa mazingira ni pamoja na kukosa nishati mbalimbali katika kupika hasa ukizingatia familia nyingi katika nchi yetu bado uwezo wao ni wa kutumia kuni na mkaa hivyo mazingira yetu bado yataendelea kuharibiwa sana kama bado elimu na nishati mbadala havitatolewa kwa makini na ukamilifu. Tunasikia kuna mkaa wa mabaki ya vyakula lakini bado elimu hiyo wananchi hawawezi kabisa na hata vifaa vya kutengeneza mkaa huo pia havipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, Wizara hii badala ya kujikita kwenye kutembelea mazingira na kutoa miti ya kupanda ni vyema ingejikita katika kutafuta elimu itakayosambazwa katika shule za msingi na sekondari ambako huko watatoa elimu juu ya nishati mbadala, kupeleka vifaa, kufundisha masuala ya majiko banifu ambayo majiko hayo hupatikana mjini tu. Hivyo wakipatikana walimu hawa wa kufundisha juu ya utunzaji majiko banifu na utumiaji wa mikaa inayopatikana kutokana na mabaki ya vyakula tutapata faida mara mbili; kwanza, itaongeza ajira kwa vijana na tutakuwa tumepiga hatua katika utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho ni juu ya elimu sahihi kuhusu mazingira. Ufike wakati sasa elimu ya mazingira itolewe katika kuanzia ngazi ya Kaya hadi Taifa.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono na kuwapongeza sana Mawaziri wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya pamoja na kazi nzuri ya usimamiaji wa mazingira inayofanyika. Napenda Wizara itoe pia kipaumbele cha vijiji ambavyo vinazunguka vyanzo vya maji kuhakikisha vyanzo hivyo vinatunzwa na kulindwa vizuri na wananchi hao. Wananchi hao inabidi na wao wafaidike na vyanzo hivyo vya maji kwa mfano; maji ambayo yanatumika Mkoani Tanga yanatoka Mto Zigi Wilayani Muheza. Tarafa ya Amani wanavijiji wanaokaa maeneo hayo kama Amani, Zirai Misarai, Mbomole, Mashewa, kwendimu na kadhalika maji wanayotumia yanatiririka bila kuwekwa vizuri. Hawasaidiwi kuweka maji hayo kuwa safi na salama. Ni vizuri Wizara ikashirikiana na Wizara ya Maji ili wananchi hawa wasigeuke kuharibu mazingira ya vyanzo hivyo. Wapewe motisha na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na pigeni kazi na nashukuru Mheshimiwa Waziri kufika Mto Zigi.

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma wanakabiliana na changamoto nyingi katika utunzaji wa mazingira hasa misitu, hivyo kunahitajika jitihada za makusudi ili kukabiliana nazo. Kwa mfano, Wilaya ya Tunduru haipaswi kuwa maskini kutokana na utajiri wa misitu iliyonayo. Hata hivyo, mojawapo ya kero ni pamoja na mifugo kuvamia katika misitu, hivyo kuhatarisha uendelevu wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wilaya hii ina misitu ya Miombo inayokadiriwa kuwa na ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 150,000, hivyo ni dhahiri kuwa uendelezaji wa misitu hii inahitaji uzalishaji mkubwa wa wananchi ili kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ipo haja ya Serikali kuhakikisha kuwa shughuli za kiuchumi hasa uanzishwaji na uendeshaji wa viwanda unafanyika kwa umakini mkubwa.

Je, mpaka sasa ni viwanda vingapi vimepewa adhabu/faini kwa uchafuzi wa mazingira mpaka Machi mwaka huu na je, ni hatua gani madhubuti zinafanyika kuzuia uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ipo hoja ya kufanya tathimini ya kitaifa juu ya athari za mazingira hasa katika sekta ya uzalishaji wa viwanda na madini. Napenda kujua ni mkakati gani ambao Serikali imeweka ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira hasa katika miradi ya madini na kuangalia jinsi ambavyo migodi hiyo inakidhi matakwa ya kisheria juu ya utumiaji na usimamimzi wa mazingira migodini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utiririshaji wa maji taka nje ya mfumo rasmi wa majitaka hasa kipindi cha mvua umeendelea kuhatarisha mazingira hasa afya za watumiaji wa miundombinu katika miji. Ni dhahiri kuwa, pamoja na kuwa na changamoto za kimazingira na miundombinu, pia ipo haja ya kufanya tathmini ya mfumo kwa utiririshaji majitaka na athari zake kwa mazingira ikiwemo binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya. Mazingira ni jambo muhimu sana katika maisha ya binadamu. Naiomba Serikali itilie mkazo sana katika suala zima la uhifadhi wa mazingira pamoja na juhudi za Serikali katika kuongeza kasi ya upandaji wa miti, lakini bado kuna mambo mengi sana yanayosababisha uharibifu wa mazingira nayo yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wakae pamoja na taasisi nyingine katika kuweka sawa sheria ya mazingira kwa kuwa wananchi wengi wanapotafuta vibali mbalimbali vya ujenzi kunakuwa na vikwazo vingi sana. Mambo yanayowekwa kwa Mtanzania wa kawaida inakuwa vigumu kuyatekeleza kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze Serikali kwa kufuatilia kwa kina kuangalia viwanda ambavyo vinakiuka taratibu za mazingira. Hiyo imesaidia sana Temeke kutokana na matatizo ya Serengeti *Breweries.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARGARETH S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira; pongezi sana kwa kazi nzuri inayofanyika. Ombi, naomba kwa heshima Mto Ugalla ulioko Usoke, Urambo usaidiwe kuondoa magugu yanayokausha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. JUMA ALI JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi wa Ibara ya 48 ya kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(Global Environment);* je, sifa zipi zinazotakiwa kwa vikundi vya kijamii vinavyotarajiwa kuandika miradi midogo midogo ili viweze kunufaika na ufadhili wa *G.E.F* katika mwaka wa fedha. Je, katika vikundi 53 vya kijamii vilivyoshauriwa na Ofisi ya Makamu wa Rais ni vikundi vingapi kutoka Zanzibar vilifaidika na ushauri huo.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote mwananchi wa Temeke hasa wakazi wa chang'ombe na Keko wanamshukuru Mheshimiwa Mpina kwa ziara zake zilizotokana na kero ya muda mrefu katika eneo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo bado nguvu kubwa ya kukomesha wachafuzi wa mazingira inahitajika. Bado baadhi ya viwanda vinatiririsha maji machafu kwenda mitaani na baharini. Tafadhali Mheshimiwa Mpina usichoke kuja Temeke ili tuzitatue kero hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda Mheshimiwa Waziri ashauriane na Waziri wa TAMISEMI ili watoe maelekezo kwa Halmashauri kuwa Kamati ya kutoa vibali vya ujenzi imjumlishe na Afisa Mazingira wa Halmashauri badala ya Mganga Mkuu. Hii itasaidia kuhakikisha hakuna kibali cha ujenzi kitakachotolewa bila tathmini ya mazingira. Kwa sasa hali hii ni mbaya na vibali hutolewa hata katika maeneo oevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa hotuba nzuri yenye kuonesha mwelekeo wa kujali maslahi ya nchi. Katika hotuba hii nitachangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Mazingira, hali ya uharibifu wa mazingira kwa sasa nchini mwetu imekuwa mbaya sana. Jamii kwa ujumla suala la mazingira imelipa mgongo, maeneo ya vyanzo vya maji shughuli za kilimo ndiyo mahali pake. Ushauri wangu shughuli za mifugo na kilimo zisiendeshwe katika maeneo hayo ili kulinda vyanzo vya maji. Pia hata shughuli za makazi kwa maana ya ujenzi wa nyumba pia upigwe marufuku, Sera na Sheria zilizopo ni nzuri, tatizo ni usimamizi wa wenye dhamana ya kusimamia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia maeneo ambayo yameathirika kwa kiasi kikubwa na uhifadhi wa mazingira kukosa rasilimali fedha kwa ajili ya kupanda miti. Napongeza uanzishwaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Mazingira, ni imani yangu maeneo ambayo yatakuwa yameathirika na mazingira yatapatiwa fedha kutoka Mfuko huo. Tusipokuwa makini vyanzo vyote vya maji vitakauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuenea kwa hali ya jangwa, maeneo mengi nchini yameshuhudia ukataji wa miti kwa matumizi ya mkaa, mbao pamoja na kuanzisha mashamba kwa shughuli za kilimo. Kasi ya ukataji wa miti imesababisha maeneo mengi kukosa mvua nchini, hali hii nchini

isipodhibitiwa nchi yetu itakuwa jangwa. Mfano mzuri katika Jimbo langu la Kilindi katika Kata za Negero, Msanja, Kilindi Asilia na Kimbe, zimeshuhudia kasi ya ukataji wa miti wa hovyo huku wahusika ambao ni Watumishi katika ngazi zote wakiacha hali hii kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa ya Wanazuoni wawili wa Chuo Kikuu cha *SUA* Morogoro, Profesa Dhahabu na Maliado, Wilaya ya Kilindi ni eneo ambalo limeathirika sana na ukataji hovyo wa miti. Taarifa yao ni ya mwaka 2003 hadi 2012 ilionyesha eneo la Kilindi lisipochukuliwa tahadhari Wilaya yake itakuwa jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sheria zilizopo na Watendaji katika maeneo ya Vijiji hadi Wilaya bado tatizo hili linaendelea. Nimwombe Waziri mwenye dhamana ahakikishe Timu Maalum inakwenda hasa kwenye maeneo ya Kata za Negero, Msanja, Kimbe na Kilindi Asilia na vijiji vyote kwenye maeneo ya kujionea uharibifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuchukua jitihada kubwa na kutenga fedha za kutosha kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi tutegemee athari kubwa zaidi. Bila msisitizo wa kusimamia sheria husika na kuwa na wataalam wa kutosha tatizo halitaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Baraza la Mazingira *(NEMC)*, Baraza hili sehemu kubwa ya shughuli zake zinafanyika mijini. Niliombe sasa Baraza litanue shughuli zake vijijini kwa kuhakikisha wanakuwa na watumishi wa kutosha. Naamini kwa dhati, shughuli nyingi za ukataji miti na shughuli za kibinadamu pamoja na ufugaji zinafanyika vijijini. Baraza lipewe uwezo mkubwa wa kisheria katika kusimamia na kuratibu misitu na kuhakikisha maeneo yetu yanalindwa. Aidha, Baraza liongezwe bajeti yao waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu suala zima la uteketezaji misitu na usababishaji wa mabadiliko ya tabianchi ambalo ndiyo tatizo sugu duniani na kwa Tanzania kupelekea kwa sasa mvua kukosekana. Naishauri Serikali kuanzisha njia mbadala ya mkaa tutapunguza ukataji miti, huko nyuma kulikuwa na mpango wa kupunguza ukataji wa mkaa kwa kuanzisha kilimo cha mibono inayotoa moto poa ambayo ingesaidia kuleta chanzo kipya cha moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi na kilimo kwenye vyanzo vya maji; elimu kwa wananchi ni ndogo kuhusu suala hilo. Niishauri Serikali yangu kuongeza juhudi ya kuelimisha wananchi, pia Serikali iangalie uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji mifugo mingi na hatari mijini; niishauri Serikali yangu kuhakikisha elimu kwa wafugaji mifugo inatolewa, upunguzaji mifugo ili kupunguza uharibifu wa mazingira kupitia mifugo mingi kuchungwa kwenye maeneo madogo. Mfano halisi ni ng'ombe wanaochungwa katika Mji wa Dodoma ambao ni Mji Mkuu wa nchi. Niishauri Serikali kuhakikisha inatoa elimu ya kutumia vinyesi vya ng'ombe hao kutengeneza gesi ili kupunguza ukataji miti kwa ajii ya Mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano; niishauri Serikali iendelee kuondoa kero za Muungano kadri zinavyozinduliwa. Niishauri Serikali kuhakikisha inajenga dhana za kujitegemea kwa kutenga fedha za ndani za kutosha kuliko kutegemea wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali iongeze fedha za bajeti kwa ajili ya kufanikisha utendaji wa Wizara hii ili kuleta afya kwa wananchi kwani haiwezi kufanya kazi zenye ufanisi bila kuwa na bajeti timilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na kunipa uwezo wa kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais kwa kazi nzuri sana ya kuendeleza uongozi bora katika nyetu. Ni mfano wa kuigwa katika uongozi wake kwa kuwa mfuatiliaji mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuonesha nia na njia ya kuboresha masuala ya mazingira kwa ujumla na pia kuonesha na kutekeleza vyema uboreshaji wa Muungano wetu, kuendelea kuboresha kwa kutatua changamoto za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri katika masuala mawili muhimu na yote yanalenga mazingira. Kwanza napongeza uzinduzi wa Mfuko wa Mazingira Kitaifa ulioanzishwa 2004, tumechelewa lakini tunasema unapoamka ndipo pamekucha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Mfuko huu tuangalie namna ya kupatia vyanzo vya kudumu ili uwe endelevu na malengo yake yatimie. Suala la athari za Mazingira linajulikana na hakuna hatua ya uhakika inachukuliwa, tunabaki kulalamika wote bila kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuhitaji Sheria mpya, zilizopo zinakidhi na pia urasimu wa kubadilisha Sheria na Kanuni zake itachukua muda. Tuhakikishe tunafuata sheria zilizopo, nashauri agizo litolewe na mmoja kati ya vigezo kwa kiongozi yoyote na mtumishi wa Serikali katika ufanisi wa kazi yake iwe masuala ya mazingira, tuzo itolewe kwa kila ngazi kwa taasisi na binafsi katika usimamizi wa mazingira na sheria zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuongelee na kuhakikisha kuwa Bunge lipitishe sheria ya kuweza kupata

vyanzo vya kudumu katika Mfuko wa Taifa wa Mazingira. Pia napendekeza kuondoa kodi katika uagizaji wa majiko yote yanayotumia gesi *(LPA)* au majiko banifu. Hii itafanya kushuka bei ya gesi na majiko yake na kupunguza uharibifu wa misitu kwa asilimia mbili au tatu. Pia tuhamasishe utumiaji wa nishati mbadala au jadilifu *(renewable energy)*. Kodi ipunguzwe katika uagizaji wa vifaa hivyo nje ya sola ambayo haina kodi kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri gharama za ukaguzi na leseni kibali cha *NEMC* ipunguzwe ili Watanzania wengi zaidi waweze kutafuta hivyo vibali badala ya kusubiri kupigwa faini ambayo wanaona ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vyanzo nashauri asilimia kumi ya tozo zote au leseni zinazotolewa na zinahusiana na masuala ya Mazingira. Mfano; leseni ya Viwanda vyote, leseni za Madini, Leseni za Ujenzi, Leseni za Utalii, Leseni za huduma za Afya Mawasiliano, Uvuvi, Mifugo, Kilimo na Leseni za uzalishaji wa Nishati. Pia tozo tunayopata kutokana na *(TFS* - Wakala wa Misitu Tanzania) ambayo ni uvunaji wa misitu yetu asilimia ishirini ya mapato hayo yarudi kuboresha mazingira. Leseni au vibali vya watumiaji maji asilimia kumi pia zirudi kuboresha vyanzo vya maji katika Mfuko wa Mazingira pia tuliweka kodi ya kuingiza magari na bidhaa chakavu huwa zinaharibu mazingira, asilimia ishirini ya mapato hayo yaende katika Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza shilingi kumi ya kila lita ya mafuta pia iende kwenye Mfuko wa Mazingira. Pia shughuli zote zinazofanyika ambazo zinaharibu mazingira, pawe na asilimia kumi ya tozo kwenye vyanzo hivyo vinavyopatikana ili mfuko uweze kuwa endelevu na mipango itimizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fedha za *EWURA*, pia asilimia kumi ziende kwenye kuboresha au kutunisha mfuko. *SUMATRA* pia katika leseni zote ichangie asilimia kumi ya mapato yake katika mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuleta hamasa *incentive* pawe na ruhusa kuweka angalau asilimia tatu au tano kama gharama *expenses* ambayo itatozwa kodi *(allowed expense)* katika *balance sheets (Income Tax Act)* na itafanya makampuni yachangie katika masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaoshughulika na utalii wapewe maeneo maalum ya kuboresha mazingira na hivyo hivyo viwanda, migodi na biashara zote zipewe maeneo maalum ya kusimamia na kuboresha mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi iondolewe katika mitambo ya kusafirisha na kurudisha bidhaa sokoni *recycling* na pia katika mitambo ya kufua umeme unaotokana na taka ngumu. Tuwe na tozo ya shilingi hamsini kwa kila mfuko wa mbolea ya dukani inayoagizwa kutoka nje ya nchi. Tunaweza kujadili na pakawa na Tume Maalum ya kuangalia vyanzo vya Mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali ifuatavyo:-

(i) Serikali itazame upya bei za gesi asilia kwani kwa sasa ni ghali ukilinganisha na maisha ya Mtanzania;

(ii) Serikali ifanye mapitio maeneo yenye makazi ya wananchi kwa wale wanaoishi karibu na vyanzo vya maji na maeneo ya miinuko katika nchi yetu. Mfano; wananchi hao wanaweza kufanya shughuli rafiki wa mazingira;

(iii) Serikali iangalie uwezekano wa kunusuru maeneo yenye uoto wa asili ili kuwa endelevu kwa kizazi kijacho;

(iv) Serikali itoe Waraka kwa *DC's (District Commissioner)* na *DED's (District Executive Director)* nchini kuhusu upandaji wa miti na mashindano ya Kaya kwa Kaya,

Kijiji kwa Kijiji, Kata kwa Kata na Wilaya kwa Wilaya na mwisho Kitaifa. Siku ya Mazingira ifanyike na kutoa zawadi;

(v) Taasisi mbalimbali ziwe na bustani za miche kama kitovu cha utoaji wa..

(vi) Tunaomba Serikali itusaidie kunusuru Maziwa madogo ya asili katika Mkoa wa Manyara; Ziwa Basutu katika Wilaya ya Hanang; Ziwa Tlawi katika Wilaya ya Mbulu; Ziwa Manyara katika Mkoa wa Arusha Wilaya ya Monduli na Ziwa Babati katika Wilaya ya Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. TWAHIR AWESU MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kunifanyia wepesi na fursa ya kupata nafasi ya kutoa mchango wangu huu kwa njia ya maandishi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri na kuamini suala la Muungano wetu ni la msingi na la umuhimu sana kwa faida ya washirika wa nchi zote mbili za Muungano wetu. Nakubali wananchi wa nchi zote mbili hawalalamikii kuwepo kwa Muungano, lawama zinakuja ni namna gani ifanyike kuuboresha na kuondoa malalamiko yaliyopo ikiwa ni pamoja na zinazoonekana kama ni kero kubwa kwa Muungano wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa vikao viwe vimekaliwa na watu wa pande zote mbili kukubaliana tatizo siyo vikao kukaliwa, tatizo kubwa hapa siyo kukaliwa kwa vikao tatizo ni kupatiwa ufumbuzi kero zile zilizolalamikiwa kutatuliwa lakini pia tatizo hapa ni kukaliwa vikao lakini wakimaliza vikao wahusika kukaa kimya wananchi wanaolalamika hawapewi taarifa za yale yaliyoamuliwa na kukubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF III)* una manufaa na faida kwa wananchi wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uendelezwe na uimarishwe. Nashauri ili makusudi yaliyoazimiwa yawafikie walengwa halisi na wale waliokusudiwa ni vyema mfuko ukabadilisha utaratibu wa kuifikia jamii inayohusika kwa kuwatumia viongozi wa kijamii wenyewe kuliko kuwatumia viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakiwemo Masheikh. Nashauri kwa nia njema kabisa viongozi wa mfuko wawatumie viongozi wa *NGO's* ili wananchi wayafaidi vyema matunda halisi ya mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii kutoa mchango wangu katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu ni muhimu sana na fahari ya kujivunia kwa nchi yetu sababu una manufaa kwa pande zote mbili za Muungano wetu na Watanzania walio wengi hatujui nchi nyingine zaidi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba kutoa mchango wangu kama ushauri kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kama ifuatavyo:-

Utunzaji wa mazingira ni muhimu sana hasa mustakabali wa nchi yetu kwa kizazi cha sasa na cha baadaye ukizingatia na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu unaotokana na shughuli za binadamu katika vyanzo vya maji, misitu na mbuga zetu za wanyama ambazo ni urithi wetu na zawadi toka kwa Mwenyezi Mungu kama zawadi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa hilo la utunzaji wa mazingira na kutokana na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na mikakati ya kuvuna na kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi

ya binadamu, mifugo na kwa matumizi ya kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na kuondokana na kilimo cha kubahatisha na kutegemea mvua ambazo kwa sasa hazina uhakika kutokana na ukame unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa ushauri kwa Serikali kuwa; tuwekeze katika kujenga mabwawa zaidi ili kuvuna na kuhifadhi maji kwa ajili ya kutunza mazingira na kulinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mabwawa hayo ni bwawa la Kidunda ambalo andiko lake la kwanza lilikuwa mwaka 1955 kabla ya uhuru na la pili ni mwaka 1962 na la tatu ni mwaka 1994 ambalo lilibadilisha wazo la awali la matumizi ya bwawa kwa uzalishaji wa umeme, ufugaji wa samaki, kilimo cha umwagiliaji pamoja na uzalishaji wa maji safi na salama kwa Mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri Serikali kurudi kwenye mipango ya awali ya Mwalimu Nyerere ya kujenga bwawa kwa ajili ya matumizi yote kwa ajili ya kukabiliana na uzalishaji wenye tija katika kilimo na kuwa na uhakika wa chakula na malighafi ya kiwanda ukizingatia kuna shamba kubwa la miwa na kiwanda cha sukari kinachojengwa kule Mkulazi ambao nao watahitaji maji kutoka katika bwawa hilo. Katika hili tutapata changamoto lakini tutangulize maslahi mapana ya Tanzania kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRARD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kuhusu uharibifu wa mazingira. Binadamu wanaharibu sana mazingira kutokana na kilimo cha mabondeni. Nashauri, Serikali iendeleze kilimo cha umwagiliaji ili kuepusha kilimo cha mabondeni

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji mbovu wa mifugo kwa mfano ng'ombe. Ushauri wangu ni kwamba, wafugaji

waelimishwe ili kufuga ng'ombe wachache kuepusha uharibifu wa mazingira na kusababisha mito kukauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *carbon trade,* naomba Serikali kuhamasisha wananchi kupanda miti kwa wingi katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kulinda mazingira pia ni biashara ya hewa ukaa ambayo itasaidia sana kuinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu, wananchi wapewe elimu ya kutosha kuhusiana na utunzaji wa mazingira, kwa mfano waepuke ukataji miti ovyo, kuchoma mkaa na ukataji wa kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Mazingira na Muungano pamoja na timu kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuishauri Serikali yangu Tukufu kuhusu suala la mazingira. Kumekuwa na mabadiliko ya tabianchi kutokana na uharibifu wa mazingira hasa kwa wananchi ambao hawajui suala zima la utunzaji wa mazingira. Niishauri Serikali yangu Tukufu ije na mkakati wa kupanda miti, hasa yale maeneo ambayo misitu imechomwa moto pamoja na vyombo vyote vya maji vipandwe miti na viwe na usimamizi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwe na sheria maalum ya kupanda miti katika kila kaya, kijiji hadi kata na kuanzia Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji wapewe sheria hizo ili wazisimamie kikamilifu. Naamini tukifanya hivyo tutakuwa tumeboresha nchi yetu kwa kurudisha uoto wa asili uliokuwepo hapo zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo wananchi wapewe miche ya miti bure. Kwa hiyo, Serikali itenge mafungu kwa ajili ya kununua miti na kuwapa wananchi. Kwa mfano, katika jimbo langu la Lushoto

wananchi wangu wapo tayari kupanda miti kwa wingi, shida ni uwezeshaji wa miche.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Ofisi ya Makamu wa Rais ipatiwe bajeti yake yote ili iweze kutimiza kazi zake kiukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchaguzi Zanzibar, Serikali ya Muungano haitaki kuiacha Zanzibar huru ifanye kazi zake kwa matakwa yake bali Tanganyika inaingilia chaguzi na hata maamuzi ya Wazanzibari hapa na pale. Inaendelea kuikandamiza *CUF* katika utendaji kazi za kisiasa na kero za Zanzibar bado mpaka sasa zinasuasua na sina hakika kama ziko tisa .

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa raia toka uchaguzi wa mwaka 2015 Zanzibar haiku shwari kwani ule umoja wa Wazanzibar kwa sasa haupo baada ya kuwa na makundi mawili mahasimu wa kisiasa yaani CCM na *CUF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi na wananchi waliumizwa katika marudio ya upande mmoja wa CCM na kuweka ari ya sintofahamu kwa raia baada ya Jeshi la Polisi na JKU kutanda mitaani na kutishia raia. Huu si utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katiba mpya; ni wazi tumepoteza pesa nyingi sana kwa kuanzisha mchakato huu kwani matakwa ya wananchi hasa ilipotokea kuachwa kwa rasimu ya katiba ya Mheshimiwa Warioba ambayo CCM iliacha na kutengeneza rasimu isiyokuwa na matakwa ya wananchi. Naomba tuanzie pale wananchi walipotaka kwenye katiba ya Warioba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi za kusingiziwa; kumekuwa na mashtaka ya kubambikiwa kesi katika Serikali

ya Muungano hasa kwa wafuasi wa *CUF*. Tunaomba Wizara hii ichukue nafasi yake ya upatanishi na kusimamia haki.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naipongeza sana Ofisi ya Makamu wa Rais, Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Kizuka kimeanzisha mradi wa kutunza mazingira kwa kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kuweka mradi wa maji. Tungeomba kufahamu Ofisi ya Makamu ya Rais inatusaidiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vikundi vingi vya hifadhi ya mazingira vikiwa na miradi ya upandaji miti na ufugaji wa nyuki. Tunaomba msaada wa ushauri na teknolojia rahisi katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuokoa mazingira akinamama wameanzisha mpango wa majiko yenye utunzaji wa mazingira, tunaomba usimamizi wa kuwasaidia akinamama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARAK S. BAWAZIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *NEMC* wanachelewesha sana utoaji wa taarifa na kuruhusu ujenzi uendelee, Tanzania ya Viwanda haitaweza kupatikana kwa uratatibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za vibali kwa mtu anayetaka kujenga kituo cha mafuta ni kubwa sana na hapo hapo mteja anatakiwa amchukue mtaalam kwa gharama zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya *Plastic* kama vinafungwa vifungwe na kama wanatoa muda watoe kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusimamisha uletaji wa mkaa mjini wakati utaratibu wa matumizi ya gesi kwa kupikia hayajakaa vizuri. Elimu itolewe kwa wananchi madhara ya ukataji wa miti na watumie nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza hotuba ya Kambi ya Upinzani ya pamoja na Serikali kufanya warsha, makongamano na mjadala mbalimbali ya kushughulikia kero za Muungano lakini kwa kuwa Muungano unahusu binadamu (watu) lazima kero zitaendelea kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika moja ya kero ya Muungano ni kitendo cha kupeleka Wanajeshi, Polisi, Mgambo, pamoja na silaha nzito na nyepesi wakati wa uchaguzi, hili jambo ni kero kwa wale wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waishio Zanzibar, nahoji je, hata Visiwa vilivyopo katika Ziwa Victoria navyo vinapelekewa vikosi na silaha kama Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri hadi kufikia hapo, wanaona ni kero na vitisho. Naishauri Serikali iache kupeleka vikosi na silaha toka Bara na kupeleka Zanzibar ili kuifanya demokrasia ya Tanzania ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zinazoingia Zanzibar, zote zinalipwa kodi lakini cha kushangaza mwananchi yoyote akinunua hizo bidhaa na kuja nazo Tanzania Bara anatakiwa alipe upya ushuru wa forodha kupitia *TRA*. Naishauri Serikali kulipia mara mbili ushuru ni udidimizaji ushuru, bidhaa zinazoingia Bara zisilipishwe forodha mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yanazingatia uwanda mpana na pia baadhi ya watu hawafahamu mazingira ni nini? mfano katika Jiji langu la Tanga yapo mambo mengi ya utunzaji wa mazingira mfano, *open space* (Viwanja vya wazi, viwanja vya michezo, Bustani za

kupumzikia lakini mengi ya hayo maeneo yanasimamiwa na Halmashauri zetu, lakini sasa yameporwa na itikadi za vyama vya siasa. Naishauri Serikali ifute usia wa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamini William Mkapa kuwa viwanja vyote vya michezo , viwanja vya wazi na bustani zimilikiwe na Halmashauri (TAMISEMI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Mipango Miji maeneo mengi katika Halmashauri zetu wanashindwa kupanga miji yetu, wanamilikisha viwanja vya wazi, michezo na bustani kwa kupima viwanja na kuwauzia kwa uroho wa kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali Afisa Mipango Miji/Ardhi atakayefanya umilikishaji ardhi hovyo awajibishwe mara moja.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja. Napenda kutoa mchango wangu kwa kuishauri Wizara hii kusimamia fedha wanazochangia wananchi wakulima wa tumbaku kupitia tozo kwenye mauzo yao namna zinavyotumika kwenye kuhifadhi Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wabunge wajue tozo ni kiasi gani zimekusanywa na kiasi hicho kimerejeshwa kwenye maeneo yaliyoathirika na uharibifu wa mazingira; kwani kuna uwezekano zikatengenezwa taarifa za fedha zilizotumika ambazo siyo sahihi kwani wananchi binafsi wanajihusisha kuhifadhi mazingira. Isije ikatokea kuwa na utaratibu hafifu fedha za tozo kwenye tumbaku zikatumika na wajanja na wakasingizia zimetumika kwa kubadilisha na juhudi binafsi za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. MOSHI J. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nawapongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Makamba kwa juhudi kubwa wanayoifanya

hasa katika ziara zinazofanyika katika nchi yetu wakihamasisha suala la hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri alipokuja Mpanda na kutoa amri ya kuondoa mabanio ya Mto Katuma ambao ulikuwa unakaribia kutoweka. Ombi langu tunaomba Ofisi yako itoe fedha kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wanaotunza Mto wa Katuma wasaidiwe fedha za kuchimba mabwawa na malambo yatakayosaidia kuacha uharibifu wa mto huo ambao ni muhimu kwa ajili ya Hifadhi ya Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni hifadhi za misitu, ni vema suala la kuhifadhi misitu iliyopo Mpanda wasiachiwe watu wa maliasili pekee kwani suala hili ni muhimu sana katika kuhifadhi misitu ambayo inafyekwa kwa shughuli za kilimo, ufugaji na nishati ya kuni. Niiombe Serikali iangalie suala hili kwa uzito mkubwa kwani shughuli hizi za binadamu zinatumia sana misitu na kutengeneza uharibifu wa mazingira. Ushauri wangu ni;

(i) Serikali isimamie suala la kilimo cha kuhamahama;

(ii) Wafugaji wafuge ufugaji wa kisasa ili tupunguze wingi wa mifugo; na

(iii) Serikali iandae mpango wa kuwawezesha Watanzania wapate gesi kwa bei nafuu ili waachane na suala la kutegemea kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa; Ziwa Tanganyika linaendelea kupungua siku hadi siku. Kama Serikali haitachukua hatua stahiki ziwa hili litapungua sana siku hadi siku. Serikali ichukue hatua ya kuweka banio nchini *DRC* Kongo, bila kufanya hivyo Ziwa Tanganyika litatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika limejaa tope, Wizara nendeni na mpeleke wataalam waangalie uwezekano wa kutoa tope na kulifanya Ziwa hilo liwe hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Waziri na timu yake kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazingira ni Mtambuka, suala la mazingira ni muhimu sana katika utunzaji na faida zake, vilevile umuhimu katika maisha ya wanadamu. Wizara takribani nne zinaingiliana katika utunzaji na usimamizi wa mazingira; TAMISEMI, Maliasili na Utalii, Ardhi, Maji na Mazingira. Hivyo basi, usimamizi katika maeneo mengi umekuwa hafifu kutokana na fedha, rasilimali watu, vitendea kazi pia Wizara kukosa wawakilishi katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, naiomba Serikali ifanye mpango ambao utakuwa unaweka mawasiliano mazuri ambayo yatakuwa na tija. Mfano, mabonde ya maziwa mbalimbali hayana usimamizi wa moja kwa moja kwenye vyanzo vyote vya mabonde kwa kuwa ofisi za mabonde zipo Kikanda na Halmashauri nyingi hazisimamii mabonde hayo. Tunahitaji Wizara zote hizi kuwa na uhusiano wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upandaji Miti, katika Halmashauri zetu zimeweza kutii maagizo ya kutenga fedha kwa ajili ya upandaji miti, tatizo ambalo litakuwa mbele yetu ni upatikanaji wa fedha za kutekeleza bajeti hiyo, vilevile usimamizi wa kuhakikisha miti inakuwa mfano mzuri, ni wakulima wa Tumbaku ambao upatiwa fedha ili kupewa miti, wengi wao huwa hawatilii maanani kuhakikisha miti inapandwa na kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku katika nishati, ili kuendelea kulinda mazingira ni muhimu kwa Serikali kuweka ruzuku katika nishati mbadala ambazo zitakuwa zinalinda mazingira, mfano matumizi ya gesi, nishati ya jua kuokoa au kupunguza matumizi ya mkaa ambao unapelekea ukataji mkubwa wa miti.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri katika Wizara hii. Pamoja na pongezi hizo nina mchango katika maeneo yafuatayo:-

Hifadhi ya Mazingira ya Bahari; ni wazi kuwa jitihada zetu za kuzuia uvuvi haramu ambao huharibu mazingira ya bahari na kuathiri maisha ya viumbe baharini bado hatujafanikiwa vya kutosha. Bado kuna matukio mengi ya uvuvi haramu ambayo yamekuwa yakitokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sababu nyingine zinazochochea uvuvi huu ni kukosa nyenzo za kisasa za kuvua kwenye bahari kuu. Huko awali tulikuwa na mradi wa *MACEMP* ambao ulikuwa unasaidia kukabiliana na changamoto hizi. Katika mradi huu wakazi wa pwani waliwezeshwa kutegemea shughuli nyingine na kupunguza utegemezi wa bahari. Kwa kuwa bado wananchi wa pwani wanaendelea kukumbana na changamoto hizi ni vema Mradi huu ukaendelea hata kwa kutumia fedha zetu za ndani baada ya kukamilika kwa muda wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Ruvuma; tabia ya kubadilika uelekeo wa Mto Ruvuma na matawi yake usiachwe bila kuwa na stadi ya kutosha. Naomba Serikali ichukue hatua za makusudi ili kudhibiti madhara yanayoweza kujitokeza hapo baadaye. 'stadi' hiyo ifanywe tangu unakoanzia na unakoingia Mto Ruvuma.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kutoa mchango wangu wa maandishi, juu ya mwingiliano kati ya Serikali za Mitaa, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na Wizara ya Maliasili na Utalii katika utunzaji wa mazingira.

Mheshimwa Mwenyekiti, kuna mwingiliano unaokinzana kati ya Taasisi za Serikali nilizozitaja, katika utunzaji wa mazingira jambo ambalo limefanya zoezi la utunzaji wa mazingira kuwa gumu. Ugumu huo

unasababishwa na kukosekana kwa Sera moja au Sheria moja inayoweka uturatibu wa kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Halmashauri za Wilaya zina Sheria ndogo zinazoruhusu, mathalani, kuvuna baadhi ya maliasili kama vile madini na magogo kwa ajili ya mbao ili kuongeza mapato ya Halmashauri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) inakataza shughuli kama hizo kwa kuwa dira na malengo ya Wizara hiyo; shughuli hizo zinaharibu mazingira. Wakati Wizara ya Maliasili na Utalii inatenga maeneo ya Hifadhi na Mapori Tengefu na hivyo kukataza wananchi wasitumie maeneo hayo kwa shughuli zao za kiuchumi. Halmashauri zinakuwa na uwezo wa kutoa vibali vya matumizi ya maeneo hayo au Wizara ya Ardhi nayo inaweza kutoa maelekezo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mkanganyiko huo, utunzaji wa mazingira unaweza kuwa mgumu kutokana na kuwa na vyombo zaidi ya kimoja, vinavyoshughulika na mazingira kwa namna moja au nyingine. Kwa sababu hiyo, napendekeza na kushauri kwamba, Serikali iwe na Sera moja ya mazingira, Sheria moja ya mazingira na chombo kimoja chenye mamlaka na masuala ya mazingira. Kwa mantiki hiyo, Wizara yoyote au Halmashauri yoyote ambayo itakuwa na shughuli ambayo itaathiri mazingira, basi Wizara au Halmashauri hiyo ilazimike kuomba kibali cha kuendesha shughuli hiyo kutoka katika Wizara au Taasisi itakayokuwa imepewa mamlaka ya kusimamia mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutumia nafasi hii kuzungumzia utunzaji wa mazingira usio na tija. Katika taaluma ya uhifadhi wa mazingira, uhifadhi wenye tija ni ule ambao unafanyika, lakini wakati huo huo kunafanyika pia uvunaji wa mazao yanayotokana na uhifadhi huo, kwa matumizi ya binadamu. Dhana hii ya uhifadhi na matumizi ya rasilimali zinazotokana na uhifadhi huo, ndiyo inayoitwa utunzaji endelevu wa mazingira (*Sustainable Environmental Management).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ipo misitu mingi ambayo imetangazwa na Serikali kuwa ni sehemu ya Hifadhi za Taifa na kwa sababu hiyo, Serikali imepiga marufuku uvunaji wa aina yoyote katika misitu hiyo. Matokeo yake ni kwamba, yapo magogo mengi yanaoza katika misitu hiyo na Taifa halipati faida yoyote kutokana na uhifadhi huo. Kwa mfano, Msitu wa Shengena katika Wilaya ya Same, umetangazwa kuwa ni Hifadhi na kwa sababu hiyo wananchi wa maeneo hayo hawaruhusiwi kufanya lolote katika msitu huo. Matokeo yake, miti mingi katika msitu huo imezeeka, magogo yanaoza, wananchi hawapati faida na wala Serikali haipati faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira kama hayo, halmashauri zenye mazingira yanayofanana na yale ya Wilaya ya Same zipewe mamlaka ya kutoa vibali vya uvunaji wa mazao ya misitu kwa usimamizi wa Maafisa Misitu wa Wilaya husika na watakaopata vibali hivyo vya uvunaji waelekezwe pia namna ya kupanda miti ili misitu hiyo iwe endelevu na hatimaye kuwa na utunzaji wa mazingira ambao una faida kwa wananchi na kwa Serikali pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAULID S. ABDALLAH MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Allah (S.W.) kwa kuniwezesha kuchangia hoja hii muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya nchi yetu ni kitu muhimu sana na yasipolindwa bila shaka madhara yake yanaweza kutuathiri sote kama Taifa bila ya kubagua nani amesababisha au nani hakusababisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya uharibifu wa mazingira ni sisi wenyewe tunaoishi na kuyatumia mazingira haya mfano, kilimo kisichozingatia uharibifu wa mazingira; kama vile kulima kwenye misitu yetu ya hifadhi, kilimo kwenye vyanzo vya maji, kulima kwenye maporomoko

bila ya kufuata kanuni ya kilimo hasa kwenye maeneo ya maporomoko. Aidha, mifugo isiyozingati mbinu za kisasa, mfano, kufuga na kulisha kwenye hifadhi za misitu na mbuga za wanyama, kufuga wanyama wengi kuliko uwezo wa ardhi iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bahari, Mito, Maziwa na Mabwawa kutumia uvuvi haramu wa mabomu au nyavu ndogo maarufu kama *jalife*. Katika yote haya tusisahau ukataji wa mkaa na kuni kama nishati hasa kwa ajili ya Majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hayo, bado tuna tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira katika majiji na njia kuu kwa uzalishaji wa taka ngumu na majitaka kutoka majumbani na viwandani. Aidha, vifungashio vya bidhaa za viwandani na vibebeo mfano, mifuko ya plastiki, maboksi na plastiki ngumu na sehemu kubwa yanayochafua na kuharibu mazingira yetu. Mfumo mbovu wa utiririshaji wa maji taka kutoka viwandani na majumbani kwenda maeneo maalum kwa ajili ya kuhifadhi, kuyatupa au kuchakata ili uweze kutumika tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni au ushauri;

(i) Mifugo yetu iwe kwa kiwango kisichoharibu mazingira hivyo basi, wafugaji wetu waelimishwe ufugaji wa kisasa wenye tija yaani mifugo kidogo tija kubwa.

(ii) Wafugaji wasihamehame kiasi ambacho wanaweza kuharibu mazingira kwa sehemu kubwa badala ya eneo dogo kama hawatahama. Pia wafundishwe kupanda nyasi kwa ajili ya malisho ya wanyama wao.

(iii) Wavuvi wadogowadogo na wale wanaotumia zana haramu, wafundishwe uvuvi bora na Serikali iwapatie vifaa vya kisasa vya kuvulia samaki ili waweze kupata mavuno mengi ya samaki jambo ambalo ndicho kivutio kikubwa cha kutumia uvuvi haramu.

(iv) Wakata mkaa; katika hili Serikali naishauri yafuatayo:-

- Mosi, Serikali iwafundishe wakulima njia mbadala ya kujipatia kipato kinyume na kuuza mkaa. Wanakijiji wengi hawana njia mbadala ya kupata fedha zaidi ya mkaa.

- Pili, kusambaza gesi majumbani katika Majiji ya Dar es Salaam na mengine. Aidha, tuna kila sababu ya kupunguza bei ya umeme ili watu wapike kwa jiko la umeme.

(v) Serikali iwe na takwimu zote za wazalishaji taka wa viwanda au majumbani na kila mtu achangie gharama za usafi na utunzaji wa mazingira kulingana na kiwango chake cha uchafuzi wa mazingira.

(vi) Serikali iwe mfano bora wa kutunza mazingira na kusimamia mazingira kwa kutumia vyombo vyake mfano mzuri, utunzaji wa mikoko Jangwani na daraja la Salenda. Serikali isiache mikoko na uoto wa asili ukifa maeneo ambayo Serikali au Ofisi ya Makamu wa Rais ni karibu yake.

(vii) Serikali isiweke ubaguzi wa utekelezaji wa Sheria. Mfano, Sheria ya mita sitini ya Mito. Kwangu Dar es Salaam Ofisi ya *DART* Jangwani na Jengo la *MOI* Muhimbili ni majengo yaliyo karibu na mito ndani ya mita sitini, lakini hayaguswi badala yake Serikali imeenda kubomoa nyumba za wananchi ambao Sheria imewakuta, jambo hili si utaratibu wa Serikali.

(viii) Serikali ishirikiane na Manispaa za Mijini zenye kuzalisha taka nyingi ili ziweze kujenga mitambo ya kuchakata taka na kuwa mbolea na manispaa zitalipa kidogo kidogo kwa Serikali; jambo hili lina faida ya mazingira, ajira, mbolea na kadhalika.

(ix) Sheria itungwe ya kudhibiti uzalishaji wa plastiki ngumu na laini ili kupunguza au kuondoa taka ambazo si rahisi kuzidhibiti.

(x) Wakulima wetu waelimishwe kilimo bora cha kisasa chenye tija. Bila shaka wananchi wakielimishwa vizuri hawana haja kwenda kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya hifadhi na maeneo ya maporomoko.

(xi) Kuanzisha *operation* ya kupanda miti mingi kuliko kasi ya wakata miti na wavuna misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. ALLY M. KESSY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Waziri Mheshimiwa January Makamba, binafsi kwa ziara yake katika Jimbo langu la Nkasi Kaskazini na kusaidia sana kuelimisha wananchi na baadhi ya Madiwani ambao wanajali maslahi yao ili wananchi wazidi kuharibu mazingira katika vyanzo vya maji na Msitu wa Fili ili tuwe na shida ya maji Namanyere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, nataka kujua mpango wa kupunguza utoaji wa maji katika Ziwa Tanganyika umefikia wapi na lini utakamilika wa Nchi za Burundi, Zambia, DRC – Congo na Tanzania. Umefikia kurudisha kibanio katika Mto Lukuga uliopo DRC – Congo ili maji yasizidi kwisha ziwani na kuhatarisha viumbe hai. Kwa sasa ziwa linapungua sana tena sana kuanzia 1960 mpaka sasa ziwa limepungua zaidi ya mita tatu za maji alama ziko sehemu ya mawe yaliyokuwa karibu na ziwa.

**MHE. OMAR A. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa January Makamba kwa hotuba yake nzuri ya Mazingira na Muungano,

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa ufupi sana katika suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira bado wananchi wanalichukulia kama ni *option* na sio lazima. Hili linatokana na kutosimamiwa vizuri sheria zake. Naiomba Serikali izingatie kusimamia na kuelimisha watu kuhusu mazingira. Bado elimu inahitajika. Mfano; kuna Sheria ya Kutotiririsha maji machafu kutoka viwandani, lakini mpaka sasa kuna viwanda vingi tu ambavyo vinatiririsha hayo maji bila hata kuyachuja. Hii inaonesha ni jinsi gani sheria bado haisimamiwi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna sheria ya kutokukata miti lakini bado maeneo makubwa nishati inayotumika kwenye kupikia ni mkaa, hakujasisitizwa wale wote wanaozalisha mkaa wawe na vitalu vya miti ili tukamilishe ile panda miti, kata mti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kuisisitiza Serikali kuwa, kuna wale watu wanaozalisha miti mbalimbali, iwawezeshe wanapohitaji msaada kwani wao ndio watunzaji wazuri wa *species* za miti mbalimbali.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pongeza nyingi kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa January Yusuf Makamba na Naibu wake Mheshimiwa Luhaga Mpina

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuelezea ari kubwa ya kimazingira inayokikabili Kisiwa cha Mafia na visiwa vidogo vidogo vinavyoizunguka Mafia. Mabadiliko ya tabia nchi kwa kiasi kikubwa vinatishia kuviondoa kabisa kwenye uso wa dunia visiwa vya Bwejuu, Jibondo, Chole na Juani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la kina cha bahari limepelekea kiasi kikubwa cha ardhi ya visiwa hivyo kumeguka. Kwa Muktadhi huu natarajia Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha hoja yake aje atueleze wananchi wa Mafia hatua ambazo Serikali inachukua katika kuokoa visiwa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafia ni Kisiwa chenye vyanzo vichache vya maji lakini kutokana na kukua kwa shughuli za kijamii vyanzo hivi vimeanza kuvamiwa na mvuto hali hii inatishia upatikanaji wa maji safi na salama, nichukue fursa hii kwa namna ya kipekee kumwomba Mheshimiwa Waziri au Naibu wake kuja kutembelea Mafia ili kujionea hali ilivyo kimazingira .

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchafu unaotupwa katika Bahari yetu ya Hindi kwa kiasi unatokana na mifuko ya *Plastic* (maarufu kama mifuko ya rambo). Kwa namna ya kipekee kabisa napenda kuomba Serikali yangu Tukufu kupiga marufuku matumizi ya mfuko na vifungashio vya *plastic*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusoma Jarida moja la uchunguzi la Kimataifa, likitoa Matokeo ya Uchunguzi ya kuonyesha kuwa kama hali ya utupaji taka baharini ilivyo sasa ikiendelea vivi hivi ifikapo mwaka 2050 ndani ya bahari kutakuwa na takataka nyingi (hususan) mifuko ya *plastic* kuliko idadi ya samaki. Hivyo, ipo haja sasa ya kupiga marufuku mifuko ya *plastic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji miti kwa madhumuni ya kuchoma mkaa, sasa ni janga la Kitaifa. Naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali ilizochukua kupiga marufuku uchomaji na usafirishaji wa mkaa. Niiombe Serikali kupunguza bei ya gesi ili wananchi wengi waweze kuhama kwenye kutumia mkaa na kutumia gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia niwatakie Watanzania wote kwa kusherehekea Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. JOYCE Y. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo mbalimbali katika hotuba hii ya bajeti ya 2017/2018 ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazingira kwa mimi, ninavyofahamu au kutafsiri ni afya kwa maono ya kwamba mazingira yakiwa machafu yataathiri afya za binadamu, wanyama au viumbe hai chochote ikiwemo mimea. Kwa hiyo, naomba sana Wizara hii ipewe kipaumbele, kiuchumi kwani ndio Wizara inayolinda maisha na afya ya viumbe hai moja kwa moja na kama mazingira hayataangaliwa basi afya na viumbe hai zitakuwa hatarini wakati wowote. Matokeo yake ni kuhatarisha uhai wa viumbe hai kupitia magonjwa na upungufu wa virutubisho mbalimbali na hatimaye hata kuwasababishia vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyoelewa wanyama, mimea tunashirikiana katika mambo mbalimbali ili kuweza kuishi mfano katika hewa ya *oxygen* na *carbondixide*. Hivyo basi, ni dhahiri mazingira ni kitu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimea vamizi, hili limekuwa ni tatizo kubwa sana katika maeneo mbalimbali ndani na hasa katika maeneo ambayo kuna mifugo na wanyama ambao wamekuwa wakitegemea majani, kama chakula. Mfano katika eneo la Ngorongoro kumekuwa na mimea vamizi sana na ambayo inakuwa kwa kasi sana siku hadi siku na kusababisha wanyama kuyatenga maeneo hayo yenye mimea vamizi *(invasive)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimea hii pia imekuwa ikiharibu uoto wa asili katika eneo la Ngorongoro na kuvuruga kabisa ekolojia. Ningeomba sana Serikali ichukue hatua za haraka katika kutokomeza mimea hii na kuendelea kuitunza mbuga ya Ngorongoro ili iweze kuiletea nchi yetu watalii na kuingiza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la mimea vamizi limelikumba eneo la hifadhi ya Mlima Rungwe ambayo ni aina ya miti inayoitwa Mipaina ambayo imekuwa ni tishio kubwa katika Mlima Rungwe. Miti hii imekuwa ikisababisha upotevu wa baianowai ya Mlima Rungwe uliopo Mkoani Mbeya na kupoteza uoto wake wa asili. Kama nilivyoshauri

katika bajeti ya Waziri Mkuu wakati nimechangia kwa kuongea, naiomba tena Serikali iangalie tatizo hili kwa karibu kabisa ili kuweza kuidhibiti mimea hii vamizi na kunusuru maeneo haya yaliyovamiwa na kibaya kabisa mimea hii imekuwa ikikausua hadi vyanzo vya maji na kusababisha ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa ukuta wa Pangani, ujenzi wa ukuta huu uliopo katika Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Pangani unaelekea kutokumalizika kwa wakati kama ilivyopangwa kumalizika Novemba, 2017, kama Serikali haitapeleka fedha za ndani kiasi cha 10% walichokubali kukitoa wakati ujenzi huu unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zingine za nje zimeshatolewa na ujenzi unaendelea vizuri katika upande wa mashariki wa ukuta huo kwani fedha za ujenzi zimetoka nje kwa wafadhili na wametoa fedha zote. Changamoto kubwa ipo katika eneo la Pangadeco na ndio eneo ambalo lina wakazi wengi ukilinganisha na eneo la mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la Pangadeco ndiko wanategemea ile 10% ya fedha za ndani ambazo Machi, 2017 zilikuwa hazijatolewa hata shilingi moja. Naishauri sana Serikali ipeleke fedha hizo ambazo ni kiasi kidogo sana ukilinganisha na kiasi kilichotolewa na wafadhili cha 90%, kama nilivyosema hapo mwanzo mazingira ni afya na kama hayatapewa kipaumbele yatahatarisha maisha na kusababisha vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo nina machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya uharibifu mkubwa wa mazingira ulisababishwa na ujio wa maelefu ya wakimbizi toka Burundi, DRC na Rwanda. Ujio huu umesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira katika Wilaya ya Kasulu,

Kibondo na Kakonko, idadi ya wakimbizi sasa ni zaidi ya 600,000. Ajabu ni kwamba katika hotuba yote ya Waziri hakuna hata mistari wala aya inayoelezea uharibifu huo wakati madhara yake kwa wakazi wa Mkoa wa Kigoma ni makubwa sana. Naishauri Serikali/Wizara ije na mpango maalum wa kuhifadhi mazingira na au kufufua maeneo yaliyoharibika sana na ujio wa wakimbizi. Mfano:

(i) Mto Makere umekufa na kukauka kabisa
(ii) Misitu katika vijiji imekatwa sana na kuharibiwa kabisa
(iii) Vyanzo vya maji *(water resources)* nyingi zimeharibika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, "*we need comprehensive program to restore the environment on area hosting refugees and communities hosting refugees in* Kigoma"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa kuhifadhi vyanzo vya maji katika Wilaya ya Kasulu na hasa vyanzo vilivyopo Kasulu Mjini. Katika eneo la Kasulu Mjini tuna vyanzo zaidi ya 200. Naomba jitihada za pamoja za Serikali/Wizara na Halmashauri ya Mji kulinda vyanzo vya maji ambavyo hatimaye hupeleka/hutiririsha maji yake katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana hatua ya Waziri kutuma wataalam wa Maji na Mazingira kuja Wilaya ya Kasulu kufanya "*study Project on that one*". Hatua ni njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Mazingira; nashauri tozo zinazotozwa na *TFS* na migodi iliyopo nchini angalau asilimia 25% ya tozo hizo zipelekwe kwenye Mfuko huo ili kulinda Mazingira ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwaka 2015/206 – *TFS* walikusanya zaidi ya shiligi billioni 50 ingekuwa busara sana kama 25% ya fedha hizi zingepelekwa kwenye mfuko huo. Tozo toka mgodini ni fedha nyingi sana na kwa hali ilivyo sasa hakuna hata senti inayopelekwa kwenye mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaweza kuleta pendekezo la sheria Bungeni ili sheria hiyo tuitunge haraka sana kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni desturi wawekezaji wa madini kupewa *Mining License* katika maeneo ya hifadhi ya misitu. Katika maeneo mengi wanayopewa hufyeka miti ovyo na kuchimba humo na kuharibu kabisa mazingira ya asili ya eneo hilo. Mfano katika Mkoa wa Geita maeneo ambayo yalikuwa na misitu mikubwa yote yamefyekwa na sasa ni jangwa. Aidha, sheria inawataka kufanya *recovery (reforestation)* baada ya kumaliza kazi (*exit plan).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba katika kipindi ambacho mgodi unaendelea kuleta madhara ya uharibifu huwapata wenyeji. Hivyo, madhara hayo huwezi kuyafidia baada ya mika 20 kwa kupanda miti. Maoni yangu ni kuwa:-

(i) Serikali ianzishe Sheria mpya ambapo mmiliki wa mgodi awajibike kutunza Maliasili zote katika eneo lake la *license* tangu siku ya kwanza ya kutoka, kwani kwa utaratibu hivi sasa mwenye *license* huangalia madini pekee (ardhini) na kutowajibika na uharibifu unaofanywa na wananchi katika eneo lake, isipokuwa kama watagusa madini. Mfano mzuri Geita Mjini msitu wote katika eneo la *GGM* umekwisha.

(ii) Serikali ianzishe mfumo maalum (*Nature Resources Extract Fund*) kama ulivyo Norway, USA na nchi za Kiarabu, maalum kwa ajili ya kuja kushughulika na *rehabilitation* kwenye maeneo yote yanayoathirika na miradi ya wawekezaji ambayo huvuruga kabisa mfumo wa maisha ya watu na wanyama wa eneo husika. Hivyo mfuko huo utasaidia kutoa elimu, majanga ya asili na kurudisha maisha yanayohusika kama kawaida baada ya miradi kukoma.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa hotuba nzuri aliyowasilisha Bungeni kwa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Napenda pia kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri sana ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015 - 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana kwa uhai wa Muungano wetu na wamefanya kazi kubwa sana ya kuondoa kero za Muungano. Kwa kiasi kikubwa Muungano wetu umetuletea sifa nyingi kutoka kila pande za dunia; changamoto kubwa tuliyonayo ni uharibifu wa mazingira na tabianchi. Katika maeneo mengi kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu. Uharibifu huo unasababisha changamoto za tabianchi ikiwemo upungufu wa mvua na majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira napendekeza Wizara iimarishe elimu ya utunzaji mazingira na pia kuimarisha ofisi na wataalam katika maeneo ya kimkakati, kama vile Mikoa ya Mbeya na Iringa ambayo ni vyanzo vikuu vya mito ikiwemo Mto Ruaha. Pamoja na elimu, wananchi wa maeneo ya kimkakati ya mazingira wanahitaji motisha ili watunze mazingira yao. Motisha kama vile kupewa kipaumbele cha nishati, miundombinu, elimu na hata kupatiwa miche bure itasaidia kwa kiasi kikubwa utunzaji wa mazingira. Maeneo haya yanahitaji upendeleo wa makusudi ili kukuza uchumi wa wananchi katika maeneo haya na kwa kiasi kikubwa kupunguza uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utunzaji wa mazingira Wizara ya Kilimo ishirikishwe ili kuhimiza kilimo cha kuhifadhi ardhi ambapo mkulima ahitaji kulima kwa jembe wala kuchoma moto. Elimu ya kilimo cha hifadhi ardhi kiendane na pembejeo bora zikiwemo mbegu bora ili wakulima waone tija ya hiki kilimo cha kuhifadhi ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa vyanzo vya mito umesababisha mito mingi kukauka na pia michanga na udongo kujaza maziwa yetu ikiwemo Ziwa Rukwa ambalo limo hatarini kutoweka. Serikali za Mitaa zihimizwe kutafuta maeneo mbadala ya uchimbaji mchanga ili kunusuru vyanzo vyetu vya mito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia hoja katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika eneo la *environmental assessment* katika miradi mbalimbali ya uwekezaji wa viwanda na hasa vituo vya mafuta ya petrol *(petrol stations).* Kuna tatizo kubwa sana juu ya upatikanaji wa vyeti vya mazingira katika miradi mbalimbali ya uwekezaji kutokana na mlolongo mrefu unaotokana na upungufu mkubwa wa wataalam wa mazingira katika halmashauri zetu za wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlolongo mrefu wa masharti ya kutimiza katika kuandaa andiko la mazingira kwenye mradi unaofanywa hutengeneza mazingira ya rushwa kubwa kwa wafanyakazi wa Idara ya Mazingira ili vyeti vya mazingira vipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo nyingi na faini kubwa zinazotolewa bila kufuata sheria za mazingira, wakati mwingine vitisho vingi na vikubwa vinavyotolewa na

watumishi/wanaohusika na mazingira katika kuhalalisha rushwa inayoambatana na gharama kubwa ya kulipia ili kupata *certificate.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *bureaucracy* katika kupatikana kwa vyeti vya mazingira inayochukua muda mrefu, jambo ambalo linakatisha tamaa wawekezaji na hatimaye kuacha kabisa kuwekeza katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ufanyike kila halmashauri kuwa na wataalam wa mazingira ili kurahisisha tathmini za mazingira kwenye halmashauri zetu. Ni vyema kuwa na kiwango cha mradi kinachotakiwa kusainiwa na Waziri ili kuruhusu vyeti vingine viweze kutolewa katika ofisi za mikoa badala ya kutegemea kila cheti kusainiwa na Waziri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu itolewe kwa wadau mbalimbali wa mazingira kabla ya kuwapa adhabu/faini ili kutoa fursa kwa wadau kutekeleza miradi yao kwa mujibu wa mahitaji ya masharti ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa masharti ya jumla ya mazingira katika kuanzisha miradi ya uwekezaji hasa *petrol stations* katika ofisi ya halmashauri, ili kuondoa usumbufu kwa wadau wa mazingira pindi wanapoanzisha miradi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama/faini za mazingira ziangaliwe upya ili kurahisisha wadau wengi wa mazingira kuweza kuzilipa bila kikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali umekuwa ni wa kutisha sana, hivyo ni vyema kuimarisha Kitengo cha Mazingira katika Halmashauri mbalimbali za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, semina mbalimbali zitolewe mpaka vijijini ambapo uharibifu wa mazingira umekuwa mkubwa kutokana na shughuli za uchumi kama ufugaji,

kilimo na uwindaji. Semina hizi zitasaidia wananchi kuona umuhimu wa kuhifadhi mazingira ili kuzuia tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Mazingira yaimarishwe katika kata ili kuepusha na kusimamia vyema uharibifu wa mazingira usiendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya magogo imekuwa ni chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira kwa kushirikiana na *TFS,* biashara hii ipigwe marufuku kwa kuwa inaathiri sana mazingira.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu waja wake wote pasipo ubaguzi. Nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii muhimu na mimi nichangie mada iliyopo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuperuzi ukurasa wa 49 wa kitabu cha Waziri kuhusu fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo. Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo upo kisheria, Sheria Na. 16 ya mwaka 2009, pamoja na nia njema ya Serikali ya Muungano wa Tanzania kuchochea maendeleo ya Jimbo, Mfuko huu bado zipo changamoto ambazo zinahitaji ufumbuzi wa kina kustawisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa fedha umekuwa adha kwa majimbo ya Zanzibar – mara nyingi kama sio zote, majimbo ya Zanzibar huchelewa kupata fedha hii wakati majimbo ya bara wanapata mapema sana. Kwa mfumo huu na ucheleweshaji huu unasababisha kudumaza maendeleo yanayokusudiwa; Zanzibar tunapata fedha hizi ambapo vitu vimepanda, thamani ya fedha yetu imeshuka. Kwa muktadha huo, naomba nipate sababu ya kucheleweshwa kwa fedha hii kwa Zanzibar. Pia nipendekeze kwa kuwa Jamhuri ya Muungano ni moja na Bunge moja, fedha hii itolewe kwa muda muafaka kwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuhusu Mfuko huu, hauongezeki tangu ulipoanzishwa wakati mahitaji yanakua, kila siku watu wanaongezeka. Naomba Serikali ipitie upya Mfuko huu ili ione mahitaji kwa sasa na kuongeza Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwiano wa ajira za Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar. Pamoja na makubaliano yaliyopo Zanzibar 21% na Bara 79%, lakini bado utekelezaji wake hauko wazi na umebakia kwenye makaratasi tu. Naomba uwekwe wazi kwa vitendo.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi; pamoja na juhudi za Serikali katika kulinda mazingira hususan pembezoni mwa fukwe za bahari na pembezoni mwa maziwa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto katika Ziwa Tanganyika; naomba Serikali iangalie upya ujenzi wa hoteli na nyumba za kuishi pembezoni mwa Ziwa Tanganyika, je, wanafuata taratibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi; kuna baadhi ya wavuvi ambao sio wazalendo ambao wanatumia baruti na nguvu ambazo hazifai katika vyanzo vya maji mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti za gesi zinazoendelea baharini, ni jambo jema Serikali kuendelea kuruhusu uchunguzi au tafiti zinazoendelea kufanywa na wawekezaji katika Bahari ya Hindi ili wagundue ni wapi na gesi ipo kiasi gani katika bahari. Wawekezaji wana vifaa vyao na sio Watanzania/uzalendo kuhusika? Je, Serikali ina uhakika gani tafiti zinazofanywa katika bahari juu ya uvumbuzi wa gesi kwamba haiathiri mazingira chini ya bahari? Je, Serikali ina mkakati gani ili inunue vifaa vya uchunguzi kujua wawekezaji hao hawaathiri mazingira baharini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya wananchi wanaotoa taarifa kwa polisi kuhusu viwanda feki vinavyotuhumiwa kuharibu mazingira, mifuko ya plastiki,

ukataji wa miti ya asili kiholela, wino – viwanda, viwanda vya viroba kiholela, uvuvi haramu. Wananchi ni wazalendo na mazingira yao lakini wanapoisaidia Serikali kuwataarifu, Serikali na hawa wanaoharibu mazingira wamekuwa wakitajwa, je, Wizara yako inatoa tamko gani? Wananchi wakiwa kimya bila kutoa taarifa kuhusu uharibifu huu mazingira mnategemea nini kama sio jangwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachina wanaojenga barabara waharibifu wa vyanzo vya maji Mkoa wa Katavi; Mto Kuchoma Wilayani Mpanda umekauka kutokana na matumizi makubwa ya maji yanayotumiwa na mkandarasi huyu. Serikali inatoa tamko gani ili kunusuru mto huu kwa matumizi ya wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Katuma pamoja na banio za umwagiliaji; pamoja na Serikali kusimamisha ujenzi wa vibanio kiholela katika Mkoa wa Katavi ambao kwa sasa wakulima wanapata maji, urasimu wa kupata vibali ili kujenga vibao vya kisasa na vinavyofuata utaratibu wa kulinda vyanzo vya maji mkoa mzima kuna vibanio sio zaidi ya vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itapunguza urasimu huu wa kupata vibali halali vya mabanio unaofanywa na baadhi ya watendaji au ni utaratibu unaofanywa na Wizara husika? Hii inaleta usumbufu mkubwa, Serikali inasema nini katika hili, waathirika wakubwa wakiwa wakulima hususan Mkoa wa Katavi. Jambo hili liangaliwe upya.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku kwa wananchi wanaokuza miche ya miti na wanaopanda miti Mafinga. Wananchi wa Mafinga na Mufindi kwa ujumla wamekuwa hodari katika kupanda miti na kutunza mazingira kwa ujumla. Hata hivyo, wananchi hawa kwa kiasi kikubwa wameachwa kama yatima hasa kutoka katika Wizara hii. Angalau Maliasili na Utalii kupitia Shamba la *Sao Hill* wamekuwa wakitoa mbegu (miche) kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunga mkono juhudi za wananchi wa Mafinga na Mufindi kwa ujumla, Wizara hii ije na mpango wa kutoa ruzuku kwa wananchi wanaojishughulisha na upandaji wa miti. Suala hili linaweza kuwa kichocheo kwa wananchi wa maeneo mengine hapa nchini kuona umuhimu sio tu wa kupanda miti kwa mazoea kama ilivyo hivi sasa. Ruzuku kwa wakulima/wananchi wanaopanda miti itakuwa kichocheo kikubwa cha lengo la kuhakikisha nchi yetu inakuwa ya kijani (ukurasa wa tisa (9)).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Usimamizi wa Mazingira; kutokana na ongezeko la majukumu, ni wazi kuwa *NEMC* imezidiwa kutokana na uhaba wa watumishi. Ni kwa sababu hiyo ndiyo maana hata elimu ya mazingira kwa umma imekuwa haifanyiki ipasavyo. Naishauri Serikali ione haja sasa ya kuongeza watumishi katika ofisi hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji miti bila kuitunza ni bure; nchi yetu imekuwa na kampeni kubwa ya upandaji miti, tukiwa *realistic* ni asilimia ndogo mno ya miti iliyopandwa ambayo inaendelea kuwepo. Nashauri Wizara ibadilishe mikakati ili tusiishie tu kuwa tunapanda miti bila kuitunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono na nawapongeza sana hasa kwa kuamua kulisimamia suala la upandaji na utunzaji wa miti. Kwimba tulipata ugeni wa Makamu wa Rais ambapo tulimweleza mipango yetu ya kupanda na kuitunza ambapo tunaanzia kwenye shule za msingi na sekondari. Tumekubaliana kila mwanafunzi anayeanza shule awe na mti wake ambao utapewa jina lake ambapo ataututunza hadi amalize darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mwanafunzi huyo huyo akiingia darasa la pili, tatu, nne, tano, sita na saba kila darasa atakuwa na mti wake, kwa hiyo akimaliza darasa la saba mwanafunzi mmoja atakuwa na miti saba. Mfano

Shule ya Msingi Kadashi ina wanafunzi 1000, kwa utaratibu huo kutakuwa na upandaji na utunzaji wa miti 1000, hii ni kwenye eneo moja la Shule ya Msingi Kadashi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Askofu Mayala aliyotembelea Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu, kuna wanafunzi zaidi ya 200, hivyo kila mwanafunzi anapoanza kidato cha kwanza hadi cha nne akimaliza *form four* atakuwa ameacha miti iliyopandwa na kutunzwa miti 800 ikiwa na majina yao. Upandaji wa miti na utunzaji wa miti kwa ajili ya mbao, kivuli, matunda na utunzaji mazingira. Naomba Wizara yako endapo kuna fungu lolote Kwimba iwe *pilot area* katika suala zima la upandaji na utunzaji wa miti. Kauli mbiu yetu ni 'upandaji na utunzaji wa miti kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe kama vichaa katika kupanda na kutunza miti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Muhongo dakika tano, jiandae *Attorney General*, jiandae Mheshimiwa Ashatu na Mheshimiwa Kairuki ajiandae.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa tu ufafanuzi kwa mambo mawili yaliyoongelewa. Kwanza ni deni la umeme la Zanzibar; napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba tunayo Kamati ambayo inaongozwa na Makatibu Wakuu wa pande zote mbili na wiki ijayo watakuja na nyaraka. Kuna maeneo wamekubaliana kuna maeneo hawakukubaliana. Kwa hiyo, nitaitisha kikao na mwenzangu wa Zanzibar ili jambo la deni la umeme tutalimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la mafuta na gesi. Kwanza siyo limetolewa kwenye mambo ya Muungano, mimi mwenyewe nilikaribishwa kwenda Zanzibar wakati ambapo Sheria ya Zanzibar ya mwaka 2016 inazinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Ambacho ni

muhimu na nimekisema mara nyingi, tusipende kuongea mafuta, mafuta, gesi, gesi nadhani cha kwanza kabisa tujue je, hayo mafuta yapo? Hiyo gesi ipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kitu cha kuongelea hapa kwanza tujue kwamba kweli yapo au hayapo, hilo la kwanza. La pili, kama yapo, hiki kugawana siyo kitu ambacho ni kigeni duniani hapa. Sisi Tanzania tumeanza majadiliano kwa gesi au mafuta yaliyoko Ziwa Tanganyika lazima tukae chini na Kongo, Zambia na Burundi, hatuwezi kukwepa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku chini Msumbiji ni lazima tufanye majadiliano na wenzetu wa Msumbiji tukienda kwenye vitalu vya kusini kabisa. Hiki siyo kitu kigeni duniani kinafahamika, kuna sheria za Kimataifa, kwenye *Arctic Circle* kuna mafuta mengi sana kule na gesi, inabidi Urusi na Ulaya wajadiliane. Kwenye mipaka ya Marekani na Canada kuna gesi na mafuta na wenyewe wanajadiliana. Nigeria na Cameroon wanajadiliana. Hivyo, ni vizuri *exploration* ifanyike upande wa Zanzibar tujue mafuta yako wapi au gesi iko wapi tukishapata ile ndiyo tutajadili namna ya kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yako upande wa Zanzibar ni mafuta yao, kama yako upande wa Bara ni mafuta yao, lakini kama yako katikati hayakuheshimu mipaka ya kisiasa na ambavyo mara nyingi ndivyo inavyotokea, kwa sababu hivi ni vitu vilivyotengenezwa kati ya miaka milioni 55,200, Zanzibar haikuwepo, Bara haikuwepo hata *Indian Ocean* ndiyo ilikuwa inaanza kutengenezeka. Kwa hiyo, tuna taratibu za Kimataifa za namna ya kushirikiana kwenye rasilimali kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar labda wanasiasa watalumbana sana lakini upande wa wataalam sisi tulitoa ahadi kuwasaidia wenzetu wa Zanzibar. Hata wiki jana badala ya kupeleka vijana Watanzania Bara 20 kwenda kusoma China mambo ya mafuta na gesi, kwa

kuwa nilitoa ahadi kwa Serikali ya Zanzibar nafasi tano tumepatia wenzetu wa Zanzibar waende kusoma kule China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwatoe hofu watu wanaosema mafuta kwanza, yakipatikana Magharibi mwa Pemba nachukulia mfano, huenda tusikwepe kujadiliana na Kenya. Kwa sababu ukiangalia mpaka wetu ukiuchora unavyokwenda huko juu kabisa ya Pemba, Pemba iko hapa, mpaka unapita hapa. Sasa kama mafuta yanaingia Kenya tutafanyaje? itabidi tujadiliane Zanzibar, Bara na Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili jambo kitaalam ni la kawaida, wala msisumbuke ninyi tulieni. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia. Nakushukuru wewe, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Makamu wa Rais chini ya uongozi mahiri wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu na wanavyoshirikiana na Rais Dkt. Mohamed Shein wa Zanzibar kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri kwa hotuba yao nzuri, ambayo imetoa taarifa ya mambo ambayo yamefanyika mwaka huu na ambayo yanategemewa kufanyika mwaka ujao. Niseme tu kwamba kwa sababu muda ni mdogo, naunga mkono hoja kabla ya muda wangu haujakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifafanue tu kwamba Mheshimiwa Ngwali amezungumza hapa juu ya Sheria ya Mafuta na hili suala la Muungano. Naomba kuwaambieni hapa kwamba moja, Katiba haikuvunjwa wakati tunatunga

sheria hii mwaka 2015 na bahati nzuri tulikuwa wote humu wengine wakaamua kuondoka tukabaki na Wabunge wawili wa *Opposition*. Sheria hii iliyotungwa inazingatia maslahi ya Muungano wa pande zote Zanzibar kama alivyosema Mheshimiwa Nahodha, kwavhiyo tuiunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 2 cha Sheria ya Mapato ya Gesi na Petroli hayatoi maelekezo kwamba Bunge la Zanzibar litunge sheria, inasema masuala ya mapato yanayotokana na gesi na petroli yatashughulikiwa kwa mujibu wa sheria zinazotungwa na Zanzibar, ndivyo hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba kuwatoa wasiwasi tuunge mkono suala hili. Tulichokifanya katika Sheria hii ya Petroli Kifungu cha 4, tulisema kwa sababu hili suala bado liko kwenye Katiba, tuliwekee utaratibu kwamba hili linabaki bado kuwa Jamhuri, lakini tukasema litasimamiwa na Serikali zote hizi mbili. Ukisoma hiki Kifungu ndivyo kilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikishasimamiwa na Serikali zote mbili, Katiba ya Zanzibar Ibara 88 inatoa mamlaka kwa Baraza la Wawakilishi kutunga sheria ku-*regulate* hiki kitu. Kwa hiyo, suala liko kwenye Katiba sawa la Muungano lakini utaratibu wa kushughulikia hayo mapato umewekwa kwenye sheria. Kwa hiyo hizi sheria hizi mbili ndicho nilichokuwa nazungumza hapa lisituchanganye sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni hili ambalo Mheshimiwa Ngwali amependekeza kwamba, tulete mabadiliko ya Katiba hapa ili tuondoe suala hili kwenye Muungano. Hili anataka tu kuharakisha hoja, kwa sababu bado tuna kiporo cha Katiba Mpya na Katiba yenyewe kilichobaki ni kupigiwa kura. Muda muafaka tutapiga kura kwa Katiba Mpya, kama wananchi watairidhia ikapita ndiyo itakuwa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi hapo Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, unajua Zanzibar tayari

imepata hii fursa, tusiwafanyie hiyana mbaya hapa, kwa sababu uliondoe kwenye Katiba sijui vitu gani, tayari wamepata hii fursa ya kusimamia hii rasilimali kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sitaki kwenda kwenye siasa ninachoweza kusema tu ni kwamba hakuna Katiba yoyote ambayo tumevunja kwenye hili. Hilo naomba kushauri hivyo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba kusema ni hili la Mheshimiwa Aeshi amelizungumzia na akaungwa mkono na Mheshimiwa Kangi Lugola. Unajua haya mambo mengine, haya masuala hoja zao hizi, haya masuala yako Mahakamani. Serikali ilipoanza zoezi hilo, watu walifungua kesi Mahakamani. Kama anachosema tumefanya maamuzi yanayovunja Katiba, Mahakama itaamua. Katiba hii msiisome upande mmoja tu isome *holistically.* Hatuwezi kuacha watu wanaumia, watu wanakuwa wahalifu, kwanza pia wanavunja sheria zile halafu tukasema eti sijui tunafanya vitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa huko vijijini huko Kahama, nimeenda kule wanasema wanaishukuru Serikali kwa hatua iliyochukuliwa. Wanasema watoto wetu walikuwa wanaenda kufa, halafu walikuwa wanashiriki uhalifu. Leo Serikali inachukua hatua hizi mnasema tuache, *that cannot be entertained. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ashatu dakika tano.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niseme machache katika bajeti hii. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nilisemee jambo moja lililosemwa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, ukurasa wa pili pale aliposema naomba kunukuu kwamba:

*"Imekuwa ni bajeti ngumu kutekelezeka kwa ushahidi wa fedha zilizotolewa, kulinganisha na zile zilizotengwa kila Wizara imekiona cha moto maana wamebanwa mpaka wamevunjwa mbavu"....Halafu paragraph iliyoendelea...**[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]***

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hayo maneno yameshafutwa tafuta maneno mengine.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kama yamefutwa basi naomba niende sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwaambia kwamba, tunatekeleza bajeti kulingana na mapato tunayoyapata. Pia lazima tufahamu kwamba katika uchumi tunafahamu mahitaji ni mengi kuliko rasilimali za kutekeleza mahitaji hayo. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba uchumi unatufundisha pia kwamba unapokuwa unatenga bajeti, bajeti ni nini? Bajeti *is an intelligent guess.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaweza kufikiria na ku-*plan* mipango yako, lakini unapoendelea kuitekeleza bajeti hiyo yapo mengine ya msingi yanayo-*emerge* na unaweza kuyatekeleza. Ndiyo maana hata Sheria ya Bajeti imetoa nafasi hiyo kwamba, yapo mengine yanayotokea na unaweza kuyatekeleza, lakini ukiwa ndani ya wigo ule wa bajeti ambayo imepitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti zilizotekelezwa hakuna jambo lolote lililotekelezwa nje ya bajeti ambayo tumeipitisha. Pia, nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba, Sheria yetu ya Bajeti, Kifungu cha 41 na Kanuni ya 28 ya Sheria

hii ya Bajeti, Namba 11 imempa nafasi Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kuweza kuhamisha fedha kutoka katika *Vote* moja kwenda *Vote* nyingine katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali yetu pia inawasilisha Bungeni Taarifa za kuhamisha matumizi hayo kutoka *Vote* moja kwenda *Vote* nyingine na nirudie kusema kwamba, hakuna sehemu ambako tumevuka pale ambapo bajeti yetu ya Serikali tulikuwa tumeipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee jambo moja ambalo limesemwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwamba, ili kutekeleza majukumu yake wamependekeza, Tume ya Pamoja ya Fedha iweze kutekeleza majukumu yake chini ya Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Katika hili naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba, ni muhimu tukaenda katika majukumu ya Tume hii ya Pamoja, majukumu yake ni yapi, ina-*deal* na mapato kutoka pande zote za Muungano na ndiyo maana ikawekwa chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii ya Pamoja imefanya ziara katika nchi mbalimbali zenye mfumo huu kama nchi yetu ya Muungano au Shirikisho, kote walikokwenda wamekwenda zaidi ya nchi tisa. Katika nchi hizi ni nchi tatu tu ambazo Tume hii ya Pamoja ya Fedha haiko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, kama ambavyo nimesema turejee kwenye majukumu ya Tume hii kabla hatujapendekeza jambo lingine ili kuweza kuhakikisha kwamba, Tume inafanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kulizungumzia jambo la *corporate tax.* Jambo la *corporate tax* lipo kisheria na linatekelezwa kwa Sheria yetu ya Mapato na naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba, kama alivyosema mchangiaji makampuni hulipa *corporate tax* kule yalikosajiliwa, lakini tunapoweza kutoa hoja zetu pia tufikirie na tuangalie manufaa ya hiki tunachokipendekeza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais. Nampongeza kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli imeeleza masuala mengi kwa kina na mafanikio mbalimbali ambayo wameyapata katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe ufafanuzi au maelezo katika hoja ya ajira katika Taasisi za Muungano pamoja na mgawo au utaratibu wa mgawo wa nafasi hizo za ajira katika Taasisi za Muungano. Iko hoja iliyotolewa hapa kwamba, suala hili halijarasimishwa, suala hili haliko kisheria, suala hili watendaji wanaweza wakaharibu wasieleze ukweli katika mgawo huu na mambo mengine. Napenda tu kusema mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa utaratibu huu haukuwepo huko nyuma. Ni jitihada katika kuondoa changamoto katika Muungano ikaonekana kuwe na utaratibu mahsusi kabisa kwa ajili ya mgawo wa nafasi za ajira katika taasisi za Muungano. Utaratibu huu pia ni wa muda katika kuhangaikia suluhisho la kudumu ambalo litasaidia kuweka nafasi hizi na utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nafasi za vyombo vya ulinzi na usalama haziko katika mgawo huu wa asilimia 21 Zanzibar na asilimia 79 katika SMT. Ukiangalia katika mwaka 2013/2014 na 2014/2015, katika nafasi zilizotolewa katika Wizara ya Mambo ya Nje asilimia 25 zilichukuliwa na SMZ na asilimia 75 ndiyo zilichukuliwa na SMT. Kwa hiyo, hata hapo utaweza kuona pia, hata ule mgawo wa asilimia 21 ulizidi mpaka asilimia 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukienda katika Taasisi za *NIDA,* ukienda katika Ofisi ya Makamu wa Rais yenyewe, Zanzibar walipata mgawo katika ajira za 2013/2014 asilimia 33. Imezidi hata ile asilimia 21 ambayo ilikuwa imewekwa katika utaratibu wa mgawo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Taasisi nyingine nia ni njema. Nyingine ajira zake zilifanyika kabla ya waraka huu haujatungwa mwaka 2013/2014, lakini bado kama Serikali pande zote mbili tumekuwa tukilifanyia kazi pamoja na Waziri wa Utumishi kutoka SMZ, SMT na Ofisi ya Makamu wa Rais, tumekuwa tukiliangalia suala hili kwa kina na Mheshimiwa Makamu wa Rais amekuwa pia akilifuatilia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayokuja katika maombi ya ajira, kwanza wengine unakuta hawajitokezi, hawaziombi. Pili, lazima tuangalie pia na sifa. Huwezi tu pia ukagawa nafasi bila kuangalia sifa na vigezo. Tumekuwa tukiendelea kuhamasisha Wazanzibari waendelee kujitokeza pamoja na Bara ili kuhakikisha kwamba asilimia 79 na asilimia 21 inaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, changamoto nyingine ambayo tunaipata katika kupata taarifa sahihi, unakuta wapo wanaotoka upande wa Zanzibar wamekuwa pia wakiomba nafasi, lakini unakuta wengine wamekuwa wakitumia anuani za kutoka Tanzania Bara. Kwa hiyo, unajikuta kuweza ku-*compute* namba kamili imekuwa kidogo ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ziko taasisi mbalimbali za kiuhasibu, nafasi nyingine katika sekta ya elimu, nafasi nyingine katika sekta ya afya, ambazo hata siyo taasisi za Muungano, Wazanzibari wamekuwa wakipata fursa na wamekuwa wakiomba, hawakatazwi. Fursa iko wazi kwa sababu, wote ni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunaendelea kufanya jitihada kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Tumeshafungua ofisi eneo la Shangani kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanaratibu ajira zote za Taasisi za Muungano pamoja na kurahisisha na kuendesha majukumu yake wakiwa Mjini Zanzibar ili kurahisisha zaidi kwa waombaji kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumekuwa tukiendelea kutangaza nafasi za ajira pia kwa kutumia Vyombo vya Habari vikiwemo vya Zanzibar ili kuwahamasisha Wazanzibari kuhakikisha kwamba nafasi zinazotangazwa waweze kuomba. Nia ni njema na tutaendelea kufanya hivyo kila mara inapobidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu ni mfupi na naomba nianze kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kisesa kwa kuendelea kuniamini na baadhi yao mko hapa kuja kushuhudia. Niendelee kuwaambia tu kwamba, kama ni Mbunge mlikwishapata na nitaendelea kuwawakilisha kikamilifu hapa Bungeni na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kujibu hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; kuna suala lililoelezwa na Kamati hapa kuhusu suala la Kamati ya Katiba na Sheria imetupongeza sana kwa hatua tulizozichukua katika suala la upungufu la Jengo la Luthuli *Two* katika Ofisi ya Makamu

wa Rais na hatua tulizozichukua. Sasa hivi nataka niwahakikishie kwamba hatua tunaendelea kuzichukua, moja ni hayo marekebisho ambayo sasa hivi yanafanyika. Pili, baada ya marekebisho hayo kukamilika ambayo yanafanywa kwa sasa hivi tutam-*engage PPRA* ili aweze kufanya ile *value for money* ili kuhakikisha kwamba, fedha za Watanzania zilizotumika zimetumika sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa zimekuja hoja za Kiongozi au Msemaji wa Kambi ya Upinzani wakati anawasilisha, alizungumza sana suala la Muungano na kuonesha kwamba, Muungano huu wakati mwingine labda anaona yeye kwamba, hauna faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida kubwa sana za Muungano na Tanzania tunatakiwa kujivunia sana Muungano huu. Moja, tuna Kifungu kile cha *GBS* ambayo kila mwaka tunatoa zaidi kati ya bilioni 20 mpaka bilioni 50 kwa ajili ya *GBS,* pia *pay as you earn* haikuwepo, leo tunatoa *pay as you earn* ya bilioni 1.75 kila mwezi na kwa mwaka tunatoa bilioni 21 za *pay as you earn(PAYE)* na hazina utata wowote katika kutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *dividend* ya *BOT* ambayo nayo inatolewa kati ya bilioni mbili mpaka bilioni nane kila mwaka na haina utata katika kutolewa. *BOT* bado inazikopesha hizi Serikali mbili, Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya kuziba pengo la mapato na matumizi. Kwa mfano, Zanzibar katika mwaka huu wa fedha ilikuwa na kiwango ambacho kinafikia mpaka bilioni 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani alisema hapa kwamba, Muungano huu umeshindwa kuchochea maendeleo na umeshindwa kuchochea mabenki kwenda Zanzibar. Tumeshuhudia wote mwaka 1990 benki Zanzibar zilikuwa mbili tu, lakini sasa benki Zanzibar zimefikia 12. Tafiti nyingi zinafanywa, anasema kwamba, hakuna

uchocheaji wa maendeleo, Benki Kuu tu yenyewe imeshafanya tafiti zaidi ya 13 Zanzibar na tafiti hizi ni kwa ajili ya maendeleo na kwa ajili ya uchumi na zimekuwa zikiwa *incorporated* katika maendeleo ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema pia makampuni mengi hayaendi Zanzibar, tukitolea mfano Makampuni haya ya Simu, hakuna Kampuni ya Simu ambayo ipo Bara hapa haipo Zanzibar. *tiGO*, *Voda, Zain,* wote wameanzisha *branch* kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo hii Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Uvuvi wa Bahari Kuu ambao unatoa faida kubwa tu, mpaka sasa hivi toka uanzishwe tunatoa zaidi ya billion nne. Mfuko wa Jimbo kila mwaka, fedha hizi hazina utata, Mheshimiwa Ngwali alikuwa anasema zina utata, hazina utata wowote, tunapeleka *1.24 billion* kila mwaka na hazina utata wowote. *TASAF* toka tuanze tumepeleka shilingi bilioni 31.5 na miradi mikubwa imefanyika ya ujenzi wa barabara na miundombinu mikubwa ya kiuchumi bilioni 31. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *MIVARF* tumepeleka zaidi ya bilioni 13.49 na miradi mikubwa imefanyika Zanzibar, barabara zaidi ya kilometa 83. Tumejenga masoko ya kisasa ambayo mpaka yana *cold room* Unguja na Pemba, yamejengwa zaidi ya bilioni 13.49 zote zimekwenda, halafu mtu anasema kwamba, haoni shughuli ambayo imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSTECH;* tumefanya miradi mikubwa ya *COSTECH,* miradi mikubwa ya utafiti imefanyika zaidi ya shilingi bilioni tatu zimekwenda katika shughuli hii na tafiti zinafanyika na Zanzibar wananufaika sana na tafiti zinazofanywa na *COSTECH* katika uzalishaji wa mpunga, uzalishaji wa muhogo na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo makampuni yetu yanafanya vizuri sana. Nani asiyejua kwamba, Bodi ya Mikopo inatoa mikopo bila kubagua watu wa kutoka pande zote mbili za Muungano? Nani asiyejua kwamba leo *TRA*

inakusanya kodi pande zote za Muungano tena kwa usahihi na kwa ufanisi mkubwa na pande mbili zote zinanufaika. Taasisi za Muungano 39 tulizonazo, taasisi 30 zote zina ofisi Zanzibar, isipokuwa Taasisi tisa tu ambazo na zenyewe tayari tumeshatoa maelekezo lazima ziwe na ofisi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa suala kwamba Taasisi hizi za Muungano hazishirikiani, ushirikiano ni mkubwa. Mmeona ushirikiano uliozungumzwa hata na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kuhusu mapato ya *ZESCO* na *TANESCO.* Pia Wizara ya Nishati na Madini kubeba mzigo wa asilimia 31 kwa ajili ya kupunguza gharama zinazolipwa Zanzibar yote hayo unasema kwamba Muungano huu hauna manufaa! Tendeeni haki Muungano, mengi yamefanyika, tutaendelea kuyaboresha na sisi tuko hapa, tunatembea kila siku kwenda Zanzibar, kwenda Unguja na kwenda Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Pemba hata ukimuuliza tu mtoto mdogo, ukiuliza Mpina, wewe sema Mpina tu, yeye atasema Naibu Waziri Muungano atamalizia. Tunafanya kazi, endeleeni sasa kutuunga mkono, ili tuweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mambo makubwa katika upande wa mazingira. Nani asiyejua hali ya mazingira ilivyokuwa Novemba mwaka 2015, Serikali ya Awamu ya Tano inapoingia madarakani? Nani asiyejua takataka zilivyokuwa zikizagaa kila mahali? Nani asiyejua majitaka yalivyokuwa yakitiririka kila mahali na kuleta athari kubwa kwa wananchi? Nani asiyejua migodi na viwanda vilivyokuwa vikichafua mazingira? Nani asiyejua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mabadiliko makubwa, leo utashuhudia na kuona jinsi maboresho tulivyofanya. Wakati tunaingia mwaka 2016 wagonjwa wa kipindupindu mwaka 2016 walikuwa 11,000 na watu waliofariki mwaka huo walikuwa 163. Leo mwaka 2017 kwa

jitihada tulizozifanya ofisi hii pamoja na Wizara ya Afya wagonjwa wa kipindupindu mwaka huu walikuwa 1,146 tu waliofariki 19. Kwa hiyo, utaona jinsi ambavyo tunafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa wanatokea baadhi ya Wabunge wanataka kuwabeba wahalifu, watu wanaopigwa faini, watu tunaowatoza, lazima mjue kuna suala la utiririshaji wa majitaka kwenye viwanda, nenda kaangalie, wagonjwa wa saratani walivyoongezeka sasa hivi. Mwaka 2006 wagonjwa wa saratani walikuwa 2,416, kila mwaka wamekuwa wakiongezeka wagonjwa wa saratani. Sasa hivi tuna wagonjwa wa saratani toka 2,416 hadi wagonjwa wa saratani 47,415. Kwa hiyo, huwezi ukakinga kifua kwa wahalifu hawa. Wahalifu hao waambiwe kufuata na kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyoingia kwenye ofisi ile tumeongeza kasi ya ukaguzi wa mazingira kuhakikisha kwamba hakuna mtu anachafua mazingira, hakuna mtu anaharibu mazingira. Wakati tunaingia uwezo wa kukagua mazingira kufikia taasisi 425, leo tumefikia taasisi 1,548 hadi kufikia hii Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mapinduzi makubwa katika ukusanyaji wa mapato, mapato *NEMC* sasa yamepanda. Tulikuta wana uwezo wa kukusanya mapato ya bilioni tano, katika muda mfupi tuliokaa tumeweza kuchochea ukusanyaji wa mapato *NEMC* hadi wamefikia bilioni 12, ongezeko la bilioni saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengine wanakaa hapa wanasema ooh! hili Baraza la Mawaziri halina Mawaziri wa kumshauri Mheshimiwa Rais. Hivi mnataka Mawaziri wa aina gani wa kumshauri Mheshimiwa Rais? Tunayafanya haya tulitakiwa kupongezwa tu. Tumefanya *transformation* hizi kuhakikisha kwamba, maendeleo yanaweza kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya *operations* nyingi mbalimbali na tozo nyingi na faini mbalimbali watu wameweza kutozwa kwa ajili ya kuhakikisha tunarejesha mazingira yetu, tutaendelea kufanya hivyo. Ukitaka uepukane na utozwaji wa faini wewe zingatia sheria hakuna mtu ambaye atakugusa, Mpina hutamuona wala *NEMC* hutawaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mapinduzi makubwa ya kuleta usafi katika nchi hii. Leo Dar-es-Salaam *(DAWASCO)* mifumo yao mibovu ilikuwa ikitiririsha taka kila leo, miundombinu imeimarika na leo taka hizo hazitiririshwi tena kwa kiwango kile kilichokuwa kinatiririshwa. Tulikwenda Kahama, tukawakuta wanatiririsha majitaka tena mbugani na kuharibu vyanzo vya maji, leo nenda, wana mfumo mzuri wa ku-*contain* majitaka hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SBL,* Mbunge wa Temeke atanishuhudia, *SBL* walivyokuwa wanatiririsha majitaka. Tumedhibiti tatizo hilo halipo tena, wananchi hawapati shida tena. Wananchi wa Keko waliokuwa wanakumbwa na mafuriko, leo hayapo tena, tumetatua tumemaliza. Mgodi wa Dhahabu wa *North Mara* walivyokuwa wakitiririsha maji yenye kemikali, tumepiga marufuku na hali ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mapinduzi makubwa sana, watu walikuwa wanashuhudia uchafuzi wa mazingira barabarani, mabasi yanatupa taka ovyo, leo tumeweka utaratibu mzuri, mnaona tangazo hilo la *SUMATRA* ambalo linamtaka kila abiria kuhakikisha kwamba anatunza mazingira, hakuna utupaji taka ovyo. Kwa hiyo, ukiona mazingira yako safi barabarani sasa hivi ujue Vyombo vya Serikali ya Awamu ya Tano viko kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchafuzi uliokuwa unafanywa na meli za mafuta na za mizigo katika bahari yetu, leo tumeweka mfumo mzuri wa uchukuaji taka, uzoaji taka na wa utupaji taka ambao unafanywa majini. Tumeweka mfumo mzuri ambao sasa hatuwezi tena kurejea kwenye uchafuzi huo uliokuwa unafanyika. Operesheni za mara kwa mara zinafanyika na hivyo hakuna uchafuzi tena uliokuwa ukiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uimara huu na kazi hii kubwa ambayo tumeifanya tumeweza kuaminiwa. Leo hii wawekezaji na wafadhili wengi ambao wanaidhinisha fedha zao kwa ajili ya kuisaidia Tanzania katika kutengeneza miundombinu ya uondoshaji wa taka na utunzaji wa maji taka wengi wamejitokeza. Hapa ninavyozungumza katika mwaka huu wa fedha kwa mara ya kwanza eneo la majitaka lilikuwa halipewi fedha. Leo kwa *DAWASA* tu peke yake wafadhili wengi wamejitokeza na tunategemea zaidi ya shilingi bilioni 800 kutoka kwenye taasisi tu moja ya *DAWASA.* Sasa mtu akisimama hapa na mbwembwe kusema kwamba eti Serikali ya Awamu ya Tano haiaminiki kwa wafadhali, wafadhili gani unaowa-*refer* wewe kama majitaka tu peke yake mfadhili tu kwa *DAWASA* peke yake ni zaidi ya shilingi bilioni 800? Tumeaminiwa na miradi inaendelea kujengwa katika majiji na miji kwa ajili ya kuboresha hali ya usafi wa mazingira katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali King alikuwa anazungumza kuhusu ahadi yangu niliyoitoa nilipokuwa Zanzibar ya kufanya tathmini katika eneo lililodidimia. Nataka nimwambie asome randama nimeshaweka, lile eneo tumekubaliana Wizarani tutalifanyia tathmini katika mwaka huu ujao wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ilitushauri kwamba tufanye *audit* eneo la Bagamoyo, Pangani, Rufiji na Zanzibar ile miradi ya mabadiliko ya tabianchi. Wakati tunaagizwa bajeti ya mwaka 2016/2017 sehemu kubwa ya miradi hii ilikuwa haijaanza, sisi tulienda kukagua miradi hii yote ilikuwa ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakuongezea dakika moja, nimekupa dakika 15 nakuongezea dakika moja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kifupi niseme kwamba sasa hivi ndiyo tunaipia miradi hii. Mradi mmoja tu ndio umefikiwa kuhakikiwa ni mradi wa Rufiji, tumeukagua na tumeugundua una kasoro na tumemwagiza Mkaguzi wa Ndani kufanya ukaguzi huo. Mkaguzi wa Ndani atakapotuletea taarifa tutawasilisha kwenye Kamati kuona *status* ya mradi huo ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na naunga mkono hoja na kwamba Serikali ya Awamu ya Tano tuko kazini, tuungwe mkono tufanye kazi ili tuonyeshe uwezo na tuibadilishe Tanzania yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ni kweli Wizara hii mnafanya kazi vizuri sana kwenye mazingira. Sasa namuita mtoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nakupongeza kwa namna ambavyo umetuongoza tangu asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa shukrani kwa wote waliochangia katika hoja yetu, kwanza kwa Kamati zote mbili, lakini pia kwa wasemaji wote wawili wa Kambi ya Upinzani kwenye masuala ya Muungano na Mazingira. Tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge wote, kwa heshima na taadhima na moyo mkunjufu na ushauri mlioutoa tutaushughulikia. Wamechangia Wabunge 57 na kwa kweli kwa hoja ya siku moja kwa Wabunge 57 ni wengi, inaonyesha ni jinsi gani ambavyo kuna hamasa kubwa katika mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mambo ambayo tutayatolea majibu sasa na kuna mengine tutayatolea majibu kwa maandishi na kuwapelekea Waheshimiwa Wabunge kwa sababu muda tulionao hapa hautatutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimefurahi na kufarijika kwamba yanapokuja masuala ya mazingira Waheshimiwa Wabunge wote wa upande huu na upande ule tunaungana. Kwa hiyo, napata faraja kwamba katika vitu vinavyoliungasha Bunge ni hifadhi ya mazingira. Hiyo inafanya kazi yangu iwe rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao marafiki wengi kwa upande ule kwa sababu ya masuala ya mazingira. Wapo watu ambao wanaonekana ni wakorofi kwa upande mmoja, lakini ukiingia ndani ya nyoyo zao ni wanamazingira wazuri sana hata Mheshimiwa Halima Mdee ni mwanamazingira mzuri sana, kwa hiyo, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu ni kwamba kwa kadri siku zinavyoenda kila Mbunge atakuwa mwanamazingira na hili linatupa faraja kubwa sana. Hii inatokana na hali halisi ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaiona katika majimbo yao na huko wanakoishi kuhusu uharibifu wa mazingira. Imani yangu ni kwamba hamasa hii itapelekea uwekezaji mkubwa katika hifadhi ya mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka haraka kwenye hoja zilizotolewa. Kwanza, ni Mfuko wa Mazingira. Watu wengi wamezungumza kuhusu hili na nimesikitika kidogo dada yangu Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware ametulaumu kwamba miaka yote mfuko upo haujaanza, nilidhani kwamba angesema hongereni angalau kwa kuanza mwaka huu na ningependa utupe moyo na utuunge mkono kwa sababu ndio tumeanza na tunahitaji *support* yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea namna ya kuupatia mfuko fedha. Sheria iliyoanzisha mfuko huu iko wazi kabisa vyanzo vimeainishwa humu. Katika nchi yetu zipo shughuli za kiuchumi na kiuzalishaji mali ambazo zinapelekea uharibifu wa mazingira. Kwa mfano, biashara ya mkaa ambapo Serikali inapata mapato, lakini biashara ile inaharibu mazingira; biashara ya magogo, Serikali inapata mapato lakini biashara ile inaharibu mazingira; uingizaji wa magari chakavu, Serikali ina-*charge* zaidi kwa shughuli hiyo lakini fedha hii haiji kwenye mazingira na uchimbaji wa madini vilevile kwenye leseni kuna *fees* zinatolewa. Kwa hiyo, sisi tunaongea na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuona ni namna gani katika hizi shughuli ambazo zinaharibu mazingira lakini Serikali inapata tozo basi sehemu ya tozo ije kwenye Mfuko wa Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Sheria ya Mazingira katika kifungu cha 213 kinaelezea *sources of funds* kwa mazingira na kinasema; *"(a) such sums of money as may be appropriated by Parliament."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hizi kinawapa nguvu Waheshimiwa Wabunge kuujaza mfuko huu pesa. Kwa hiyo, hatuna sababu ya kulalamika kuhusu fedha kidogo kwenye hifadhi ya mazingira wakati sisi wenyewe Wabunge tuna uwezo wa kuwa-*appropriate* pesa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa kuhusu suala la Baraza la Rufani. Na mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge aliyesema kwamba Waziri siyo kazi yako kupiga faini, ile ni kazi ya Mkaguzi wa Mazingira na imeandikwa kwenye sheria. Nakubaliana kabisa na yaliyoelezwa kwamba wewe ni mamlaka ya rufaa kwa anayepigwa faini na hata mimi nikifanya kitendo kile naweza kukatiwa rufaa kwenye Baraza la Rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini moja ya changamoto ya kutokuwepo kwa Baraza ni mfuko huu kutokuwa na pesa kwa sababu ukienda kwenye sheria kifungu cha 205 vyanzo

vya fedha za Baraza la Rufani kinasema ni Mfuko wa Mazingira. Kwa hiyo, kama Mfuko wa Mazingira hauna fedha Baraza la Rufani halipo. Kwa hiyo, utaona kuna muunganiko wa ujenzi wa kitaasisi wa hifadhi na usimamizi wa mazingira. Kwa hiyo, tukilimaliza suala la Mfuko wa Mazingira tutakuwa tumemaliza suala la Baraza la Rufani vilevile. Nadhani Mheshimiwa Gekul ndiye aliyezungumzia jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kuhusu fedha kidogo kwenye hifadhi ya mazingira ukweli upo wazi, wote mnaona. Jawabu ni moja kupanga fedha zaidi na pili kuujaza mfuko. Hata hivyo, kuna jambo lingine tumelifanya na nimesema kwenye hotuba kwamba mwaka huu sasa tumefanikiwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sekretarieti ya Mkoa na Wizara itakuwa na kifungu kwenye bajeti kinaitwa kifungu cha hifadhi ya mazingira kwa sasa hakuna. Wenzetu watakapokuwa na vifungu hivyo wataamka na kupanga shughuli za hifadhi za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunahangaika kutafuta ufadhili kwenye hifadhi ya mazingira kutoka kwa wenzetu sehemu mbalimbali. Tumeeleza asubuhi kwamba kwa jitihada za ofisi yetu tumeweza kufanikisha upatikanaji wa shilingi bilioni 230 kwa ajili na mradi wa maji. Tunaendelea na nataka niwahakikishie kama Mungu akipenda na kama tutaendelea kuwepo kwenye nafasi hizi nikisimama tena hapa mwakani, nitakuja na habari nzuri zaidi kuhusu upatikanaji wa fedha nyingi zaidi kutokana na ufadhili. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viroba Mwanasheria Mkuu ameliongelea sina haja ya kurudia sana lakini napenda kukumbusha tu kwamba Serikali ilitoa taarifa ya kwanza kabisa ya dhamira yake ya kupiga marufuku viroba na mifuko ya plastiki Bungeni hapa kwenye bajeti ya mwaka jana mwezi Mei na mpaka shughuli ile imesimamishwa ilikuwa Machi 1 ni miezi kumi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sikubaliani kabisa na hoja kwamba hakukuwa na taarifa ya kutosha. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichokuwepo ni kwamba wenzetu kwa kuzoea ile habari kwamba Serikali ikisema haitendi kuna watu kabisa waliingiza mitambo wakatengeneza *stock* mpya. Ukienda kwenye *Hansard* hapa Bungeni utaona hilo, lakini tarehe 16 Agosti, pia tukatoa taarifa kwa umma kwamba tutapiga marufuku viroba tarehe 01 Januari 2017, lakini unakutana na mtu anakuambia mimi nimeingiza mzigo juzi. Sasa kama unaagiza mzigo wakati ukiwa na taarifa kwamba Serikali ina dhamira gani kuhusu biashara hiyo yanayokukuta ni kwamba umeamua wewe mweyewe yakukute. Licha ya hivyo, Serikali itaendelea kufanya mazungumzo na wafanyabiashara hawa ili kuangalia utaratibu nzuri wa namna ya kumaliza kabisa shughuli hii. Wote tunakubaliana kuna manufaa makubwa zaidi kwenye kupiga marufuku shughuli hii kuliko kuacha iendelee, hilo halina ubishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upandaji miti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza kuhusu utaratibu wa upandaji miti hapa nchini. Tunafahamu kwamba tangu uhuru nchi yetu imefanya jitihada mbalimbali za kupanda miti, lakini hatukupa mafanikio ya kuridhisha. Mkakati mpya tulioutengeneza umezingatia sababu za kufeli kwa mipango ya siku za nyuma, umeshirikisha sekta binafsi na mamlaka zote, tumeandika kila kata hapa nchini inastawi mti gani na unapaswa kupandwa wakati gani. Mkakati huo tutautoa kwa ajili ya kuelimisha Wabunge na wananchi jinsi ya kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa nchini idadi ya miti yote iliyopo asilimia kumi tu ndiyo ya kupanda asilimia 90 ndio miti ya asili inayoota yenyewe. Kwa hiyo, namna nzuri ya kuwa na miti hapa nchini ni kuhifadhi ile ambayo tunayo tayari, ile miti ya asili. Kwa sehemu kubwa nchi yetu ina miti ya miyombo ambayo inaamka kwa haraka zaidi pale inapoachwa ikue. Kwa hiyo, kikubwa zaidi ni kuacha kupanda miti na kupanda miti vilevile lakini matumaini makubwa yapo kwenye kuhifadhi miti na misitu tuliyo nayo. Ipo miradi mingi zaidi na taratibu nyingi tutazitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu Mheshimiwa Pauline amesema asubuhi kwamba kuna harufu ya kifisadi kwenye baadhi ya miradi, lakini hakutusaidia kwamba ni katika eneo gani hasa kwa sababu ufisadi upo wa namna nyingi. Je, ni kwenye *procurement* au malipo? Namwomba hata kwa kuninong'oneza anieleze ili nilishughulikie jambo hili kwa sababu ni jambo hatutaki liwepo kwenye ofisi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwakikishie kwamba miradi hii kwa masharti ya ufadhili wake kila mwaka inakaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali. Kumefanyika ukaguzi 2013/2014, 2014/2015 na ripoti ya 2016 inakuja na wamejiridhisha kabisa kwamba miradi ile iko safi kabisa na inatekelezwa kwa kiwango kilichotarajiwa. Kwa hiyo, sisi tunaamini kabisa kwamba hakuna tatizo lolote lakini kama dada yangu Mheshimiwa Pauline una taarifa naomba unijulishe ili nianze kufuatilia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu matumizi ya mkaa. Matumizi ya mkaa ni changamoto kubwa na ni sababu kubwa inayopelekea uharibifu wa mazingira nchini mwetu. Sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais tumeamua kuchukua *leadership* kwenye jambo hili kwa sababu ndugu yangu na mzee wangu Mheshimiwa Profesa Maghembe mkaa kwake ni chanzo cha mapato, wakati mimi kwangu mkaa ni uharibifu wa mazingira. Mimi nina *interest* kubwa zaidi nchi yetu ika-*transition* kutoka kwenye matumizi ya mkaa kwa sababu kwa kadri siku zinavyoenda nishati za kupikia mbadala zinaendelea kuwa nafuu na zinaweza kushindana kwenye soko la mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulifanya kongamano kubwa ambalo tuliliongoza na wadau wote wa utengezaji wa mkaa. Tumeamua kuanzisha shindano kubwa kabisa la kitaifa na wale majasiriamali wote wanaoweza kutengeneza nishati mbadala waje watuonyeshe tutawapa zawadi. Zawadi ya kwanza kabisa itakuwa zaidi ya shilingi milioni 400 na tutawawezesha kupanua biashara yao hiyo, viwanda vya mkaa vitaanzishwa ili taratibu tuondoe mkaa kwenye soko

siyo kwa kuupiga marufuku bali kwa kuufanya ushindwe kwa bei na nishati nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba kuna Wakuu wa Wilaya na baadhi ya maeneo wamepiga marufuku usafirishaji wa mkaa kutoka kwenye maeneo yao ni hatua njema. Hata hivyo, lazima twende nayo taratibu kwa sababu mji kama Dar es Salaam ambapo asilimia 60 ya mkaa unatumika Dar es Salaam na pale hakuna sehemu unaweza kuzalisha mkaa, kwa hiyo, lazima tuwezeshe watu kupata nishati inayolingana na bei ya mkaa ndipo tuweze kupinga marufuku kabisa matumizi ya mkaa. Huko ndiko tunakoelekea, hii *road map* ambayo tunakuja nayo itaeleza miaka mingapi na kwa utaratibu gani tutaondoa matumizi ya mkaa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu pia katika mkaa unaozalishwa nchini kwa sehemu kubwa mkaa huo unakwenda kuchoma nyama Uarabuni. Ukienda kwenye bandari zile za Bagamoyo, Mbweni majahazi na majahazi yamejaa mkaa unaenda Unguja. Unguja haiwezi kutumia mkaa wote ule unaoenda kule, ukifika Unguja unapanda tena unaenda Mombasa - Shimoni. Ukifika kule unawekwa kwenye magunia mazuri *made in Kenya* unaenda kuchoma nyama Uarabuni. Nataka niombe ruhusa ya Mheshimiwa Rais niende Kenya nikazungumze na wenzetu ili tuweze kuona namna gani tunaweza kushirikiana pamoja na Wizara Maliasili kupiga kabisa marufuku suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea kuhusu namna tunavyoweza kuzibalisha taka ngumu ziwe rasilimali. Sisi kwenye ofisi yetu hazipiti wiki mbili tunapokea mwekezaji, mapendekezo, *proposal* ya mtu anayetaka kuzalisha umeme kwa kutumia taka. Bahati mbaya sana hawa watu wanaoleta hii miradi wanazunguka sana hawajui pa kuanzia. Wengine wanaanzia *TANESCO*, wengine Wizara ya Nishati, wengine TAMISEMI, wengine wanakuja kwetu na wengine wanakwenda EWURA. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba hapa nchini mpaka sasa hakuna mradi uliofanikiwa kwa sababu hakuna mwongozo

na utaratibu wa kushughulikia miradi hii wakati taka zipo nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Makamu wa Rais mwezi Mei ataitisha kikao ambacho kitakuwa ni kati ya sisi Wizara ya Nishati, TAMISEMI Halmashauri za Majjiji zote *EWURA* na *TANESCO* na kikao hicho ndicho kitaamua kuhusu mwongozo wa kukaribisha uwekezaji wa sekta binafsi kwenye shughuli ya kuchakata kata. Kwa wale Waheshimiwa Wabunge ambao wamekuwa na hoja hizi, naomba wawe na subira Serikali itatoa mwongozo kutoka kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu namna gani tunaweza kurahisisha na kuharakisha uwekezaji wa sekta binafsi katika kuchakata taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira ya bahari na pwani, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza kuhusu mambo mawili. Kwanza, uvuvi haramu lakini pili watu wanaokaa pwani wanajua jinsi fukwe zinazovyoliwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Sisi ofisi yetu inao mkakati, Mheshimiwa Ghasia na Waheshimiwa wengine wameongea, mtakumbuka miezi mitatu iliyopita ofisi yetu sisi na mimi niliongoza nilikuwa Mwenyekiti wa kikao cha Mawaziri kama sita hivi tena wazito, Mheshimiwa Mwinyi, Mheshimiwa Mwingulu, Wizara ya TAMISEMI na Maliasili ambapo tulikaa na kutengeneza mkakati wa pamoja wa kukabiliana na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wiki chache zijazo mtaona operesheni kubwa ya Kiserikali, tusingependa kuizungumza kwa sababu tunakabiliana na watu wanaofanya kazi shughuli haramu ambayo itamaliza kabisa tatizo hili la uvuvi haramu. Vilevile tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya mabadiliko ya tabia nchi katika maeneo ya kanda za Pwani kwa kujenga kuta kama tunavyojenga pale *Ocean Road,* Pangani, Kigamboni na Zanzibar lakini kupanda mikoko kama tunavyofanya kule Rufiji. Kwa hiyo, tunaendelea kutafuta fedha nyingi kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Zanzibar, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King wameongelea, hii ndiyo dhamira yetu. Ule mradi aliouongelea Mheshimiwa Shamsi nimechukua mawazo yale na tutaupanua na kuukuza. Shida kubwa ya wavuvi wadogo ni kuweza kufika mbali. Kwa hiyo, ili uwasaidie, usiwasadie kwa namna ambayo wataendelea kufika pale pale karibu. Kwa hilo, tumelichukua na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunaamini kwamba mchango wa Tanzania Bara kwa maendeleo ya Zanzibar siyo wa Serikali peke yake bali hata mfumo wa uchumi unaowezesha biashara kubwa zaidi na rahisi zaidi kwa pande zote mbili ili Zanzibar uchumi wake uhamasike zaidi kutokana na kuwa karibu na sehemu yenye uchumi mkubwa zaidi. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikisha wenzetu wataalam wa biashara na uwekezaji ili tuweze kukamilisha hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Ally Saleh Ally bahati mbaya hayupo sijui amekasirika labda ana udhuru...

**MBUNGE FULANI:** Yupo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Yuko wapi Ally Saleh?

Nimekuona Alberto, mimi nataka nikuambie rafiki yangu kwamba Muungano *is a fact of life* yaani lazima tukubaliane wote hapa na hata kama hukubali na kama viongozi lazima tuwe *honest* kwamba hatuna namna nyingine zaidi ya Muungano. Mwingiliano ni mkubwa, ni wa muda mrefu na gharama ya kuuondoa ni kubwa zaidi kuliko juhudi tunazoweza kuzitumia kuzirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani uwekezaji kwenye kuimarisha Muungano ni muhimu zaidi kuliko tafakuri ya namna tunavyoweza kuachana. Kwa hiyo, napenda

juhudi za wanasiasa wa pande zote mbili ziwe katika kuuimarisha Muungano huu. Mnanifahamu mimi ni mtu ambaye sina tatizo na mawazo ya aina yoyote na hakuna hoja inaweza kutufarakanisha au kututenganisha kwenye Muungano. Kwa hiyo, siasa nzuri zaidi ndugu zangu siyo siasa ya kuubeza Muungano ni ya kujenga, siasa nzuri zaidi siyo ya kuupa jina baya ili uhalalishe kuumong'onyoa. Siasa nzuri ni kuupa hadhi yake unaostahili ili tuweze kuwekeza katika juhudi za kuuimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ally Saleh amesema kwamba utaratibu wa kutatua kero haufai, lakini nitaka nimwambie tu kwamba utaratibu huu wa tangu mwaka 2006 ndiyo umetupunguzia kero kutoka 15 mpaka tatu sasa hivi. Kwa hiyo, ndugu yangu kama kuna mawazo ya utaratibu bora zaidi sisi tuko wazi kabisa na mimi nipo tayari kupokea mawazo kuhusu utaratibu bora wa kushughulikia kero za Muungano kwa sababu nchi hii ni yetu sote na mawazo bora zaidi ya kuimarisha Muungano ofisi yetu inayapokea. Kwa hiyo, tupendekeze tu kama yapo mawazo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kuhusu kukauka kwa mito, vyanzo vya maji na maziwa, ni kweli. Katika ziara zangu nchini nafanya makusudi kutembelea vyanzo vya maji, maziwa na mito. Nimetembelea Ziwa Tanganyika, Ziwa Jipe, Chala, Natron, Manyara, Eyasi na nimejionea mwenyewe jinsi gani tunavyoelekea kwenye kuangamia.

Waheshimiwa Wabunge, ninaposema kuelekea kuangamia ninamaanisha hivi, ukienda kule Jipe utaona zile jamii za pale hata aina ya samaki wanazovua ni visamaki vidogo, mtu akitaka kwenda kuvua ni lazima apite kwenye magugu yaliyojaa kwenye ziwa. Lile ziwa nusu liko upande wa Tanzania na nusu liko upande wa Kenya. Ukipiga picha ziwa lile utaona upande wa Tanzania ndiyo kumejaa magugu, upande wa Kenya kuna hoteli pembeni ya ziwa watu wanaogelea, hii ni aibu kubwa kwa nchi yetu na hii tunafanya wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais tumeamua kwamba tutaanzisha mradi mkubwa kabisa wa kitaifa wa kutunza maziwa madogo madogo katika nchi yetu. Nimewaambia kabisa wataalam wa Wizara nitawapa likizo ya wiki tatu wakakae mahali waandike mradi wa maziwa madogo nane hapa nchini na namna tunavyoweza kuyahifadhi. Kwa hiyo, tutawaletea taarifa hiyo tutakapokuwa tumekamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie hali ya uharibifu wa vyanzo vya maji ni kubwa sana tutapoteza mito katika nchi hii. Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme, watoto na wajukuu zetu watakuja kutushangaa sisi tulikuwa ni watu wa namna gani ambao tulikuwepo na kushuhudia na kuwezesha upoteaji wa kitu kama mto, unawezeshaje mpaka mto upotee? Kwa hiyo, ngoja niishie hapo nisije nikasema maneno mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *NEMC,* Waheshimiwa Wabunge wamesema kwamba kuna haja kubwa ya kujenga uwezo wa *NEMC* na hilo tunalifanya. Ni taasisi ambayo imepewa mamlaka makubwa lakini uwezo wake wa kitaasisi na fedha hauendani na majukumu iliyopewa na sheria. Kwa moja ya kazi yetu sisi ni kujenga uwezo wa taasisi hii ili iendane na hadhi na heshima ya taasisi yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye nchi nyingine Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC* analindwa kutokana na kazi kubwa anayoifanya. Nchi hii Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC* anaweza akapita kantini hata hujui ni nani wakati ni taasisi kubwa yenye mamlaka makubwa kabisa inayoweza kuzuia hata ndege zisiruke kwa sheria hii. Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC* anaweza akasema *Emirates* isiondoke mpaka nijihakikishie kwamba haivujishi mafuta, ndiyo nguvu ya kisheria ya taasisi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi moja ya majukumu yetu tangu tulipoingia Wizarani ni kujenga uwezo wa kitaasisi, ndiyo maana tumefufua Mfuko na Baraza la Rufaa. Watu wa *NEMC* mkiongea nao watawambia, *NEMC*

tuliyoikuta na *NEMC* ya sasa kama alivyosema Naibu Waziri ambayo ilikuwa inakusanya shilingi bilioni 5 sasa hivi 12 ni tofauti. Kazi hiyo itaendelea na katika siku chache zijazo mtasikia kazi tutakayoifanya *NEMC* ya kubadilisha mambo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee wangu Mheshimiwa Nsanzugwanko ananiangalia sana nataka niseme jambo lake, mwaka jana wakati tunawasilisha bajeti hapa, Mheshimiwa Nsanzugwanko na Mheshimiwa Bilago walisimama na kushika mshahara kwa kusema kwamba hatujazungumza lolote kuhusu uharibifu wa mazingira unaofanywa na wakimbizi. Nataka niwaambie kwamba baada ya lile jambo mimi nikafanya safari kwenda kwenye kambi za wakimbizi, bahati mbaya sikusema kwenye hotuba na nikatembelea Nyarugusu, Makere, Mtabila na vijiji vyote vinavyozunguka kambi za wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawaita wakuu wote wa *UNHCR* kule Kigoma na nikawapa maelekezo yafuatayo siyo kwa mdogo ni kwa barua. Kwanza, makambi yote ya wakimbizi Tanzania yafanyiwe *EIA*. Sheria yetu inasema, maeneo ya makazi makubwa lazima yawe na *environmental impact assessment* lakini nilistajabishwa kwamba makambi yale yalikuwa hayana *environmental impact assessment.* Kwa hiyo, kwanza tukawapiga faini kwamba hawakuwa na *EIA* lakini pia tukawalazimisha wafanya *EIA* ambayo itatoa masharti ya matumizi ya eneo lile ikiwemo hifadhi ya mazingira, hilo ni agizo la kwanza nililowapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo la pili nililowapa, ni kwamba walikuwa na *pilot project* ya kuwapa majiko ya gasi wakimbizi. Tukasema kwanza isiwe *pilot* iwe ni mradi, lakini usiishie kwa wakimbizi bali uishie pia kwa jamii inayozunguka kambi hizo ili wasikate kuni. Agizo la tatu nililowapa ni kwamba wachangie kwenye miradi ya maendeleo katika vijiji vinavyozunguka makambi ya wakimbizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua alininong'oneza kwamba atashika tena mshahara lakini naamini taarifa hii

itamridhisha na ataachia mshahara wangu kwa sababu kazi tumefanya na tunafuatilia. Ulinituma na nimeenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ulisema kwamba Kasulu kuna tatizo la vyanzo vya maji na tumepeleka timu na tutaandika mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba nimalize kwa kusema kwamba kazi tuliyopewa na Taifa ya kusimamia uimara wa Muungano tunaifanya vizuri, naamini kabisa kwamba katika kipindi cha mwaka mzima uliopita, hamjasikia kelele, malalamiko kuhusu Muungano kama mlivyokuwa mmezoea kusikia siku za nyuma. Hili jambo halijatokea kwa ajali kwamba watu wamelala ni kwamba kuna kazi imefanyika ya kuhakikisha kwamba tunapunguza kero na malalamiko. Muungano na jina baya la Muungano halipo tena kwenye vichwa vya habari. Hii siyo kwa sababu akina Mheshimiwa Ally Saleh wanachapana bakora kule hapana, hii ni kwa sababu tumefanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wote mnafahamu kwamba hifadhi ya mazingira kama alivyosema Naibu Waziri na Mwenyekiti imeongezeka na tutaendelea kufanya kazi kubwa, naomba muendelee kutuamini na kutuwezesha. Kama mnavyojua sisi ni rafiki wa watu wote na kwa maneno hayo, nategemea hatutapata shida sana kwenye kupitisha bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wote waliochangia na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**Fungu 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*........................Sh.4,914,608,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye *Vote* 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na hoja yangu inakwenda kwenye *Subvote 1001* lakini inakwenda kwenye *Item 220700 - Rental Expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka uliopita wa 2016/2017 kulikuwa na shilingi milioni 218, safari hii ongezeko ni mara tatu kuna shilingi milioni 647. Kwa mujibu wa maelezo ya randama fedha hizi ni kwa ajili ya kulipia gharama za ukodishaji ndege na magari wakati wa safari za Makamu wa Rais na ujumbe wake nchini pamoja na gharama za kumbi za mikutano. Kwa kuwa Serikali hii ya Awamu ya Tano wanasema ni Serikali ya kubana matumizi lakini imekwenda kwa ongezeko la mara tatu, tunaangalia wanabana matumizi kweli au ni danganya toto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kufahamu pamoja na randama hii Serikali ina maelezo ya ziada? Pamoja na randama yenu kusema kwamba mnakodi ndege na magari ongezeko la mara tatu na mnasema mnabana matumizi, maneno mnayosema ndiyo vitendo vyenu? Hasa mtuambie ukweli ulivyo, ufafanuzi ukoje, kutoka shilingi milioni

218 mpaka shilingi milioni 647 uhalisia uko wapi na dhana nzima ya kubana matumizi? Naomba ufafanuzi wa kina, mtulie Mawaziri, mtupe jibu ambalo ni maridhawa, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masoud, kwanza kwa pesa hizi na kazi ya *Private Office* ya Mheshimiwa Makamu bado ni pesa ndogo. Kuna kazi nyingi sana Ofisi ya Makamu wa Rais inafanya. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli umenisaidia hata hizi zilizopangwa ni ndogo na zimeongezeka kwa sababu zile zilizopangwa mwaka jana hazikutosha na tumelazimika kuingia kwenye madeni. Ndiyo maana tumeweka sasa gharama halisi walau pamoja na ukomo wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadhi na heshima ya nafasi ya Makamu wa Rais ni kubwa sana. Hatustahili kulalamika kwa shilingi milioni 600 kumwezesha Makamu wa Rais azunguke na kufanya kazi yake kama msaidizi wa kwanza kabisa wa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumzi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kif.1001–*Administration and HRM Division*……………........................Sh.1,940,260,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilishaletewa majina na chama kwa mujibu wa Kanuni, tunaanza na Mheshimiwa Paresso.

**MBUNGE FULANI:** Ni Mheshimiwa Gekul.

**MWENYEKITI:** Sasa majina mnaleta ninyi na kama kuna mabadiliko lazima Kiti mkipe taarifa, jina hapa ni Paresso.

**MBUNGE FULANI:** Ni Mheshimiwa Gekul.

**MWENYEKITI:** Sasa semeni basi makubaliano yenu maana mnanibishia mimi tena mwenye biashara hapa? Haya Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Sisi ni wale wale hakuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi langu ni moja tu ambalo nahitaji kupata sasa ufafanuzi wa kina wa Serikali kuhusu Mfuko wa Mazingira katika nchi yetu. Nimepata majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba hata yeye katika kitabu cha hotuba yake analiomba Bunge ushirikiano. Pia Kamati iliyoshughulikia hotuba hii katika Wizara hii na wenyewe wamelisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wenzetu katika dunia Mfuko huu umeshaanza kufanya kazi *GEF* ambapo Wizara hii wameomba miradi minne sasa iweze kuwa-*facilitate.* Cha kushangaza ni miaka 13 Serikali haipeleki fedha katika mfuko huu ambao umeanzishwa kwa mujibu wa sheria. Pia hata fedha ambazo walipatiwa Wizara hii zaidi ya shilingi bilioni nane mwaka uliopita katika Wizara yao ni shilingi milioni 300 tu Serikali imeweza kutoa zaidi ya shilingi bilioni saba hazijatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo *NEMC* ndiyo wanabeba Wizara hii. *NEMC* wanakusanya shilingi bilioni 15 na *this time projection* yao ni shilingi bilioni 15.6 na wakati bajeti ya Wizara ni shilingi bilioni 15. Cha kusikitisha zaidi pia, Wizara hii wamepunguziwa fedha zao kutoka shilingi bilioni 20 na kwenda shilingi bilioni 15 ambazo *NEMC* lazima wazibebe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu niiombe kauli ya Serikali, Mheshimiwa Waziri yeye anaomba Bunge, Waziri

wa Fedha yuko hapa, Waziri Mkuu yuko hapa, watuambie ni kwa kiasi gani Serikali itakwenda kupeleka fedha kwenye Mfuko huo wa Mazingira ili uweze kusaidia masuala mazima ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo sitaridhika na majibu ya Serikali nitatoa hoja ya kuondoa shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, lakini Kiti kilishatoa maagizo Waziri na Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulikia Wizara hii, watakwenda kwenye Kamati ya Bajeti kujenga hoja kwa pamoja kwa mujibu wa Kanuni zetu ili Serikali ione umuhimu wa mazingira haya sababu bila mazingira tutapata matatizo sana mbele ya safari. Iko hoja amezungumza Waziri mwenyewe kuwa iko michango ambayo Hazina inakusanya kwa niaba ya mazingira lakini haiendi kwenye mazingira. Mheshimiwa Waziri malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati nahitimisha hoja, kwanza kwenye kuleta hoja hapa ni sahihi kabisa. Msingi wa hoja ya Waziri ni kuomba pesa Bungeni, kwa hiyo, tumekuja kuomba pesa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kama nilivyoeleza kwenye hotuba na kwenye kuhitimisha hoja kwamba tunayo mazungumzo ndani Serikali kati ya sisi na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuhusu vyanzo hivi ambavyo kwa *nature* yake vinahusika na mazingira. Biashara ya mkaa, magogo, magari chakavu na leseni za madini ambayo yanaharibu mazingira kwa sehemu kubwa. Kwa hiyo, mazungumzo yanaendelea na hayajafikia muafaka lakini tunaamini kwa sababu tulianza tangu mwaka jana tutaelewana ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mkisoma sheria pia Bunge na lenyewe lina nafasi yake vilevile katika jambo hili. Sisi tutaendelea kwenye Serikali kwa sababu ukisoma kifungu cha 213(2)(a) cha Sheria ya Mazingira kinaeleza nafasi ya Bunge kuhusu Mfuko wa Mazingira. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Mimi sihitaji kupoteza muda kama vile ambavyo unaongoza Bunge letu na hili unaliunga mkono, niombe sasa Kiti chako iwe ni azimio la Bunge kwa sababu tukimwachia Waziri na mazungumzo yake na Serikali ndiyo imechukua muda mrefu wa miaka kumi na tatu. Mheshimiwa Waziri hayuko mbali na wewe hauko mbali niombe busara sasa ya Kiti sasa litoke azimio la Bunge utuhoji ili Serikali wakatuletee kutoka kwenye vyanzo hivyo ambavyo hata sisi kambi rasmi ya Upinzani tumevitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hatuna utaratibu huo, Kiti kimeshaielekeza Kamati ya Bajeti kukaa na Serikali ambayo *a pound of flesh* tayari tulishaipata sasa unatafuata *drop of blood.* Kwa hiyo, mimi nafikiri ukubali tu kauli ya Serikali ni safi na Kiti kitasimamia hoja hiyo na kuhakikishia kuwa mazingira ni muhimu kwenye nchi yetu. Mheshimiwa Hashim Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa huzuni kubwa na unyonge mkubwa na huruma kubwa, kwanza pamebakia kama siku mbili kutimia miaka 53 ya Muungano wetu huu ambao ni muhimu na wa aina yake. Masikitiko yangu hivi juzi ndege iliyokuwa ikifanya utafiti imezuiwa kwa sababu gani za msingi? Hakuna kitu cha ajabu, niendelee kuwashukuru Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa msaada mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ni sehemu ndogo, inategemea mapato haya lakini kitu cha ajabu katokea mtu tu kutoka *Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA )* kuja kuzuia. Hebu waelezeni Wanzanzibari kweli tumewafanyia haki? Kuna msemo husemwa na waislam, nguruwe haramu lakini mchuzi wake unaunywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu mtufahamishe mimi elimu yangu ni ndogo. Mheshimiwa Waziri kwanza nitakuwa

sijakufanyia haki kwa kazi uliyoifanya kwenye mambo ya Muungano lakini Naibu Waziri Mheshimiwa Mpina umefika mpaka Pemba nawapongeza kwa dhati. Mheshimiwa hapa nitashika mshahara wako mpaka nipate darasa au elimu ya kutosha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Nitajibu na yeye atasaidia kujazia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muache yeye aseme halafu wewe utamalizia, Mheshimiwa Mbarawa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili kuna utaratibu ambao unatakiwa ufanywe kabla ndege kuja hapa nchini. Ndege ile ilipokuja waliomba kibali *TCAA* kwa ajili ya matengenezo, sio utafutaji wa mafuta. Mheshimiwa Balozi, Makamu wa Pili wa Rais alinipigia simu mimi akaniambia mpaka sasa Mheshimiwa tumekwama tusaidie. Nikafuatilia *TCAA,* baada ya kwenda *TCAA* wakanionyesha kibali ambacho kimeombwa kutoka Zanzibar kwa ajili ya matengenezo. Nikawaambia sasa waombe kibali kingine, wakaomba kibali kwa ajili ya kwenda kutafuta mafuta na tumefanya kazi hiyo kwa muda wa siku mbili tukawapa kibali hicho. *(Makofi)*

Tatizo lililokuwepo hawakufuata utaratibu na kila nchi ina utaratibu wake. Hawezi kutoka mtu *somewhere* akaleta ndege tu bila kufuata utaratibu. Hii nchi ina usalama, ina utaratibu wake ni lazima tusimamie kanuni. Bunge hili lako Tukufu ndilo limeweka sheria na kanuni hizo lazima tusimamie utaratibu kwa maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshiwa Waziri una la kuongeza?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemfahamu sana...

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa Jaku.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano linajitosheleza kabisa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kwa darasa hili nililopewa. Cha kusikitisha hawa *TCAA* hii ndege walitaka ilale Tanzania Bara...

**MBUNGE FULANI:** Aaah.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Sizungumzi kwa kubahatisha, kama utataka ushahidi nitafute nikupe, lakini kipi cha msingi kwa ndege ilale Tanzania Bara? Kwa nini msifike mahali mkakaa wenyewe Serikali mbili mkashughulikia tatizo hili kabla ya kuruka ndege. Ndege ile ndani kulikuwa na watu wa Jeshi kama usalama upo wa Jeshi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku umeridhika na majibu ya Serikali maana naona unakuja na hoja nyingine. Umeridhika na majibu ya Serikali?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi pia nilivyochangia kwa maandishi tunarudi pale pale uliposema Kiti kimeagiza Wizara ikakae pamoja na Kamati ya Bajeti, lakini mimi sijaridhika na hilo. Mimi naomba lijadiliwe, Wabunge 400 hapa watakuwa na mawazo mengi zaidi kuliko hiyo Kamati ndogo. Mwaka jana ni hivi hivi tujikumbushe historia, mwaka jana tu siyo siku nyingi tukapigwa chenga ya mwili mfuko ule tukapitishiwa tu shilingi bilioni moja ya kupitishia kama *conduit* hakuna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kutoa hoja tujadili masuala ya huu Mfuko wa Mazingira na vyanzo vyake tuvijadili kwa kina hapa na tutoe mapendekezo yetu kwamba tunapendekeza moja, mbili, tatu halafu tukubaliane na Kamati kule itaenda kumalizana na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, lakini najua ugumu wake naomba ijadiliwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Soni kaa.

Utaratibu wa kikanuni hapa tunapitisha bajeti ya Wizara, sasa wewe unatakiwa kama huridhiki na majibu uombe *issue* yako ijadiliwe, ikishajadiliwa itarudi tena kwako kupigiwa kura, hakuna hoja ya azimio la Bunge. Naelewa *concern* yako, nakuelewa vizuri sana lakini *this is how it works.*

Sasa wewe acha Waziri akujibu kama huridhiki toa hoja huridhiki unataka hili suala lijadiliwe lipate nguvu baadaye tutakuja kukuhoji tena. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Majibu ni yale yale.

**MWENYEKITI:** Majibu ni yale yale.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijaridhika naomba suala hili lijadiliwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa toa hoja yako, tuendelee.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huu Mfuko wa Mazingira ambao uliundwa 2004 mpaka leo hauna chanzo cha kudumu cha mapato. Kuna maeneo ambayo napendekeza ambayo ingeweza kuchangiwa na wala hatutaki...

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MWENYEKITI:** Aah, aah, ninyi ndiyo mnaendesha Bunge huko? Endelea bwana. *(Kicheko)*

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vyanzo ambavyo nimependekeza ambavyo napenda viwe vya kudumu katika kuchangia Mfuko huu. Moja, asilimia 10 ya mapato ya leseni itumike kwa ajili ya mfuko huu. Hatutaki chanzo kipya yaani wananchi wasitozwe kodi yoyote mpya, hizi hizi za zamani zinazohusiana na mazingira ziende huko. Kwa mfano, leseni za viwanda, migodi yote, za biashara zote, masuala ya nishati, mawasiliano, *EWURA* pamoja na masuala ya maji yote wote hao waendelee kuchangia asilimia 10 ya mapato yao yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa ujenzi, upande wa *SUMATRA* na masuala ya afya. Leo tunatumia shilingi bilioni 38 kupeleka matone ya *vitamins* kwa watoto lakini tungetumia pesa kidogo tu shilingi bilioni moja kwenda kwenye mazingira tukapanda miti ya matunda tungekuwa hatuna haja ya kutumia shilingi bilioni 38, tungeboresha mazingira huko huko tunapata afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia leseni mbalimbali za kilimo, mifugo, uvuvi na napendekeza shilingi 10 kwa lita ya mafuta iende kwenye mfuko huo. Pia masuala ya mawisiliano, leseni zote za mawasiliano tulishaweka kodi ya tozo kwenye magari chakavu na bidhaa chakavu zinazoingia nchini *20 percent* lakini hakuna hata shilingi yake inaaenda kwenye mazingira na lengo ya kodi hiyo ilikuwa inaharibu mazingira. Mbali na hiyo, kuna masuala mbalimbali mfano ya ujenzi, michoro mbalimbali ya *architecture* kwamba aina fulani ya majengo yakijengwa basi tozo yake iende huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa iMwenyekiti, pia mbolea tunayoagiza kutoka nje ya nchi, napendekeza kwamba shilingi 50 kwa kila mfuko pia iende kwenye mfuko huu. Tunaomba Serikali ikae iangalie kwenye mitambo yote ambayo inaingizwa kwa ajili ya kuanzisha nishati mbadala *(renewable energy)* pia ziondolewe kodi lakini pia mitambo ya kuchakata taka ngumu iondolewe kodi. Vilevile tungepata *relief* kwenye *income tax* iwe ni kama gharama kwamba asilimia fulani kama ni 2 - 5 iruhususiwe kampuni zozote zitakazochangia

kwenye masuala ya mazingira iwe ni *incentive* kwao wasitozwe kodi kwenye hilo ili iweze kuingia kwenye suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja suala hili lijadiliwe kwa kina ili hivi vyanzo na vingine Wabunge watakavyochangia viingie kwenye Mfuko huo wa Mazingira. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Jitu Soni kwa mchango wake mzuri sana. Vilevile niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote wa kambi zote mbili kutoka Chama Tawala lakini naona hoja hii imeungwa mkono pia na upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ulishaifanyia maamuzi lakini kwangu hiyo siyo hoja, nachotaka kusema ni kuhusu mfumo na utaratibu wa kikanuni wa kuendesha mijadala na kwenda kuhitimisha hoja kwa misingi ya kikanuni. Anachokisema Mheshimiwa Jitu na kukipendekeza kinakwenda kwenye hitimisho la hotuba ya bajeti ya Serikali na hotuba ya bajeti ya Serikali inaenda sambamba na *Finance Bill* Ambayo ndiyo mapendekezo anayoyasema Mheshimiwa Jitu Soni tukapate wapi fedha. Sasa kama tunazumgumza *Finance Bill* kwa mujibu wa kanuni hatuwezi kuizungumzia hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachopenda kushauri, kwa heshima yote ya michango ya Waheshimiwa Wabunge lakini na *concern* yao kubwa ya kutunza mazingira, Kanuni ya 105 ambayo ndiyo inaongoza majadiliano kipindi hiki cha Kamati inatuambia kabisa kwamba; "Baada ya Bunge kukamilisha mjadala wa Makadirio ya Wizara zote, ndani ya siku sita kabla ya Hotuba ya Bajeti Kusomwa Bungeni, Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti itafanya majumuisho kwa kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili

utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha, na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ndiyo itakuwa hoja ya kwanza ya msingi ndani ya *Budget Committee* lakini baada ya *Budget Committee* ndiyo kutakuja sasa mapendekezo ya *Finance Bill* wakati tunahitimisha hotuba ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nikuombe, ili jambo hili liweze kufanyika vizuri mapendekezo yaliyosemwa tusiyawahishe sasa, yapelekwe kwenye *Budget Committee* yafanyiwe kazi vizuri lakini wakati huo Waziri wa Fedha atakapoleta matumizi ya vyanzo vya fedha na jinsi zitavyotumika itakuwa ni wakati mzuri sana wa kuweza kuhitimisha suala hili vizuri kama tunavyofikiria...

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kusema hayo ili tuende sambamba na mjadala wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe subiri kwanza.

Mheshimiwa Jitu umeridhika na majibu ya Serikali maana hii ni *commitment.* Kanuni yetu ya 105 ndivyo inavyosema na wewe ni Mjumbe wa Kamati hiyo na Kamati ya Uongozi kwenye Kanuni ya 105 nayo inakuwa ni Kamati ya Bajeti. Kwa hiyo, *it is a very serious* na *pertinent issue*.

Kwa hiyo, mimi nakuomba tukubaline na Serikali na tuende nayo pamoja ili sasa tuisimamie pamoja na lile suala la kupigwa changa la macho ulilosema mwanzo tuhakikishe halitokei tena kwa sababu bila mazingira nchini mwetu nchi itaharibika kabisa. Sasa simama kubali maana wewe ndiyo mwenye hoja. *(Makofi)*

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ambayo ametoa Mheshimiwa Waziri lakini pia kwa imani kubwa ambayo ninayo najua na wewe utasimamia vizuri tukiwa pamoja kwenye Kamati ya Bajeti, nakubali kwamba itaenda huko na tutaijadili vizuri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, tunataka watu wenye muono kama huo. Waheshimiwa naongeza muda nusu saa kwa mujibu wa Kanuni. Sasa namuita Mheshimiwa Ahmed Ngwali.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudie suala nililochangia kuhusu *oil* na *gas.* Kama majibu hayatakuwa sahihi au yatababaisha nitakamata shilingi ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema dhamira ya kuanzisha sheria tatu za mafuta na gesi mwaka 2015 kwa haraka sana, moja katika jambo lililowavutia watu wengi na hasa Wazanzibar ilikuwa ni jambo la mafuta kuondolewa katika mambo ya Muungano. Hilo ndilo jambo lililokuwa na mjadala Zanzibar nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukizitazama hizo sheria zenyewe zilizopitishwa ni za kimuungano. Nikasema ukitizama Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa kwa ukurasa, mstari kwa mstari, hakuna mahali popote walipoahidi Katiba Mpya. Kwa hivyo, hilo jambo halionekani katika mazingira hayo.

Vilevile ukitizama ahadi zote za Rais hakuna mahali popote ambapo Rais kasema juu ya Katiba Mpya. Ukitizama bajeti hakuna mahali popote ambapo pesa zimetengwa kwa ajili ya Katiba Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nikasema kwa sababu Serikali haina fedha au haionekani mahali popote ikizungumzia juu ya Katiba Mpya, tulete hoja hapa Bungeni kwa kutumia Katiba Ibara ya 98(1)(b), tupige kura ya *two third majority* kwa pande zote mbili za Muungano ili tuliondoe jambo la mafuta na gesi katika mambo ya Muungano, hiyo

ndiyo hoja yangu. Jambo hili halitahitaji fedha wala kitu chochote, litahitaji tuje kwa wingi tupige kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu hizo sheria zote zilizotungwa ukizitizama haziondoi jambo la mafuta na gesi katika Muungano, hiyo ndiyo hoja yangu. Nikaenda mbali nikasema Sheria ya *Revenue* ya Mafuta iliyotungwa ya mwaka 2015 imekwenda mbali mpaka kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano imeruhusu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ahmed Ngwali.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Bado.

**MWENYEKITI:** Umeanza na utaratibu mzuri tu wa hoja yako ya kuzuia mshahara wa Waziri, baadaye ukaanza kujichanganya tena humu ndani. Hoja yako ni moja tu, wewe unazuia mshahara kwa sababu unaona sheria hii bado haijakaa vizuri. Sasa masuala ya hoja ya kupiga kura huo ni utaratibu mwingine siyo wa hatua hii. Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuombe Mheshimiwa Ngwali, hizi sheria hazikupitishwa haraka haraka labda kwa namna ya kuwaonea watu. Tulikuwa wote hapa, mimi nilikuwa *Attorney General* mkakimbia, tukabaki hapa na Wabunge wawili, namkumbuka Mheshimiwa Hamad Rashid.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zote jinsi zilivyo, iko The *Tanzania Extractive Insudutries (Transparency and Accountability) of 2015, The Oil and Gas Revenue Management Act* na *The Petroleum Act* zile hazikuvunja Katiba yoyote na ninazo hapa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ni hili analozungumza Mheshimiwa Ngwali kwamba tulete utaratibu wa kufanya mabadiliko kwenye ile Katiba chini ya Ibara ya 98 ya Katiba, sawa. Hata hivyo, ambacho Serikali tunashauri ni kwanza kwa nini unataka uliondoe kwa sababu mpaka ilivyo sasa hivi Zanzibar imekuwa na mfumo wake wa kisheria, imekuwa na mfumo wake wa kitaasisi wa kusimamia yenyewe rasilimali hii ya gesi na mafuta. Kwa hiyo, *so far* hakuna kitu ambacho kinatufanya tuharakishe mpaka hapa katikati tulete mabadiliko ya Katiba badala ya kusubiri mpango uwepo wa kupiga kura ya maoni kwa ajili ya Katiba ambayo inapendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri, hayo mambo unayoyasema ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi mimi sina, inawezekana hayamo humo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli ni kwamba hata kama hayamo ni kwa sababu tayari yapo kwenye sheria ya Kura ya Maoni juu ya kupiga kura, yapo kwenye Sheria hii ya Mabadiliko ya Katiba *(The Constitutional Review Act).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Rais alipolizindua Bunge hapa utakumbuka alisema anatambua ana kiporo cha Katiba Mpya ambapo hatua iliyobaki ni ya kupiga kura ya maoni.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sasa mnataka *commitment* ipi ya Rais? Siku anazindua Bunge hapa...

**MBUNGE FULANI:** Rais amesema hana ajenda hiyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekumbuka kumbe mlitoka, alisema hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa *AG.*

**MBUNGE FULANI:** Amesema hana ajenda ya Katiba.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Hapana, ratiba yake ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kumshauri Mheshimiwa Ngwali kwamba kilio cha Wazanzibar miaka nenda rudi ya kwamba waweze kusimamia hii rasilimali ya mafuta kimetekelezeka. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Bado.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Bado kitu gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar leo wana sheria yao ya kusimamia mafuta, wameunda taasisi ya kusimamia mafuta na kama mafuta yamepatikana kule Serikali ya Jamhuri ya Muungano haijawaingilia, sasa wanachotaka ni nini?

Kwa hiyo, naomba kushauri kwamba Mheshimiwa Ngwali kwenye hili anawahisha tu hoja. Naomba aelewe tu maelezo ambayo Serikali imeyatoa kuhusu suala hili halafu tuendelee na bajeti.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngwali ndege imeshapewa kibali na inalala Zanzibar. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linayo mamlaka ya kukabidhi mamlaka yake kwa mamlaka nyingine. Kama watu wa Zanzibar lengo lao lilikuwa ni kusimamia rasilimali ya mafuta na gesi na sheria iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya hivyo, ambaye anatakiwa kuchukua hatua kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kama hajaridhika ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuishtaki Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Mahakama Maalum ya Katiba, humu ndani hatuna *locus standi.* Mambo hayo yapelekwe kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kama hairidhiki wataamua kuishtaki Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndipo Mahakama ya Katiba itakapoitwa kulijadili jambo hilo na kulitolea uamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maadam Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetunga sheria, imeweka vyombo, tumuombe Mwenyezi Mungu, *Inshallah,* mafuta yapatikane, Zanzibar ineemeke, Tanzania ineemeke wote tusonge mbele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngwali.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, tunaomba utaratibu.

**MWENYEKITI:** Subiri kwanza Mheshimiwa Msigwa. Mheshimiwa Ngwali.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mwanasheria Mkuu anajua na Profesa Kabudi anajua na jambo hili lipo wazi kabisa kwamba kifungu 2(2) cha *Oil and Gas Revenue Management Act* kimevunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 64(3) na Mwanasheria Mkuu kakiri kwa sababu sheria ilitoa mamlaka kwa Zanzibar kutunga vyombo siyo kutunga Sheria ya Mafuta ambayo sheria yenyewe inafanana *copy and paste* na Mwanasheria Mkuu kama hunayo Sheria ya Zanzibar niitoe, *copy and paste* hakuna kitu ambacho... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ahmed Ngwali kwa hatua hii wewe unatakiwa useme mimi sijaridhika, natoa hoja maana muda wako unazidi kwenda ili sasa kama Wabunge wataridhia waijadili tuipigie kura. Halafu ukitaka utachukua ushauri uliopewa na Waziri wa Katiba na Sheria kushauri mamlaka zingine, endelea.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijaridhika na natoa hoja jambo hili lijadiliwe. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG,* Mheshimiwa Kabudi, Mheshimiwa Alberto, Mheshimiwa Profesa Muhongo, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Masauni na Mheshimiwa Khatib. Haya tunaanza na Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nataka kumuunga mkono Mheshimiwa Ngwali kwa anachokisema. Mwanasheria Mkuu hapa amekubaliana kabisa kwamba sheria ile imevunjwa, sijui amekwenda wapi. Hapa tunajadili suala ambalo kiudhati Katiba ya Jamhuri ya Muungano imesema hakuna sheria wala kanuni itakayokuwa juu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mpaka sasa inatambua kama gesi na mafuta bado yapo chini ya uangalizi wa Katiba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kama kuna njia zozote nyingine zilizofanyika hizo za kusema tu kwamba eti wameipa mamlaka Zanzibar, hiyo ni danganya toto hakuna ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi hapa umetoka, Mjumbe kutoka Baraza la Wawakilishi amekuja hapa na malalamiko akisema ile ndege tu ya utafiti imezuiwa, je, ni jambo gani lingine ambalo litaruhusiwa? Tufike mahali tuutendee haki ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutuambia kwamba litakuwa kwenye Katiba Mpya itakayokuja kwanza siyo tu Katiba Mpya imewekwa kiporo bali kiporo kimechacha. Kwa mujibu wa sheria iliyoleta suala la Katiba Mpya hakuna tena hilo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amethibitisha kwamba hana mpango na Katiba Mpya, amelitolea kauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka ni mamlaka kamili, iletwe sheria ya dharura ili tujadili humu na ipigwe kura ya maoni tuamue na tuone wenzetu wa CCM Zanzibar na hili nalo watalipinga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Alberto.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nataka kuelezea kwamba haya yanayosemwa mambo ya Muungano yamekuwa yakivumiliwa mara nyingi sana na kwa sababu ya utata uliopo Zanzibar imekuwa ikivunja sheria na Katiba. Kwa mujibu wa Katiba mambo ya bandari ni suala la Muungano lakini kuna *Tanzania Port Authority* na Zanzibar kuna yake. Suala la elimu ya juu Zanzibar imetengeneza mfumo wake. Kwa hiyo, haya yapo siku nyingi sana na yanaachiwa kwa ajili ya kuilinda Zanzibar, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, asubuhi nilisema hapa kwamba kweli tumekubaliana kwamba kuwe na asilimia 79 kwa 21 ya ajira za Muungano, Waziri anasema hakuna haja ya sheria, utaratibu ndiyo kwanza unaanza, matokeo yake ni kama haya yaliyotokea juzi. Mwalimu wangu Profesa Kabudi anasema mwenye *locus* ni Serikali ya Zanzibar na kwenda kushtaki ni kwenye Mahakama ya Katiba. Sasa nataka kumuuliza Mahakama ya Katiba imeundwa? Lingine yeye anajua kwamba hapa hatuundi vyombo, tumetengeneza *GFC* lakini kwa miaka 31 haijaundwa, sawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, mimi nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa kwamba Bunge hili halina mamlaka ya kuiambia Zanzibar itunge sheria, ile ni kanuni sasa siyo sheria, matatizo yatakuja katika utekelezaji. Wawekezaji wakija wakitizama sheria ile wakiona kumbe inaamuriwa na Serikali ya Muungano itengeneze itakuwa ni kanuni, bado *overall* ni sheria ya Muungano pamoja na ugawaji wa rasilimali na ukataji wa vitalu ni huko kwenye Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, tunataka kwa kifungu alichokitaja mtoa hoja iletwe Sheria ya Mabadiliko ya Katiba hapa kwa sababu tusidanganyane hakuna Katiba Mpya na tumeanza kunyofoa vitu vya Katiba Mpya tunavipenyezapenyeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi sipo mbali na wenzangu lakini ieleweke kwamba jambo lolote lililoko katika Katiba kama sheria mama haliondoshwi kienyejienyeji, mazungumzo na maelewano ni jambo lingine. Hapa amezungumza Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali tatizo ni nini zaidi. Amesema ukiangalia Ibara ya 98(1)(b) inatosheleza hilo jambo kuliweka vizuri kwamba tutakuja nalo hapa, tutapiga kura na hakuna hata upande mmoja utakataa. Sasa wengine wanasema mnawahisha, hakuna kuwahisha kwa sababu mwarobaini wa jambo hili ilikuwa liwekwe katika Katiba Mpya lakini hakuna mwangaza wa aina yoyote ya Katiba Mpya hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sisi tukasema kuna ubaya gani wa kutumia Ibara ya 98(1)(b) jambo hili likaletwa hapa Bungeni tukaliamulia tukamaliza, hakuna anayewahisha. Jambo dogo kigugumizi cha nini, tatizo ni lipi? Hili siyo jambo kubwa, tukubaliane tu. Hakuna haja ya kuchukua muda kusema tulirefushe, nia ni safi sote pamoja. Kwa nini kama nia ni safi kwa pamoja sote jambo hili lisiletwe hivi sasa wakati mambo ndio yanaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri Serikali ikubali tu baadhi ya mambo mengine, ikubali ukweli huu ukweli ulivyo kwamba yaani mwarobaini wa hivi sasa twende kwenye Ibara ya 98(1)(b) mambo yakae sawa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kubenea na Mheshimiwa Profesa Muhongo ajiandae.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ngwali. Sisi sote tuliopo kwenye Bunge hili Tukufu tumeapa kulinda na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameapa kulinda na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waziri Mkuu ameapa kulinda na kutetea katiba. Rais ameapa kulinda na kutetea Katiba na wewe umeapa kulinda na kutetea Katiba. Sio vyema kabisa kwamba Bunge lako Tukufu likaridhia uvunjaji wa Katiba unaofanywa hivi sasa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mafuta na gesi ni la Muungano. Mafuta yenyewe yanachimbwa kwenye bahari na bahari ni suala la Muungano. Serikali ya Zanzibar inapoambiwa inapewa madaraka yote ya kutunga sheria, hili jambo sisi hatulikubali. Katiba hii mpaka leo inamtambua Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Katiba hii haimtambui Makamu wa Pili wa Rais wala Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Bunge ndiyo chombo kikuu kinachosimama kwa niaba ya wananchi, kwa nini tunaruhusu mambo haya? Hiyo Katiba Mpya inayozungumzwa, Katiba Pendekezwa Mheshimiwa Profesa Kabudi anajua imepitishwa katika mazingira ambayo Taifa limegawanyika, haitekelezeki. Katiba yenyewe ina kasoro hata za uandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana Bunge hili likakubaliana kabisa kwamba suala ambalo Mwanasheria Mkuu na Serikali inalitetea halikubaliki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Muhongo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niwapatie mambo ya kitaalam zaidi halafu utaona kama siasa zako zina-*fit* hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili bomba tunalolijenga la kutoka Uganda mpaka Tanga kwenye Ziwa Albert, Serikali ya Uganda imegundua mafuta tani bilioni 6.5 ndiyo tunalijengea bomba ni ya Serikali ya Uganda na upande wa Magharibi Serikali ya Congo vilevile imegundua mafuta. Kwa hiyo, hapo suala utaachana na Katiba ya Uganda, Katiba ya Congo na utakuja kwenye taratibu za kimataifa, mipaka kimataifa. Kwa hiyo, tuwe na Katiba ama tusiwe na Katiba utafutaji wa mafuta upande wa Zanzibar ni lazima utaangukia mipaka ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali la kwanza nimuulize yule mpaka wa Tanzania Bara na Zanzibar upo wapi?

**MBUNGE FULANI:** Chumbe.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Haya, ni kama unatambulika kimataifa sio Bungeni humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kwamba upande wa Mashariki mwa Kisiwa cha Pemba na upande wa Mashariki wa Kisiwa cha Unguja na Mashariki mwa Kisiwa cha Mafia tukienda kama kilometa 200 huko tunafika mahali tunaingia kwenye maji ambayo hayapo upande wa Serikali ya Muungano.

Kwa hiyo, kimataifa mipaka inayotambulika ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Afadhali hili jambo tulitatue sisi wenyewe kwa sababu kama nilivyowaeleza hata Ziwa Tanganyika tukipata mle gesi suala la mpaka ni lazima litaenda kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu Mheshimiwa Mbunge ninachoomba ni kwamba kwanza afadhali utafiti ufanyike na hiyo kampuni anayoisema *TPDC* ndiyo imetoa ushauri kwa Serikali ya Zanzibar kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Profesa. Namuita Profesa Kabudi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nianze pale alipomalizia Mheshimiwa Profesa Muhongo. Kabla ya kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *semester* iliyopita nimefundisha *Law of the Sea.* Kulitoa suala hili katika orodha ya mambo ya Muungano tutakuwa tunavunja sheria za kimataifa. Gesi na mafuta mengi yapo katika *Exclusive Economic Zone* na siyo katika *territorial sea.* Someni Sheria ya *Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act* ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika *Exclusive Economic Zone* hatuna *sovereignty ownership,* tunaruhusiwa kutumia *living and non-living resources. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo basi ndiyo maana Sheria ya *Territorial Sea and Exclusive Economic Zone* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Waziri mhusika ni Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Kwa sababu eneo hilo ni eneo la kimataifa sisi tuna haki ya kutumia rasilimali hai na zisizo hai ndani ya eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo sheria hii iliyotungwa na Bunge iko sahihi, inasema; *"Oil and gas revenue derives from oil and gas operations or activities undertaking within Tanzania Zanzibar shall be governed and administered in accordance with the laws of Tanzania Zanzibar."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijasema tunga sheria, *shall be governed in accordance with the laws of Zanzibar, which means what? The Parliament of Tanzania recognizes the sovereignty of the Parliament of Zanzibar. Which means what? That law which is governed is a law. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ikija kwenye ngazi za kimataifa nataka niwaambie hivi na sio mkataba huu tu, chukueni hata *Multilateral Environmental Agreements* zinapokuja ndani ya nchi zinatekelezwa Zanzibar na Tanzania

Bara. Anayetoa taarifa kwenye vyombo vya kimataifa ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu nje ya Tanzania hakuna jambo ambalo siyo la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yasiyo ya Muungano...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mpina.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha Baraza la Mawaziri wa pande zote mbili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tarehe 13 Januari, 2017, jambo hili lilipoletwa kwenye kikao kile na taarifa zilivyokuwa, kwanza chimbuko lake kwa nini tulifika pale, ni kwa sababu hii ilikuwa moja ya kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utatuzi wa kero hiyo ya Muungano ikaamuliwa kwamba sasa tuanze kulifanyia kazi jambo hili. Jambo hili likawasilishwa kwenye Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na ikakubalika kwamba kweli hili jambo lijadiliwe ili pande zote hizi mbili zifanye hii shughuli ya uchimbaji wa mafuta na gesi kwa kujitegemea ili kuiondoa kero hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikao hivyo vimeenda na Wanasheria Wakuu wa Serikali wa pande zote mbili walikaa wakakubaliana lakini pamoja na sekta ya nishati upande wa Zanzibar na upande wa Tanzania Bara zikakubaliana. Mwisho tukafikia maamuzi kwamba basi zitungwe sheria ambazo zitaruhusu pande hizi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa *Chief Whip* wa Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekwisha....

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, limekwisha kwa maana ifuatayo na utahoji, utaratibu unao utatuhoji, lakini mimi nawarudisha kwenye Kanuni, kazi yangu ni Kanuni. Kanuni ya 64 kuhusu utaratibu wa shughuli zinazofanyika ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(c) kinasema kabisa kwamba kama jambo lolote ambalo lilijadiliwa na kutolewa maamuzi kwenye mkutano uliopo ama uliotangulia ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahususi, jambo hilo halina nafasi tena ya kuendelea kujadiliwa humu ndani. Jambo hili la sheria hizi lilishafanyiwa maamuzi na tulishalipigia kura na lilishapitishwa na tayari ni jambo halali la kisheria. Kwa hiyo, kwa mujibu tu wa Kanuni ukiacha wasomi hao waliozungumza, Mheshimiwa Profesa Kabudi hapa ametupeleka kwenye dhana halisi ya kitaalam, mimi nadhani utuhoji tu, kwa mujibu wa Kanuni jambo hili tulishalifunga na Kanuni inatuongoza utaratibu wa mambo yote yakishakuwa yamejadiliwa na kufungwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nadhani uendelee na utaratibu wako wa Kikanuni, tutafikia maamuzi tumalizie hoja hii kwa utaratibu unaotakiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngwali funga hoja yako.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijua kwamba watakuja na wataeleza na nakubaliana na Mheshimiwa Profesa Kabudi kaelezea kinagaubaga kwamba jambo hili halitoki katika mambo ya Muungano. Sisi hiki ndicho ambacho tulikuwa tunakitaka, kujua hiki ni kiini macho ama vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusema Serikali leteni hapa hoja ya kutumia Ibara ya 98(1)(b) tuliondoe jambo la *oil and gas* katika mambo ya Muungano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngwali...

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hoja yangu...

**MWENYEKITI:** Kwa hatua ya sasa hivi hoja yako useme mimi nasema tuhoji Bunge kwa sababu hiyo hatua yako wewe sasa hivi haipo, haina...

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tupige kura.

**MWENYEKITI:** Hiyo ndiyo hoja ya msingi. Waheshimiwa Wabunge, sasa nawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Waliosema siyo wameshinda.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Tuhesabu kura.

**MWENYEKITI:** Waliosema sio wameshinda. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kura zihesabiwe.

**WABUNGE FULANI:** Tuhesabu kura.

**MWENYEKITI:** Waliosema sio wameshinda.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kura zihesabiwe.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Tuhesabu kura.

**MWENYEKITI:** Kaa chini.

**MWENYEKITI:** Kaa chini. Jamani, Bunge hili linakwenda na Kanuni...

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Tuhesabu kura.

**MWENYEKITI:** Nasema hivi hoja ya kuhesabu kura ipo lakini yule anayesema aungwe mkono na watu kumi, hakuna mtu aliyeunga mkono, mmechelewa, imekwisha, *gone with the wind* inaitwa. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye *guillotine*. Katibu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama)*

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza. Kanuni ziko *very clear,* someni Kanuni ya 79, sio mnasimama tu hivi, kila kitu kinakwenda kwa utaratibu humu ndani. Katibu, *guillotine.*

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kif. 1001– *Administration and HRM Division*................................Sh.1,940,260,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts*.................. Sh.339,381,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning Division*...........Sh.637,132,000/=
Kif. 1004 – *Government Commun. Unit*......... Sh.198,596,000/=
Kif. 1005 – *Internal Audit Unit*..........................Sh.207,690,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Mgt. Unit*................. Sh.144,764,000/=
Kif. 1007 – *Information and Communication Techn Unit* ......... Sh.179,290,000/=
Kif. 1008 – *Legal Services Unit*........................ Sh.175,414,000/=
Kif. 2001 – *Union Secretariet*.......................... Sh.546,440,000/=
Kif. 5001 – *Environment*............................. Sh. 3,845,568,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kif. 1001 – *Administration and HRM Division*..................................Sh.1,000,000,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning Division*..........Sh.334,454,000/=
Kif. 5001 – *Environment*................................ Sh.5,453,998,437/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza shughuli yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka 2017/2018 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nawapongeza sana Mawaziri wawili, mmefanya kazi nzuri siyo kwenye bajeti tu *you are doing a good job even* kwenye nchi. Tutaomba tu Serikali iunge mkono Wizara hii, *survival* ya nchi hii ni Wizara hii, bila usalama wa mazingira *we are done. (Makofi)*

Baada ya maneno haya, niwatakie kila la heri na naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.08 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 25 Aprili, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*